# UCHANGANUZI WA HOTUBA ZA MWALIMU NYERERE KWA MKABALA WA NADHARIA YA BALAGHA

**YASIN SALIM MUSA**

**Tasnifu hii Imewasilishwa katika "*Board of Post Graduate Studies*" ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu (Ph.D Kiswahili) ya Chuo Kikuu cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**SEPTEMBA, 2015**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo Kikuu chochote.



**18 / 09 / 2015**

**Yasin S. Musa**

**AD 12/0263/10**

**IDHINI**

Tasnifu hii Imewasilishwa Kutahiniwa kwa Idhini yetu kama Wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi............................................. Tarehe.............................................

**Dkt. Furaha Chai**

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu

Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Sahihi............................................. Tarehe.............................................

**Prof' James Onyango Ogola**

Idara ya Taaluma za Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.

## HATI LINZI

©2015

**Yasin Salim Musa**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kutafsiri, kunakili, au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton

## TABARUKU

Kwa mwanangu Habiba; kazi hii iwe chambo cha usomi na mwelekeo mwema wa maisha yako Duniani na Akhera - Allwahumma Amin.

## SHUKRANI

Ufanisi wa tasnifu hii ni mchango wa watu wengi ambao kwa pamoja ningependa kuwashukuru. Baada ya kumshukuru Allah kwa kuniwezesha kuendelea kiusomi hadi kiwango cha uzamifu; kwa dhati ya nafsi yangu nawashukuru wasimamizi wangu: Profesa Ogola Onyango na Dkt Furaha Chai. Kwao nimejifunza mengi. Ingawa walikuwa na majukumu mengi yaliyowahitaji kila uchao, hawakusita kunitengea muda kila nilipokuwa nahitaji msaada wao. Kwa moyo mkunjufu, waliniongoza kuanzia katika kuandika pendekezo hadi kufikia hitimisho la tasnifu hii. Wema wao si rahisi kuuelezea ukafikia ukomo wa utoshelezi wa nafsi. Hii ni kutokana na jinsi walivyokuwa wakinichukulia sawa na mwana wa familia zao. Walikuwa wakinikarimu nyumbani kwa chakula na malazi, wakinichanganya na familia zao ili nisijihisi upweke – huku wakinifanyia tafrija mjini na chuoni. Kama hiyo haitoshi, Dkt Furaha Chai akinitengea chumba cha kulala takriban kila nilipokuwa nikisafiri kwa ajili ya usomi, akinichukuwa kwa gari lake kwenda na kurudi nyumbani kwake na akinisafirisha pia kila nilipokuwa nikielekea Uganda au Tanzania (nyumbani).

Zaidi ya hayo, wasimamizi wangu 'hawa' pindi walipobaini kwamba nimepata magumu katika kulipa karo, daima walikuwa wakiniusia nisikate tamaa, wakiniasa nifanye jitihada za kuikamilisha tasinifu hii, huku wakiutenga muda zaidi - wakinipa tarehe za papo kwa papo kama mshawasha wakunifanya niweze kukamilisha utafiti huu kwa haraka. Nawashukuru sana, mvuvumko wa wema wao kwangu ulinitia ari na wepesi wa kuikamilisha kazi hii. Na daima nimebakia nikijiuliza "Utawapata wapi watu watakaokuhangaikia kuhusu mafanikio yako hata iwe wagharamike juu yako kwa hali na mali? Dkt Furaha Chai, Profesa Ogola Onyango na Profesa Beja Karisa ni mfano wa kuigwa si tu kwamba wamenifunza hata nikahitimu kozi hii ya uzamifu lakini wamenifunza maisha, uvumilivu, uungwana, huruma na moyo wa kuwasaidia wengine kiusomi. Kwa hakika namwomba Mwenyezi Mungu awabariki kwa wema wao hapa Duniani na baada ya Mauko yao.

Sanjari na shukrani kwa wasimamizi wangu pia heshima na taadhima nazitoa kwa Profesa Beja Karisa kama nilivyokwisha kudokeza hapo awali. Profesa Beja Karisa alikuwa katika mstari wa mbele katika kunifunza na kunielekeza mengi tangu shahada yangu ya kwanza hadi hii ya uzamifu. Kwa hiari, aliutenga muda wake na amali zake ili niweze kufanikisha utafiti huu. Kwa nia njema alikuwa akifuatilia maendeleo yangu. Mara nyingine alikuwa akinihitaji nyumbani kwake (Kilifi) kwa ajili ya kunisaidia na akiutenga muda wake mchana na usiku hadi tatizo alilolibaini liwe limekwisha. Zaidi ya hayo alikuwa akijitolea kunilisha na kunipa mahala pa kulala na akinisafirisha huku na kule kwa ajili ya ufanisi wa utafiti

wangu. Alinichanganya pia na familia yake kama alivyokuwa akinifanyia Dkt Furaha Chai. Na kila nilipokuwa nikiondoka kurudi nyumbani alikuwa akiosha gari lake mafuta toka Kilifi hadi Mombasa kama alivyofanya wakati nilipokuwa nikiwasili Mombasa kuelekea Kilifi. Na ndiyo kusema daima sitawasahau (Dkt. Furaha Chai, Profesa Ogola Onyango na Profesa Beja Karisa kwa wema wao). Kwa hakika nainyanyua mikono yangu kwa Mola Karima awabariki kwa kila jema.

Nawashukuru pia walimu wote wa Chuo Kikuu cha Egerton kwa mchango wao mkubwa ambao kwa namna moja au nyingine waliniwezesha kusonga mbele hadi kuukamilisha utafiti wangu. Hasa nikikumbukia hatua nilizopitia za utetezi wa pendekezo langu hadi kuhitimisha tasnifu hii, walinishauri mengi ya manufaa. Namwomba Mwenyezi Mungu awalipe kila la Kheiri.

Bila kumsahau Dkt. Badru Matasi, aliyenisaidia, akaniusia na kunielekeza pia kwa mawazo na kwa matendo mema kuhusu jinsi ya kuuendea usomi wangu. Nitamkumbuka daima aliponikuta ofisini nikiwa nimesononeka sana akiniuliza kulikoni! Nikimjibu sijui kulikoni kuhusu usomi wangu. Alinishika mkono na tukawa mguu mosi mguu pili nje huku akiniusia nisikate tamaa kwani Mwenyezi Mungu ndiye mweza- atakaloamua ndilo litakalokuwa. Kwa hiyo, ridhika nalo. Mawazo yake daima nilikuwa nikiyazingatia na yamenifaa sana. Kwa hakika namwombea kwa Allah amfungulie milango ya baraka na amani Duniani na Akhera.

Naukumbuka uongozi wa IUIU. Jitihada zao zilionyesha kilele dhidi ya usomi wangu, wema wao sitausahau; walinipa barua ya kuomba msaada wa fedha. Ahsanteni sana kwa kuujali usomi wangu. Kwa uthibati wa nafsi yangu namwomba Allah ayaauni matendo yao. Allahumma Amin.

Kwa heshima na taadhima nawashukuru wazazi wangu kwa kunilea na kunisaidia kiusomi kadiri ya walivyojaaliwa. Nakuomba Allah uwalipe kila la kheiri Duniani na Akhera.

Wakadhalika namkumbuka mlezi wangu Sheikh Saidi Musa. Daima alikuwa akinihurumia kutokana na magumu yaliyokuwa yakinifika wakati wa kuiandika tasnifu hii. Suala la kukosa karo lilimtia simanzi kubwa lakini kwa muda wote akawa akinihimiza nisikate tamaa. Na katika jambo jema ambalo sitalisahau kamwe ni pale alipodiriki kunihimiza nioe ingawa nipo katika mchakato wa kozi nzito. Alikuwa akiniombea dua huku akinipigia simu za kuniliwaza. Na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu akanijaalia nikaoa na kumpata mtoto kabla ya kuhitimu

kozi hii. Kwa hakika ushauri wake ulinifaa sana. Namwomba Allah amfungulie milango ya Baraka, amzidishie imani na amjaaliye mwisho mwema. Allahumma Amin.

Pia nawashukuru Mwl. Fihiri Kiskeni na Mwl. Kurwa Mushi walionisaidia pakubwa. Walinipokea DSM na kunikarimu kwa chakula na malazi huku wakinielekeza namna ya kuwapata wasailiwa wa deta ya maoni. Mbali na hayo, walikuwa wakinipatia usafiri ndani ya mji ili nisipate magumu katika utafiti wangu. Mara nyinyine wakinipa fedha za kusafiri kutoka DSM hadi Uganda na mara nyingine kutoka Uganda hadi DSM. Hakika, kwa dhati ya nafsi yangu, namwomba Allah awalipe malipo mema Duniani na Akhera. Allahumma Amin.

Changamoto ya nafsi yangu ni pale Mwl. Idd Kikong'ona ambapo wakati mmoja niliposafiri DSM nikiwa mgonjwa, alinichukuwa hadi hospitalini, kutoka Kinondoni Shamba hadi Magomeni kwa Wachina na kugharamia gharama zote ambapo nisingeweza si tu kwa kufika katika kituo cha afya lakini nilikuwa nimeishiwa sana kifedha. Fauka ya hayo, alinisaidia kuniongoza kwa baadhi ya wasailiwa wa deta ya maoni. Kwa hakika mchango wake sitausahau milele. Namwomba Allah amlipe kila la kheiri Insha'allah.

Nawakumbuka walimu wote wa IUIU, Dkt. Mayaka Gwachi wa Laikipia University - Kenya, Sheikh Mohamed Qassim, Answar Kachwamba, Twahir Rwamraza, Jumbe Ali Jumbe, Hassan Imam na Khudhaifa Khofu - wote wa Ubungo I. H. & Collage of Education, walinisaidia sana: Wengine wao walinisaidia kwa fedha, vitabu, majarida na magazeti kwa ajili ya kuufanisisha usomi wangu. Namuomba Allah awalipe kila la kheiri.

Fauka ya hao, namsihi mke wangu (Amina husein) aniwie radhi kwa mengi, kutokana na kizunguukuti cha usomi. Suala la fedha lilikuwa gumu. Ilinibidi nijidundulize kila mara ili niweze kwenda chuoni kwa masomo. Namwomba Allah (SW) amjaaliye uvumilivu zaidi, moyo wa amani na umakinifu wa njia iliyonyoka - iwe ni faraja kwake Duniani na Akhera.

Ndugu zangu wote ambao kwa namna moja au nyingine walinivumilia na hata wakajitolea kunisaidia ili niweze kuhitimu kozi yangu hii: Rajabu, Aisha, Kasim, Mustafa, Rahim na Amina. Namwomba Mwenyezi Mungu awalipe kila la kheiri

Naushukuru uongozi wa wilaya ya Kinondoni kwa kuniruhusu kufanya utafiti katika eneo hilo. Na ninawashukuru pia wasailiwa wote kwa kuniridhia nikawasaili hata nikapata deta ya maoni. Mwenyezi Mungu awalipe mema kwa mema mliyonifanyia. Amin.

# IKISIRI

Mshawasha wa idhaa ya taifa wa kuzipeperusha hotuba za Mwalimu Nyerere hewani kila uchao kabla ya utafiti huu, ulikuwa bado haujafahamika. Katika kuziba mwanya wa kielimu, utafiti huu ulichanganua hotuba zake ili kubaini ikiwa kuna maudhui mahsusi na mbinu za kiisimu zinazozua ushawishi katika hotuba zake hasa kwa mkabala wa Nadharia ya Balagha. Madhumuni ya Utafiti huu yalikuwa ni: Kutambulisha maudhui mahususi yaliyomo katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere; kubainisha jinsi mitindo katika hotuba za Mwalimu Nyerere inavyotumika kushawishi hadhira; na kupambanua athari zinazoikumba hadhira ya wasikilizaji ama wasomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere. Maswali ya utafiti yalikuwa ni: Hotuba za Mwalimu Nyerere zina maudhui gani mahsusi yanayoweza kutambulishwa? Mwalimu Nyerere alitumia mitindo gani katika hotuba zake kushawishi hadhira? na Hotuba za Mwalimu Nyerere zina athari gani mahsusi kwa hadhira? Nadharia ya Balagha iliyoasisiwa na Aristotle ndiyo iliyoongoza utafiti huu. Hotuba teule ishirini na sita za kimaandishi zilichanganuliwa kwa njia ya uchunguzi wa yaliyomo ili kupata deta ya maudhui na mitindo ili kukidhi madhumuni ya kwanza na ya pili utafiti huu. Deta ya maoni ya watu ishirini na sita wenye desturi ya kusikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kupitia redio ya Taifa (T B C) ilikusanywa ili kukidhi madhumuni ya tatu. Uchanganuzi wa deta ulifanyika kwa kutumia mbinu ya kithamano na ya kiwingidadi. Mbinu hizo pia ndizo zilizotumika katika kuelezea matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba kulikuwa na maudhui ya: Umoja wa kitaifa na wa Wafanyakazi, Azimio la Arusha: Ufaafu wake, kupaa na kutunguliwa kwake, Uongozi bora: Uwajibikaji, Makemevu kuhusu Rushwa, Ukabila na Udini, Umuhimu wa Sheria, Demokrasia, Ubaguzi, Onyo kwa Idd Amin; Kilimo kwanza na Elimu kwa wote. Pia mbinu za kiisimu zifuatazo zilibainika: maswali ya kibalagha; tashbiha; tashhisi; tashtiti, takriri neno, tafsida; tafsida kengeushi, istiara, mafumbo, kinaya, kejeli, uchanganyaji ndimi, usimulizi misemo, methali na uchimuzi. Na maoni ya wasailiwa kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere ilibainika kwamba hadi hivi leo Watanzania wangali wakizitafakari na kuzifurahia hotuba za Mwalimu Nyerere kiasi cha kuzichukulia kama dira ya maongozi yao. Ni imani ya mtafiti kwamba, utafiti huu utachangia katika taaluma ya uchanganuzi usemi na usomi wa balagha katika hotuba.

## ABSTRACT

Among the many things that made Mwalimu Nyerere, the first president of Tanzania, porpular to Tanzanians and the rest of the world up to now are his speeches and the style in which they were delivered on different occasions. This popularity has continued even after having passed away in 1999 as manifested in continued airing out of the speeches on daily basis on the Tanzania Broadcasting Corporation. The reasons for according those speeches such priority had not yet been empirically established. This study, therefore, sought to analyse those speeches from the rhetorical perspective in order to bridge the knowledge gap. The objectives of the study were to establish the various themes embedded in Mwalimu Nyerere’s speeches and how style is used to persuade the audience that listen to them. It was hypothesized that Mwalimu Nyerere used to apply specific themes and styles in delivering his speeches and that the speeches had certain effects on the listeners. The study was guided by the Rhetoric Theory of Aristotle. Twenty six Speeches of Mwalimu Nyerere were collected from Mwalimu Nyerere Foundation libraries and analysed by using content analysis to establish themes and styles. Opinions were obtained from twenty six respondent to establish effect of speeches on audiences. The study revealed that Mwalimu Nyerere's speeches have specific themes which include: Unity; Importance of sticking to law; Corruption; Exemplary leadership; Significance of the Arusha Declaration; Workers' Unity; Education for all; A warning to Idd Amin; Democracy; The Ups and Downs of the Arusha Declaration. Furthermore; the speeches exhibited the use of rhetoric manifested in various linguistic devices and dramatic techniques intended to persuade the listenership. These include: Similes, Personification, Satire, Repetition, Metaphor, Parables, Irony, Code mixing, Proverbs and Narratives. The study shows that through such use of language, Mwalimu Nyerere’s speeches continue to attract the attention of many Tanzania to the extent that they regard them as guiding principles in as far as exemplary leadership is concerned. This study is a contribution to Discourse Analysis and the application of rhetoric in speeches. It is anticipated that it will benefit subsequent researchers, Sociolinguistics, politicians and community at large.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI.......... ii**

**HATI LINZI.......... iii**

**TABARUKU.......... iv**

**SHUKRANI.......... v**

**IKISIRI.......... viii**

**ABSTRACT.......... ix**

**YALIYOMO.......... x**

**ORODHA YA MAJEDWALI.......... xiv**

**VIFUPISHO VYA MANENO.......... xvi**

**VIFUPISHO VYA HOTUBA.......... xvii**

**SURA YA KWANZA : UTANGULIZI.......... 1**

1.1 Usuli wa Mada.......... 1

1.2 Mada ya Utafiti.......... 4

1.3 Madhumuni ya Utafiti huu.......... 4

1.4 Maswali ya utafiti.......... 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti.......... 5

1.6 Upeo wa Utafiti.......... 5

1.7 Maelezo ya Istilahi.......... 6

**SURA YA PILI : MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA.......... 7**

2.1 Utangulizi.......... 7

2.2 Mapitio ya Maandishi.......... 7

2.2.1 Maandishi kuhusu Maudhui ya Hotuba.......... 7

2.2.2 Maandishi kuhusu Mitindo katika Hotuba.......... 10

2.2.3 Mandishi kuhusu Athari katika Hotuba.......... 13

2.3 Misingi ya Nadharia.......... 17

2.4.1 Sababu za Kuchagua Nadharia ya Balagha.......... 18

2.5 Fahiwa kuhusu Balagha.......... 19

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.......... 22**

3.1 Utangulizi.......... 22

3.2 Mahala pa Utafiti.......... 22

3.3 Kundi Lengwa.......... 22

3.3.2 Maoni ya Wasailiwa.......... 22

3.4 Deta ya Utafiti.....22
3.5 Utaratibu wa Ukusanyaji wa Deta .....23
3.5.1 Hatua za Ukusanyaji Deta ya Maudhui na Mitindo.....23
3.5.2 Hatua ya Ukusanyaji wa Deta ya Maoni.....23
3.6 Uchanganuzi wa Deta .....23
3.6.2 Mauhui kuhusu Uongozi Bora .....24
3.6.2.1 Mfano wa Jinsi Deta ya Hotuba Ilivyochanganuliwa kwa njia ya Kithamano.....24
3.6.3 Maudhui ya Umoja wa Kitaifa.....25
3.6.3.1 Mitindo Iliyotumika katika Maudhui ya Umoja wa Kitaifa .....26
3.6.4 Maudhui kuhusu Rushwa.....28
3.6.4.1 Mitindo Iliyotumika katika Maudhui - Kuhusu Rushwa .....29
3.7 Jinsi Deta ya Maoni Ilivyochanganuliwa kwa njia ya Kithamano .....33
**SURA YA NNE : UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA .....35**
4.1 Utangulizi.....35
4.4.1 Maudhui ya Umoja wa Kitaifa (Muungano).....48
4.4.1.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Umoja wa Kitaifa (Muungano).....49
4.4.2 Maudhui kuhusu Kupuuza na kutokuijali Katiba .....56
4.4.2.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Kupuuza na kutokuijali Katiba .....56
4.4.3 Maudhui kuhusu Umuhimu wa Sheria .....58
4.4.3.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Umuhimu wa Sheria .....59
4.4.4 Maudhui kuhusu Rushwa.....61
4.4.4.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Rushwa .....62
4.4.5 Maudhui kuhusu Ukabila na Udini .....67
4.4.5.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Ukabila na Udini.....67
4.4.6 Maudhi kuhusu Umoja wa Wafanyakazi .....73
4.4.6.1 Mitindo Iliyotumika katika Maudhui ya Umoja wa Wafanyakazi .....74
4.4.7 Maudhui kuhusu Kilimo Kwanza .....75
4.4.7.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Kilimo Kwanza.....76
4.4.8 Maudhui kuhusu Rai ya Tanzania ya Kutofungamana na Upande wowote .....80
4.4.8.1 Mitindo iliyotumika kuhusu Maudhui ya Kutofungamana na Upande wowote.....80
4.4.9 Maudhui kuhusu Uwajibikaji.....85
4.4.9.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Uwajibikaji .....86
4.4.10 Maudhui kuhusu Uongozi Bora .....94

4.4.10.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Uongozi bora ............................................96
4.4.11 Maudhui kuhusu Ufaafu wa Azimio la Arusha ........................................................107
4.4.11.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Ufaafu wa Azimio la Arusha ...................108
4.4.12 Maudhui kuhusu Ubaguzi .........................................................................................115
4.4.12.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Ubaguzi ...................................................116
4.4.13 Maudhui kuhusu Elimu kwa Wote ..........................................................................118
4.4.13.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Elimu kwa Wote .....................................120
4.4.14 Maudhui kuhusu Onyo kwa Idd Amin.....................................................................126
4.4.14.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Onyo kwa Idd Amin ...............................127
4.4.15 Maudhui kuhusu Demokrasia ..................................................................................131
4.4.15.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Demokrasia .............................................133
4.4.16 Maudhui kuhusu Kupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha .............................136
4.4.16.1 Mitindo katika Maudhui ya Kupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha .........140
4.6 Hisia za Hadhira kuhusu Hotuba za Mwalimu Nyerere ................................................156
4.6.2 Maoni ya Kijumla kuhusu Ushawishi wa Hotuba za Mwalimu Kwa Wasailiwa.........166
4.7 Mpangilio wa Hotuba za Mwalimu Nyerere ................................................................175
4.7.1 Utangulizi wa Hotuba za Mwalimu Nyerere .............................................................175
4.7.2 Uendelezaji wa Hotuba za Mwalimu Nyerere ...........................................................176
4.7.3 Hitimisho la Hotuba za Mwalimu Nyerere ................................................................176
4.8 Matokeo ya Utafiti .........................................................................................................177
**SURA YA TANO : MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....................180**
5.1 Utangulizi.......................................................................................................................180
5.2 Muhtasari wa Utafiti huu ..............................................................................................180
5.3 Hitimisho........................................................................................................................181
5.3.1 Maudhui Mahsusi Yaliyomo katika Hotuba za Mwalimu Nyerere .............................181
5.3.2 Mitindo Mahsusi Yaliyomo katika Hotuba za Mwalimu Nyerere...............................181
5.3.3 Athari Mahsusi Zilizomo katika Hotuba za Mwalimu Nyerere...................................181
5.4 Mapendekezo ................................................................................................................182
5.4.1 Mapendekezo Kuhusu Waneni Wengine....................................................................182
5.4.2 Mapendekezo kuhusu Tafiti nyingine.........................................................................183
**MAREJELEO ..................................................................................................................184**
**VIAMBATISHO ...............................................................................................................188**
KIAMBATISHO ‘A’: MWONGOZO WA MASWALI KWA WASAILIWA. ................188

KIAMBATISHO 'B': HOTUBA ZILIZOCHANGANULIWA ............................................190
KIAMBATISHO 'C': AINA YA HOTUBA, MAHALA PA HUTUBIO NA MWAKA HUSIKA ............................................................................................................................192
KIAMBATISHO 'E' BARUA YA MAOMBI KUHUSU KUFANYA UTAFITI ................193
KIAMBATISHO 'F' BARUA YA RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI............................194
KIAMBATISHO “G” : RAMANI KUONYESHA ENEO LA UTAFITI HUU...................195

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 1: Mfano wa Jinsi Deta ya Hotuba Ilivyochanganuliwa Kiwingidadi........................23
Jedwali 2: Mfano wa Jinsi Deta ya Maoni Ilivyochanganuliwa kwa njia ya Kiwingidadi......29
Jedwali 3: Maudhui Mahsusi na Mbinu za Kibalagha (Mbinu za Kiisimu)............................36
Jedwali 4: Maudhui ya Umoja wa Kitaifa ............................................................................146
Jedwali 5: Maudhui kuhusu Kupuuza na Kutokujali Katiba ................................................147
Jedwali 6: Maudhui kuhusu Umuhimu wa Sheria ..............................................................147
Jedwali 7: Maudhui kuhusu Rushwa ....................................................................................147
Jedwali 8: Maudhui kuhusu Ukabila na Udini.....................................................................148
Jedwali 9: Maudhi kuhusu Umoja wa Wafanyakazi............................................................149
Jedwali 10: Maudhui kuhusu Kilimo Kwanza.....................................................................149
Jedwali 11: Maudhui kuhusu Kutofungamana na Upande wowote......................................150
Jedwali 12: Maudhui kuhusu Uwajibikaji ...........................................................................150
Jedwali 13: Maudhui kuhusu Uongozi Bora........................................................................151
Jedwali 14: Maudhui kuhusu Ufaafu wa Azimio la Arusha .................................................151
Jedwali 15: Maudhui kuhusu Ubaguzi.................................................................................152
Jedwali 16: Maudhui kuhusu Elimu kwa Wote ...................................................................152
Jedwali 17: Maudhui kuhusu Onyo kwa Idd Amin .............................................................153
Jedwali 18: Maudhui kuhusu Demokrasia...........................................................................153
Jedwali 19: Maudhui kuhusuKupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha .......................154
Jedwali 20: Umaratokezi wa Mbinu za Kiisimu na Asilimia yake kwa Maudhui yote yaliyobainika katika Utafiti huu..........................................................................154
Jedwali 21: Maudhui mahsusi, Maoni na Athari za Wasailiwa............................................156

## ORODHA YA VIUNZI VYA UTAFITI

2.4 Kiunzi 1: Msingi wa Kidhana wa Utafiti ........................................................................ 18
2.6 Kiunzi 2 : Nadharia ya Balagha ya Aristotle ..................................................................... 20

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| CCM | : | Chama Cha Mapinduzi |
| UK | : | Ukurasa |
| DSM | : | Dar es Salaam |
| NML | : | Nadharia ya Mtindo ya Leech |
| TUKI | : | Taansisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| TANU | : | Tanganyika African National Union |
| T B C | : | Tanzania Broadcasting Corporation |
| NKN | : | Nadharia ya Kitendo Neni |
| TANAPA | : | Tanzania National Park |
| TPDF | : | Tanzania People's Defence Forces |
| Mt | : | Mtakatifu |
| Bw | : | Bwana |
| Mwl | : | Mwalimu |

## VIFUPISHO VYA HOTUBA

| | | |
|---|---|---|
| MTU | : | Muungano wa Tanganyika na Unguja (Aprili 25, 1964) |
| SS | : | Sisa ya Serikali (Juni 8, 1965) |
| MUSW | : | Maendeleo ya Uchumi na Siasa za Watanzania (Juni 1966) |
| EK | : | Elimu ya Kujitegemea (Mei 4, 1967) |
| UV | : | Ujamaa Vijijini (Septemba 1967) |
| SU | : | Sikukuu ya Uhuru (Desemba 9, 1967) |
| MJW | : | Maana ya Jeshi la Wananchi (Julai 27, 1968) |
| KK | : | Kupanga ni Kuchagua (Mei 28, 1969) |
| JU | : | Juu ya Uchaguzi (Oktoba 24, 1970) |
| EHM | : | Elimu Haina Mwisho (Mkesha wa Mwaka 1970 na 1971) |
| MM | : | Madaraka Mikoani (Mei 1972) |
| MMT | : | Mkutano Mkuu wa TANU (1973) |
| ME | : | Maana ya Elimu (1975) |
| AMWW | : | Azimio la Musoma na Wajibu wa Walimu (Februari 8, 1975) |
| AAMK | : | Azimio la Arusha baada ya Miaka Kumi (Januari 1977) |
| MAV | : | Mwalimu Atangaza Vita (Novemba 2, 1978) |
| OIA | : | Onyo kwa Idd Amin (Desemba 9, 1978) |
| NSM | : | Njaa si Jambo la Mzaha (Machi 5, 1981) |
| SE | : | Semina ya Elimu (Oktoba 22, 1984) |
| AW | : | Awaaga Wanajeshi (Agosti 2-3, 1985) |
| KW | : | Kuwaaga Wananchi (Novemba 1985) |

| | | |
|---|---|---|
| KK2 | : | Kujitawala ni Kujitegemea (Februari 5, 1987) |
| CCM | : | Chama Cha Mapinduzi (Oktoba 22, 1987) |
| TM | : | Tuwashe Mwenge (Februari 18, 1992) |
| N | : | Nyufa (Machi 13, 1995) |
| TTT | : | Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi (Mei 1, 1995) |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Hotuba ni mawazo na maoni yanayotolewa na mhutubu kwa hadhira katika sherehe iliyoandaliwa rasmi kwa madhumuni mahsusi. Hotuba inaweza kuwa ya masimulizi au ya kuandikwa kwa minajili ya kusomwa. Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mbele za watu (TUKI, 2004).

Hotuba za Marais wa nchi mara nyingi huchukuliwa kama sera za maongozi ya nchi. Miongoni mwao kuna walio na vipaji vya kuyapanga maneno kiasi cha kuivutia hadhira kuzipenda hotuba zao, wakazikariri na hata kuziingiza katika utekelezaji wa maisha ya kila siku. Mwalimu J. K. Nyerere, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni miongoni mwa viongozi kama hao. Hotuba zake hadi hivi leo zingali zinazingatiwa na Watanzania, na katika asasi nyingi zinazohusu maisha yao ya kila siku kama vile siasa na elimu. Usikilizaji na usomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere umeleta changamoto kwa wananchi ndani na nje ya nchi kiasi cha wengine kuamini kwamba mawazo yake ndiyo dira na maongozi ya sera za nchi hadi hivi leo. Imani hii inapata mashiko kutokana na wasifu wa malezi yake na pilika zake za kimaisha; ambapo ilibainika kwamba, ingawa alikuwa ni mtoto wa Chifu, mtazamo wake haukuathiriwa na mawazo na hadhi za kichifu. Badala yake alipenda haki sawa kwa wote. Makuzi haya yalikuwa msingi mkubwa katika usomi wake; ambapo (Mwalimu) baada ya kumaliza elimu ya shule ya msingi Mwisenge mkoani Musoma, alijiunga na shule ya Sekondari Tabora na baadaye akapata Diploma ya Ualimu katika Chuo cha Makerere Uganda, mwaka 1945. Fauka ya Makerere Mwalimu alifundisha kwa muda katika shule ya Sekondari ya Mtakatifu Maria, Tabora kabla ya kwenda Edinburgh University, Scotland ambapo alizawadiwa Shahada ya uzamili. (Mwisige; mwaka 2009)

Mwalimu alipokuwa masomoni alikuwa akishiriki katika midahalo mbalimbali iliyohusu masomo yake lakini pia yaliyogusa maendeleo ya watu hasa Watanganyika. Kuna ubainifu kwamba Mwalimu alionyesha uwezo wa hali ya juu katika midahalo iliyokuwa ikiendelea shuleni. Mbali na kuonekana akizitetea haki zake na za wenzake shuleni, hakulisahau taifa lake hasa ilipobainika kwamba sheria za kikoloni zilikuwa zikiwakandamiza Watanganyika. (Mwakilasa, Mwaka 2009)

Machungu ya Mwalimu kuhusu unyanyaswaji na Wakoloni. Ulianza kuzaa matunda alipokuwa anafundisha “Mtakatifu Maria Secondary school”. Mwalimu alisaidia kuanzishwa kwa duka la ushirika ili kuendeleza mapambano ya kupinga manyanyaso waliyokuwa wakiyapata kutoka kwa wakoloni wakati huo. Kwa mwegemo huo alikubali wadhifa wa kuwa katibu wa tawi la “Tabora African Association”, wadhifa ambao ulimfanya atambuliwe na kuaminiwa. Lakini kuthaminiwa zaidi kulitokana na kuitumia elimu yake kwa manufaa ya umma. (Mwakilasa, 2009)

Mwalimu alichaguliwa kuwa Rais wa Tanganyika Africa Association (TAA) mwaka 1953 wakati akiwa Mwalimu katika shule ya Sekondari Pugu, Dar es Salaam. Katika harakati za kufanikisha ukombozi wa Tanganyika, alijikusuru kutembea kwa miguu toka Pugu (nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam takriban kwa mwendo wa kutwa nzima) hadi jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya mikutano ya kupigania uhuru. Mwaka 1954 Mwalimu alichaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa TANU (Tanganyika African National Union) na kwa hivyo, akawa na kazi mbili kwa wakati mmoja. Ingawa alikuwa akipata mshahara mzuri katika ajira ya ualimu, alikubali kuwa Rais wa TANU (Mwalimu wa Watanganyika wote) bila mshahara. Jambo ambalo lilikuwa ni kujitoa muhanga hasa ilipokuwa haijulikani hatma ya kisiasa kwa mapambano ya Watanganyika dhidi ya wakoloni. Wakoloni walitumia njia nyingi ili Mwalimu aachane na TANU. Walitambua kwamba Mwalimu alikuwa tishio kwao katika maswala ya kudai uhuru. Lakini kutokana na msimamo aliokuwa nao Mwalimu alikataa kata kata kuacha uongozi wa chama - kwa ghera ya kupigania uhuru.

Tarehe 22/3/1995, Mwalimu kwa hekima zake na bila kinyongo aliwasilisha barua ya kujiuzulu Ualimu kwa Mwalimu Mkuu wa Sekondari ya Pugu. Bila kificho alichagua kuendelea kuwa kiongozi wa chama ili apate muda mwingi zaidi wa kuungana na wananchi katika mapambano dhidi ya Ukoloni. Maamuzi haya yalikuwa ni changamoto na taswira nzuri kwa Watanganyika, kwa maamuzi yake ya kuwa "Mwalimu" wa Watanganyika wote.

Hii ndiyo kusema, historia yote ya siasa ya Mwalimu ni historia ya "ujenzi wa Taifa la Tanzania" na kama ilivyo kwamba "kuongoza ni kounyesha njia". Mwalimu katika maongozi yake yote aliishi kwa kuzingatia misingi ya chama; jambo ambalo lilimwezesha kutumia njia nzuri katika kupigania uhuru wa Tanganyika na Afrika nzima kwa hekima na kwa ushujaa wa hali ya juu.

Kuna ukubalifu kwamba miaka 24 ya uongozi wa Mwalimu si tu kwamba aliwezesha kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika katika muda mfupi sana na bila kumwaga damu, pia aliweza kuzishawishi pande mbili za Tanzania Bara na Visiwani – kwa wakati huo Tanganyika na Unguja na kwa hivyo kuzaliwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ingawa Tanzania ilikuwa ni nchi mojawapo maskini katika Bara la Afrika baada ya kutawaliwa kwa muda mrefu, chini ya uongozi wake, Watanzania waliweza kuimarisha misingi ya maendeleo na kuendesha mapambano dhidi ya maadui ujinga, maradhi na umasikini.

Chini ya uongozi wa Mwalimu, wananchi Watanzania walijimudu kisiasa hususani katika ulinzi wa nchi yao. Wananchi wengi waliyatambua matatizo yaliyokuwa yakiikabili nchi yao. Walitambua kwamba, mafanikio na maendeleo yao yatatokana na juhudi na maarifa yao wenyewe.

Kwa uzingatifu wa misingi ya siasa ya ujamaa na kujitegemea Mwalimu aliwaongoza Watanzania hata wakaweza kujihimu kwa: makazi, chakula, maji safi, elimu bora na huduma za afya. Mfumo huu uliwawezesha Watanzania kuwa wamoja mbali na uwepo wa makabila zaidi ya 120. Watanzania si tu kwamba waliweza kutambulika kama "Watanzania", lakini wenye kuunganishwa kwa lugha moja ya Kiswahili.

Fauka ya hayo, Mwalimu alikuwa mstari wa mbele na msemaji mkuu wa nchi maskini duniani. Katika kupigana na uonevu wa kisiasa na kiuchumi - alijifunga kibwebwe kuzitetea nchi za ulimwengu wa tatu kwa minajili ya kulinda uhuru na umoja wa Afrika. Kwa kumbukizi ni kwamba, baada ya uhuru wa Tanganyika, Mwalimu aliendeleza vita dhidi ya wakoloni ili kulifanya Bara la Afrika liwe huru kikamilifu. Kwa msimamo huo, Tanzania iliheshimiwa sana na mataifa mengi duniani. Mwaka 1985 Mwalimu alifikia kilele cha Uongozi wake. Baada ya kuliongoza taifa la Tanzania takriban kwa muda wa miaka 24, Mwalimu aling'atuka kwa hiari yake mwenyewe. Uamuzi wake ulileta changamoto kubwa kwa viongozi wengine wa Afrika. Mwalimu alionyesha uungwana wa kukubali kuachia madaraka kwa hiari pasina kushinikizwa na raia au nguvu za kisiasa kutoka ndani na nje ya nchi. Hakuwa ni mwenye uchu wa madaraka, aliridhia kuwa raia wa kawaida na akarudi kijijini kwake Butiama kuwa mkulima. Ingawa hivyo, alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa nchi za kusini (South Commission); chombo ambacho alikisimamia hata kikaweza kutetea kuondolewa kwa madeni ya nchi maskini duniani.

Kwa majonzi yasiyo mithilika; Alhamisi ya tarehe 14/10/1999, saa nne unusu asubuhi kwa majira ya Afrika Mashariki, Mwalimu Nyerere aliaga dunia kutokana na ugonjwa wa kansa ya damu katika hospitali ya Mtakatifu Thomas, Uingereza. Ingawa Baba wa Taifa hatunaye tena duniani hivi leo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ingali inamuenzi kwa hali na mali. Kwa kuonyesha ukipaumbele kwa kile kinachoaminiwa kama njia bora ya kumuenzi baba wa Taifa. Serikali ya Tanzania imeipa dhima taasisi ya TANAPA kuhakikisha kwamba raia wote wanajuzwa wasifu wa Baba wa Taifa kupitia hotuba zake kwa mazungumzo na kwa maandishi. Ili kulitekeleza hilo kwa ufanisi, redio ya Taifa (TBC) hurusha hotuba zake kwa dakika 15 kila siku, kuanzia saa11:00 alfajiri na usiku kuanzia saa mbili na dakika 15 na kabla na baada ya taarifa ya habari kwa sikukuu za serikali au miezi inayoandamana na tarehe za uzawa wake na kufa kwake.

Kadhalika kuna vitabu vingi vimeandikwa kuhusu hotuba zake kama vile *Nyufa* (1995), *Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi* (1995) na kadhalika. Pamoja na njia hizo kutumika kama mbinu adhimu ya kuwajuza wananchi namna bora ya kumuenzi baba wa Taifa; pia lengo kuu ni kuhakikisha kwamba yale aliyoyazungumza, akayasimamia katika utekelezwaji enzi za uhai wake yanaendelezwa katika vizazi vilivyopo na vijavyo.

Hotuba za Mwalimu daima zimekuwa zikifurahikiwa na wengi. Ingawa hivyo, sababu za ushawishi wake kwa wasomaji au wasikilizaji zilikuwa hazijulikani. Hivyo, utafiti huu ulikusudia kuzichunguza ili kubaini ila ya ushawishi huo kwa hadhira.

### 1.2 Mada ya Utafiti

Hotuba za Mwalimu Nyerere zimekuwa na ushawishi mkubwa kwa Watanzania kiasi kwamba zinapewa ukipaumbele wa kuundiwa taasisi mbalimbali kwa minajili ya kuzihifadhi, kuzichapisha na kuzitangaza kwa kurushwa hewani kila uchao ili wananchi wapate wepesi wa kuuelewa wosia wa Baba wa Taifa. Ingawa hivyo sifa za lugha zinazozua ushawishi na ukipaumbele huo zilikuwa hazijulikani kadiri ya ufahima wa mtafiti. Hivyo, hivyo utafiti huu ulifanyika kwa azma ya kudhihirisha sifa hizo na kubainisha jinsi zinavyowaathiri wasikilizaji na wasomaji wa hotuba hizo.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti huu

(i) Kutambulisha maudhui mahususi yaliyomo katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere

(ii) Kubainisha jinsi mitindo katika hotuba za Mwalimu Nyerere inavyotumika kushawishi hadhira

(ii) Kupambanua athari zinazoikumba hadhira ya wasikilizaji ama wasomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere.

## 1.4 Maswali ya utafiti

(i) Hotuba za Mwalimu Nyerere zina maudhui gani mahsusi yanayoweza kutambulishwa?

(ii) Mwalimu Nyerere alitumia mitindo gani katika hotuba zake kushawishi hadhira?

(iii) Hotuba za Mwalimu Nyerere zina athari gani mahsusi kwa hadhira?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Hotuba za Mwalimu Nyerere zinaushawishi mkubwa kwa Watanzania wanaozisikiliza na kuzisoma. Hata hivyo, sifa za lugha zilizokuwa zikizua ushawishi huo zilikuwa hazijawekwa bayana kadiri ya ufahima wa mtafiti; kwa kubainisha sifa hizo; na kudhihirisha jinsi hotuba zilivyokuwa zikiwaathiri Watanzania. Utafiti huu utachangia elimu na maarifa katika taaluma ya Uchanganuzi Usemi; na inatarajiwa kwamba watafiti wengine katika eneo la Uchanganuzi Usemi watafaidika na utafiti huu kwani umeweka msingi kwa tafiti za baadaye hususani katika uchanganuzi wa Kibalagha.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulifaywa katika wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam Tanzania. Hii ni kwa sababu wilaya hii si tu kwamba ina watu wengi zaidi ya wilaya nyingine nchini Tanzania; lakini nikitovu cha usafiri kwa raia wanaoingia na kutoka mikoani; na kwa hivyo, ilikidhi viwango vya ubora katika utafiti huu kutokana na sifa ya kuwajumuisha Watanzania wengi takriban kutoka kila pembe ya nchi.Wilaya hii ilimpa mtafiti nafasi ya kuzichunguza hotuba za Mwalimu Nyerere na kubaini jinsi ambavyo hotuba hizo zinavyowashawishi raia kila wanapozisikiliza au kuzisoma. Utafiti huu ulishughulikia hotuba za Mwalimu Nyerere peke yake kwa sababu ndizo zilizopewa ukipaumbele tofauti na za viongozi wengine. Hotuba zilizohusishwa katika uchunguzi huu ni hotuba teule 26 zilizohifadhiwa kimaandishi. Hotuba hizo zilikusanywa kutoka katika maktaba za Taasisi ya Mwalimu Nyerere.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

Balagha - Ni elimu ya usemaji. Ufasaha wa kusema. Ni uulizwaji wa maswali usiohitaji majibu. Balagha ni ustadi wa kutumia lugha ili kushawishi au kufurahisha. Ni kutilia chumvi jambo linalozungumzwa.

Dafina - Ni hazina kwa jambo fulani au kitu fulani.

Iktisadi - Uchumi; Matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo.

Itikadi - Imani ya mtu kuhusu jambo au kitu fulani.

Juza - Ni hali ya kumwezesha mtu kuelewa jambo ambalo hakuwa akilielewa vyema hapo awali.

Kibebeo - Ni hali ya kukichukulia kitu au jambo fulani kama nyezo au daraja ya kukifanya kitu hicho au jambo hilo liweze kuendelea au kusonga mbele.

Mbinu za kiisimu - Ni ubora wa matumizi ya lugha yenye kuhitaji ufafanuzi

Ushawishi - Ni hali ya kuwahamasisha watu juu ya jambo fulani.

Muktadha - Mazingira au hali ambamo tukio au jambo hutendeka. Mazingira ya neno katika tungo au sentensi yenye kuonyesha uhusiano wake na maneno mengine. Ni hali au wakati wa jambo fulani lilikotokea au kutendeka.

(i) **Ethosi**: Ni mhimili wa nadharia ya Balagha unaomhitaji mchunguzi uneni kubaini hulka ya mneni kwa hadhira yake. Hususan: Uwezo wa jambo analolizungumzia msemaji, Namna anavyolichukulia suala analolizungumzia na ubinadamu alionao mzungumzaji kwa hadhira yake.

(ii) **Logosi**: Ni mhimili wa nadharia ya Balagha unaomhitaji mchunguzi uneni azingatie vile ambavyo mneni alivyoibua hoja au maswali yenye kumpa msikilizaji kutafakari badala ya kujibu; kuchunguza jinsi mneni alivyoibua maswali isiyohitaji majibu (Balagha).

(iii) **Pathosi**: Ni mhimili wa nadharia ya Balagha unaomhitaji mchunguzi uneni kutathmini hisia za wapokeaji usemi kulingana na uzito wa hoja zilizomo katika usemi huo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia maandishi yanayohusiana au kutofautiana na utafiti huu ili kuonyesha pengo la kielimu linalotakikana kuzibwa. Maandishi yenye kuambatana na madhumuni yamepitiwa na kuhakikiwa kwa kina hususani yanayohusu maudhui, mitindo katika hotuba na yale yanayohusu athari kwa wasikilizaji na wasomaji. Aidha, imeangazia nadharia iliyomwongoza mtafiti katika utafiti huu na kutaja mihimili iliyotumika kukidhi mahitaji ya madhumuni ya utafiti na maswali yake.

## 2.2 Mapitio ya Maandishi

Mapitio ya maandishi na uwasilishaji wake ulifanywa kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti huu

### 2.2.1 Maandishi kuhusu Maudhui ya Hotuba

Mahadi (2001) aliuzungumzia umma wa Kiislamu nchini Uganda ya kwamba umezorota kwa sababu mambo muhimu ya utamaduni wa Kiislamu yamepuuzwa na Waislamu. Mifano aliyoitoa ni pamoja na maisha ya kifamilia, utamaduni wa miskiti na mfumo wa kisheria. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa Waislamu wengi hawafungi ndoa kulingana na mafundisho ya Kiislamu. Alieleza kwamba nikahi hufanyika baada ya mwanamume kuishi na mwanamke kwa muda mrefu bila ruhusa kutoka kwa wazazi. Aidha alieleza kuwa wanawake wa Kiislamu waliotalakiwa na waume zao huolewa na wanaume wengine bila kuzingatia Edda. Zaidi ya hayo alibaini kuwa kinyume na mafundisho ya Kiislamu, wanaume hutangamana na wanawake katika mikutano na kusalimiana nao kwa mikono. Kuhusu mfumo wa kisheria alisema kwamba Waislamu wa Uganda hawajawahi kuonja mfumo wa sheria za Kiislamu. Alielezea matumaini yake kuwa kufuatia mabadiliko katika vipengele vya katiba kulikuwa na uwezekano wa mahakama za sharia (yaani mahkama za makadhi) kuanzishwa kwa manufaa ya Waislamu. Akizungumzia utamaduni wa miskiti, Mahdi alisema kuwa ingawa Waislamu wanakisiwa kuwa asilimia 25% ya idadi ya wakazi wa Uganda, idadi ya wanaosali sala tano miskitini ni ndogo. Alieleza kwamba miskiti mingi hujaa tu siku ya Ijumaa.

Utafiti wa Mahadi ulikuwa ni muhimu sana katika utafiti huu. Usahali wake wa hotuba hasa katika maswala ya mwathiriko wa hadhira kutokana na mafundisho ya kidini, ilikuwa ni changamoto katika utafiti huu ingawa kwa tofauti kwamba ulishughulikia hotuba za kisiasa za Mwalimu Nyerere kwa kuangazia maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu, mpangilio wa hotuba na athari wazipatazo wasomaji au wasikilizaji wa hotuba hizo.

Elia (1989) alishughulikia fani ya hotuba na maendeleo yake katika jamii ya Waarabu. Alionyesha msimamo wake kuwa hotuba ni utanzu ambao daima hulenga kuathiri na kuridhisha, kuelezea imani za mneni na mtazamo wake juu ya matatizo yanayomkumba mwanadamu. Alieleza kuwa hotuba humtoa msikilizaji katika hali moja na kumpeleka katika hali nyingine na katika itikadi moja hadi nyingine huku ikimpa msukumo wa kutenda tendo zuri ambalo hapo mwanzoni alikuwa na mtazamo hasi juu yake. Alifafanua kuwa lengo la hotuba ni kubadilisha mtagusano wa fikra zilizomo kwenye ubongo ili ziwe hisia zenye kumwathiri msikilizaji na kumfanya atende kitendo ambacho mwanzoni hakuweza kukitenda. Alieleza kuwa, pamoja na kuwa na ujuzi kwamba heri ni bora kuliko shari, heshima ni bora kuliko unyonge na haki ni bora kuliko batili; lakini ujuzi huo hauwezi kuathiri matendo ya mwanadamu mpaka ashawishiwe ili kuibua hisia na hamasa. Aidha, alibaini kuwa shahidi hawezi kujitoa muhanga kwa ajili ya dini kwa vile anajua ukweli, bali hufanya hivyo kunatokana na kuhamasishwa. Alieleza kuwa matumizi ya picha za kibunifu ni nyenzo muhimu katika hotuba kwa sababu huibua hisia na kumfanya mwanadamu kuathirika na kile akionacho mbele yake kuliko anavyoathirika na fikra zilizoko ubongoni.

Kuhusu misingi ya hotuba alieleza kuwa ubunifu na ujenzi wa hotuba au mtindo wake una hatua mbalimbali zinazopaswa kuzingatiwa. Alitaja kuwa ubunifu huhusiana na mtindo na maudhui ambapo huenda ukamfaidi mzungumzaji wakati anapotunga na kuitongoa hotuba yake. Alibainisha kwamba ubunifu wa namna hiyo huwa una vipengee viwili; vya ndani na nje. Katika ufafanuzi wake alisema: vipengee vya ndani ni pamoja na vithibitisho ambavyo hudhihirisha ukweli wa jambo kwa namna hasi au chanya na kwamba si kitu kingine isipokuwa hoja zilizovyazwa picha nyingi za ubunifu na hisia; na ambazo hubadilika kutoka katika udhanifu na ubahatishaji hadi uyakinifu wa kisaikolojia na kihisia. Alieleza kuwa kipengele kingine kinachoweza kumfaidi mneni hususani kwa upande wa kuwaathiri wasikilizaji ni utambulishaji ambapo inatakikana kuchukuwa wazo na kulielezea kwa kubainisha sifa zake bainifu zilizodhahiri, au kulielezea kwa kutumia tashbiha na stiara; na kuonyesha aina zake ili asiache sura yoyote ya kauli bila kuigusia. Alibaini kuwa kipengele cha nje huwakilisha mada ambazo mneni anapaswa azigusie; ambazo ni pamoja na dini,

itikadi na desturi. Akiuzungumzia muundo wa hotuba, Elia (1989) alisema kwamba hatibu katika enzi za kimajumui alikuwa akiingia moja kwa moja katika mada yake pasina utangulizi kwa sababu ya tabia yake ya uwazi, matumizi ya nguvu katika kudhihirisha hisia; na kutokana na ukweli kwamba alisukumwa kutoa hotuba na hisia za kuhamasisha au kuzingatia mazingira anuai. Alibainisha kuwa miongoni mwa mada zilizoshughulikiwa ni mawaidha, wosia na ndoa. Aidha alieleza kuwa khatibu kwa enzi hizo za kimajumui alikuwa akitegemea sana matumizi ya maneno yenye hekima, methali na ushairi ili matamko yake yalete umakinifu kwa wasikilizaji. Wakadhalka alielieleza kwamba mabadiliko ya kisiasa, kidini na kijamii yalipelekea pia hotuba kunakshiwa kulingana na mabadiliko ya kinyakati na kwa hivyo khatibu walilazimika kuzielekeza hotuba zao katika mwegemo huo ili kuupasha umma mafundisho faafu.

Kazi ya Elia ilikuwa na mchango mkubwa sana kwa utafiti huu kwa sababu ilizungumzia fani ya hotuba na maendeleo yake na jinsi ambavyo fani hiyo ilivyoweza kumwathiri msikilizaji na kumfanya atende kitendo ambacho asingeweza kukitenda kabla ya kusikiliza hotuba. Wakati ambapo pia katika uchanganuzi wa hotuba za Mwalimu Nyerere pia mtafiti alijikita katika kubaini mbinu za kiisimu kwa jinsi ambavyo zinaweza kumwaathiri wasikilizaji au wasomaji wa hotuba hizo hata ikawa niwatende kama ambavyo Mwalimu aliwataka. Aidha ilipendekeza mbinu ambazo mneni anaweza kuzitumia ili kuibua hisia anuai kwa hadhira lengwa jambo ambalo pia utafiti huu ulifaidika kwalo hasa ikisadifu kwamba kusudio kubwa lilikuwa ni kubaini ikiwa kuna ushawishi uliokuwamo katika hotuba za Mwalimu Nyerere kiasi cha kupelekea wasomaji au wasikilizaji kumzingatia kiongozi huyo kwa yale aliyokuwa akiwaelekeza kupitia katika hotuba zake; fauka ya kwamba hayuko tena duniani. Ingawa hivyo, utafiti wa Elia pia ulitofautiana na utafiti huu kwa sababu yeye alishughulikia fani ya hotuba na maendeleo yake katika jamii ya Waarabu wakati ambapo utafiti huu ulishughulikia maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio wa hotuba za Mwalimu Nyerere; na kubaini ushawishi wake kwa hadhira inayozisikiliza au kuzisoma hotuba zake.

Van (1993) alichanganua hotuba ya kisiasa iliyotolewa na mbunge wa House of Commons - aliyeitwa Fox - ambaye alikuwa mwakilishi wa chama cha wahafidhina.  Hotuba hiyo ilikusudia kumtetea mkuu wa shule ya Bradfold aliyeandika makala iliyoelekea kuleta mabishano makubwa juu ya elimu yenye msingi wa tamaduni nyingi.  Kwa kuchunguza matamko tendi katika hotuba ya Fox, Van aliweza kutambulisha kiwango cha madai yaliyotolewa na kukisia athari zake kwa hadhira mbalimbali.Van alifichua kwamba, wapinzani wa Fox katika bunge walidhihirisha uwongo na upendeleo kwa maelezo yao. Watu

wengi nje ya bunge hawakujua uwongo huo, jambo ambalo lilionyesha umuhimu wa mahusiano kati ya vitendo neni kwa ubaguzi wa hotuba ambamo zinatolewa. Van alibaini kwamba, hotuba ya Fox ilieleza hisia zinazostahili kutiliwa maanani kuhusu mandhari hasa kwa kuzingatia kwamba, House of Commons imepambwa na ishara za nguvu za serikali za bunge la Uingereza linalorejelewa kama mama wa Demokrasia. Utafiti wake ulitoa mwanya wa kielimu katika utafiti huu hasa pale ilipobainika kwamba yeye alichunguza hotuba lakini hakuchunguza hotuba za marais hususani Mwalimu Nyerere katika kubaini maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio uliomo katika hotuba hizo; jambo ambalo utafiti huu uliufanyia kazi.

### 2.2.2 Maandishi kuhusu Mitindo katika Hotuba

Owiti (2005), alitafiti lugha ya matangazo ya televisheni ili kuona namna matangazo hayo yanavyowaathiri vijana wa kike wa shule za upili katika miji ya Kenya. Alitumia N K N na N K I. na kugundua kwamba matangazo hayo yalitumia mitindo mbalimbali ya kiuneni na yasiyokuwa ya kiuneni kuathiri vijana hao kwa namna tofuati tofauti kama vile: kupenda, kuchukia na kuvutiwa kusiko kuwa tu kwa bidhaa lakini pia kwa wahusika wa matangazo hayo. Kazi ya Owiti inatofautiana na utafiti huu kwa sababu yeye alishughulikia matangazo kwa kutumia nadharia ya N K N na N K I wakati ambapo utafiti huu ulizingatia nadharia ya Balagha katika kubaini madhumuni mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio wa hotuba kwa jinsi zinazopelekea hotuba za Mwalimu Nyerere kuwa na ushawishi mkubwa kwa Watanzania na pengine ulimwenguni kwa ujumla.

Bloommaert (1990) alichunguza vipengele vya mtindo wa Kiswahili katika siasa kwa misingi ya kuifanya mifumo ya siasa za Kiafrika kuwa za kimataifa. Kilichomsukuma kufanya uchunguzi kama huo ni kutokana na madai kwamba jazanda ya Kiswahili hudhirihisha mwambatano wenye mwegemo wa fikra za kijadi. Akitolea mfano wa siasa za Kitazania na mfumo wa kijamii kwa upande mmoja na aina ya mitazamo ya kisiasa inayotambulika kimataifa kwa upande mwingine. Alichunguza mtindo katika hotuba nne za Rais mstaafu wa kwanza - Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alizowasilisha kati ya 1967 na 1970.

Mada za hotuba hizo zilikuwa ni Nguzo tano za ujamaa, moyo kabla ya silaha, Uhuru na mandeleo na Elimu ya kujitegemea. Alibainisha kwamba matini ya hotuba zilizowasilishwa kimaongezi, hotuba mbili zilizokuwa zimeandikwa zilikuwa na sentensi kati ya 245 na 396 ilihali zile zilizowasilishwa kimaongezi zilikuwa na sentensi kati ya 145 na 169. Alibaini kwamba, mambo mengi yanaweza kuelezwa kimaandishi kuliko kimaongezi na kwamba

muda na kiwango cha ufafanuzi wa mada husika ndio unaoamua uteuzi wa njia ya kuwasilisha ujumbe. Kadhalika alibaini kwamba, baadhi ya sifa za kimtindo za uwasilishaji huwasilisha mtindo wa kimbari wa Kiafrika ili hali zile zilizobaki si ngeni kwa msomaji wa kimagharibi. Alieleza mtindo wa Nyerere na fikra zake juu ya siasa hutofautiana na mahusiano na majaribio ya kimagharibi kwa namna mbili:

(a) Njia ya mawasiliano anasema, Mwalimu Nyerere alikuwa akitumia Kiswahili badala ya lugha yoyote ya Ulaya. Tofauti na viongozi wengine wa kiafrika na wa ulimwengu wa tatu. Na wala Mwalimu Nyerere hakuwa mchanganya ndimi. Kadhalika alibaini kwamba, Mwalimu alichagua lugha ya kienyeji (Kiswahili) ili itumike katika siasa za Kiafrika badala ya lugha za kikoloni ambapo yeye aliona kuendekeza lugha za kigeni ni kujivyaza utumwa.

(b) Siasa zilizojengwa juu ya msingi wa vijiji, mtafiti alibaini kwamba Nyerere aliamua kujitenga na mtazamo au fikra za Kiimla zinazotazama siasa kama tatizo la mjini na badala yake akahamisha shughuli za kisiasa vijijini. Umathubuti wa ubainifu wake ni kielelezo cha jaribio kwa uamuzi wa kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya chama na serikali badala ya jiji la viwanda; la Dar-es-Salaam. Fauka ya hayo, alieleza kwamba mtindo wa kimaingiliano alioutumia Nyerere ulitegemea vibadiliki viwili:

(i) Mada: Utanzu wa kutolea taarifa mpya na kufafanua hoja ulikuwa wa kiuandishi. Hotuba za kimaongezi hazikuwa na taarifa mpya na kazi yake ilikuwa ni uimarishaji wa kauli zilizotolewa mwanzo na kutafuta maamuzi ya kisiasa kwa kuiomba hadhira moja kwa moja.

(ii) Hadhira lengwa: Mahusiano kati ya hadhira na mzungumzaji huathiri uteuzi wa utanzu. Nyerere alipokuwa akihutubia jeshi alikuwa akilazimika kusema ukweli na kuyachukulia mambo kwa wepesi bila kupuuza jambo lolote kama ambavyo angefanya mbele ya hadhira ya siku ya kuadhimisha siku ya uhuru.

Matokeo ya uchanganuzi wa Bloommaert yalionyesha kwamba mtindo alioutumia Mwalimu Nyerere ulitofautiana na ule wa kimagharibi kutokana na matumizi yake ya Kiswahili na kuhamishia msingi wa harakati za kisiasa huko vijijini. Vinginevyo kazi hiyo ilibainisha kuwa sifa za kimtindo za hotuba za Nyerere zilitokana na misingi ya kimawazo na balagha ya kimagharibi aliyoitegemea kuelezea fikra hizo.

Kazi ya Bloommaert ni adhimu kwa utafiti huu. Ingawa Bloommaert alishughulikia hotuba za Mwalimu Nyerere kama ilivyoshughulikiwa katika utafiti huu, lakini kazi yake ilitofautiana na ya utafiti huu kwa sababu yeye alichunguza lugha aliyokuwa akiitumia Mwalimu Nyerere katika uwasilishaji wa hotuba zake wakati ambapo utafiti huu ulikusudia kuchunguza maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio uliomo katika hotuba zake na athari yake kwa hadhira. Hivyo, kutokana na tofauti zilizomo, utafiti wa Bloommaert ulitoa mwanya wa kielimu ambao utafiti huu ulikusudia kuuziba.

Oglivy (1963) alifanya utafiti wake juu ya lugha inayotumika katika utangazaji na alitaja maneno ambayo aliyachukulia kuwa ni yenye ufanisi katika matangazo. Maneno hayo ni pamoja na "***mpya***", "***huru***", "***ajabu***", "***zuri***" na "***bora zaidi***". Alieleza kwamba, lugha ya matangazo hutoa ushawishi kwa kutumia maneno yakiutendakazi kwa uweledi na kwa uangalifu katika kufanikisha madhumuni mahsusi. Kazi yake ilikuwa na manufaa si haba - katika utafiti huu kwa sababu ilitumika kama kielelezo cha matumizi ya lugha kwa namna ambayo hufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa hotuba za kisiasa kwa viongozi wa nchi. Ingawa utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kutokana na kuwa umeangazia lugha ya matangazo hasa katika utendeshaji wa maneno ulichangia katika kubaini pengo la kielimu. Utafiti huu ulijikita katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere kwa lengo la kubainisha maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio wa hotuba uliomo katika hotuba hizo.

Geis (1982), alichunguza lugha ya matangazo hasa yale ya televisheni huko Marekani. Alimulika mbinu za kiisimu zinazojitokeza wazi wazi katika matangazo kama vile matumizi ya neno "Saidia" katika vishazi. Alibaini kwamba watangazaji hupendelea matumizi ya lugha yasiyo dhahiri. Kwa hakika utafiti wa Gres ulikuwa ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu uligusia suala la ushawishi na ulichangia kubaini sababu zilizotumika ili kuleta ushawishi kwa wasikilizaji wa hotuba za kisiasa. Hata hivyo. haukugusia lugha ya hotuba za Marais hususani Mwalimu Nyerere. Hivyo, hilo ni pengo ambalo utafiti huu uliazimia kuliziba.

Paxon (1985) alizungumzia sheria za mtindo kwa mwandishi wa kibiashara. Alisema kuwa maneno na maana yapaswa vipewe heshima inayostahili. Hivyo ni kwa sababu mzungumzaji au mwandishi asipotumia maneno kwa uangalifu, anaweza kusababisha maafa kama yale yaliyowakumba Wajapani. Alieleza kuwa aliyekuwa waziri mkuu wa Japani kuanzia tarehe sita Aprili hadi kumi na sita Agosti mwaka wa 1945 hakukuwa ni mwenye kuimudu lugha

yake na kutokana na kukosea katika neno moja, dunia ilibadilika kiasi kisichowezekana kukadiriwa.

Paxon alifafanua kuwa nchi ya Japani ilikuwa imepokea andiko lililoitaka kusalimu amri mara moja katika siku za mwisho za vita vya pili vya dunia. Lakini Suzuki alitumia tamko lilitafsiriwa kuwa alikuwa amepuuza tangazo lililomwihitaji asalimu amri, kumaanisha kwamba hakukuwa na la kusema wakati huo. Alieleza kuwa, kwa vile wafasiri wa kijapani hawakutambua maana aliyokusudia waziri mkuu, tafsiri waliyoifanya ilipelekea Marekani kutupa mabomu ya atomiki huko Hiroshima na Nagasaki yaliyokomesha vita; lakini yakaua Wajapani zaidi ya 120,000 na kuiingiza dunia katika enzi ya atomiki.

Na hii ndiyo kusema kwamba, kazi ya Paxson inamtagusano na utafiti huu hasa: Kwa jinsi iligusia matumizi ya matamko na ambavyo yaliweza kuathiri hadhira, na kwamba alishughulikia matini andishi jambo ambalo pia ni sawia na utafiti huu ambapo hotuba andishi za Mwalimu Nyerere ndizo zilizoshughulikiwa. Na kwa ubainifu wake kwamba matamko yaliwapelekea Wamarekani kuzua athari hasi na kusababisha madhara makubwa katika jamii ya wajapani; utafiti wake ulikuwa ni kiilelezo faafu ambapo utafiti huu nao ulijikita katika kuangazia athari za wasikilizaji na wasomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere na kubaini kwamba zilikuwa zikiwashawishi kwa mwegemo chanya katika kuzisoma au kuzisikiliza hotuba hizo kila uchao - katika kuya faidi yaliyomo.

### 2.2.3 Mandishi kuhusu Athari katika Hotuba

Matasi (2014) alishughulikia hotuba za ijumaa ambapo alidhihirisha vitendo neni vinavyojitokeza katika hotuba hizo na athari zake kwa wasikilizaji wa Bugisu Mashariki mwa Uganda. Kilichopelekea kufanya hivyo ni malalamishi kwamba baadhi ya maimamu hutoa matamko yenye athari hasi kwa maamuma. Utafiti wake ulibainisha kwamba matamko ya hotuba yalikuwa na athari hasi kwa asilimia 48 huku athari chanya zikiwa na asilimia 52. Mtafiti huyu alitumia Nadharia ya vitendo neni iliyoasisiwa na Austin 1962 na kuendelezwa na Searle (1969). Wakadhalika alitumia mbinu ya kiwingidadi katika uchanganuzi wa deta yake. Utafiti wa Matasi ijapokuwa ulishughulikia hotuba; unatofautiana na wangu kwa vile aliangazia hotuba za ijumaa; ambapo utafiti wangu ulishughulikia hotuba za kisiasa. Hata hivyo utafiti wake uliufaa utafiti wangu kwa sababu alishughulikia athari za matamko kwa wasikilizaji wa hotuba kwa hivyo ulikuwa ni kielelezo kwa utafiti huu ambapo uliangalia jinsi wasikilizaji na wasomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere jinsi wanavyoshawishika kutokana na matumizi ya lugha yaliyomo katika hotuba zake.

Ogola (2007), alichunguza namna lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao. Alibainisha vitendo neni vinavyojitokeza katika matamko ya kuhamasisha wanawake na jinsi wanavyoweza kuathirika navyo. Katika utafiti wake aliongozwa na N K N, iliyoasisiwa na Austin (1962). Data aliyoipata aliichanganua kwa kutumia mbinu ya wingidadi na kithamano. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kwamba lugha inayotumika wakati wa uhamasishaji wa wanawake ina vitendo neni na athari chanya kwa wasikilizaji. Matokeo hayo yalionyesha kwamba lugha inayotumika kuwahamasisha wanawake kuhusu haki zao ilikuwa na athari hasi - hayakuwa na mashiko kwa sababu kilichogunduliwa kutokana na utafiti ilikuwa ni kinyume chake. Pamoja na hayo, kazi ya Ogola ilihusiana na utafiti huu kwa vile ilidhihirisha vitendo neni vya lugha ya uhamasishaji wa wanawake na athari zake; wakati ambapo utafiti huu pia ulichunguza hotuba teule za Mwalimu Nyerere zinazorushwa hewani kupitia radio ya Taifa (T B C) Ingawa kwa kutumia mkabala wa Uchanganuzi Usemi na kwa kutumia nadharia ya Balagha; lakini kwa kuangalia jinsi ambavyo maudhui, mbinu za kiisimu na mpangilio wa hotuba jinsi zinavyoishawishi hadhira kupenda kusikiliza au kuzisoma hotuba zake.

Fauka ya hayo, kazi ya Ogola ilikuwa na faida kubwa katika utafiti huu kwa sababu mbinu alizotumia katika ukusanyaji na uchanganuzi wa deta ndizo utafiti huu pia ulizitumia kama kibebeo cha kusaidia kupekua ili kubainisha sifa za kiushawishi zilizomo katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere zinazorushwa hewani kupitia redio ya taifa (T B C)

Walya (1995) alichunguza mawaziliano kiusemi na athari za semi hizo kwa wafanyakazi wa benki juu ya wateja wao kwa kutumia N K N. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa wafanyakazi wa benki hutumia lugha kwa nia ya kupata wateja na kuwashawishi waweze kufurahia huduma zao. Pamoja na kwamba Walya alitumia N K N kinyume na utafiti huu ambao ulitumia nadharia ya Balagha, Utafiti wa Walya uliufaa sana utafiti huu kutokana na kujikita kwake katika muktadha wa kiusemi. Utafiti huu nao ulijikita katika uchunganuzi usemi kwa nia ya kubaini ushawishi uliopo katika hotuba za Mwalimu Nyerere zinazorushwa hewani kupitia redio ya T B C. Ulitumia Nadharia ya Balagha kinyume na ule wa Walya uliotumia nadharia ya N K N.

Wardhaugh (1992) alishughulikia utendaji na uzungumzaji; na kuelezea kwamba matamko yanaweza kutambuliwa kwa namna mbalimbali. Ubadilishano wa matamko unaoweza kurejelewa kama mazungumzo, hutazamwa kama vitendo na siyo tu kubadilishana kwa maneno. Akimnukuu Grice (1975), alisema kwamba mazungumzo yanaweza kuendelea kati

ya mtu mmoja na mwengine kwa sababu tunakuwa na utambuzi wa malengo ya kawaida katika mazungumzo na njia mahsusi za kutekeleza malengo hayo.

Fauka ya hayo, Wardhaugh alieleza kwamba katika mazungumzo yoyote yale huwa kuna mambo maalum yanayowezekana katika wakati maalum; hii ni kwa sababu kuna vizuizi vinavyodhibiti uzungumzaji ambavyo humwekea mzungamzaji mipaka kuhusu nini anatakikana atambue. Akimwegema Grice kwa kanuni yake ya ushirikiano wa mazungumzo alifafanua kwa kusema kwamba, katika mazungumzo mtu anatakikana kutilia maanani sheria ya kijumla; kwamba awe anashiriki na msikilizaji au wasikilizaji wake katika shughuli ambayo ni yenye manufaa kwa wote; manufaa ambayo ni kuelewana.

Ingawa Wadhaugh hakushughulikia hotuba lakini utafiti wake uliufaa utafiti huu kutokana na jinsi alivyojihusisha na sheria ya uzungumzi; kwa minajili ya kubaini uelewa kwa wasikilizaji kwa yale yanayozungumziwa juu yao; ambapo utafiti huu nao ulishughulikia hotuba za kisiasa kwa uchunguzi wa jinsi gani mneni anawashawishi wasikilizaji wake kumridhia anachowaeleza: kwa kuangazia maudhui, mtindo na mpangilio wa uneni wake. Na kwa hivyo, utafiti wa Wadhaugh ulichangia pakubwa utafiti huu katika kubaini iwapo wasikilizaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere hushawishika kwa hotuba zake kiasi cha kupenda kuzisikiliza au kuzisoma kwa ajili ya manufaa ya maisha yao ya kila siku.

Kathleen, Bruce, Dauglas na Alan (2001) walishughulikia kaida za uzungumzi wa hadharani na kubaini kwamba kuna tanzu nne za uzungumzi za kimsingi ambazo hushirikiana ili kuzalisha mchakato wa uzungumzi ambazo ni: mzungumzaji, ujumbe, wasikilizaji na muktadha. Walieleza kuwa mzungumzaji ndiye chanzo cha ujumbe, ambaye huleta mtazamo wake binafsi na mazoea yake katika shughuli ya kuwasiliana. Walieleza pia kuwa ujumbe huundwa kwa ukweli wa yaliomo, mitazamo ya mzungumzaji na thamani ama faida za mada na kwamba ujumbe huo huwasilishwa kwa kuteua maneno na fikra ambazo hupangiliwa katika ruwaza maalum. Walibaini kuwa msikilizaji hutoa maarifa ya awali, mitazamo na hamu kwa hali ya uneni na pia mwitikio wa kiuneni na usio wa kiuneni kama vile mikunjo ya nyuso, kucheka, kupiga miayo au kuuliza maswali. Wakadhalka walisema kwamba mwitikio hurejelea ujumbe ambao wasikilizaji huutumia kabla ya wakati au baada ya kutoa hotuba na kwamba muktadha unaweza kuwa mandhari halisi ambamo uzungumzi hutokea au matarajio ya jamii na sheria za kitamaduni ambazo huwepo wakati wazungumzaji na wasikilizaji wanapoingiliana.

Kathleen na wenzake waliendelea kueleza kwamba kwa vile kuhutubia hadhira ni mchakato wa kimaingiliano, kuna majukumu fulani ambayo yanapaswa yatekelezwe kwa wasikilizaji. Hivyo ni kwa sababu kila mzungumzaji anapohutubia hadhira huwa anachangia utaratibu mzima uliokusudiwa katika kuijenga jamii na ama kuathiri maisha ya wengine. Kwa hivyo, uzungumzi hauna budi kuzingatia kipengee cha maadili ambayo humlazimu mneni kuangalia masuala ya haki na dhuluma, uzuri na ubaya, usahihi na usosahihi. Watafiti hawa pia walidai kuwa maswali kadha wakadha yanayohusiana na maadili hujitokeza wakati wa kuandaa na kuwasilisha hotuba. Walishikilia kuwa kuaminika kwa mneni ni nyenzo muhimu ya kuiathiri hadhira yake. Hivyo ni kwa sababu uaminifu hupewa mtu na ni muhimu hususani katika enzi ambamo makundi mbalimbali ya watu yanapoingiwa na sintofahamu katika kuelewa nia za wenzao. Na kwa hivyo, kuonyesha ubingwa katika uzungumzi ni muhimu kwani huchangia pia hali ya kuaminika kwa hadhira. Hii ilimaanisha kwamba, ingawa mzungumzaji anaweza kujua mengi kuhusu mada kupitia uzoefu wake fulani; anashauriwa kuchukua muda asome zaidi, apate ushauri wa mabingwa wengine, ili aone ni vipengee gani katika mada ambavyo vingeweza kuwafanya wasikilizaji wake washiriki katika uzungumzi atakaouendeleza kwao. Walidai pia kwamba ufasaha, kujiamini na udhibiti wa sauti navyo pia huchangia uaminifu kwa sababu huonyesha kuwa mzungumzaji ni mwenye ujuzi.

Watafiti hawa walisisitiza stadi za kimaongezi ya kwamba hupatikana kupitia mazoezi ya wazungumzaji; na wengi waliofaulu ni wale wanaowajali wengine hivi kwamba hujihusisha na kukidhi mahitaji ya wasikilizaji wao na kuwatatulia matatizo yao. Aidha walidai kuwa wazungumzaji wazuri hutambua na kuheshimu wasikilizaji na mahitaji yao kwa hiyo, huwa na "hisia za kibalagha". Walieleza kuwa hisia za kibalagha ni kiasi ambacho wazungumzaji:

(i) Hutambua kuwa wasikilizaji wao ni tofauti na ni wenye tabia changamani. Ingawa mzungumzaji huyo hawezi kuongea kwa kila mmoja katika hadhira lakini anaweza kuheshimu maoni yao.

(ii) Huufanya ujumbe wao urandane na hadhira maalum. Wazungumzaji waliomakini huwasilisha maoni yao kwa kila kundi la wasikilizaji wakitumia vithibitisho kutokana na mazoea ya wasikilizaji wao; na kutumia lugha faafu kwa kundi linalozungumziwa. Walitoa mfano wa wanasiasa ambao huzungumza juu ya masuala na matatizo ya kawaida.

(iii), Hutafuta kimakusudi na kuitikia miitikio ya hadhira. Kwa kuitikia mitazamo inayoonyesha kutatizika au kucheka na kupiga makofi, wazungumzaji hutambua

hali ya kimaingiliano katika mawasiliano. Utambuzi wa wasikilizaji, na kwa hivyo, ni kiungo muhimu katika mchakato wa uzungumzi.

(iv), Lakini pia hutambua kuwa ushajihisho wa maneno kwa tatizo liliojiri katika jamii laweza pia lisiondoe tofauti zilizopo baina ya wanajamii hao.

Kwa hakika kazi ya Katheleen na wenzake ilikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa sababu ilishughulikia uzungumzi unaofanywa mbele ya hadhira, jambo ambalo pia ni sanjari na utafiti huu ambao ulikuwa ukichunguza hotuba za Mwalimu kuhusu uwasilishaji wake ikiwa zilikuwa na maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio maalumu kiasi cha kuifanya hadira ishawishike kwazo.

Na ama kuhusu kuangazia kwao na kubaini kwamba hotuba zinaweza kuwasilisha athari chanya au hasi, kwa hakika kuliipatia mwelekeo utafiti huu kwa sababu utafiti huu pia ulikuwa ukiangazia kubaini ushawishi uliomo katika hotuba za Mwalimu Nyerere; ambapo mbali na maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio pia ulichanganua athari wazipatazo wasikilizaji wa hotuba hizo. Halikadhalika, kaida za uzungumzi walizozipendekeza zilichangia sana kuleta natija katika nadharia tete za utafiti huu ingawa matokeo ya pande mbili yalitofautiana kutegemeana na mada lengwa

## 2.3 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Balagha iliyoasisiwa na Aristotle (367 BC), hii ni nadharia ya uchunguzi wa Lugha kwa mkabala wa ushawishi. Aristotle anabainisha kwamba, nadharia ya Balagha imejikita katika mihimili mikuu mitatu: kwanza, maudhui yaliyomo katika usemi; pili, mtindo katika mbinu za kiisimu; na tatu, mpangilio wa usemi. Ufafanuzi wake ni kwamba:

(a) **Yaliyomo katika usemi**: Aristotle anamaanisha kumchunguza mhutubu au matini yake katika kiwango cha Logosi, Pathosi na Ethosi yake:

(i) **Kiwango cha Logosi**: Hapa anahimiza mchunguzi azingatie vile ambavyo mzungumzi alivyoibua hoja au maswali yenye kumpa msikilizaji kutafakari badala ya kujibu (mbinu ya kuuliza maswali isiyohitaji majibu).


(ii) **Kiwango cha Pathosi**: Arisitotle anahimiza mchunguzi atathmini hisia za wapokeaji usemi kulingana na uzito wa hoja zilizomo katika usemi huo.

(iii)**Kiwango cha Ethosi**: Aristotle anatoa ufahima kwamba wapo wazungumzaji wenye sifa na tabia zinazowapelekea kuheshimiwa na kuenziwa kabla na baada ya usemi wao kwa hadhira. Hivyo, ni vyema mchunguzi kuzingatia sifa bainifu zifuatazo: Uwezo wa jambo analolizungumzia msemaji, Namna anavyolichukulia suala analolizungumzia na ubinadamu alionao mzungumzaji kwa hadhira yake.

(b) **Mtindo**: Hapa Aristotle anamaanisha mchunguzi ajikite katika kuangalia vile ambavyo mbinu za kifani zilivyopelekea hotuba au usemi kuwa na ushawishi mkubwa kwa hadhira.

(c) **Mpangilio wa hotuba au usemi**: Kadhalika Aristotle anahimiza mpangilio wa hotuba uzingatiwe. Mchunguzi azingatie (jinsi ambavyo mzungumzaji alivyoanza hotuba au usemi wake kwa hadhira), mwili wa usemi huo (jinsi mzungumzaji alivyojenga na kuendeleza hoja zake) na kisha achunguze vile alivyohitimisha usemi wake.

**2.4 Kiunzi 1: Msingi wa Kidhana wa Utafiti**




Katika kiunzi hiki, ombwe lenye anuani ya *hotuba* kwa mishale ilivyojitokeza ni kuonyesha kwamba utafiti huu ulihusu "hotuba". Na ombwe la kati linaonyesha mambo mahsusi yaliyochunguzwa. Kisha ombwe lenye anuani ya *athari* ni tathmini ya ikiwa upokezi wa hotuba hizi kwa hadhira ulikuwa ni hasi au chanya.

### 2.4.1 Sababu za Kuchagua Nadharia ya Balagha

Ilikuwa ni imani ya mtafiti kwamba nadharia hii ya Balagha inge kuwa faafu katika uchunguzi wa hotuba za Mwalimu Nyerere. Hii ni kutokana na vigezo vya mihimili yake vyenye umbo la mdudu; ambapo kwa kawaida hotuba za wengi hujivyaza sura hiyo. Kwa mnasaba huo, nadharia hii ilisadifu zaidi kuliko nadharia zingine kama ambavyo inge dhaniwa kulikoni. Kwa mfano:


(a) Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi (NUHU) inasisitiza mahusiano ya kimamlaka kati ya wenye mamlaka na wasio na mamlaka na kwamba wenye mamlaka ndio wenye nguvu. Hakika mwegemo wa nadharia ya (NUHU) unakinzana na ule wa balagha ambao unahusu ushawishi. Hivyo, (NUHU) si nadharia Mwafaka katika utafiti huu.

(b) Kielelezo cha mtindo wa Leech (N M L). Utafiti huu haukutumia kielelezo hiki cha mtindo cha Leech katika utafiti wake kwa sababu inaongoza kombo katika uchunguzaji wa hotuba. Nadharia inagusia kipengele kimoja cha mtindo tena katika fasihi lakini haigusii uzingatifu wa mtindo, maudhui na mpangilio wa hotuba. Wakati ambapo nadharia ya Balagha inagusia vipengele hivyo vitatu ambapo kila kimoja huangalia mchango wake katika ushawishi wa hotuba

### 2.5 Fahiwa kuhusu Balagha

Kwa mujibu wa Assakakiy (1983) Balagha ni ufasaha wa lugha. Ni taaluma inayochunguza usemi ili kudhihirisha umaanisho ndani yake, ujumi na mambo mengine, kwa kuzingatia muktadha. Balagha inazingatia pia jinsi maana moja inavyoweza kuelezewa kwa njia tofauti ili kupata makusudio fulani. Wakadhalika Assakakiy alibaini kwamba, balagha ndiyo huwapatia adibu nyenzo zinazosaidia katika maelezo yake na kupata muonjo wa kazi ya kifasihi ama kuizalisha (kuibuni) pindi anapopata weledi wa kifani. Alieleza kuwa mwana balagha anapaswa kutumia lugha ambayo ni chombo cha mawasiliano, kwa njia mahsusi ili aweze kuathiri wasikilizaji au wasomaji. Nyenzo anazotumia mzungumzaji au mwandishi ni mbinu mbalimbali za kiisimu kama vile tashbiha, istiara, tashhisi,takriri, majazi na kadhalika.

**2.6 Kiunzi 2 : Kiunzi cha Nadharia ya Balagha cha Aristotle**



### 2.6.1 Ufafanuzi kuhusu Umbo la Kiunzi (2.6)

Umbo hilo; lililopo katika ukurasa wa 20, ni kiunzi cha nadharia ya Balagha ya Aristotle (367 BC). Mhimili wake mkuu ni maudhui kwa mwegemo wa vipengele vya Logosi (mtindo na mpangilio ukiwemo ndani yake); Ethosi; na pathosi. Kwa ufahima kwamba Logosi - ni pale ambapo mchunguzi anazingatia vile ambavyo mzungumzi alivyoibua hoja au maswali yenye kumpa msikilizaji kutafakari badala ya kujibu (mbinu ya kuuliza maswali isiyohitaji majibu); Ethosi - ni pale ambapo mchunguzi atachunguza tabia ya mneni; hasa ikisadifu kwamba wapo wazungumzaji wengine wenye sifa na tabia zinazowapelekea kuheshimiwa na kuenziwa kabla na baada ya usemi wao - kwa hadhira. Kwa hivyo, ni vyema mchunguzi kuzingatia: uwezo wa jambo analolizungumzia msemaji, namna anavyolichukulia suala analolizungumzia na ubinadamu alionao mzungumzaji kwa hadhira yake. Pathosi - ni pale ambapo mchunguzi atatathmini hisia za wapokeaji usemi kulingana na uzito wa hoja zilizomo katika usemi huo. Hivyo, usawiri wa umbo la kiunzi linafasirika kama ifuatavyo:

(a) Umbo la pembe tatu katika kiunzi hicho linaonyesha Logosi, Ethosi na Pathosi mithili ya mafiga. Yaani usemi unaowasilishwa kwa hadhira unahitaji ubebeke vizuri.

(b) Umbo la dufu (duara) lililoizunguka pembe tatu ni kuonyesha jinsi ambavyo pembe hizo tatu zinavyohitajiwa zishirikiane (zihusishwe) kwa pamoja katika kufanya tathmini kuhusu ushawishi wa ujumbe bebwaji wa mneni kwa hadhira - ikiwa ni chanya au hasi.

(c) Umbo la dufu lililo na anuani ya *Hotuba*; na kwa mishale ya kwamba liko juu ya mafiga matatu (umbo la pembe tatu) ni kuonyesha jinsi ambavyo usemi uliokusudiwa kuwafikia hadhira - ya kwamba ni jambo zito linalohitaji uangalifu. Ushawishi kuhusu kilichomo; cha weza kuwa chanya au hasi na kwa hivyo kubeba dhana ya kwamba mafiga matatu ni kishiko imara; na pungufu yake ni udhaifu.

(d) Umbo la dufu lenye anuani ya *Athari* na kuonyeshwa kwa mishale ambayo chanzo chake ni katika dufu la 'Hotuba' - ni udhihirisho wa kwamba uchunguzi kuhusu hotuba (usemi) kwa uzingatifu wa mihimili ya Nadharia ya Balagha, hatma ya ushawishi wa mneni kwa hadhira – utakuwa na athari; ama chanya au hasi.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa deta. Katika mbinu za ukusanyaji wa deta mtafiti alizingatia hatua zifuatazo: Mahala palipofanyiwa utafiti, deta ya utafiti, uteuzi wa sampuli, namna deta ya utafiti ilivyokusanywa. Uchanganuzi wa deta na mikabala ya uchanganuzi wake.

## 3.2 Mahala pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam nchini Tanzania; ambapo kwa sensa ya 2012 Tanzania ilikuwa na idadi ya watu wapatao 44,929,002; jiji la Dar es Salaam likisheheni watu 4,364541 na wilaya ya Kinondoni ikiwa na jumla ya watu 1,775,049 zaidi ya wilaya ya Temeke na Ilala. Taswira hii ya wilaya ya Kinondoni ya kuwa miongoni mwa eneo la jiji la Dar es Salaam; lakini lenye watu wengi kuliko wilaya zingine ilikuwa ni kivutio kwa mtafiti kuitumia wilaya hiyo kama kiwakilishi kwa nchi nzima; kutokana na kwamba vigezo hivyo havipatikani kwa urahisi katika wilaya zingine nchini Tanzania.

## 3.3 Kundi Lengwa

Kundi lengwa katika utafiti huu lilikuwa ni Hotuba zote za Mwalimu Nyerere zilizochapishwa. Kwa kutumia mbinu ya kimakusudi hotuba 26 ziliteuliwa kuwakilisha sampuli ya utafiti huu.

### 3.3.2 Maoni ya Wasailiwa

Wasailiwa 26 waliteuliwa kimakusudi ili kuwakilisha maoni ya Watanzania wote. Hii ni kwa sababu si tu kwamba wilaya hiyo ina watu wengi lakini pia ni kitovu cha usafiri kwa raia wanaoingia na kutoka mikoani.

## 3.4 Deta ya Utafiti

Mtafiti alikusanya deta ya aina tatu: Maudhui mahsusi yaliyomo katika hotuba za Mwalimu Nyerere, mitindo mbalimbali iliyomo katika hotuba za Mwalimu Nyerere na maoni (athari) ya wasikilizaji kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere.

### 3.5 Utaratibu wa Ukusanyaji wa Deta

Utaratibu uliotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa deta ulikuwa wa uchanganuzi wa yaliyomo wa matini za hotuba za Mwalimu Nyerere. Wakati ambapo katika deta ya maoni mtafiti alitumia utaratibu wa upimaji hali

#### 3.5.1 Hatua za Ukusanyaji Deta ya Maudhui na Mitindo

(i) Mtafiti alisoma matini za hotuba teule za Mwalimu Nyerere

(ii) Mtafiti alidondoa maudhui ya hotuba teule za Mwalimu Nyerere

(iii) Mtafiti alidondoa mbinu za lugha katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere

(iv) Mtafiti alianisha maudhui na mbinu za lugha za hotuba teule za Mwalimu Nyerere; ili kubaini jinsi mbinu za lugha zilivyotumika kuelezea maudhui katika kuishawishi hadhira

#### 3.5.2 Hatua ya Ukusanyaji wa Deta ya Maoni

Deta ya maoni ilipatikana kwa kutumia vifaa viwili, kwanza hojaji (Rejelea kiambatisho "A" na pili, kwa kutumia mahojiano ya kina.

### 3.6 Uchanganuzi wa Deta

Maudhui na mitindo yalipangwa katika kategoria mbalimbali na kuelezwa yalivyotumika. Wakati ambapo maoni yalipangwa na kutathminiwa iwapo yalielekea kuwa hasi au chanya. Fauka ya hivyo, aina zote za deta zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kithamano na kiwingidadi na matokeo yakawasilishwa kwa kutumia majedwali na maelezo ya kina.

**Jedwali 1: Mfano wa jinsi Deta ya Hotuba ilivyochanganuliwa Kiwingidadi**

| Hotuba | Maudhui | Mtindo | Kurasa |
|---|---|---|---|
| AW | Uongozi bora | Takriri neno | (UK 19:1-2: AW) |
| KK | Muungano | Tashbiha. | (UK 1:4: KK) |
| N | ” | Tashbiha na takriri neno | (UK 10:3: N) |
| N | Rushwa | Takriri neno na tashtiti | (UK 15:3/16:1: N) |
| | ” | Msemo | (UK 9:2: MMT) & (UK 46:2: AA) |

Kwa kuzingatia **J1:** Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuzipatia hotuba vifupisho. Kwa mfano: KK = Kupanga ni Kuchagua; N = Hotuba ya Nyufa; na kadhalika. Hatua ya pili, mtafiti alipambanua maudhui na mtindo kwa nia ya kubaini ikiwa kuna ushawishi wenye athari chanya au hasi kwa hadhira.

### 3.6.2 Mauhui kuhusu Uongozi Bora

Ilikuwa ni rai ya Mwalimu Nyerere kwamba mara baada ya kung'atuka kwake; Rais atakayefuata asiongoze kwa zaidi ya miaka kumi. Ingawa hivyo, rai yake ilipokelewa na Watanzania kwa mitazamo tofauti. Wapo waliohisi kwamba, ikiwa Mwalimu ataachia ngazi nchi ingeyumba na kwa hivyo umoja, amani na utulivu uliowagharimu kwa muda mrefu ungetoweka. Lakini wengine walifurahia kung'atuka kwake. Kwa maana ya kwamba wangepata fursa ya kuyashawishi matakwa yao binafsi. Hata hivyo, kwa uoni wa Mwalimu ilikuwa ni Watanzania watambue kwamba alikwisha amua kung'atuka; na kwa hivyo hapakuwa na simile katika kuyakubali maamuzi hayo. Kwa wale waliofurahia kung'atuka kwa Mwalimu wakihisi kwamba wamepata mwanya wa kupenyezea hujuma zao; ilikuwa ni watambue kwamba hawataweza kufua dafu. Ingawa anang'atuka lakini jitihada za kupambana na maovu zilikuwa zipalepale. Na ndiyo ikawa Mwalimu akiwashawishi Watanzania wahakikishe hawatoi mwanya kwa Mabepari mithili ya hao wanofurahia kung'atuka kwake; wahakikishe kipindi cha uchaguzi wanawachagua viongozi bora na sio bora viongozi. Iwe ni ghera kwa kila Mtanzania kumchagua kiongozi shupavu, mchapakazi na mwenye uwezo wa kusimamia katiba ya nchi ili haki iwaendee Watanzania wote kwa uadilifu.

#### 3.6.2.1 Mfano wa jinsi Deta ya Hotuba ilivyochanganuliwa Kithamano

***Maswali ya kibalagha na Takriri neno***: *"Tunatoka wapi, tuko wapi na tunakwenda wapi. Na kama tunataka kwenda huko, tufanyeje ili tufike huko"*. (UK 2: 5- 3: 1: TTT).

Kauli hizi zilikuwa ni chagizo ya Mwalimu inayotoa mwangwi kwa wananchi kuhusu kutafakari kabla ya maamuzi; na umuhimu wa kufanya tathmini katika matendo ya kila siku. Ilikuwa ni imani yake kwamba wale wote wenye nia njema na jamii, watakuwa tayari kuikubali mbiu ya kukosoa na kukosolewa ili kujikwamua zaidi kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni lakini pia kujenga taifa lenye umoja amani, upendo na mshikamano.

### 3.6.3 Maudhui ya Umoja wa Kitaifa

Ilikuwa ni kumbukizi za Mwalimu kwamba, kabla ya kuzaliwa Tanzania, iliyokuwa ikiitwa Tanganyika, na serikali ya Unguja, pande hizi mbili zilipitia katika kipindi kigumu zaidi. Shime ya kuwepo kwa umoja wa kitaifa baina ya Watanganyika na Wazanzibari ilitokana na ushawishi wake (Mwalimu Nyerere) kuhusu umuhimu wa Muungano. Kwa historia ni kwamba nchi hizo mbili kabla ya kuvamiwa na Wakoloni, wananchi wake walikuwa kitu kimoja, walishirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa lakini ikawa ni watenganishwe na Wakoloni ili waweze kuwatawala kwa urahisi, hasa kwa itikadi waliyokuwa nayo kwamba, wao ndio wenye uhalali wa kuwatawala wengine popote ulimwenguni mintaarafu ya rangi zao. Ingawa hivyo, kwa umoja wao, waliweza kuwapiga vita na wakawashinda. Tanganyika na Unguja wakawa huru na kwa hivyo, Wakoloni wakafungasha virago vyao na kurudi makwao.

Kwa mbiu ya ***"Sahau Ukabila!"*** chini ya misingi ya chama cha TANU enzi hizo, Watanganyika na Wazanzibari waliweza kuungana na kuzalisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964. Ingawa hivyo, mara baada ya Mwalimu kung'atuka, aliingiwa na tashwishi kutokana na ubainifu wake kwamba, Muungano wa Jamhuri ya Tanzania ulikuwa umetikiswa. Baadhi ya Watanzania walikuwa wakiwashawishi wenzi wao wasiukubali tena Muungano kwa madai kwamba hauwanufaishi watu wa pande mbili kwa usawa; yaani Tanganyika na Zanzibar. Kwa mfano madai ya kwamba: ***"wengine wana bendera na wimbo wa taifa wakati wengine hawana"***. Madai ambayo Mwalimu aliyaona kwamba ni yenye kuwagawa Watanzania wasipate kuendeleza umoja na upendo waliokuwa nao tangu azali.

Kwa hivyo, mbiu ya Mwalimu ikawa ni kuwatahadharisha Watanzania dhidi ya wadau hao ya kwamba ni maadui wanaopaswa kupigwa vita kwa udi na uvumba. Fauka ya hayo, Mwalimu alikuwa akitumia maneno: ***"kupanga ni kuchagua"*** kama mtawalia wa maudhui kuhusu umoja wa kitaifa (Muungano). Umoja aliusawiri kama kibebeo cha maneno ***“kupanga ni kuchagua”*** kwa ufahima wa jinsi Watanzania walivyoweza kuyafikia maamuzi ya malengo yao kwa usahihi tangu mapambano yao ya kumng'oa Mkoloni hadi kupata uhuru na baadae kuziunganisha nchi mbili (Tanganyika na Zanzibar) na kuzaliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Umoja ulikuwa ndio silaha ya maongozi ya maisha yao uliyowapelekea kuimarisha uchumi, ulinzi, siasa na utamaduni; lakini pia mapambano dhidi ya maadui ujinga, maradhi na umasikini.

Taswira ya umoja na maamuzi bora kuhusu kipi kipewe kipaumbele (***kwa maana ya "kupanga ni kuchagua"***) ni udhihirisho na utashi uliotokana na makaribisho ya Mwalimu Nyerere wakati alipokuwa akiwakaribisha wageni waalikwa katika mkutano wa chama cha TANU. Kauli zake zilisheheni ujumbe maalumu kwa mataifa ya kimagharibi yaliyowahi kulitawala Bara la Afrika. Aliwashutumu kutokana na madai yao kwamba wao (Wazungu) ni katika mataifa yaliyohalalishwa na Mungu kuwatawala watu wengine kadiri wapendavyo. Ujumbe bebwaji wa Mwalimu uliwatanabahisha Watanzania kwamba Wazungu wa kikoloni hawana budi kutambua kwamba nafasi ya kulidhalilisha bara la Afrika imepitwa na wakati. Mithali ***"kupanga ni kuchagua"***, Watanzania wamekwisha chagua kwamba umoja ndio silaha pekee na hakuna awezaye kuwatikisa tena, wamejipanga na wapo tayari kwa lolote dhidi ya maadui wa ndani na nje kwa azma ya kuulinda utu na heshima ya taifa lao.

#### 3.6.3.1 Mitindo Iliyotumika katika Maudhui ya Umoja wa Kitaifa

**Tashbiha**: "*Udugu wetu ni kama bahari…"* (UK 1:4: KK).

Fahiwa kuhusu neno ***"udugu"*** imefananishwa na eneo pana na refu lenye mkusanyiko wa maji mengi ambayo mwanadamu akiyazamia ingawa kwa nyenzo na kwa ufundi au kipaji alichojaaliwa na Mungu; kama sio majaaliwa yeke Mwenyezi Mungu ni muhali kuibuka. Na ndiyo Mwalimu akisema: **"*Udugu wetu ni kama bahari - hata iwe ni kwa kuizuia mito yote inayomwaga maji yake baharini kamwe hakuna awezaye kuutikisa umoja wa Watanzania; na kwa Waafrika wenzao".*** Amabapo hii ni kumaanisha kwamba, uimara wa umoja wa Watanzania na Waafrika wenzao unahawilishwa na kuwa sawa na uimara wa bahari. Kumaanisha kwamba hata kama awe ni adui mwenye mbinu za kifani; kamwe hatoweza kuwatenganisha kwa namna yeyote ile.

Hii ndiyo kusema kwamba, kauli alizozitumia Mwalimu zilikusudiwa kuwashawishi Watanzania waudumishe udugu wao wa tangu azali, udugu ambao haukuwa wa kulazimishwa bali ulikuwa ni wa hiari ya moyoni mwao wenyewe. Ulikuwa wa kusaidiana kwa hali na mali, udugu wenye mapenzi ya dhati na yasiyo na kifani kwa mwingine kuweza kutabiri aila iliyomo moyoni mwa mwingine. Na kwa umoja wao thabiti iwe ni sababu ya kuzivunja nguvu za maadui wasioitakia Tanzania na pengine Afrika kwa ujumla - uhuru na amani ya kudumu.

**Tashbiha na takriri neno**: "*Dhambi ya ubaguzi ukisha kuitenda inaendelea: ni kama ukila nyama ya mtu utaendelea kuila*". (UK 10:3: N).

Kauli hizi ni mwendelezo wa tahadhari ya Mwalimu kwa wale waliokuwa wanaukataa Muungano. Neno ***dhambi*** ni malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu anayoyatoa kwa viumbe wake wanaomkosea kwa kuacha kutenda mema hapa duniani. Kwa hivyo aliahidi kuwaadhibu - ama hapahapa duniani au kwa maisha ya baada ya kufa kwao. Hivyo, kiimani viumbe wote wa Mwenyezi Mungu - akiwemo mwanadamu; wanatakiwa wamtii Mwenyezi Mungu kwa kila alilowaamrisha ili maisha yao hapa duniani na baada ya mauko yao yawe ni ya amani na furaha.

Kwa mwegemo wa muktadha wa uvunjifu wa Muungano (umoja), ndiposa Mwalimu aliwafananisha wale wote wenye kuhusika katika kuwashawishi wengine wauvunje Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar ya kwamba, ***ni sawa na kula nyama ya mtu***. Kwa msisitizo wenye uchungu wa moyoni akisema: ***ukila nyama ya mtu utaendelea kuila*** **-** kumaanisha kwamba, ikiwa miongoni mwa Watanzania kana watakaohusika katika kuuvunja Muungano, haina maana kwamba wao watasalimika. Ingawa watu watatengana kutokana na fitina zao, kutengana huko kutajenga uhasama ambao kila tapo litajinadi kwa ubora ama likihisi kwamba linaonewa na tapo lingine lililotengana nalo. Taswira yake ni kupelekea migogoro na hata mauaji ambapo kila mmoja atahisi anaguswa kwa namna moja au nyingine hasa ikiaminiwa kwamba mwanadamu silka na asili yake ni moja; kwa maana ya uzawo wa Nabii Adam; ambapo kila mmoja atakuwa anahusiana na mwingine kidugu. Ndiyo Mwalimu akasema: ***"dhambi ya ubaguzi ni sawa na kula nyama ya mtu; na kwamba mwenye desturi hiyo daima hawezi kuiacha***; ni dhulma ambayo itaigusa jamii nzima. Kila mmoja atajibu mashambulizi ima kwa kuitetea haki yake au ya ndugu yake - hadi kufikia tone la damu ya mtu wa mwisho.

Hivyo, Watanzania wanatahadharishwa wasihusike kwa kutenda dhambi hiyo ya kuwabaguwa ndugu zao hata ikawa ni wauvunje Muungano. Watambue kwamba Mwenyezi Mungu hatawahurumia kwa kosa hilo la kuwafitinisha wengine. Badala yake, wasimame kidete katika kupambana na wanafiki wanaowachonganisha; ili wadumishe umoja na amani yao ya tangu enzi za umajumui; waishi kwa furaha na mwisho wao uwe mwema.

### 3.6.4 Maudhui kuhusu Rushwa

Rushwa ni katika maswala yaliyomkera Mwalimu katika kipindi cha maongozi yake na hata baada ya kung'atuka kwake. Ni miongoni mwa matatizo ambayo Mwalimu aliyavalia njuga kwa hima ya kuyatokomeza. Ingawa hivyo, kila uchao "rushwa ilionekana kuota mizizi"; na ndio ikawa daima akijiuliza kwamba, ni kwa jinsi gani watu wanaziweka roho zao rehani kwa kuiuza au kuinunua "haki" - kwa kutumia rushwa; hata iwe viongozi wa nchi nao wahusike (katika ulaji rushwa) ilhali sheria kuhusu makataa yake zingali mikononi mwao. Kwa kumbukizi za Mwalimu Nyerere, ilikuwa ni imani yake kwamba tatizo la Watanzania kuhusika katika rushwa linge kuwa ni masimulizi kwa enzi za maongozi yake na sio baada ya kung'atuka kwake. Enzi za maongozi yake (Mwalimu Nyerere) tatizo la rushwa lilipokuwa limeshamiri - walifanya jitihada za kulikomesha kwa haraka.

Mbali na sheria zilizokuwa zikitekelezwa na mahakama, kama viongozi wa chama na serikali; tatazo la rushwa liliundiwa kanuni kupitia chama cha TANU na baadae CCM. Kwa ilani ya kumtaka kila mtu akiri kwa dhati ya moyo wake kwamba: "***Rushwa ni adui wa haki. Sitatoa wala sitapokea rushwa***". Pamoja na hayo, waliunda sheria za utekelezwaji wake. Sheria ilikuwa; baada ya mahakama kuthibitisha kwamba mtuhumiwa kala au kapokea rushwa; Mwalimu alisema: hawakuiachia mahakama uamuzi peke yake; bali ilipitishwa sheria kwa mtuhumiwa kupewa kifungo cha miaka miwili na viboko kumi na viwili wakati wa kuingia na kumi na viwili wakati wa kutoka – ikiaminiwa  kwamba, viboko kwa mtu mzima na hasa kwa mwanamume ilikuwa ni aibu kumaanisha kwamba, akitendewa hivyo mbele ya familia yake itakwa ni aibu kwake na kwa familia yake hata wanapotangamana naye baada ya kumaliza kifungo chake; fedheha ya matendo yake; yalionekana yakiendelea kumwandama; kwa maana ya kuisuta nafsi yake kwa kumtumbukiza katika uovu wa rushwa.

Suala la rushwa enzi za maongozi ya Mwalimu; lilikuwa ni limulikwe katika nyanja zote za maisha ya Mtanzania. Na kila Mtanzania ikawa ni ajihadhari kwa rushwa - ima kwa kuitoa au kwa kuipokea. Na ndiposa Mwalimu akiliona tatizo la rshwa enzi za maongozi yake lilikuwa na ahueni tofauti na siku za usoni baada ya kung'atuka kwake. Hivyo, changamoto ya Mwalimu kwa Watanzania ikawa ni alikemee kwa matendo (tatizo la rushwa); bila ya kumuonea mtu yeyote haya; ima kwa wadhifa wake au kwa utaifa wake; maadam tu! athari yake inawaendea Watanzania.

#### 3.6.4.1 Mitindo Iliyotumika katika Maudhui - Kuhusu Rushwa

**Msemo**: "*Samaki mmoja akioza wote huoza.*" (UK 9:2: MMT) & (UK 46:2: AA)

Haya yalikuwa ni makemevu dhidi ya wale walioukuwa wakiukejeli uendelevu wa umoja na amani uliopo miongoni mwa Watanzania; na kwa hivyo Mwalimu aliionya jamii isiwafumbie macho maadui ili wasipate mwanya wa kuwaathiri wengine kwa tamaa zao. Usadifu huu ni kutokana na viongozi waliokuwa wakihimiza umoja na amani chini ya misingi ya ujamaa lakini ikawa ni wapenyeze matakwa yao binafsi ya kujiimarisha kiuchumi huku umma ukiendelea kutaabika kwa umasikini, na kwa hivyo wananchi wakihoji kwamba ni kwa jinsi gani inawezekana katika nchi ya kijamaa – wachache waweze kujipatia fedha za kujianzishia shughuli kubwa kubwa za kibiashara kiasi cha kujenga tofauti ya kimapato ndani ya nchi masikini. Hali iliwapelekea wananchi kuona ya kana kwamba wanafanyiwa kejeli kwa kuhimizwa kuishi kijamaa ilhali misingi yeke haisimamiwi ipasavyo.

**Jedwali 2: Mfano wa Jinsi Deta ya Maoni Ilivyochanganuliwa kwa njia ya Kiwingidadi**

| **Hotuba** | **Maudhui mahsusi** | **Mtindo** | **Maoni / Hisia** | **Athari** | **Ushawishi Chanya (+)** | **Ushawishi Hasi (-)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| AW | Uongozi bora | Takriri neno | Lakini kwa nini watu wengine wajione ni mabwana kiasi cha kuwaburuza wengine kama watumwa wao. Kuna haja ya sheria za nchi zibadilishwe na kuhakikisha kiongozi si tu kwamba ni mchapakazi lakini mwenye kuilinda, kuiheshimu na kuisimamia barabara katiba ya nchi - inatekelezwe na raia wote wa Watanzania. Lakini kwa nini | **Kuchukia** | | **–** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | viongozi hawakubali kukosolewa pindi wanapokwenda kombo? … wanalindana? Huwa inaniuma sana ikiwa kiongozi kabainika katenda kosa halafu badala ya kufukuzwa ana hamishwa kituo. Je, hayo ndiyo maadili ya uongozi. Hakika raia huwa inawaudhi sana. Kunahaja kila unapowadia uchaguzi kuhakikisha anapatikana kiongozi anayelitambua tatizo hili la kulindana; lakini la kutoiheshimu katiba ya nchi - alikomeshe. Na watambue kwamba ili kuleta ufanisi hawana budi kuwa bega kwa bega na raia waliowachagua / wanaowaongoza. vinginevyo watambue kwamba raia watakapozinduka hawataipata salama. | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KK | Muungano | Tashbiha Uongozi bora | Wakoloni walituonea sana, lakini baada ya Mwalimu kutushawishi kuhusu Muungano, tumekuwa imara. Kamwe hakuna wakututingisha tena. | Kuchukia | | – |
| N | Muungano | Tashbiha na takriri neno | Tatizo la mdororo wa umoja na amani kwa Watanzania; kwa kiwango kikubwa linatokana na “ubaguzi” unaoendelezwa na baadhi ya Watanzania. Yu wapi Baba wa Taifa; alilikemea tatizo hili hata ikawa ni Watanzania wasifike ndani na nje ya nchi; wakitambulika kwa utaifa wao. Ingawa wana makabila zaidi ya ishirini na tatu. Hakika kuna haja ya viongozi wa leo kuzifuata nyayo za Mwalimu Nyerere kindakindaki. | Kusikitika | | – |
| MMT & AA | Rushwa | Msemo | Yote tisa; lakini adhabu kwa walarushwa huwa inaniuma sana. … Ingawa wenye utashi wa kuitumia rushwa kama | Kuchukia | | – |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | njia ya mafanikio yao ni wachache; wengi hujikuta wakizamishwa katika mtego huo; hasa ikisadifiwa kwamba adhabu kuhusu kosa la rushwa ni kwa mtoaji na mpokeaji. Lakini kwa nini sheria hii isibadilike? Wanaowashawishi wenzao ikawa ndio wahukumiwe. Kuna haja ya mabadiliko. Ingawa zilikuwa ni jitihada za Mwalimu enzi za maongozi yake; hakuwa Mungu na wala katiba hiyo siyo Msahafu au Bibilia. Katiba mpya ni muhimu ikazingatia kipengele hicho; na iwe na mikakati ya kukomesha rushwa. | | | |

Imebainika kwamba, hotuba za Mwalimu huwashawishi Watanzania ima kwa kusikiliza au kwa kuzisoma. Ufahima huu unatokana na maoni ya wasailiwa kama inavyodhihirika katika jedwali 2. Ambapo kwa asilimia 67 kwa yale waliyosailiwa kwa kuzingatia maudhui na mitindo kama ilivyobainika katika jedwali 2; wameonyesha kukubaliana na yale ambayo Mwalimu Nyerere aliyaendeleza katika hotuba zake.

### 3.7 Jinsi Deta ya Maoni Ilivyochanganuliwa kwa njia ya Kithamano

**MW 1:** *Hotuba zake ni nzuri sana, zina konga takriban kila nyanja ya maisha. Ingawa anapokemea jambo mara nyingi hana tafsida na kwa hivyo watu wengi huhisi kwamba alikuwa na jeur, lakini kusema la kweli zinaelemisha*.

Maoni haya yanaonyesha kwamba kuna Watanzania ambao hutambua kwamba hotuba za Mwalimu zina manufaa makubwa kwa jamii ya Watanzania. Hata kama kuna baadhi ya Watanzania wanaoguswa kwa kuzisoma au kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere; kukosolewa huko hakuwakatishi tamaa ya kuendelea kuzisoma au kuzisikiliza hotuba hizo kutokana na faida nyingi zilizomo ndani yake. Hii ni kwa sababu Mwalimu alikua haongelei jambo moja tu katika hotuba zake. Kwa hivyo huwavutia watu wengi kutaka kujua mengi yaliyotagaa ndani ya hotuba zake. Na hii ndiyo kusema kwamba hata kama mtu ataudhika kwa jambo moja lakini atayafaidi mengi zaidi katika hotuba hiyo hiyo moja.

**MW 2:** *Hotuba ilinitia mshawasha wa kuyatathmini matendo yangu ya kila siku. Hakika kuna umuhimu wa kumweka Mwenyezi Mungu mbele kwa kila jambo.*

Maoni haya yalitolewa kutokana na matamshi ya Mwalimu Nyerere pale alipokemea suala la ubaguzi. Ilibainika kwamba kuwatenga wengine kieneo au kwa rangi zao ni katika madhambi makubwa. Madhara yake huanzia hapa hapa duniani: kutokana na chuki na hata kupelekea vita. Kwa maonyo hayo, kunathibitisha kwamba hotuba za Mwalimu zenye makemevu zinauzingatifu mkubwa kwa Watanzania pengine ni kutokana na ufasaha wa lugha na mbinu anuai alizokuwa akizitumia; ama mazoea yake ya kuongea mambo kwa ushahidi ambao unawapelekea wengi kumpenda na kumzingatia kwa kila alilolionya au kuwaelekeza. Hivyo, ingawa wengine wanaudhika kwa baadhi ya matamshi yaliyomo katika hotuba zake, lakini nafsi zao huwarudi na ikawa ni wajirekebishe kwa ajili ya kuleta utangamano mzuri kijamii.

**MW 3:** *Kwa nini hotuba za Mwalimu Nyerere zinapewa ukipaumbele hivyo: uongozi wa kitaifa umeziundia taasisi, asasi za kitaifa zimepewa dhima ima ya kuzihifadhi au kuzirusha hotuba hizo hewani. Baadhi ya viongozi kama Karume; Jamhuri ya Muungano mbona haifanyiwi kama anavyomfanyiwa Mwalimu Nyerere? Ni kama imemsahau ya kwamba naye aliwahi kuwa miongoni mwa waasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Fauka ya hivyo, hivi leo kiongozi wa serikali akionekana anatenda kinyume na alivyotenda au kuhimiza Mwalimu – inakuwa nongwa. Kwani yeye alikuwa Mungu? Kama ni uchumi, siasa, kilimo au elimu - kunamabadiliko makubwa; mambo mengine lazima watu wayazungumze kinyume na alivyokuwa akihimiza Mwalimu. Kwa mfano enzi za maongozi yake; nyingi ya*

*sera ilikuwa ni kufyaata mkia tu! hakuna aliye furukuta mbele yake. hakuna aliye ruhusiwa kuhoji au kutoa ushauri mbele yake. iwe ni pembejeo za kilimo au fani za kiusomi - hivi leo mawasiliano yamo kiganjani na sio kuyafuatilia katika kituo cha tarafa au wilayani tena. Lazima Watanzania wabadilike; wazisome alama za Nyakati.*

Haya ni matamshi ya wasailiwa baada ya tafakuri kuhusu kauli ya Mwalimu Nyerere kwamba, **"*Walimu watayarisheni watoto wenu kwa maisha watakayokweda kuishi katika vijiji vyao. Basi full stop*"** (UK 4:3: EKT). Kwa hivyo ikionekana kwamba kauli hizo huenda zinge kuwa ni faafu kwa wakati huo; na badala yake ni itambulike kwamba, nchi haiwezi kujifunika kwa mwamvuli wa kutohitaji chochote kutoka kwa majirani zake au ughaibuni. Raia wataurarua mwamvuli huo; wanahitaji kuyajua mengi yaliyoizunguka dunia kutokana na teknolojia iliyopo hivi leo; ambapo kwa utangamano wa mawasiliano wenye kasi isiyo na kifani kila uchao; mwanadamu atahitaji kuyapata mabadiliko yanayojiri ulimwenguni; na anaweza kuyahimu maisha yake popote katika ulimwengu huu tulionao. Hivyo, kauli za namna hiyo zimepitwa na wakati. Hivyo, Watanzania hawana budi kuzisoma alama za nyakati. Hii ndiyo kusema, ingawa hotuba hizo zingali zinarushwa hewani; lakini si kila jambo lililomo katika hotuba zake kwamba lina umuhimu wa kutekelezwa na ama kufanywa sera ya kuwaongoza Watanzania wa leo; na badala yake ushawishi wa kusikilizwa au kusomwa kwa hotuba hizo - kwa siku za usoni huenda ukuwa ni wa kihistoria tu!

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imejishughulisha na uwasilishaji pamoja na uchanganuzi wa deta ya utafiti huu amabyo ni hotuba za Mwalimu Nyerere; na maoni ya wasikilizaji na wasomaji kuhusu hotuba hizo. Deta iliyokusanywa iliorodheshwa na kuchanganuliwa kithamano na kiwingidadi ili kukidhi mahitaji ya mada ya utafiti huu ambayo yalikuwa ni kubainisha sifa za lugha zinazowapelekea Watanzania kushawishika kiasi cha kuwafanya wapende kuzisoma na kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kila uchao.

Madhumuni ya utafiti yalikuwa kutambulisha maudhui na mitindo mahususi yaliyomo katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere; na kupambanua athari zinazoikumba hadhira ya wasikilizaji ama wasomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere. Kwa hivyo, deta iliyokusanywa imechanganuliwa na kuelezwa kwa kina ili kujibu maswali ya utafiti sanjari na mihimili ya nadharia ya balagha iliyotumiwa katika utafiti huu.

Uchanganuzi huu umedhihirisha maudhui mahususi ambayo ni: umoja wa kitaifa, kupuuza na kutokuijali katiba, umuhimu wa sheria, rushwa, ukabila na udini, umoja wa wafanyakazi, kilimo kwanza, kutofungamana na upande wowote, uwajibikaji, uongozi bora, ufaafu wa Azimio la Arusha, ubaguzi, elimu kwa wote,  onyo kwa Idd Amin, demokrasia; na kupaa na kutunguliwa kwa Azimio la Arusha. Fauka ya hayo; tashbiha,takriri, tafsida kengeushi, maswali ya kibalagha, tashtiti, uchimuzi, methali, tashhisi, sentensi changamano na ambatano, uchnganyaaji ndimi, uzungumzi nafsi, istiara, unukuzi,msemo, usimulizi, viambishi nafsi, vimilikishi, vihisishi, fumbo, kinaya, kejeli, sentensi fupifupi, vinyume na taswira – zilitumika  kuelezea maudhui hayo. Kwa ubainifu huo, jedwali lifuatalo linadhihirisha mbinu za kibalagha kulingana na maudhui yaliyoendelezwa katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere.

**Jedwali 3: Maudhui Mahsusi na Mbinu za Kibalagha (Mbinu za Kiisimu)**

| Maudhui Mahsusi | Mitindo iliyobainika | Ukurasa |
|---|---|---|
| **Umoja wa Kitaifa (Muungano)** | *Tashbiha* | (UK 1:4: KK) |
| | *Takriri* | (UK 8:2: TTT) |
| | *Tafsida kengeushi na takriri* | (UK 9:4: N) |
| | *Tashbiha na takriri* | (UK 10:3: N) |
| | *Maswali ya kibalagha na ukatizaji wa maneno* | (UK 11:2: N) |
| | *Tashtiti, uchimuzi na takriri* | UK 4:3: MTU) |
| | *Methali* | (UK 3:1: MMT) |
| | *Tashbiha, takriri na maswali ya kibalagha* | (UK 7:2: N) , (UK 8:2: N) na (UK 9:2: N) |
| **Maudhui kuhusu Kupuuza na Kutokujali Katiba** | *Takriri* | (UK 12:3/3:1: N) |
| | *Takriri na tashhisi* | (UK 13:3 / 14:1: N) |

| | | |
|---|---|---|
| **Maudhui kuhusu Umuhimu wa Sheria** | *Swali la kibalagha na takriri* | (UK 14:2: N) |
| | *Tafsida kengeushi, sentensi changamano na ambatano* | (UK 14:3/15:1: N) |
| **Maudhui kuhusu Rushwa** | *Takriri na tashtiti* | (UK 15:3/16:1: N) |
| | *Tashhisi, takriri na uchanganyaji ndimi* | (UK 15:3 / 16:1: N) |
| | *Maswali ya kibalagha, tafsida kengeushi, uzungumzi nafsi na takriri* | (UK 17:2: N) |
| | *Takriri na maswali ya kibalagha* | (UK 18:2: N) |
| | *Istiara, tashhisi na tafsida kengeushi* | (UK 19:1: N) |
| | *Unukuzi* | (UK 44:2: AA) |
| | *Msemo* | (UK 9:2: MMT) & (UK 46:2: AA) |

| | | |
|---|---|---|
| **Maudhui kuhusu Ukabila na Udini** | *Usimulizi, tashhisi unukuzi na maswali ya kibalagha* | (UK 23:1-3: N) |
| | *Maswali ya kibalagha na tashhisi* | (UK 24:4/25:1: N) |
| | *Tashhisi na takriri* | (UK 26:1: N) |
| | *Takriri* | (UK 12:3/3:1: N) |
| | *Maswali ya kibalagha na tashhisi* | (UK 26:2/27:1-2: N) |
| | *Viambishi nafsi na vimilikishi* | (UK 9:3: KW) |
| | *Takriri,kinyume, taswira na uchanganyaji ndimi* | (UK 18:1: AW) |

| | | |
|---|---|---|
| **Maudhi kuhusu Umoja wa Wafanyakazi** | *Vihisishi na maswali ya kibalagha* | (UK 5:1: TTT) |
| | *Uzungumzi nafsi, maswali ya kibalagha na vihusishi* | (UK 6:2: TTT) |
| | *Istiara na takriri* | (UK 7:2: TTT) |
| **Maudhui kuhusu Kilimo Kwanza** | *Tashbiha, tafsida kengeushi na maswali ya kibalagha* | (UK 9:2-3: MUSW) |
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 10:2: MU) |
| | *Tafsida kengeushi* | (UK 10:4: MU) |
| | *Takriri* | (UK 11:2: SU) |
| | *Takriri* | (UK 4:5: MMT) |

| | | |
|---|---|---|
| **Rai ya Tanzania ya Kutofungamana na Upande Wowote** | *Takriri na tashbiha* | (UK 2:4: MUSW) |
| | *Tashtiti na takriri* | (UK 5:5: MUSW) |
| | *Takriri na maswali ya kibalagha* | (UK3: 1-3: MUSW) |
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 4:5: MUSW) |
| | *Tafsida kengeushi* | (UK 5:4: MUSW) |
| | *Takriri* | (UK 5:2: MUSW) |
| **Maudhui kuhusu Uwajibikaji** | *Maswali ya kibalagha* | (UK 3.3: SU) |
| | *Takriri* | (UK 10:2: SU) |
| | *Takriri* | (UK 11:1: SU) |
| | *Takriri* | (UK 4:3-4: OIA) |

| | | |
|---|---|---|
| | *Tashbiha, takriri na fumbo* | (UK 11:2: SU) |
| | *Takriri na tashtiti* | (UK 11:5: MU) |
| | *Tafsida kengeushi na takriri* | (UK 17:1 MU) |
| | *Usimulizi, vihisishi na takriri* | (UK 7:4: N) |
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 23: 3: TTT) |
| | *Istiara na tashbiha* | (UK 2:3: KW) |
| | *Tashbiha* | (UK 5:2: AA) |
| **Mauhui kuhusu Uongozi Bora** | *Takriri, swali la kibalagha na tashhisi* | (UK13:3: KW) |

| | |
|---|---|
| *Takriri* | (UK 19:1-2: AW) |
| *Takriri* | (UK 19:3; 20:1: KW) |
| *Maswali ya kibalagha* | (UK 1:3, 2: 5, 3: 1: TTT) |
| *Maswali ya kibalagha na Takriri* | (UK 2: 5- 3: 1: TTT) |
| *Maswali ya kibalagha* | (UK 3:1: TTT) |
| *Takriri na tashhisi* | (UK 13:3 / 14:1: N) |
| *Tashtiti* | (UK 26:2: TTT) |
| *Istiara* | (UK 26:3: TTT) |
| *Takriri na maswali ya kibalagha* | (UK 27:2 - 4: TTT) |
| *Takriri* | (UK 5:3: N) |

| | | |
|---|---|---|
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 1:2-3: MU) |
| | *Maswali ya kibalagha na takriri* | (UK 9:2-3: MU) |
| | *Takriri* | (UK 1:2: KW); (UK 9 – 11:3:KW) |
| **Maudhui kuhusu Ufaafu wa Azimio la Arusha** | *Tafsida kengeushi* | (UK 29:3: AA) |
| | *Takriri* | (UK 9:3: TTT) |
| | *Tashtiti na takriri* | (UK 11:3: TTT) |
| | *Takriri na kinaya* | (UK 12:3: TTT) |
| | *Maswali ya kibalagha na takriri* | (UK 10:1: TTT) |
| | *Istiara na maswali ya kibalagha* | (UK 10:2: TTT) |

| | | |
|---|---|---|
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 17:1 -20:2: TTT) |
| | *Kejeli na takriri* | (UK 22:1: TTT) |
| | *Maswali ya kibalagha na tafsida kengeushi* | (UK 23:2: TTT) |
| | *Takriri na sentensi fupifupi na tashbiha* | (UK 21:3; 4 -5: N) |
| **Maudhui kuhusu Ubaguzi** | *Maswali ya kibalagha* | (UK 7:2: OIA) |
| | *Tashhisi na tafsida kengeushi* | (UK 25:3: N) |
| **Maudhui kuhusu Elimu kwa wote** | *Takriri* | (UK 4:1: AM) |
| | *Tashhisi na takriri* | (UK 8:1: AM) |
| | *Vihisishi na maswali ya kibalagha* | (UK 11:2: AM) |

| | |
|---|---|
| *Maswali ya kibalagha na tashhisi* | (UK 2:1: ME) |
| *Maswali ya kibalagha na takriri* | (UK 17:3; 18:1: AM) |
| *Uchanganyaji ndimi* | (UK 2:1: ME) |
| *Uchanganyaji ndimi na tashhisi* | (UK 3:1: ME) |
| *Uchanganyaji ndimi* | (UK 4:3: EKT) |
| *Msemo* | (UK 6:3: ME) |
| *Maswali ya kibalagha na uchanganyaji ndimi* | (UK 4:1: EKT) |
| *Maswali ya kibalagha na takriri* | (UK 39:1: EKT) |
| *Methali* | (UK 6:2: SE) |

| | | |
|---|---|---|
| **Madhui kuhusu Onyo kwa Idd Amin** | *Takriri* | (UK 3:3: MAV) |
| | *Tafsida kengeushi* | ( UK 3:7: MAV ) |
| | *Maswali ya kibalgha, tusimulizi na kinaya* | (UK 12:4: OIA) |
| | *Takriri na tafsida kengeushi* | (UK 1:5/2:1: OIA) |
| | *Istiara na takriri* | (UK 3:5-4:1: OIA) |
| | *Maswali ya kibalagha, tashbiha, tafsida kengeushi, uzungumzi nafsi na takriri* | (UK 7:4-8:1: OIA) |
| **Maudhui kuhusu Demokrasia** | *Tashbiha* | (UK 2:3 TM) |
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 6:1: TM) |
| | *Msemo* | (UK 14: 2: TM) |

| | | |
|---|---|---|
| | *Uchimuzi* | (UK 15:1: TM) |
| | *Uchimuzi* | (UK 16: 3: TM) |
| | *Usimulizi* | (UK 1: 3: KK2) |
| | *Istiara* | (UK 1:4: KK2) |
| | *Tashhisi* | (UK 2:2: KK2) |
| **Maudhui kuhusu Kupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha** | *Maswali ya kibalagha* | (UK 5: 5: KK2) |
| | *Takriri na tashbiha* | (UK 12:2: TTT) |
| | *Maswali ya kibalagha* | (UK 10:1: KK2) |
| | *Tafsida kengeushi* | (UK 13: 2: MMT) |
| | *Takriri na usimulizi* | (UK 9:1: MU) |
| | *Maswali ya kibalagha na takriri* | (UK 9:2-3: MU) |
| | *Takriri* | (UK 2:1: AA) |

Kwa kuzingatia Jedwali 3: ufuatao ni uchanganuzi (wa maudhui na mitindo) na ufasiri wake

### 4.4.1 Maudhui ya Umoja wa Kitaifa (Muungano)

Ilikuwa ni kumbukizi za Mwalimu kwamba, kabla ya kuzaliwa Tanzania, iliyokuwa ikiitwa Tanganyika; na serikali ya Unguja; pande hizi mbili zilipitia katika kipindi kigumu zaidi. Shime ya kuwepo kwa umoja wa kitaifa baina ya Watanganyika na Wazanzibari ilitokana na ushawishi wake (Mwalimu Nyerere) kuhusu umuhimu wa Muungano. Kwa historia ni kwamba nchi hizo mbili kabla ya kuvamiwa na Wakoloni, wananchi wake walikuwa kitu kimoja. Walishirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa, lakini ikawa ni watenganishwe na Wakoloni ili waweze kuwatawala kwa urahisi. Walikuwa na itikadi kwamba, wao ndio wenye uhalali wa kuwatawala wengine popote ulimwenguni mintaarafu ya rangi zao. Ingawa hivyo, kwa umoja wao, waliweza kuwapiga vita na kuwashinda. Tanganyika na Unguja zikawa nchi huru na kwa hivyo, Wakoloni wakafungasha virago vyao na kurudi makwao.

Kwa mbiu ya ***"Sahau Ukabila!"*** chini ya misingi ya chama cha TANU enzi hizo, Watanganyika na Wazanzibari waliweza kuungana na kuzalisha Jamhuri ya muungano wa Tanzania mwaka 1964. Ingawa hivyo, mara baada ya Mwalimu kung'atuka, aliingiwa na tashwishi alipobaini kwamba muungano wa Jamhuri ya Tanzania ulikuwa umetikiswa. Baadhi ya Watanzania walikuwa wakiwashawishi wenzi wao wasiukubali tena muungano kwa madai kwamba hauwanufaishi watu wa pande mbili kwa usawa, yaani Tanganyika na Zanzibar. Kwa mfano, madai ya kwamba: ***"wengine wana bendera na wimbo wa taifa ilhali wengine hawana"***. Ni madai ambayo kwa Mwalimu aliyaona kwamba ni yenye kuwagawa Watanzania wasipate kuendeleza umoja na upendo waliokuwa nao tangu azali.

Kwa hivyo, mbiu ya Mwalimu ikawa ni kuwatahadharisha Watanzania dhidi ya wadau hao; ya kwamba ni maadui wanaopaswa kupigwa vita kwa udi na uvumba. Fauka ya hayo, Mwalimu alikuwa akitumia maneno: ***"kupanga ni kuchagua"*** kama mtawalia wa maudhui kuhusu umoja wa kitaifa (muungano). Umoja aliusawiri kama kibebeo cha maneno ***“kupanga ni kuchagua”*** kwa ufahima wa jinsi Watanzania walivyoweza kuyafikia maamuzi ya malengo yao kwa usahihi tangu mapambano yao ya kumng'oa mkoloni hadi kupata uhuru na baadae kuziunganisha nchi mbili (Tanganyika na Zanzibar) na kuzaliwa Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Umoja ulikuwa ndio silaha ya maongozi ya maisha yao uliyowapelekea kuimarisha uchumi, ulinzi, siasa na utamaduni, lakini pia mapambano dhidi ya maadui ujinga, maradhi na umasikini.

Taswira ya umoja na maamuzi bora kuhusu kipi kipewe kipaumbele (***kwa maana ya "kupanga ni kuchagua"***) ni udhihirisho na utashi uliotokana na makaribisho ya Mwalimu Nyerere wakati alipokuwa akiwakaribisha wageni waalikwa katika mkutano wa chama cha TANU. Kauli zake zilisheheni ujumbe maalumu kwa mataifa ya kimagharibi yaliyowahi kulitawala Bara la Afrika. Aliwashutumu kutokana na madai yao kwamba wao (Wazungu) ni katika mataifa yaliyohalalishwa na Mungu kuwatawala watu wengine kadiri wapendavyo. Ujumbe bebwaji wa Mwalimu uliwatanabahisha Watanzania kwamba Wazungu wa kikoloni hawana budi kutambua kwamba nafasi ya kulidhalilisha bara la Afrika imepitwa na wakati. Mithali ***"kupanga ni kuchagua"***, Watanzania wamekwisha chagua kwamba umoja ndio silaha pekee na hakuna awezaye kuwatikisa tena. Wamejipanga na wapo tayari kwa lolote dhidi ya maadui wa ndani na nje kwa azma ya kuulinda utu na heshima ya taifa lao.

#### 4.4.1.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Umoja wa Kitaifa (Muungano)

**Tashbiha**: "*Udugu wetu ni kama bahari…"* (UK 1:4: KK).

Dhana ya ***"udugu"*** imefananishwa na eneo pana na refu lenye mkusanyiko wa maji mengi ambayo mwanadamu akiyazamia ingawa kwa nyenzo na kwa ufundi au kipaji alichojaaliwa na Mungu; kama sio majaaliwa yeke Mwenyezi Mungu ni muhali kuibuka. Ndiyo maana Mwalimu alisema: **"*Udugu wetu ni kama bahari*** *- hata iwe ni kwa kuizuia mito yote inayomwaga maji yake baharini kamwe hakuna awezaye kuutikisa umoja wa Watanzania na kwa Waafrika wenzao"*. Amabapo hii ni kumaanisha kwamba, uimara wa umoja wa Watanzania na Waafrika wenzao unahawilishwa na kuwa sawa na uimara wa bahari. Kumaanisha kwamba hata kama awe ni adui mwenye mbinu za kifani kamwe hatoweza kuwatenganisha kwa namna yeyote ile.

Hii ndiyo kusema kwamba, kauli alizozitumia Mwalimu ilikuwa ni kuwashawishi Watanzania waudumishe udugu wao wa tangu azali. Udugu ambao haukuwa wa kulazimishwa bali ulikuwa ni wa hiari ya moyoni mwao wenyewe hususani katika kusaidiana kwa hali na mali. Udugu wenye mapenzi ya dhati na yasiyo na kifani kwa mwingine kuweza kutabiri ila iliyomo moyoni mwa mwingine. Umoja wao thabiti ulikuwa ndiyo sababu ya kuzivunja nguvu za maadui wasioitakia Tanzania na pengine Afrika kwa ujumla - uhuru na amani ya kudumu.

**Takriri**: *"Nchi hii, Tanganyika, ni nchi changa. Watu wake waliwekwa katika sehemu inayoitwa moja na Wajerumani. Wamakonde na Wazanaki hawakuwa wamoja. Waliwekwa pamoja na Wajerumani ili watawaliwe. Jitihada ya kuwafanya wawe pamoja na kuanza kusema "Ninyi ni Wamoja" haikufanywa na Wajerumani: Kwa sababu Wajerumani ambao wangeweza kusema "Ninyi ni Wamoja" lengo lao halikuwa ni kujenga umoja. Wajerumani walichoweza kusema ni kwamba 'Ninyi ni Tofauti', Ninyi ni Tofauti! Ili waendelee kuwatawala.* (UK 8:2: TTT)

Ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania watambue kwamba maendeleo ya nchi yangali yanahitaji mwendo kasi. Zaidi ya hayo, yanahitaji umoja thabiti na wenye kufasirika katika matendo ya maisha ya Mtanzania ya kila siku; kwa kumbukizi aliwataka Watanzania watambue kwamba: "***Tanganyika ilikuwa ni nchi changa***". Tangu ilipojikomboa kutoka katika makucha ya Wakoloni ilikuwa haina maendeleo ya aina yoyote. Kwa hivyo, njia pekee waliyoibaini wananchi wa wakati huo ni kuwa na umoja thabiti jambo ambalo Wakoloni pia waliliona kwamba lingekuwa hatari kwao. Fauka ya hayo, Mwalimu aliwakumbusha kwamba: "(Enzi za ukoloni – Watanganyika) ***watu wake waliwekwa katika sehemu inayoitwa moja na Wajerumani. Wamakonde na Wazanaki hawakuwa wamoja. Waliwekwa pamoja na Wajerumani ili watawaliwe"***; akimaanisha kwamba Ujerumani ilikuwa ni wawatambue Watanganyika kwa makabila yao ili waweze kuwatawala kwa urahisi. Watanganyika waliishitukia hila hiyo na ikawa ni zifanyike jitihada za kuifuta sumu hiyo kwa kuwa na umoja uliomadhubuti zaidi.

Kwa ufahima zaidi, Mwalimu aliwakumbusha kwamba "***Jitihada ya kuwafanya (Watanganyika) wawe pamoja na kuanza kusema "Ninyi ni Wamoja" haikufanywa na Wajerumani: Kwa sababu Wajerumani ambao wangeweza kusema "Ninyi ni Wamoja" lengo lao halikuwa ni kujenga umoja. Wajerumani walichoweza kusema ni kwamba 'Ninyi ni Tofauti', Ninyi ni Tofauti! Ili waendelee kuwatawala".*** Ufahima huo uliwapelekea Watanganyika kuimarisha chama chao "TANU" ambapo miongoni mwa shabaha zake zikiwa ni kuufuta ukabila chini ya mbiu ya "***Sahau Ukabila!***" Kwa hivyo, kuifanya mbinu ya Wakoloni kuwa pindupindu, Watanganyika wakajikomboa kutoka katika makucha ya Wakoloni mwaka 1961 na hatimaye wakawashawishi wenzao Wazanzibari kuungana; na kuzalisha Jamhuri ya Muungano Watanzania mwaka 1964. Hivyo, kumbukizi hizi za Mwalimu kuhusu mtagusano wa madhila waliyokumbana nayo Watanzania enzi za ukoloni ni uamsho kwa Watanzania wa leo ili watambue kwamba hawanabudi kumakinika hasa

katika mpwito wa maisha ya muungano wao. Aidha, aliwataka waitambue azali ya udugu wao na waudumishe hata kwa vizazi vijavyo.

**Tafsida kengeushi na takriri**: "*... mtu mwenye akili hawezi kufikiri Uzanzibari ni ufahari: hana akili…. Zanzibar wanaweza wakajitenga hivi kwa ujinga, kwa ulevi, lakini kwa ujinga, hasa kwa viongozi wao".* (UK 9:4: N)

Kauli hizi alizitoa Mwalimu Nyerere pale ilipotokea baadhi ya Watanzania wakiwashawishi wenzao wasiukubali Muungano. Mwalimu aliuona ushawishi wa namna hii - ni kana kwamba washawishi hawafikirii madhara na hatima yake. Ambapo madhara yake si tu kwamba ni migogoro na husda kutokana na wengine kuhisi kwamba wametengwa lakini pengine waweza kupelekea mauaji yasiyokuwa na tiba mbadala. Kwayo nia ya mkengeuko kwa mrudiorudio wa maneno *'**ujinga' na 'ulevi'*** **–** ni kuwazindua waelewe kwamba mtu mwenye hali hizo hawezi kuyafanya mambo kwa busara. Hata kama ni kiongozi, si rahisi akaweza kutoa maamuzi faafu kwa wengine.

Mwalimu alipobaini kwamba baadhi ya viongozi ni wahusika katika kuwashawishi wengine wasiukubali Muungano alisema: ikiwa hivyo basi ni ***wajinga na walevi***. Huo ni msisitizo uliokusudiwa kuwafanya Watanzania wapuuze wale wote wanaotaka kuwatenganisha kwani nia yao (hao wasiopenda Muungano) ni kuwatenganisha wananchi ili malengo yao yaweze kufanikiwa kwa urahisi. Sumu hiyo ni sawa na ile ya Wakoloni - pindi walipobaini kwamba wasingeweza kuyafikia malengo yao ikiwa Watanzania wangeendeleza umoja wao wa tangu azali na ndiyo maana wakawagawa katika makabila kwa kuwafanya wajitambue kwa makabila yao ama kwa maeneo yao; wasishirikiane ili iwe ni uhasama baina yao na kwa hivyo wautumie mwanya huo kupenyeza matakwa yao. Hivyo, uwazi wa kauli hizi ni udhihirisho wa mguso wa nafsi kwa wapenda amani dhidi ya wanafiki (wenye kutaka kuwatenganisha Watanzania). Kwa hivyo, matamshi hayo pia yanakuwa na nguvu za kuwashawishi Watanzania wasiwafumbie macho (wanafiki) hata kidogo bali waendeleze umoja wao. Kupitia umoja huo, wanaweza kuhakikisha kuwa wanawatokomeza maadui hao ili Muungano wao uendelee.

**Tashbiha na takriri**: "*Dhambi ya ubaguzi ukisha kuitenda inaendelea: ni kama ukila nyama ya mtu utaendelea kuila*". (UK 10:3: N).

Kauli hizi ni mwendelezo wa tahadhari ya Mwalimu kwa wale waliokuwa wanaukataa Muungano. Neno ***dhambi*** ni malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu; anayoyatoa kwa viumbe

wake wanaomkosea kwa kuacha kutenda mema hapa duniani na kwa hivyo akiahidi kuwaadhibu - ama hapahapa duniani au katika maisha ya baada ya kufa kwao. Hivyo, kiimani viumbe wote akiwemo mwanadamu wanatakiwa kumtii Mwenyezi Mungu kwa kila alilowaamrisha ili maisha yao hapa duniani na baada ya mauko yao yawe ni ya amani na furaha.

Kwa mwegemo wa muktadha wa uvunjivu wa Muungano (Umoja), ndipo Mwalimu akawafananisha wale wote wenye kuhusika katika kuwashawishi wengine wauvunje Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar kwamba, ***ni sawa na kula nyama ya mtu***. Kwa msisitizo wenye uchungu wa moyoni alisema: ***ukila nyama ya mtu utaendelea kuila*** **-** kumaanisha kwamba, ikiwa miongoni mwa Watanzania watahusika katika kuuvunja Muungano haina maana kwamba wao watasalimika. Hata kama watu watatengana kutokana na fitina zao, kutengana huko kutajenga uhasama, ambapo kila tapo litajinadi kwa ubora ama likihisi kwamba linaonewa na tapo lingine lililotengana nalo. Hali hii husababisha migogoro na hata mauaji ambapo kila mmoja atahisi anaguswa kwa namna moja au nyingine; hasa ikiaminiwa kwamba mwanadamu silka na asili yake ni moja.  Kwa vile binadamu wote walitokana na Nabii Adam kila mmoja atakuwa anahusiana na mwingine kidugu. Ndiyo maana Mwalimu akasema: ***"dhambi ya ubaguzi ni sawa na kula nyama ya mtu; na kwamba mwenye desturi hiyo daima hawezi kuiacha***; ni dhulma ambayo itaigusa jamii nzima. Kila mmoja atajibu mashambulizi ima kwa kuitetea haki yake au ya ndugu yake - hadi kufikia tone la damu ya mtu wa mwisho.

Hivyo, Watanzania wanatahadharishwa wasihusike kwa kutenda dhambi hiyo ya kuwabaguwa ndugu zao hata ikawa ni wauvunje Muungano. Watambue kwamba Mwenyezi Mungu hatawahurumia kwa kosa hilo la kuwafitinisha wengine. Badala yake anawataka wasimame kidete katika kupambana na wanafiki wanaowachonganisha ili wadumishe umoja na amani ya tangu enzi za umajumui waishi kwa furaha na mwisho wao uwe mwema.

**Maswali ya kibalagha na ukatizaji wa maneno**: "*... Hambaki. Kwani mtasemaje? Mtakuwa mmesha sema sababu ya kuwafanya 'wale ni wao' na 'ninyi ni ninyi', 'wao' vipi ... ; halafu mbaki ninyi?*". (UK 11:2: N).

Haya ni maonyo ya Mwalimu kwa Watanzania watambue kwamba suala la ubaguzi ni baya, hatma yake ni kuendeleza visasi hadi tone la damu ya mtu wa mwisho. Kauli "***hambaki"*** ni yenye fahiwa ya kutahadharisha kwa lililotendwa kwamba lilikuwa halipaswi kutendwa. Ambapo kwa mfungamano wa maneno **"kwani mtasemaje?"** ni kuonyesha msisitizo wa

mkengeuko huo uliotendwa kwamba hautakuwa na simile tena. Madhara yake yakishatokea hakuna jema tena. Ni sawa na maji yaliyokwisha mwagika hayazoleki tena. Fauka ya hayo, maneno: ***"Mtakuwa mmesha sema sababu ya kuwafanya 'wale ni wao' na 'ninyi ni ninyi', 'wao' vipi …; halafu mbaki ninyi?"*** - Yametumika kudhihirisha uzito wa kosa na ni kielelezo cha ufafanuzi kwamba ubaguzi ni katika madhambi makumbwa ambayo hayavumiliki kwa wanadamu wema mbele ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, ushawishi wa Mwalimu ni tahadhari na wito kwa kila Mtanzania; na pengine kwa yeyote mpenda amani. Wasijaribu kutopea katika maswala ya kuwabagua wengine ima kwa dini, kabila au kieneo. Aliwataka watambue kwamba madhila yake hayana kikomo. Ni mfano wa jambo baya; ambapo Mwalimu akiufananisha ubaya huo sawa na **"*kula nyama ya mtu*"** kwa ufahima wake kwamba "***Ukila nyama ya mtu utaendelea kuila***". Si tu kwamba hali hiyo hupelekea ugomvi, na hata kulipizana visasi. Pia hupelekea mauaji ambayo ni endelevu. Upande wa waliouliwa mtu wao nao pia watalipiza kwa kumuua mtu wa upande ule uliouwa. Na ndiyo ikawa ni aseme: ***"Hambaki. Kwani mtasemaje?*** Mtakuwa mmesha sema sababu ya kuwafanya ***'wale ni wao' na 'ninyi ni ninyi', 'wao' vipi … ; halafu mbaki ninyi?"*** kwayo ni muhali na siyo silka ya mwanadamu kufanyiwa dhulma halafu akae kimya. Bali huiona haki si ya kuombwa tena; bali ni aitafute kwa nguvu zote hata ikibidi kwa kujitoa muhanga.

Fauka ya hayo, taswira ya ushawishi wake (Mwalimu) pia ni kuwaonya Watanzania wasithubutu kwa hoja yoyote ile kuhusu kuunakshi ubaguzi na watambue kwamba Mwenyezi Mungu atakaposhusha adhabu yake haitachagua; bali jamii nzima itaangamia na wafitini wakiwemo ndani yake.

**Tashtiti, uchimuzi na takriri**: *"Serikali zetu zimekubaliana kuleta umoja kwa sababu moja tu. Umoja ni nguvu ya nchi zetu na ni nguvu ya Afrika. Hapana sababu nyingine. Sababu za Umoja wa Afrika ziko Afrika. Hazitoki Moscow au Washngton. Wale wanaojribu kuona vita vyao na ugonvi wao katika kila jitihada ya Afrika kuungana wanaitukana Afrika. AFRIKA IMEKUWA AFRIKA INA UTASHI WAKE. Hatuundi umoja huu ili tusaidie imani fulani ya siasa za dunia hii. Tunaunda Umoja wetu kwa sababu ya kuimarisha bara letu na hasa sehemu hii ya bara letu."* (UK 4:3: MTU)

Kauli hii ni ya kuwazindua Watanzania na pengine Wafrika kwa ujumla watambue kwamba wanapoungana na kuwa kitu kimoja, watapata nguvu ya kijumla kiasi cha kuwawezesha kuwa na sauti ya pamoja na yenye nguvu mbele ya bara lao la Afrika. Wakiwa mtu mmoja mmoja haitakuwa rahisi si tu katika kupata maamuzi yenye mashiko lakini pia kukubalika

mbele ya wengine. Ndio sababu Mwalimu akasema tena: *"**Serikali zetu zimekubaliana kuleta umoja kwa sababu moja tu. Umoja ni nguvu ya nchi zetu na ni nguvu ya Afrika.*** Kumaanisha kwamba, ushawishi wake ulikuwa ni wakuwataka Watanzania na Wafrika kwa pamoja watambue kwamba maendeleo ya nchi zao na Afrika kwa ujumla yataletwa na wao wenyewe na siyo kwa kutegemea misaada na ama ufadhili; jambo ambalo ni udhalili, na kushikiwa akili katika kila maamuzi ya msingi. Na kwa msisitizo wa kuifuta sumu hiyo ya utegemezi alisema: ***Sababu za Umoja wa Afrika ziko Afrika. Hazitoki Moscow au Washington*"**.

Mwalimu aliwataka watanzania wajiamini na wawe kifua mbele kama udhihirisho kwa wale wote wasiowatakia mema – watambue kwamba si tu **"*Watanzania wamekwisha jipanga na wana umoja thabiti;*** *lakini* ***AFRIKA IMEKUWA AFRIKA NA INA UTASHI WAKE"***. Kumaanisha madui ni watambue kwamba uimara wa nchi ya Tanzania ni kurunzi ya bara la Afrika; Waafrika wamekwisha amua kuwa kitu kimoja na kamwe hawatatikiswa tena; daima wamekwisha itakadi kwamba umoja ndiyo njia pekee ya kuwakomboa kutoka katika unyonge na udhalili ima kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Ni imani yao kwamba, "umoja ni nguvu - Waafrika wakiamua kuungana wanaweza; na sauti yao itasikika kimataifa na kuwa dira ya maongozi mema.

**Methali**: "*Ukiona vinaelea vimeundwa.*" (UK 3:1: MMT)

Kauli hii inamaanisha kwamba, vizuri vinavyowavutia watu machoni ni vyema watu wakatambua kwamba vimefanyiwa juhudi kubwa hata vikaweza kuonekana ni vya mafanikio na vyenye kuwavutia watu machoni. Kwa muktadha wa umoja na amani kwa Watanzania; utumizi huo wa lugha ni tathmini ya Mwalimu Nyerere kwa jinsi walimwengu wanavyoisawiri Tanzania kwa umoja na amani; na ndiposa (Mwalimu) akiwataka watambue kwamba, zilifanyika jitihada si haba ndiposa yakafikiwa mafanikio hayo - ya Watanzania kuwa ni wamoja na wenye amani.

**Tashbiha; takriri na maswali ya kibalagha**: "*Nchi yetu ni kama nyumba mpya. Nchi changa ni sawa sawa na nyumba mpya* (UK 7:2: N); … *Tanzania imetikiswa; Tanzania ni hivyo hivyo. Tulijenga nchi mpya imara, ni imara tu na uimara wake ulikuwa unasifiwa sifiwa sana. Lakini tumetikiswa na nyufa tumeziona….* (UK 8:2: N); S*asa ni nyufa gani hizo?* (UK 9:2: N)

Kauli: ***Nchi yetu ni kama nyumba mpya*** humaanisha kwamba inapendeza na inaonekana vizuri. Inavutia machoni mwa watu hususani kwa mpangilio wake wa tangu msingi na kwa nakshi zilizopambwa kwa maana ya mpangilio uliopelekea hata kutambulika kuwa ni nchi huru. Na aliposema: ***Nchi changa ni sawa sawa na nyumba mpya.*** Huu ni mtagusano wa fikra kuhusu uchanga wa nchi kuwa sawa na nyumba mpya. hapa fahiwa yake ni kuwazindua Watanzania watambue kwamba nchi ya Tanzania haina muda mrefu tangu ijikomboe kutoka katika makucha ya Wakoloni. Ingali bado ni changa katika kuinukia kiuchumi na kisiasa ikilinganishwa na nchi zingine zisizo za ulimwengu wa tatu. Aidha kulingana na muktadha huo pia Mwalimu aliwataka Watanzania watambue kwamba taifa lao si tu kwamba linahitaji ulinzi lakini litajengwa na wao wenyewe.

Kutokana na uchanga wa nchi ya Tanzania kiuchumi na kisiasa aliwataka Watanzania watahadhari kupotoshwa kwani wakikosa umoja basi watakuwa wamefungua mianya ya maadui ima wa ndani au wa nje watakayoitumia kuwatenganisha. Fauka ya hayo Mwalimu aliusawiri uchanga huo kama matatizo yaliyochimuka ambapo kwa uoni wake ilikuwa ni yafanyiwe hima ya kuyazuia yasiendelee. Takriri neno, sitiara na maswali ya kibalagha aliyabainisha matatizo hayo moja baada ya jingine kwa kusema… ***Tanzania imetikiswa*** (UK 8:2: N). Na akauliza tena … ***Sasa ni nyufa gani hizo?*** (UK 9:2: N); na kwa hivyo kumpelekea kuzitaja nyufa hizo (matatizo hayo) kama ifuatavyo:

(i) ***Muungano*** - ambapo baadhi ya Watanzania walikuwa wanawashawishi wenzi wao wasiukubali Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibarna badala yake uvunjike ili kuwa na nchi mbili. (UK 9 – 12: N)

(ii) ***Kupuuza na Kutokujali Katiba*** - Yaani viongozi kuendesha mambo bila kujali Katiba ya nchi. (UK 12 – 14: N)

(iii) ***Kuendesha mambo bila kujali sheria*** (UK 14 – 15: N)

(iv) ***Rushwa*** – Yaani viongozi kulegeza ukamba katika kukemea suala la rushwa. Kiasi kwamba ikaonekana kutendwa pasi na aibu yoyote (UK 15 – 22: N)

(v) ***Ukabila na Udini*** - kuchukuliwa kama kigezo cha umaarufu wa mtu hususan katika maswala ya uchaguzi wa viongozi wa nchi (UK 22 – 30: N)

Hivyo, kwa hima, Mwalimu aliwashawishi Watanzania wazinduke na wayatambue matatizo yaliyoikumba nchi yao. Wafanye jitihada za kuyazuia yasiendelee. Vinginevyo watambue kwamba nchi yao itameguka vipande vipade (hawatakuwa na umoja tena) na kwamba amani iliyowagharimu kwa muda mrefu itatoweka na iwe muhali kuirejesha tena.

### 4.4.2 Maudhui kuhusu Kupuuza na kutokuijali Katiba

Kulingana na tathmini ya Mwalimu Nyerere mara baada ya kung'atuka kwake alibaini kwamba uongozi ulioshika hatamu za kuliongoza taifa la Tanzania haukuwa madhubuti katika kuilinda na kuisimamia katiba ya nchi. Kwa uoni huo aliwataka viongozi wajirudi hasa ikisadifu kwamba miongoni mwa sheria zilizomo katika katiba ya nchi ndizo zilizowaweka madarakani. Wakadhalika, aliwazinda watanzania watambue kwamba nikatika utaratibu wa Mwenyezi Mungu wa kuwataka viumbe wake katika jamii zao wawachague miongoni mwao kuwa viongozi; wakuwaongoza wengine. Lakini watambue kwamba, hawataongoza kwa matakwa yao bali kwa sheria zilizokubaliwa na jamii husika.

Fauka ya hayo, aliwataka Watanzania watambue kwamba, sheria zilizokubaliwa ziiongoze jamii zikiwekwa kando (zikiwa hazitekelezwi) malengo ya nchi (jamii) kamwe hayatofikiwa. Nchi itakuwa haitawaliki; kila mtu atajichukulia sheria mikononi mwake. Wababe watataka wazifaidi amali za umma kibabe; na wanyonge wataendelea kunyong'onyea na huku wakifanywa watumwa wa kuwanufaisha wababe katika ardhi yao. Hivyo, ulikuwa ni wito wake kwa Watanzania wazinduke; waitambue dhima yao; na wailinde katiba ya nchi kwa faida ya umma.

#### 4.4.2.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Kupuuza na kutokuijali Katiba

**Takriri**: "*Rais tunayemtaka ni Mtanzania. Huwezi kumpata Rais Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika. Anatoka ama Zanzibar ama Tanganyika, lakini hatumchagui kwa sababu ya Uzanzibari wake, hatumchagui kwa sababu ya Utanganyika wake. Na, akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai. …"* (UK 12:3/3:1: N)

Nia ya Mwalimu kwa kauli hizi ilikuwa ni kuwataka Watanzania waitekeleze na kuisimamia katiba ya nchi yao pasi na kumhofia yeyote - kwa wadhifa wake, kwa umaarufu wake au kwa eneo analotokea. Chembelecho uongozi kwa Watanzania; Mwalimu alisema: ***Huwezi kumpata Rais Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika***. Kwa ufahima kwamba maadam Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, yeyote mwenye sifa ya kuwa kiongozi wa Watanzania anaweza kutokea sehemu yoyote kati ya hizo mbili. Almuhimu ikiwa ana sifa za uongozi bora. Kwa takriri neno alisema: "(Kiongozi wa Watanzania) ... ***hatumchagui kwa sababu ya Uzanzibari wake, hatumchagui kwa sababu ya Utanganyika wake. Na, akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai.*** Nia yake ni kukemea swala zima la ubaguzi hususani wa kieneo. Na pia

akiwatahadharisha Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanailinda na kuiheshimu katiba ya nchi kikamilifu. Viongozi wachaguliwe kwa mujubu wa katiba; na waitumie katika maongozi ya nchi kama inavyoelekeza na siyo vinginevyo. Na ikiwa kiongozi atakwenda kinyume na inavyoelekeza katiba ya nchi; kwa maoni ya Mwalimu mtu wa namna hii ***hafai*** kuchaguliwa katika wadhifa wowote wa kiutawala.

**Takriri na tashhisi**: "*... rais wa nchi yetu anachaguliwa kutokana na katiba ya Tannzania. Na akichaguliwa, anaapishwa. Kama ni Mkristu, kwa Bibilia, kama ni Mwislamu, kwa Kuruani. Hatujachagua mtu asiyeamini Mungu, lakini tukimchagua, tutatafuta utaratibu wa kumuapisha. Ataapa! Hata asiyekuwa muumini, tutamwapisha kwamba atailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania. Asipoilinda, tunajua ni msaliti. Tutamwapisha. Ataapa! lazima kabisa, hata kama si muumini. Kwa mujibu wa katiba yetu sisi, si lazima mtu awe anamwamini Mungu kuwa Rais, hata kidogo. Lakini, tutakuapisha! Umechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Unaapa kulinda. Ataapa kwa huyo Mungu wake au akili yake anayoijua; lakini atatuapia. Ataapa kusudi tuweze kumshitaki kama akikiuka.*" (UK 13:3 / 14:1: N)

Neno "***kuapa***" ni mtu kuiweka roho yake rehani - kwa Mwenyezi Mungu (kwa kujishitaki kwa Mwenyezi Mungu) kwamba ikiwa atatenda kinyume na ukweli ulivyotakikana; Mwenyezi Mungu amlaani kwa kiapo chake; ampe adhabu ima kwa alivyojielekeza au kwa atakavyoamua mwenyewe Mwenyezi Mungu. Fauka ya muktadha wa takriri hii, kiapo hicho ni mtawalio wa nafsi katika kuonyesha uzito wa jukumu la uraisi, kwamba ni sharti rais ashike hatamu ya kuiongoza nchi kwa kufuata sheria zilizowekwa na sio kwa matashi binafsi. Hivyo, takriri neno "***kuapa***" pia ni changamoto kwa mtu na maamuzi yake katika maswala yanayohusu uongozi - kwamba sijambo rahisi bali ni zito na lenye hukumu ima kutoka kwa wanadamu wenyewe kwa wenyewe au kutoka kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Na hii ndiyo kusema; Mwalimu alikuwa akiwashawishi Watazania watambue kwamba uongozi ni dhima inayohitaji umakinifu mkubwa na sio kwa mtu kuuonea gere kiasi cha hata kutoa hongo ili apate kuingia madarakani.

**Takriri na tashhisi**: *Mtu ambaye hawezi kuitetea Katiba ya nchi yetu, hawezi kuilinda, hawezi kuisimamia baada ya kiapo, hatufai! aende akaendeshe shamba lake huko. Hawezi kuwa Rais wa nchi yetu. Tunamchagua kwa mujibu wa Katiba, tunamwapisha kuwa Katiba ailinde, aitetee kwa moyo kabisa kabisa bila woga. Hawezi, hatumtaki kuwa kiongozi wetu. Anaweza kuwa rafiki yetu sana, anaweza kuwa kabla hajafika kwenye vikao vyetu hatuwezi*

*kunywa chai, brand au wiski, lakini hiyo ni shauri nyingine. Lakini kwa Urais wa nchi, hatufai. ..."* (UK 13:3 / 14:1: N)

Hizi ni kauli zinazodhihirisha ya kwamba, Mwalimu alipata tashwishi kuiona katiba ya Tanzania inapuuzwa hasa na viongozi ilhali ndio mhimili mkuu wa sheria zote katika nchi. Kwa kumbukizi za maongozi yake daima aliwaasa Watanzania watambue kwamba ulinzi na heshima ya nchi yao uko mikononi mwa Watanzania wenyewe. Hasa kwa kuithamini katiba ya nchi na kuifanya iwe ndio dira ya nchi kwa malengo yao yote. Kwa mwegemo huo, Mwalimu iliingiwa na simanzi hata ikawa ni asisitize tena kwa kuseme: *"**Mtu ambaye hawezi kuitetea Katiba ya nchi yetu, hawezi kuilinda, hawezi kuisimamia baada ya kiapo, hatufai!"*** **-** ni maneno yenye mkururo wa fikra, yenye kuonyesha masikitiko kuhusu ukiukwaji wa katiba ya nchi. Ni tafakuri ya mneni ya kana kwamba anahisi pasi na kuyarudiarudia kwa walengwa anaowataka waupate ujumbe wake kuhusu kutokuiheshimu katiba ya nchi - hawatokongwa moyoni ipasavyo.

Mwalimu anaonekana akitakriri fikra zake kwa kuwashangaa viongozi waliopewa mamlaka ya kuliongoza taifa la Tanzania halafu ikawa hawautambui wajibu wao kisheria; tena ndani ya sheria ambazo ndizo zilizotumiwa kuwavyaza nyadhifa za uongozi walizonazo. Alimwona kiongozi wa namna hiyo (asiye ilinda katiba ya nchi) ni bora "***aende akaendeshe shamba lake huko"*** akimaanisha kwamba, kiongozi asiye na sifa za uongozi (anayeongoza nchi kwa matakwa yake); ni bora aachie ngazi (wadhifa) aliopewa na wananchi; aende akajishughulishe na mambo yake binafsi. Pasi na kuchelea alisema (kiongozi wa namna hiyo) "***hatufai"*** kwa maana ya Watanzania watambue ya kwamba ni kiongozi asiye na msaada wowote kwa umma. Akionewa haya, akaendelea kuwa madarakani, ni kuitwisha serikali mzigo usiokuwa na manufaa yeyote hasa ikisadifu kwamba anahitaji kulipwa mshahara ilahali utendaji wake hauonekani na hana manufaa yeyote kwa jamii zaidi ya maslahi yake mwenyewe. Hivyo, ulikuwa ni wito wa Mwalimu kwa viongozi kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinatekelezwa kikamilifu ili haki ziweze kuwafikia raia wote kwa uadilifu.

### 4.4.3 Maudhui kuhusu Umuhimu wa Sheria

Suala la kuendesha mambo bila kujali sheria za nchi ni katika matatizo ambayo Mwalimu Nyerere aliyabaini mara baada ya kung'atuka kwake. Safu ya uongozi uliokuwa unaiunda serikali kuu ulisawirika ya kwamba haikuwa ikizingatia sheria katika usimamizi wa malengo yaliyoihusu jamii ya Watanzania. Kwa maoni yake mambo yaliendeshwa kiholela kiasi cha kuwafanya wananchi wasijue mwelekeo wa machweo na mawiyo ya maisha yao. Kutokana

na ufahima wa Mwalimu, kutokutekelezwa kwa sheria za nchi si tu kwamba huwapelekea wananchi wengi kukosa imani na viongozi wao; lakini pia serikali hupoteza dira katika kusimamia malengo ya nchi. Hivyo, maadui wa ndani na nje ya nchi kuitumia fursa hiyo kwa kufanya lolote walitakalo. Hali hii huipelekea nchi isitawalike kwa matakwa ya raia wake na badala yake wananchi wa kipato cha chini ambao ndio wengi, watafanywa ngazi ya kuyawazesha matakwa ya wachache wenye nguvu - kuzihodhi amali za nchi pasi na kigugumizi kutokana na sheria za nchi kuwa chapwa.

#### 4.4.3.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Umuhimu wa Sheria

**Swali la kibalagha na Takriri**: "*... Nchi zinaongozwa na watu, kumbe zinaongozwa na nani? Hakuna malaika. Ndivyo alivyotaka Mungu. Tujiongoze wenyewe: sisi hawa hawa. Lakini haziongozwi na akili za mtu. Zinaongozwa kutokana na sheria.*" (UK 14:2: N).

Matamko hayo yamebeba maana nzito ambayo imekusudiwa kuwazindua wananchi wa Tanzania. Ni uamsho wa Mwalimu kwa Watanzania watambue wajibu wao kama wanadamu hapa duniani. Kwamba mbali na ushirikiano katika kuyatenda mambo ya kuwafaa katika maisha yao hawanabudi kuwa na kiongozi baina yao. Ndiyo maana akasema: **" ... *Nchi zinaongozwa na watu, kumbe zinaongozwa na nani?*** Kumaanisha kwamba, Watanzania ni watambue kwamba hakuna mtu au kiumbe chochote hata mfano wa "***Malaika***" atakayekuja kuwaongozea nchi yao. Kwa mwegemo huo akasisitiza tena kwa kusema **"*hakuna malaika*"** akimaanisha kwamba "***Malaika***" ni viumbe wenye sifa ya utukufu, wasiomuasi Mola wao kwa lile waamrishwalo, hawamkosei katika utekelezaji wa majukumu yao tofauti na mwanadamu ambaye anasifa ya kokosea na uhiari wa kuifuata njia ya heri au shari.

Mwalimu aliwataka Watanzania watambue kwamba si katika utaratibu wa Mwenyezi Mungu kuwaagiza malaika duniani kwa ajili ya kuwatendea wanadamu majukumu yao ya kuwaongozea katika pilikapilika zao za kimaisha - kama walivyotakiwa na muumba wao ili waweze kuyafikia malengo ya maisha yao hapa duniani. Kwa uzito huo, Mwalimu aliwasisitiza tena na tena kwa kusema: ***"ni sisi hawa hawa"*** akimaanisha ni wanadamu (Watanzania) wenye jukumu hilo la kuiongoza nchi yao wenyewe. [Na kwamba wasimtafute Mwenyezi Mungu muhali ikiwa watabweteka kwa kutokutekeleza wajibu wao hapa duniani wasidhani kwamba Mwenyezi Mungu atawatuma malaika kuja kuwatendea majukumu yao. La hasha!] Ni wanadamu (Watanzania) wenyewe wajifunge kibwebwe wazitumie neema walizojaliwa na Mungu wao kama vile akili, afya, ukamilifu wa viungo na mazingira faafu washirikiane kwa pamoja katika kuyatenda majukumu yao ambapo kwa ufanisi wake ni

waione ni dhima kumpata kiongozi wa kuwatangulia katika maamuzi na utendaji wa mambo yao kijamii.

Mwalimu aliendelea kutomelea kwa kuwatanabahisha Watanzania watambue kwamba mwanadamu si kitu fahari mbele ya Mwenyezi Mungu bali ni dhaifu na mwenye elimu kidogo tu! - aliyotunukiwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, hawezi kuyaongoza mambo bila ya kuzingatia sheria. Ndiyo maana akasemat ena: … ***(Nchi) Lakini haziongozwi na akili za mtu. Zinaongozwa kutokana na sheria."*** Yaani wanapomtafuta kiongozi ni watambue kwamba ni mwanadamu mwenzao ambaye ana madhaifu kama wao. Hivyo, ni lazima kiongozi awe na tahadhari, asiongoze nchi kutokana na utashi wa nafsi yake kwa sababu akifanya hivyo ataitumbukiza nchi katika maangamizi na badala yake anapaswa kushikamana na sheria za nchi zilizowekwa ili kulinda maslahi ya wananchi na taifa zima kwa ujumla.

Chembelecho utii wa sheria za nchi, Mwalimu iliwazindua Watanzania kuhusu uongozi mwema. Matumizi ya balagha kwa jinsi yalivyotumika yalikusudiwa kuzivuta fikra za hadhira kuhusu makemevu ya viongozi kuongoza pasi na kuzingatia sheria za nchi. Hivyo basi, watanzania walishawishiwa watambue kwamba wana dhima ya kuhakikisha kila unapowadia uchaguzi wa viongozi – wahusike kikamilifu katika kumpata kiongozi mwema na mwenye kufuata sheria zilizowekwa kwa minajili ya kudumisha umoja, upendo na amani miongoni mwao.

**Tafsida kengeushi, sentensi changamano na ambatano**: "*... . Haiwezekani mtu anapata ushauri kwa mkewe, kesho tunakuta jambo fulani. Eh! ... Hamwezi kutawaliwa hamtambui na hata hamjui mkewe kesho atamwambia nini!"* (UK 14:3/15:1: N).

Ijapokuwa kunauwezekano kiongozi yeyote kupata ushauri kutoka kwa mke wake, jambo lisilokubalika kwa mtazamo wa Mwalimu ni ushauri unao kinzana na katiba. Kusema haiwezekani na hali inawezekana ni matumizi ya lugha yanayolenga kuonyesha kwamba yeye haridhiki na jinsi serikali inavyoendeshwa. Kwa hiyo kuruhusu hali hiyo kuendelea ni sawa na kuthubutu kupotoshwa na tashwishi za mwanamke ambazo zinaweza kuiangamiza jamii. Tamko hilo lilitolewa kwa nia ya kuwashawishi Watanzania kukataa kuongozwa na viongozi wasio kuwa na msimamo hata wakapuuza sheria za nchi.

Kauli "…***hamwezi kutawaliwa hamtambui na hata hamjui mkewe kesho atamwambia nini!***" – Ni udhihirisho wa udhaifu katika jamii ambapo mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu na asiye na mamlaka mbele ya wanaume katika kutoa maamuzi mazito

yanayoihusu jamii. Kulingana na jinsi uongozi wa Tanzania ulivyosawiriwa na Mwalimu inaelekea kwamba nchi ilikuwa imekosa dira kutokana na ukiukwaji wa sheria. Ndiyo maana zikamchomoka fikra kengeushi kuonyesha jinsi alivyoguswa moyoni. Hii ni njia mojawapo ya kuwakemea viongozi ambao kwa maoni yake ni wazembe katika majukumu waliyokabidhiwa na raia wao hata ikawa ni wazikiuke sheria zilizomo katika katiba ya nchi kwa matashi binafsi. Kwa mkengeuko huo, Mwalimu aliwashawishi Watanzania wote kuhakikisha kwamba kila unapowadia uchaguzi Watanzania hawana budi kushiriki katika uchaguzi; na wawe wamakinifu ili wawapate viongozi wema, waadilifu na wenye kufuata sheria za nchi kwa manufaa ya jamii na taifa zima kwa ujumla.

### 4.4.4 Maudhui kuhusu Rushwa

Rushwa ni katika maswala yaliyomkera Mwalimu katika kipindi cha maongozi yake na hata baada ya kung'atuka kwake. Ni miongoni mwa matatizo ambayo Mwalimu aliyavalia njuga kwa hima ya kuyatokomeza. Ingawa hivyo, kila uchao "***rushwa***" ilionekana kuota mizizi na ndio ikawa daima akijiuliza kwamba, ni kwa jinsi gani watu wanaziweka roho zao rehani kwa kuiuza au kuinunua "***haki***" - kwa kutumia rushwa. Hata iwe viongozi wa nchi nao wahusike (katika ulaji rushwa) ilhali sheria kuhusu makataa yake zingali mikononi mwao! Kwa kumbukizi za Mwalimu Nyerere, ilikuwa ni imani yake kwamba tatizo la Watanzania kuhusika katika rushwa lingekuwa ni masimulizi kwa enzi za maongozi yake na sio baada ya kung'atuka kwake. Enzi za maongozi yake (Mwalimu Nyerere) tatizo la rushwa lilipokuwa limeshamiri - walifanya jitihada za kulikomesha kwa haraka.

Mbali na sheria zilizokuwa zikitekelezwa na mahakama, viongozi wa chama na serikali, tatazo la rushwa liliundiwa kanuni kupitia chama cha TANU na baadaye CCM Kwa ilani ya kumtaka kila mtu akiri kwa dhati ya moyo wake kwamba: "***Rushwa ni adui wa haki. Sitatoa wala sitapokea rushwa***" - waliunda sheria za utekelezwaji wake. Sheria ilikuwa baada ya mahakama kuthibitisha kwamba mtuhumiwa kala au kapokea rushwa, mtuhumiwa alipewa kifungo cha miaka miwili na viboko kumi na viwili wakati wa kuingia na kumi na viwili wakati wa kutoka. Iliaminiwa kwamba, viboko kwa mtu mzima na hasa kwa mwanamume ilikuwa ni aibu. Akitendewa hivyo, mbele ya familia yake itakuwa ni soni (aibu) kwake na kwa familia yake. Hata wanapotangamana naye baada ya kumaliza kifungo chake, fedheha ya matendo yake yalionekana yakiendelea kumwandama. Kwani angeisuta nafsi yake kwa kumtumbukiza katika uovu wa “rushwa”. Suala la rushwa enzi za maongozi ya Mwalimu; lilikuwa ni limulikwe katika nyanja zote za maisha ya Mtanzania. Kila Mtanzania ikawa ni

ajihadhari kwa rushwa - ima kwa kuitoa au kwa kuipokea. Na ndiposa Mwalimu akiliona tatizo la rushwa enzi za maongozi yake lilikuwa na ahueni tofauti na siku za usoni baada ya kung'atuka kwake. Kwa hivyo, changamoto ya Mwalimu kwa Watanzania ikawa ni alikemee kwa matendo (tatizo la rushwa) bila ya kumuonea mtu yeyote haya; ima kwa wadhifa wake au kwa utaifa wake maadam athari yake inawaendea Watanzania**.**

**4.4.4.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Rushwa**

**Takriri na tashtiti**: " *... Tulitaka watu wajue tutakuwa wakali sana na wala rushwa ndani ya serikali na wale wanaotoa rushwa. Mwanzo kabisa wa kujitawala tulitaka kila mmoja ajue....*" (UK 15:3/16:1: N)

Usanjari wa takriri: (UK 15:3/16:1: N) ni utumizi wa lugha wenye udhihirisho wa maongozi ya Mwalimu Nyerere; ambapo kwa kumbukizi zake (Mwalimu) ni kwamba, silaha mojawapo waliyoitumia kuhusu ulaji rushwa enzi za maongozi yake ni pale walipoudhirishia umma wa Watanzania msimamo wa serikali mapema, mara tu baada ya kujikomboa kutoka katika makucha ya Wakoloni kwamba daima ***"viongozi wa serikali watakuwa wakali sana na wala rushwa"***. Msimamo ambao si tu kwamba ulikuwa ni wa kuwaonya Watanzania wasithubutu kujihusiaha na rushwa lakini umuhimu wa viongozi katika kuikemea rushwa. Kwa pamoja watambue kwamba serikali itakapowabaini hawatoipata salama. Nia na madhumuni ikiwa ni kuhakikisha kwamba kila mmoja katika jamii anaipata haki yake kwa wakati na kwa uadilifu.

**Tashhisi, takriri na uchanganyaji ndimi**: "*Tukapitisha sheria kwamba mtu akila rushwa, eh! Kiongozi wetu anakula rushwa: anayetoa, aliyepokea, wazanaki wanasema manzi ga nyanza ...*" (UK 15:3 / 16:1: N).

Hizi ni kumbukizi za Mwalimu enzi za maongozi yake; ambapo Watanzania wanazinduliwa wazisute nafsi zao – kwa leo yake suala la rushwa limeonekana ni la kawaida. Rushwa inatedwa bila ya aibu. Tofautu na enzi za maongozi ya Mwalimu ambapo ingawa ilikuwepo lakini kwa leo yake baada ya kung'atuka ilitia fora hata ikawa ni aikumbuke enzi zake. Kwa mshangao alisema: **"*eh! Kiongozi wetu anakula rushwa"***. Kumaanisha kwamba, ilikuwa ni muhali watu kujidhihirisha hadharani hasa kwa viongozi ilikuwa ni aibu kubwa zaidi. Viongozi ndio walioamua iwepo sheria ya kuchapwa viboko wakati wa kuingia na kutoka jela; na ulikuwa ni wito wa viongozi kwa pamoja kuhakikisha kwamba wanaisimamia sheria za nchi. Hivyo, kiongozi kuonekana ya kwamba ndiye mvunjaji wa sheria ilikuwa ni aibu zaidi kuliko raia wa kawaida. Na ndio leo yake ikishangaza si tu inatendwa hadharani; lakini na viongozi wakihusika na kuhusishwa bila ya hofu ya kumuonea nani aibu.

Mwalimu aliendeleza simanzi yake na kuishangaa Tanzania ya leo yake kwa kusema: ***“Manzi ganyanza”*** – maneno ambayo ni ya lugha ya Kizanaki kumaanisha kutomchelea yeyote kwa kosa alilotenda. Ambapo kwa kuhawilisha na tatizo la ***“rushwa”*** kwa enzi za maongozi yake (Mwalimu) – alikuwa akiudhihirishia umma kwamba, hakuna aliyehurumiwa madhali kabainika ima ni mtoaji, mpokeaji, ni kiongozi au si kiongozi ni raia au si raia Watanzania wote waliipata adhabu sawa: viboko kumi na viwili wakati wa kuingia jela na kumi na viwili wa kati wa kotoka; tena kwa mbiu kwamba akamuonyeshe mkewe (majeraha kwa ulaji rushwa wake). Ikiaminiwa kwamba adhabu hiyo inge mfunza kukataa kutoa au kuipokea rushwa. Na kwamba awe tayari kumfichua anayemshawishi kwa rushwa.

**Maswali ya kibalagha, tafsida kengeushi, uzungumzi nafsi na takriri neno**: *Safari moja, Mgiriki mmoja alipita pita anajitapatapa humu anasema "mimi serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwangu". Nikasema "mshenzi sana huyo. Serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwake? Anamfuko mpana kiasi gani?". ... ni kasema "huyo mshenzi anasema hivyo?". Nikajua anahonga watu. Hawezi kusema hivyo bila kuhonga watu lakini vigumu kumpata. Lakini nikaona, hata hivyo, nitamfundisha tu. Nikamtia ndani. Nikatiwa msukosuko hapa! "Mwalimu mwachie" ni kawaambia "simwachii, hana adabu" Mzee Kenyatta akaniletea ujumbe akisema "huyo mtu tunamfahamu, bwana mwachie" Nikasema "simwachii hata kidogo. Simwachii. Siwezi kumwachia, hana adabu, anasema serikali yangu yote iko mfukoni mwake! Simwachii hata kidogo ...*” (UK 17:2: N)

Kauli hizi, ni katika kumbukizi za Mwalimu Nyerere enzi za maongozi yake kwamba, walikuwa hawamchelei ye yote pindi ilipokuwa ikibainika kwamba amehusika katika kutoa au kupokea rushwa. Uongozi wa serikali haukuiachia mahakama peke yake kutoa hukumu. Mfano wa kumbukizi ni ule wa Mdiplomasia wa Kigiriki. Pindi alipodiriki kuutangazia umma kwamba serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwake. Kauli ambazo Mwalimu aliziona ni za kijeuri - hata akafikia kuuliza umma wa Watanzania kibalagha: *"….**Serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwake? Anamfuko mpana kiasi gani?**"* aliwashawishi Watanzania waitambue kwamba matamshi hayo ni ya kuwadharau Watanzania pamoja na uongozi wao ya kwamba si lolote si chochote mbele yake (huyo Mdiplomasia). Na ndiposa Mwalimu akiyaona matamshi ya namna hiyo ya kwamba ya na mizizi ya rushwa; kwani ni muhali kwa nchi kwa taswira ya ukubwa na vilivyomo ndani yake kusemwa kwamba mtu anaweza kuiweka nchi katika mfuko wake wa nguo anayovaa. Hata kama ingekuwa si katika mfuko wa mtu na nguo yake, lakini pia hakuna awezaye kushona mfuko wakuitosheleza nchi

kuingia ndani yake. Kwa hivyo (Mdiplomasia huyo) aliyatamka maneno hayo bila ya hofu kutokana na hongo alizokuwa akizitoa kwa viongozi kiasi cha kuamini kwamba hata akifanya kosa hatafanywa lolote.

Kwa matamshi hayo, nui ya Mwalimu ilikuwa ni kuwashawishi Watanzania wajiepushe na wajihadhari na walarushwa. Wawe wamakinifu kwa kila unapowadia wakati wa uchaguzi ili kuwapata viongozi wenye machungu wa kuiona rushwa kwamba ni tatizo. Wwawe wenye uwezo wa kuikemea na kuitokomeza popote itakapobainika katika maisha ya Mtanzania. Wahakikishe wanawapata viongozi wasio wala rushwa lakini wenye uwezo wa kuikemea rushwa bila ya kumuonea mtu yeyote aibu kwa jinsia, hali au hadhi yake. Kwa sifa kwamba awe ni kiongozi atakayethubutu kusema *"**Rushwa kwangu ni mwiko**"* na matendo yake pia yasadifu kauli hiyo, hata kama ni jamaa au rafiki zake wa karibu - wanamwingiza katika rushwa awe na uwezo wa kuwaambia kwa dhati kabisa kwamba: *"**Ikulu ni mahala patakatifu. Mimi sikuchaguliwa na wananchi wa Tanzania kuja kupageuza kuwa pango la walanguzi**"*. Kwa maana kauli iwe ni ya kutoka moyoni ili kuwafanya wamheshimu na wasirudie tena kumghilibu kwa rushwa.

**Takriri na maswali ya kibalagha** *hatukuwa tuna utani utani juu ya mambo haya ya rushwa, juu ya mambo haya ya rushwa hatukuwa na utani na mtu. Rushwa ni jambo la hatari kabisa, huwezi kuinunua haki. Haki hainunuliwi, thamani yake ni shilingi ngapi?*" (UK 18:2: N)

Kauli hizi ni uamsho kwa Watanzania watambue kwamba haki ya mtu haiwezi kununuliwa kwa thamani yoyote ile iwayo. Wala haki haiwezi kumithilishwa kwa jitihada yoyote ya mwanadamu ama kiumbe chochote chenye uhai na kisicho na uhai. Kumaanisha kwamba, uratili wake (uzito / mizania ya - haki) anaujua Mwenyezi Mungu Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo.

Kutagaa kwa rushwa takriban kwa kila Nyanja ya maisha ya Mtanzania, kulimpelekea Mwalimu kuikumbukia enzi ya maongozi yake; hata ikawa ni aseme: "***… hatukuwa tuna utani utani juu ya mambo haya ya rushwa***" kumaanisha kwamba, kwa uzito wa ubaya wa rushwa, kwa yeyote aliyehusika hawakumchelea ima kwa hadhi yake au kwa utaifa wake daima Watanzania walitakiwa watambue kwamba: ***Haki hainunuliwi***, na kwamba daima ilikuwa ni iwapitikie kwa kuzisuta nafsi zao kwamba ikiwa wangeitenda; ***thamani yake ni shilingi ngapi?***" kumaanisha kwamba haki si jambo la kuweza kuthamanishwa na kitu au jambo lolote. Kwa hivyo, ni wajibu wa kila mtu kwa nafasi yake kutekeleza wajibu wake ili iwe ni sababu ya mwingine kuipata haki yake pasi na kutaabishwa. Kama ilivyo ada kwamba

kila mwanadamu anawajibu kwa mwingine na hayo ni katika maumbile waliojaaliwa na Muumba wao Mola wa viumbe vyote. Na hii ndiyo kusema: kwa kutambua kwamba watu wanategemeana ni sababu toshelezi kwamba kila mmoja anahaki ya kumtendea mwingine haki yake kwa uadilifu. Kwa hivyo, ushawishi wa Mwalimu kuhusu rushwa kwa Watanzania ulikusudiwa kuwafanya watambue kwamba kuikubali rushwa ni kuikubali dhuluma. Hii ina maana ya kwamba, haki ni amana ambapo kila mmoja atawajibika kwa Mola wake kwa jinsi alivyowatendea viumbe wengine haki zao (alivyowajibika katika kuwapatia watu wegine haki zao kwa wakati na kwa uadilifu). Huo ukawa ni wito kwa Watanzania na pengine kwa walimwengu wote kuipiga vita rushwa kwa mbiu kwamba "*Rushwa ni adui wa Haki. Haki hainunuliwi !"*

**Istiara, tashhisi na tafsida kengeushi**: "*Rushwa ya Tanzania siku hizi haina aibu. Tanzania! Sasa kananuka.*" (UK 19:1: N)

Kwa kauli hizi; tendo rushwa linapewa sifa za Mwanadanu; mwanadamu ambaye anawezekana akahisi aibu au furaha na wenzake wakambaini. Kwa hivyo, muktadha wa kauli kwamba: *"**Rushwa ya Tanzania siku hizi haina aibu***" hudhihirisha hali ya kuonyesha fedheha; ambapo kwa hulka ya mwanadamu matendo yanapovishwa sifa za mwanadamu au mwanadamu anapojivua au kuvuliwa sifa zake, ni kuonyesha udhalili dhidi yake kwa kuvuliwa heshima yake ya kimaumbile. Ndiyo iwe ama amejidhalilisha mwenyewe au na kiumbe mwenzake. Ni uhawilisho wa tendo la rushwa kuonekana kwamba si jambo la aibu tena. Ni udhihirisho wa kwamba madhali mwanadamu ndiye mtendaji wa tendo hilo, inapokuwa limevikwa sifa ya kwamba halina aidu tena; ni kumdhihirishia mwanadamu huyo mwenye kulitenda kwamba amejivua utu na heshima yake na kwa hivyo yu ana fanya mambo ya aibu hadharani tena bila ya hofu ya kuonekana kwamba anadhalilika. Anadhihirishia umma jinsi ambavyo amechujuka utu wake; ameikosa thamani ya kimaumbile si tu mbele ya wenzake lakini pia hata kwa muumba wake; ambapo kwa hakika ya mwananadamu ni miongoni mwa viumbe waliobara ikiwa watauheshimu utu wake na heshima yake mbele ya viumbe wengine.

Fauka ya hiyo kauli kwamba '***Tanzania sasa kananuka"*** wakadhalka ni mtagusano wa uhamishaji wa sifa za mwanadamu au kiumbe kingine chenye uhai – ambacho kwa sifa ya kunuka anaweza / kinaweza kuipata. Kwa hivyo kuonyesha udhalili wake wa kutokusifiwa tena kwa uzuri. Ambapo kwa muktadha wa rushwa; nchi ya Tanzania inapewa sifa ya kunuka; kuonyesha kwamba si yenye kupendeza tena kwa kusifiwa kwa mazuri imekosa

hadhi kwa watu kuipupia kwa mafanikio; kumaanisha kwamba, watu wanaona dhiki kuishi katika mazingira ambayo hayawavutii. Ni kero katika kuyaendea maisha yao – hawawezi kuipata haki yao bila ya kuinunua (kujihusiha kwa rushwa) na kwa hivyo nchi haitamaniki kutokana na kukithiri kwa rushwa.

**Unukuzi**: *"… Njoo kesho inaweza kuwa ni njia ya kuomba rushwa".* (UK 44:2: AA)

Hizi ni kauli zinazoonyesha simanzi kwa raia wanaotenzwa nguvu kwa haki zao. Kauli ***"Njoo kesho"*** ni ishara ya vitabia lugha vinavyochakachua fikra za mwanadamu kwa kumfanya aitenze nafsi yake kwa rushwa kwa minajili ya kuiokoa haki yake iliyotiwa kitanzi na mwenye mamlaka; (***"Njoo kesho")*** ni kauli ambazo hazina mashiko hasa zinapotumiwa na watendaji ofisini. Kukataa kwao kutoa majibu sahihi, au kutoa huduma inayotakiwa kwa wakati na kwa uadilifu, sio kuonyesha kwamba hayo ndiyo mamlaka bali ni kuonyesha kwamba wakipewa chai kidogo mambo yanaweza kuharakishwa. Kwa hiyo, simanzi hii ya wanyonge ya kununuliwa haki zao kijanja kwa maneno ya ***"Njoo kesho'*** ni ushawishi wa kuwazindua Watanzania ili wawe macho kila unapowadia wakati wa uchaguzi na wawapate viongozi wanaoitambua dhima ya uongozi. Mtawalio wa fikra zao iwe ni kwamba daima wanahitajika wawe waadilifu popote watakapokuwa katika mpwito wa maisha yao kama viongozi jamii.

**Msemo:** "*Samaki mmoja akioza wote huoza*." (UK 9:2: MMT) & (UK 46:2: AA)

Haya yalikuwa ni makemevu dhidi ya wale walioukuwa wakiukejeli uendelevu wa umoja na amani uliopo miongoni mwa Watanzania. Kwa hivyo, Mwalimu aliionya jamii isiwafumbie macho maadui ili wasipate mwanya wa kuwaathiri wengine kwa tamaa zao. Usadifu huu ni kutokana na viongozi waliokuwa wakihimiza umoja na amani chini ya misingi ya ujamaa lakini ikawa ni wapenyeze matakwa yao binafsi ya kujiimarisha kiuchumi huku umma ukiendelea kutaabika kwa umasikini. Kwa hivyo, wananchi wamekuwa wakihoji kwamba ni kwa jinsi gani inawezekana katika nchi ya kijamaa – wachache waweze kujipatia fedha za kujianzishia shughuli kubwa kubwa za kibiashara kiasi cha kujenga tofauti ya kimapato ndani ya nchi masikini. Hali hii iliwapelekea wananchi kuona kana kwamba wanafanyiwa kejeli kwa kuhimizwa kuishi kijamaa ilhali misingi yeke haisimamiwi ipasavyo.

#### 4.4.5 Maudhui kuhusu Ukabila na Udini

Haya yalikuwa ni matatizo miongoni mwa matatizo mengi ambayo Mwalimu aliyabaini mara baada ya kung'atuka kwake. Baadhi ya Watanzania walijinasibu kwa ukabila na udini kama chambo cha kuyafanikisha matakwa yao kupitia umma wa Watanzania. Baadhi ya viongozi waliwaghilibu wananchi ili wawaunge mkono katika kupata madaraka. Makabila yalichukuliwa kama kibebeo cha kieneo katika kumkubali nani awe kiongozi wao ima wa jamii au kitaifa. Baadhi ya wananchi walivutika kiimani kwa fikra kwamba nchi ingetawaliwa kwa kuzingatia imani ya dini yao. Kwa uoni huo, Mwalimu aliwatahadharisha Watanzania wajiepushe na unasaba huo kwa hofu ya kuwatumbukiza Watanzania katika vita vya wenyewe kwa wenywe na kuipoteza hali ya amani iliyokuwapo tangu azali.

##### 4.4.5.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Ukabila na Udini

**Usimulizi, tashhisi unukuzi na maswali ya kibalagha**: *"... yuko mama mmoja anatoka Uganda. Katika mazungumzo yake akaniambia. Mzee, mimi nilikuwa nafanya kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na, tulipokuwa katika Jumuiya, tulikuwa tunawajua Watanzania: si lazima watuambie. Sisi wa Uganda, tulikuwa tunajuana kwa makabila yetu. Wa – Kenya walikuwa wanajuana kwa makabila yao. Watanzania hatujui makabila yao hata kidogo. Ilikuwa ni tofauti ya wazi kabisa. Sisi tunasemana kwa makabila. Kenya wanasemana kwa makabila. … tukiungana hivi, nchi hizi zikawa nchi moja ukabila wa Kenya utapungua, ukabila wa Uganda utapungua. Kwa nini? Kwa sababu, katika nchi moja hivi ya Afrika Mashariki, Wakenya watajiita Wakenya. Mkitutazama hivi Watanzania mtaanza kuzungumza matatizo yenu 'sasa tuna matatizo', mnamtafuta mchawi. Mchawi yule mtamtafuta kwa Watanzania kwa Waganda. Ninyi mtajiita Wakenya, hamtatafuta kwa Wakikuyu na Wajaluo, hawatajibagua hivyo. Ndani ya shirikisho, hamwezi kujibagua hivyo mkajiita 'sisi Wakikuyu' 'sisi Wameru' hata kidogo! Mtasema 'sisi Wakenya' "* (UK 23:1-3: N)

Ni kwa kupitia ufa huu wa ukabila na udini ambapo Mwalimu aliitumia balagha hii kuwatahadharisha Watanzania ubaya wa kuuendekeza ukabila na udini katika mambo yanayohusu umma. Aliwakumbusha jinsi ambavyo Watanzania walivyokuwa wakiishi kidugu kiasi ya kwamba wange taniana kwa makabila yao au kwa dini zao. Ikawa ni utani na sio udhati wa mwingine kuuingiza katika utendaji. Fahiwa ya matunda yake, wapenda amani ulimwenguni ikawa ni waisifie Tanzania ya kwamba ni kama "kisiwa cha amani" kutokana na upendo na ushirikiano uliomo baina yao. Watanzania ambao utambulisho wao mbele ya wengine ni "Utanzania" na sio vinginevyo kwa makabila yao ingawa ni zaidi ya mia moja na ishirini na tatu. Kwa maono hayo, ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania ni kuwahimiza

watambue kwamba, njia bora ya kuufuta ukabila na udini ni watu kuzifua nyoyo zao kwa kuzungumza na kutenda mambo ya umoja kwa pamoja. Wasijali kabila au dini ya mtu. Pia ikiwa ni kiongozi basi awe ni kiongozi wa Watanzania wote na sio kuuweka mbele ukabila, udini au sehemu alikotokea.

**Maswali ya kibalagha na tashhisi**: *"… "Tunataka Rais wetu". Kwa Tanzania, haiwezekani ukampata Rais ambaye hana kabila. Utampata wapi?. Hatuwezi kuwa na Rais ambaye hana kabila. Atakuwa na kabila. Hatuta mkataa mtu kwa sababu ya ukabila wake. Kumbe tutafanyaje? Lakini, hatutamchagua mtu kwa sababu ya ukabila wake. Hatuwezi kumkataa mtu kwa sababu tunasema 'fulani tunaona anazo sifa za kuweza kuwa kiongozi wetu lakini ah! bwana ni Mkara! Mkara huyu sifa zote anazo lakini tunasema 'ah! Jamaa ni Mkara', hatutafanya hivyo. Hatutamkataa kwa sababu ya kabila lake. Tukifanya hivyo, tunafanya dhambi kubwa.* (UK 24:4/25:1: N)

Kutokana na mkengeuko wa wagombea nafasi ya urais kuwa ya kuzingatia udini na ukabila; kwa dhana kwamba ni muhali kumpata kiongozi asiyekuwa na dini au kabila. Hali hii ndiyo iliyomfanya Mwalimu kuuliza kibalagha kwamba ***Utampata wapi?*** Kumaanisha kwamba haiwezekani kweli kumpata mgombea asiyekuwa na dini au kabila lake. Kwa hivyo akauliza tena kibalagha kwamba: ***Kumbe tutafanyaje?*** Kwa jawabu kwamba uzingatuvu ni lazima uwe ni kwa kutathmini sifa za kiongozi bora ambazo ni pamoja na kutojali dini au kabila lake ikiwa tu sio mwegemo anaouchukulia kama kigezo cha kumwezesha kupata kura na kwamba sio mtazamo atakaouzingatia katika maongozi yake. Kwa hiyo, mbinu ya lugha iliyotumia Mwalimu ni mshawasha kwa Watanzania, akiwataka wawachague viongozi wenye sifa na watambue ya kwamba udini na ukabila ni tatizo linalohitaji kutokomezwa pasina kumchelea yeyote kwa hali, hadhi au kwa mali yake.

**Tashhisi na takriri**: *Lazima tumpate rais atakayesema "Lo! Tunakwenda wapi huku, tunaanza kuzungumza ukabila na ukaburu!. Akemee na, akiukemea, watu wanamwamini waseme 'huyu anasema inatoka moyoni hasemi tu kwenye… '* (UK 26:1: N)

Haya ni makemeo ya Mwalimu kuhusu tatizo la ukabila kwa Watanzania. Matumizi haya ya lugha ni taswira ya jinsi ambavyo ***ukabila na udini*** ulivyokuwa enzi za maongozi ya Mwalimu. Haukushamiri kama ulivyokuwa baada ya kung'atuka kwake. Imekuwa ni mshangao ukabila kuchukuliwa kama nyenzo ya kuyawezesha matakwa (malengo) binasfi kupenyeza kwa urahisi katika asasi za umma; ikiwa ni pamoja na kumpata mgombea ama

kiongozi kwa njia isiyo ya halali. Hali hiyo imepelekea amani ya nchi kuyumba. Kwa taswira hiyo, suluhisho pekee lilonekana ni kumpata kiongozi (Rais) asiye mkabila lakini mwenye utambuzi kwamba ukabila ni tatizo; mwenye uwezo wa kulikemea tatizo la ukabila na udini; na anayeaminika na Watanzania kutokana na uaminifu wake ya kwamba makemevu yake yanatoka mwoyoni.

**Takriri**: "*Rais tunayemtaka ni Mtanzania. Huwezi kumpata Rais Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika. Anatoka ama Zanzibar ama Tanganyika, lakini hatumchagui kwa sababu ya Uzanzibari wake, hatumchagui kwa sababu ya Utanganyika wake. Na, akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai. …"* (UK 12:3/3:1: N)

Nia ya kauli hizi ni kutoa tahadhari kwa Watanzania hususani wapiga kura - kuzitambua sifa za kiongozi wa nchi ya Tanzania ambapo kauli **"*Rais tunayemtaka ni Mtanzania***" ni sharti linalowahusu Watanzania wote kwamba wawe makini kila unapowadia uchaguzi wamchuguze mgombea kwa kuzingatia sifa ya uraia wa Tanzania. Na kwa tamko: Lakini pia takriri ya tamko: ***"Huwezi kumpata Rasi Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika.*** Ni kumaanisha kwamba huu ni utanabahisho unaohalisika kwamba haiwezekani kweli kumpata rais Watanzania akawa si Mzanzibari au Mtanganyika. Na ndiyo ikawa ni aithubutishe kauli hiyo kwamba ukweli huo hauwezi kufutika ni lazima Rais huyo awe: ***"Anatoka ama Zanzibar ama Tanganyika"*** huo uliokuwa ufahima wa Mwalimu kwa Watanzania watambue kwamba sehemu hizi mbili (Zanzibar na Tanganyika) ndizo zilizoungana na kuzaliwa Tanzania. Hivyo, ni busara Utanzania ukazingatiwa zaidi ya mtu kwa eneo lake anakotokea kwa minajili ya kudumisha Muungano na kuepuka athari zinazoweza kupelekea ubaguzi wa kieneo na kwa hivyo kuuvunja Muungano.

Na kwa tashwishi, Mwalimu aliwatahadharisha Watanzania tena na tena kuhusu mgombea yeyote ambaye angependa kuwa kiongozi wa Watanzania ya kwamba, Watanzania wasihofu kumpembua sifa zake bainifu na kwa tashtiti akisema: ***"… akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai.*** Kumaanisha kwamba Watanzania hawana budi kuwa makini wakati wa uchaguzi hasa pale viongozi wanapojinadi na kujinasibu kwa sera zao; wasisite kuwafayia tathmini kwa minajili ya kumpata kiongozi bora na sio bora kiongozi. Lakini pia kwa hofu ya kuzuka kwa ubaguzi wa kieneo; udini au ukabila; Watanzania hawanabudi kuwa macho; hasa wakati wa uchaguzi wa viongozi.

**Maswali ya kibalagha na tashhisi**: *"... kwa kujua kwamba mimi ni mkatoliki, basi akaandika tu mahala kwamba 'Mwalimu yule ni Mkatoliki kajaza Baraza la Mawaziri Wakatoliki watupu'. Ah! Nikaiona ile, nikamwambia Bibi Joan Wicken, alikuwa ananisaidia, 'je ni vipi, mimi si jui dini za watu hawa, nifanyie uchunguzi katika Baraza la Mawaziri dini zao zikoje maana sijui kabisa.'. nilikuja kuwashtukia, ah! Kumbe huyu Mkatoliki au kumbe huyu nilikuwa simjui ... tulikuwa hatujali kabisa dini ya mtu hata kidogo. Tulikuwa hatuchagui mtu kwa dini yake, kwani anakuja kusalisha hapa? Tunachotaka ni Rais wa Tanzania, tutajuaje kama ana dini au ni dhehebu gani, hatujali kabisa.'* (UK 26:2/27:1-2: N)

Hizi ni kumbukizi za Mwalimu kuhusu mapambano dhidi ya udini enzi za maongozi yake. ambapo Mwalimu akiuona ni uzushi ya kwamba amehiari kuukumbatia ukatoliki Ikulu. Mbali na kutaka uchunguzi ufanyike aliziona shutuma hizo ya kwamba ni majungu ya nayokusudiwa kumvunja nguvu katika jitihada zake za kukemea udini na ukabila. ukabila na udini haukupewa nafasi enzi za maongozi ya Mwalimu Nyerere. Walionekana watu kwa dini zao katika mambo ya ibada. Lakini lilipojiri swala la kijamii wote kwa pamoja waliungana na wakaziweka dini zao katika nafsi zao na kadamnasi yake wakiungana pasi na ya tashwishwi yoyote. Ndoposa kwa mkengeuko wa baadhi ya Watanzania kuhusu udini na ukabila, baada ya kung'atuka kwake aliikumbukia historia ya maongozi yake; kwa kusema: ***"… tulikuwa hatujali kabisa dini ya mtu hata kidogo"*** … ***kwani anakuja kusalisha hapa?*** – Akimaanisha kwamba, swala la mtu kwa dini yake halikuwa ni jambo la kutiliwa maanani katika mambo yaliyoihusu jamii nzima. Watu walielimika na ikwa si hoja kwa mtu kumpitikia ya kwamba dini yake iwe ni kigezo cha kuzingatiwa katika mambo yanayoihusu jamii nzima. Watu walijihisi ni wa moja, wakishirikiana kwa kila jambo na kwa hivyo, amani na upendo vikawa ni mtawalio wa maisha yao. Daima maisha yalikuwa ni ya kidugu na yenye amani. Kwa hiyo ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu Nyerere kwa Watanzania wote watambue kwamba udini ni sumu mbaya katika jamii inayoweza kuwatenganisha kwa umoja wao na amani ikatoweka na ikawa muhali kuirejesha tena. Aliwataka (Watanzania) watambue kwamba serikali yao haina dini na kwa hivyo viongozi na hasa rais wamchaguaye ni sharti aelewe hivyo; na iwe ni dhima kwa kila Mtanzania kwamba sumu ya Udini na Ukabila haipenyezi katika maisha yao ya kila siku.

**Viambishi nafsi na vimilikishi**: *Kila mmoja wenu anakabila lake. Inasemekana kwamba yako zaidi ya makabila 123 ya kienyeji katika Tanzania, mbali na vikundi mbalimbali vya watu vyenye asili ya makontinenti mengine. Lakini hamkuruhusu kamwe jambo hili liathiri mwelekeo wa kisiasa, au maendeleo ya uchumi wetu. Mmewachagua watu wakushika*

*wadhifa wa kisiasa, au wa kazi za kuajiriwa, kulingana na sifa zao au uwezo wao, bila ya kujali kabila au rangi zao. Mimi napata sifa duniani kote kwa kukosekana Ukabila au Ubaguzi wa rangi katika Tanzania, lakini nyie ndio mlioleta hali hiyo, … nawashukuruni sana. Na hivi ndivyo ilivyo kuwa kwa upande wa dini, karibu Watanzania wote tunamwamini Mungu; lakini wenginine ni Waislamu wengine Ni Wakristo, wengine ni waumini wa dini zao za jadi, na wachache wengine ni Wahindu au Mabuda au wafuasi wa dini nyingine. Kwa hiyo tumejenga na kudumisha taifa lisilo na dini isiyo rasmi, na chama kisichokuwa na dini rasmi, nchi ambayo kila mmoja wetu anao uhuru wa kufuata dini anayoitaka na hakuna anayebaguliwa kwa sababu ya imani yake kwa Mungu"* (UK 9:3: KW)

Matamko hayo yanatudhihirishia sifa za matumizi ya lugha. Ni udhihirisho wa kwamba Mwalimu alikuwa ni mweledi wa kuzitumia mbinu anuai katika kuivutia hadhira yake. Weledi wa uteuzi wa maneno; ambapo kwa kauli hizo kuna matumizi ya viambishi nafsi ya pili, hali ya wingi na vimilikishi vionyeshi kama vile ***"mmoja wenu" "hamkuruhusu" "mnawachagua" "nyie" "mlioleta"*** na katika kuhitimisha kauli zake pia zimesawiri mbinu hiyo hiyo; akisema: Watanzania ***"nawashukuruni sana"***. Fahiwa kwa alichokuwa amekusudia ni kuwazindua Watanzania na kuwaandaa kwa ujumbe aliokusudia kuwafikisha.

Kisha Mwalimu alitumia **iltifati** kana kwamba anaitaka hadhira yake itazame upande mwingine wa matukio muhimu ambayo wanapaswa wote kwa pamoja kujifaharisha kwayo. Kwa hivyo, anaamua kutumia nafsi ya kwanza hali ya wingi: ***"tunaamini Mungu", "tunajenga na kudumisha taifa"***; na huku akitumia utohozi: ***"Makontinenti"*** kama ufahari wa kuonyesha kwamba hata kizungu anaweza kukifinyanga kwa minajili ya kupata analolihitaji, lau kama si mapenzi kwa lugha yake ya Kiswahili ambapo kuidumisha na kuiendeleza - ni heshima na uzalendo kwa taifa la Tanzania.

**Takriri, kinyume, taswira na uchanganyaji ndimi**: *"… kuziongoza nchi changa hizi kuna matatizo ya ajabu; na viongozi wengine hupata bahati nzuri na wengine huwa hawana bahati. Mimi nimekuwa miongoni mwa viongozi wachache sana wenye bahati kubwa kabisa ya kuaminiwa moja kwa moja na wananchi wenzangu. Tangu kabla ya uhuru wazee wangu waliniamini sana tulipo anzisha TANU; wazee wangu waliniamini japo mimi nilikuwa kijana mdogo niliporudi kutoka uingereza; nilirudi mwaka 1952 nikiwa na miaka 30. Waliponichagua kuwa "President" wa African Associastion" mwezi April, 1953 nilikuwa na miaka 31. Kijana mdogo tu natoka "University" nina miaka 31, watu wazima wakanichagua kuwa "Presidenty" wa African Association" Wakaniaamini wazee hao moja kwa moja watu*

*wazima. Siku hizo nilikuwa navaa kaptura (Short) na "Stockings"; ninyi hamvai, mimi nilivaa! Wazee hao ndio walinifanya nikaacha kuvaa kaptura; hawakuniambia niache kuvaa, lakini kila nikija kwenye mkutano na wazee hawa, wazee wa mjini watu wazima, waungwana sana, wamevaa kanzu; na mimi kijana mdogo na kaptura yangu, lakini wazee wangu wameniamini katika jambo kubwa hili. Na nimeanza kuwatobolea jitihada za kutafuta uhuru ili kujitawala. Niliamua mwenyewe kuacha kuvaa kaptura!*" (UK 18:1: AW)

"***Kuongoza nchi changa kuna matatizo ajabu***". Ni matatizo ajabu pengine kutokana na wingi wake nap engine kutokana na sura mbalimbali ambazo matatizo hayo huchukuwa. Yumkini hali hii hujitokeza kutokana na sifa bainifu ya nchi "***hizi***" zaweza kuwa nchi za Afrika Mashariki, nchi za Afrika nzima alimradi nchi za ulimwengu wa tatu. Nchi hizo hazija stawi kisiasa na kiuchumi, hazijakomaa katika elimu na maarifa na mtazamo wake wa kilimwengu si mpevu. Kwa hiyo, ni nchi changa kama neno "***changa***" lilivyo.

Matatizo yanayozikumba nchi hizi ni mengi. Miongoni mwake ni husda, choyo, tama, ufisadi, dhuluma, utovu wa nidhamu, ushindani usiokuwa na maana, rushwa, ukabila, umasikini na kadhalika. Kulingana na matatizo hayo, viongozi hupata shida wanapotakiwa kushika hatamu za uongozi. Wanaowapa shida ni wale wanaotaka nyadhifa za urais, ni wale wanaopanga mipango ya serikali, ni wale wanaopigania maslahi yao binafsi, na ni wale wasioheshimu katiba na uongozi wao. Kiongozi asipoheshimiwa, fursa za kuaminiwa huwa finyu sana. Kwa hivyo, katika mazingira ya namna hii, kuaminiwa kwa Mwalimu Nyerere alikuchukulia kwa bahati kubwa sana. Hii ni kwa sababu, pamoja na kuwa alikuwa mdogo sana kwa umri, watu wazima walimpokea na ijapokuwa anavaa kaptura kutokana na ujana wake, wazee wavaa kanzu, Waislamu walimwamini na kumfanya kiongozi wao. Wazee hao chambilicho Mwalimu, walikuwa waungwana na wazuri sana, kwa sababu hawakujali mambo mengine kama vile umri, kabila na dini bali walijali elimu yake na uwezo wa kuongoza nchi.

Katika kuelezea mambo hayo, na ili kuwashawishi wasikilizaji na wasomaji wa hotuba yake kuzingatia taarifa anayoitoa, Mwalimu alitumia balagha. Ushawishi huo umejikita katika matumizi ya takriri ambapo amerudiarudia: maneno, "***sana***", "***wangu***", "***mimi***", "***kavaa***", "***waliniamini***", "***nilikuwa***" na virai "***navaa kaptura***", "***watu wazima***", "***moja kwa moja***" na "***wazee hao***". Aidha ametumia vinyume kama vile "***watu wazima***", "***kijana mdogo***"; "***wazee***", "***kijana***", "***nimengi***", "***mimi***" na "***hamvai***", "***nilivaa***". Wakadhalika, alitumia mbinu ya taswira ili kuondoa utata. Kwa mfano: Anaposema "***wazee hawa***", mtu anaweza kuuliza ni

wazee gani ? jibu ni kwamba ni wazee wa mjini, ni watu wazima, wenye desturi ya kuvaa kanzu, na ni waungwana sana. Halafu katika kuelezea wasifu wake wakati huo tunaelezwa kwamba alikuwa kijana mdogo sana, mwenye umri wa miaka 31, alikuwa na ari ya kutafuta uhuru na alikuwa mtiifu kwa wanaomzidi umri kwa sababu alielewa kwamba hawakumtaka avae kaptura na ijapokuwa alikuwa ndiyo mtindo wa vijana, yeye alitii na kuvaa suruali na kukubali kutwishwa mzigo mzito (wa urais) wanaoubeba watu wazima.

### 4.4.6 Maudhi kuhusu Umoja wa Wafanyakazi

Mwalimu Nyerere aliwatanabahisha wananchi umuhimu wa kuunda umoja wa vyama vya wafanyakazi makazini. Hii ilikuwa ni kwa uoni kwamba wafanyakazi wa aina na wa fani mbalimbali huwalalamikia waajiri wao ima kwa kunyanyaswa au kufanyishwa kazi ngumu huku wakilipwa mishahara midogo isiyoendana na utendakazi wao.

Katika ushawishi wake kuhusu uanzishwaji na uimarishwaji wa vyama vya Wafanyakazi, aliwakumbusha Watanzania historia ya umoja wa vyama vya Wafanyakazi ya kwamba ulianzia huko Marekani na Ulaya. Kutokana na waajiri kuwadhulumu Wafanyakazi haki zao, ndio ikawa Wafanyakazi waanzishe umoja wa vyama vya Wafanyakazi ili kutetea haki zao walizokuwa wakidhulumiwa na waajiri wao. Kwa mtazamo huo, Mwalimu aliona swala la kuwepo kwa vyama vya Wafanyakazi kama jambo la busara kuendelezwa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo ili matajiri wenye uchu wa utajirisho kiasi cha hata kuwadhulumu Wafanyakazi haki zao wasipate mwanya wakuwadhulumu tena. Lakini pia kuwafanya Wafanyakazi wajiamini kazini ya kwamba mwajiri atakayewadhulumu haki zao chombo chao kitashika hatamu ya kuwatetea.

Wakadhalika ufahima wa maelezo ya Mwalimu ulikuwa ni kuwatanabahisha Wafanyakazi popote walipo watekeleze wajibu wao pasi na kupatilizwa nyuma na kwamba wawe wepesi wa kuzisuta nafsi zao kabla ya kuwalaumu wengine kwa madhaifu yao. Katika ufanisi wake; Mwalimu aliwashawishi Watanzania kuhakikisha ya kwamba wanaongozwa na viongozi bora, wamakinifu katika kuitambua haki na kuisimamia kwa uadilifu katika jamii.

#### 4.4.6.1 Mitindo Iliyotumika katika Maudhui ya Umoja wa Wafanyakazi

**Matumizi ya vihisishi na maswali ya kibalagha**: "*... ALAA! Bwana mkubwa, kazi tufanye sisi halafu utupe mshahara mdogo tukufanyie kazi wewe? Basi uone kama tutakufanyia*" (UK 5:1: TTT)

Wafanyakazi wa aina na wa fani mbalimbali huwalalamikia waajiri wao ima kwa kunyanyaswa au kufanyishwa kazi ngumu huku wakilipwa mishahara midogo isiyoendana na utendakazi wao. Udhia huo ndio uliompelekea Mwalimu kutoa mfano wa jinsi ambavyo kilele cha maonevu kinapofikia ukomo; ya kwamba utu na amani vimepotoweka, Wafanyakazi hufikia kusema: ***ALAA! Bwana mkubwa, kazi tufanye sisi halafu utupe mshahara mdogo tukufanyie kazi wewe? Basi uone kama tutakufanyia"***. Ku maanisha kwamba Wafanyakazi wanapofikia kudhihirisha mkururo wa hasira baada ya kuvumilia kwa muda mrefu, hatma yake ni kufanya mgomo wakutoendelea kufanya kazi hadi hapo watakapotendewa haki sawa kutokana na utendakazi wao.

Hivyo, ushawishi wa Mwalimu kwa Wafanyakazi ni kuwazindua watambue kwamba, njia pekee ya kuondokana na dhuluma zinazotokana na waajiri wao kazini ni kuunda umoja wa vyama vya Wafanyakazi na kuhakikisha kwamba umoja huo unafanya kazi barabara katika kutetea haki zao wanazodhulumiwa na waajiri wao. Akawatahadharisha waajiri waepukane na dhuluma za kuwanyonya Wafanyakazi kwa uoni kwamba pindi Wafanyakazi watakapo baini kwamba wanadhulumiwa, hawataipata salama. Kazi zao zinaweza kuvurugwa kutokana na migomo; na ama zisitendwe tena kwa ufanisi na kusababisha malengo ya maendeleo yasifikiwe kama ilivyotarajiwa.

**Uzungumzi nafsi, maswali ya kibalagha na vihusishi**: "*... kama watakuwa wananiambia mmoja mmoja, nitawafukuza. Unakuja peke yako na unaniambia. Lakini mzee sasa mimi nataka uniongeze mshahara. Nitakuambia. Unaniambia nini wewe? Unasema nikupe mshahara wa shilingi ngapi? Utajibu. Ah! Kama utavyoona, lakini uniongeze. Mungu anaona na Mtume. Nikaona kidomodomo chake huyu! Nitakuambia: Unataka mshahara huo ninaokupa? Nyamaza na nenda kafanye kazi huku utachagua. Kama hutaki, toka. Kazi sikukuomba ulikuja mwenyewe. Nitakutisha hivyo ukifikiri mchezo, nitakufukuza. Na wenzako watajua kafukuzwa kwanini yule. Amedai mshahara mwingi. Mimi kimya! Wengine hawatathubutu tena maana watafikiri. Nikisemasema hapa na mimi nitatimuliwa na watoto wana njaa. Nikitimuliwa nitapata taabu. Wewe unaonaje?* (UK 6:2: TTT)

Kauli hizi ni uzinduo kwa Watanzania kuhusu Wafanyakazi wasiotambua haki zao kuwa wanadhulumiwa ama wanatambua lakini hawana umoja. Mwalimu anawazindua watambue ya kwamba, pasi na umoja, hali hii huwapelekea waajiri kujiamini na kuwatendea wafanyakazi lolote watakalo kwa ajili ya kujinufaisha kadiri wapendavyo. Hivyo, Mwalimu anawashawishi wafanyakazi wawe na umoja (waunde vyama vya wafanyakazi); kwa imani kwamba, umoja wenye utendaji ndio unaoweza kuwekewa mizani baada ya muda ili kutathmini mafanikio na madhaifu ya utekelezwaji wake.

**Istiara na takriri**:"*... Zamani vyama vya wafanyakazi vilianzisha mshikamano wa wafanyakazi Duniani. Kauli mbiu yake ilikuwa Wafanyakazi Duniani Unganeni. Hamna cha Kupoteza Isipokuwa Minyororo yenu. Kwa kuungana hamna chochote mtakachokipoteza isipokuwa minyororo yenu kwa kuwa mmefungwa minyororo na mmenyonywa: unganeni.* (UK 7:2: TTT)

Huu ulikuwa ni uamsho kwa Wafanyakazi watambue kwamba, umoja ndio utakaowasaidia kutetea haki zao wanazodhulumiwa na matajiri wao kazini. Maneno ***"Hamna cha Kupoteza Isipokuwa Minyororo yenu***" ni uhamishaji wa hisia. Minyororo ni mithili ya kamba ndefu yenye uimara na isiyoweza kukatika kwa wepesi. Ambapo watumwa kwa kudhibitiwa na Wakoloni enzi hizo, walifungwa minyororo ili wasiweze kuwaponyoka wanakotakiwa kwenda kufanyishwa kazi za kujitoa muhanga. Kwa hivyo, ni tafakuri kwa jinsi Wafanyakazi wanavyotenzwa nguvu na waajiri wao, kwa hisia sawa na walivyokuwa watumwa wakitenzwa nguvu na Wakoloni enzi hizo. Na kwa neno **"*unganeni"*** ni tafakuri ya na suluhisho kulingana na muktadha wa maudhui yaliyoendelezwa; ya kwamba Wafanyakazi watakapokuwa na umoja thabiti wataweza kuzitetea haki zao wanazodhulumiwa na waajiri wao kazini. Hivyo, gharama ya Wafanyakazi kwa ajili ya kujinasua kwa mikatale ya waajiri wanaowadhulumu haki zao ni kuungana; kuwa na umoja. Kwa kufanya hivyo ndio kusema: "hawatapoteza chochote zaidi ya kuikata minyororo waliyofungwa na waajiri wao. Watakuwa huru. Daima hawatadhulumiwa tena.

### 4.4.7 Maudhui kuhusu Kilimo Kwanza

Tangu azali kwa Watanzania kilimo kimekuwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wao. Mazao ya chakula kama mahindi, maharagwe na karanga; mazao ya biashara kama: katani, pamba na kahawa; na ufugaji kama vile wa ngo'mbe, mbuzi, kondoo, kuku na aina ya ndege wengine; wamekuwa wakishamirishwa takribani katika kila pembe ya nchi hususan vijijini. Enzi za uhai wake Mwalimu aliwahimiza Watanzania kutambua kwamba kilimo ndiyo uti wa

mgongo wa uchumi wa taifa lao. Kwa hivyo, hawanabudi kukipa kipaumbele. Mwamko huo uliwapelekea Watanzania kukiimarisha kilimo kwa kujiwekea malengo ya kujitosheleza kwa mazao ya chakula na biashara. Waliweza kufanya tathmini kwa kila ulipomalizika msimu wa mazao au kila mwaka. Ilikuwa ni imani ya Mwalimu kwamba kwa kufanya hivyo, wakulima wataweza kugundua madhaifu yao na hata kufikiri mbinu nyingine zitakazoweza kuwapatia mafanikio zaidi.

#### 4.4.7.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Kilimo Kwanza

**Tashbiha**: "… *maisha bora maana yake siyo kupata fedha tu za kununulia nguo, kujenga barabara, na kadhalika, ingawa mambo hayo nayo ni muhimu, maana ya maisha bora ni kutolazimika kufanya kazi kama Punda* (UK 9:2-3: MUSW)

Nui ya tashbiha hii ni kuwazindua Wakulima waweze kuzibadili mbinu za kale; hususani zana za kilimo na pembejeo; ziwe za kisasa ili kuwezesha kuzalisha mazao kwa wingi na yaliyo bora zaidi; na kwa hivyo kujitosheleza kwa chakula na fedha. Lakini kujihimu kwa afya bora; kuimarisha miundo mbinu kama vile barabara kwa ajili ya usafirishaji wa mazao ima kutoka shambani kwenda katika maghala maalumu au sokoni. Na kwa hivyo, uwezekano kuzisaidia sekta zingine kama vile elimu: ujenzi wa majengo ya shule na kadhalka; ili kupata wataalamu wa kilimo na wafani nyingine.

**Tafsida kengeushi na maswali ya kibalagha**: *"… mtu ye yote anayetembea katika nchi hii ataona jinsi watoto wetu walivyo wanyonge, wengine wamelegea hata hawana nguvu za kucheza, na wengine wakicheza huchoka upesi sana. … lakini ingawa jambo hili linajulikana sana ukiwaambia wananchi wafuge kuku watakuuliza: tutawauza wapi? Au tutauza wapi mayai? Haya ni maswali ya kijinga sana … wanaonunua kuku na mayai hununua kwa ajili ya chakula. Wafugaji nao hawana budi wafuge kwa ajili ya chakula chao wenyewe na watoto wao. Kwa nini kuwe mtu hata mmoja kijijini asiyefuga kuku? chakula cha kuku hao ni mabaki ya shamba tu, …* (UK 9:2-3: MUSW)

Hizi ni kauli zilizokuwa zinawazindua Watanzania waliomo vijijini ya kwamba wawekeze zaidi katika kilimo cha mazao ya chakula, ya biashara na mifugo. Hii ni kutokana na mazingira faafu waliyonayo; ambapo kwa uwepo wa ardhi yenye rutuba mazao ya aina mbali mbali yanaweza kumea na kuzalisha matunda bora. Mifugo hunawiri kutokana na wingi wa malisho na yasiyo na gharama kubwa; kutokana na mabaki ya mazao yanayolimwa. Ingawa hivyo, Mwalimu alipigwa na butwaa kutokana na kauli za wakulima kwamba: **"*wakifuga kuku watawauza wapi?*" au "*watauza wapi mayai?"*** Sintofahamu hii ilimkera Mwalimu

hata ikafikia kuwajibu wale wote wenye mawazo ya namana hiyo, kwa kusema: “***Haya ni maswali ya kijinga sana…”*** kumaanisha kwamba Watanzania wenye mawazo ya namna hiyo walipaswa watambue kwamba, wanaonunua kuku na mayai hununua kwa ajili ya chakula. Kwa hivyo, wafugaji nao hawana budi wafuge kwa ajili ya chakula chao wenyewe na watoto wao.

Tafakuri ya Mwalimu ilikuwa ni kwamba, ikiwa Watanzania wangetanabahi na wakawa ni wepesi wa kiutendaji: ***“… pasinge tokea mtu hata mmoja kijijini asiyefuga kuku?”*** – tafakuri ambayo ilimpelekea kujiuliza jinsi ambavyo ilivyowepesi kwa Wakulima kujihusisha na ufugaji wa kuku; hasa ikisadifu kwamba kwa Mkulima hahitaji kugharamika zaidi kutokana na kwamba “***chakula cha kuku hao ni mabaki ya shamba tu*!;** hivyo Mkulima anaweza kujihusisha na ufugaji zaidi kuliko mtu wa mjini.

Hivyo, ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania, ulikusudiwa kuwazindua ili watumie mazingira ya ardhi yao yenye rutuba vizuri na kwa aina mbali mbali ya mazao; ukiwemo ufugaji. Hii ni kwa sababu chakula cha mifugo hiyo kinatokana na mabaki ya mazao mengine kama vile mahindi, maharagwe na mtama. Kwa imani kwamba, natija hiyo itawawezesha kujitosheleza kwa lishe bora: (Aina ya nyama, mayai, samaki, maziwa, ama chakula kingine cha aina ya protini) na kulifanya taifa la Tanzania liwe ni taifa la watu wenye nguvu na fikra faafu katika kuendeleza maendeleo ya nchi kiuchumi, kisiasa na kijamii.

**Maswali ya kibalagha**: "*Lakini je, kila Mkulima katika sehemu zile zinazostawi karanga analima karanga za kutosha kwa chakula chake mwenyewe na watoto wake? Karanga, Maharage, Mboga, ni vyakula vizuri vinavyofaa kujenga mwili na ubongo. .... Matunda je? Bado tunafanya kana kwamba matunda ni chakula cha Wazungu tu; au sana sana cha watoto, na hata kwa ajili ya hao hao watoto bado tunategemea bahati njema ya mti uliota wenyewe karibu na nyumbani".* (UK 10:2: MU)

Huu ulikuwa ni ufahima wa Mwalimu kuhusu maongozi yake kwa jinsi alivyowahimiza raia Watanzania wazijali afya zao kwa lishe bora. Ambapo aliwazindua kwa maswali yasiyohitaji majibu **"*Lakini je, kila mkulima katika sehemu zile zinazostawi Karanga analima Karanga za kutosha kwa chakula chake mwenyewe na watoto wake?*** Kwa tafakuri kwamba, ikiwa Watanzania wangemakinika, wangeliwezesha taifa la Tanzania kuwa la watu wenye nguvu na uwezo wa kufikiri sawia. Ikiwa kilimo wangekifanya ndiyo mtawalio wa fikra zao katika kujihimu kwa chakula, malazi na mavazi. Aliwarai Watanzania wasijivyaze kasumba za

kikoloni kwamba kila kizuri ni muhimu na haki ya Mzungu na sio Mwafrika kwa rangi yake. Ni sintofahamu ambayo Mwalimu aliona inahitaji kurekebishwa kwa haraka. Akijiuliza jinsi ambavyo Watanzania wamezungukwa na mazingira yenye kupatikana kwa lishe bora lakini wasivichukulie vyakula hivyo kama jambo la muhimu kwao. Kwa hivyo, aliwauliza tena: ***"Matunda je?"*** akionyesha jinsi ambavyo (matunda) yanavyochukuliwa kana kwamba ni vitu vya kianasa kwa watu wa nasaba bora ama kwa watoto wadogo ambao daima huonekana ni watu wa kubembelezwa bembelezwa kwa vitu vitamu vitamu au kwa kutokana na himizo la madaktari hasa inapokuwa watoto mara nyingi kinga yao iko chini kiafya.

Hivyo, Mwalimu aliwataka Watanzania wazinduke kwa minajili ya kuiondoa kasumba hiyo. Alizisuta nafsi zao kwa kusema: ***"… hata kwa ajili ya hao hao watoto bado hutegemea bahati njema ya mti uliota wenyewe karibu na nyumbani".*** Kumaanisha kwamba, Watanzania hawanabudi kumakinika kwa lishe bora kwa minajili ya kujenga afya zao. Wasitegemee bahati bali wafanye mipango madhubuti ya kuzalisha matunda yatakayowafaa, wao na watoto wao, kwani yakiwa katika mazingira ya nyumbani na katika milki yao watayachuma kila uchao.

**Tafsida kengeushi**: "*Tabia yetu hii kuhusu chakula hutokana na ujinga, upuuzi, lakini pengine uzembe pia. Baadhi ya watu wetu hawatambui mambo wanayoweza kuyafanya, au kwa nini ni muhimu kuyafanya mambo hayo; na wanaona rahisi zaidi kuendelea katika nia zile zile za kizamani, kuliko kufanya juhudi ya kubadili hali ya maisha yao.* (UK 10:4: MU)
Kutokana na baadhi ya Wakulima kuendekeza ukale katika uzalishaji mali. Mwalimu aliisawiri tabia hiyo ya kana kwamba ni: **"*ujinga, upuuzi na uzembe.*"** hasa ikisadifiwa kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa la Tanzania. Yalikuwa ni mategemeo yake kwamba kila mmoja angelitambua hivyo na kwa hivyo kilimo kikapewa kipaumbele - kwa kutumia mbinu bora na za kisasa ili kuzalisha zaidi tofauti na ilivyokuwa zamani na uduni wake kuhusu zana za kilimo. Hivyo, ufahima kuhusu nia ya kauli hizo, ilikuwa ni kuwazindua Watanzania watambue kwamba maendeleo yao yatatokana na jitihada na maarifa yao wenyewe. Kwa kuyatumia vyema mazingira ya vijijini kuna uwezekano wa kujipatia mazao ya chakula na ya biashara kwa wingi mfano ni mazao ya pamba, korosho, tumbaku na ngano, matunda na aina nyingine za mbegu kama vile maharage na karanga.

**Takriri**:*"Lazima tujifunze kufanya kazi kwa akili, kama kuna mafunzo tunayoweza kusoma darasani, ama kama kuna vitabu tunavyoweza kujisomea wenyewe, basi lazima tusome. Lakini vile vile lazima tuwe radhi kujifunza kutoka kwa watu wengine wenye ujuzi zaidi au*

*ujuzi tofauti. Lazima tujifunze kutoka kwa watu. Wanaopata mazao zaidi, au walio na mifugo mizuri, au wanaoweza kufanya vitu vingine vinavyofanya maisha yao yawe bora na ya kitajiri zaidi. Na tusione aibu kujifunza hata kama Mwalimu mwenyewe ni mtoto Sana, au mzee sana na hakusoma; au kama anatoka katika kabila jingine, au hata katika taifa jingine. Lazima tujifune kutoka mahala popote tunapoweza kupata elimu. Mungu hakutupa kitu bora kuzidi kama elimu; na kuunoa ubongo ni jambo la lazima."* (UK 11:2: SU)

Kauli hizi zinatilia mkazo suala la kupata elimu na maarifa iwe ni kwa kupitia darasani, kujisomea mwenyewe kwenye vitabu au kuipata kutoka kwa watu wenye ujuzi hata kama ni watoto, wazee au wale ambao hawakusoma. Kinachoakisi msisitizo huo ni uradidi wa neno ***"Lazima", "tujifunze", "kujifunza";*** *matumizi ya visawe vya elimu:* ***"ujuzi", "kujifunza", "kusoma"*** *na* ***"kuunoa ubongo";*** ambapo kwa pamoja yanashajiisha watu juu ya umuhimu wa kupata elimu na maarifa. Ambapo kwa kumbukizi, mara tu baada ya kujipatia uhuru; mbiu ya Mwalimu kwa Watanzania ilikuwa ni kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anatambua kwamba kuipata elimu ni haki yake na kwamba elimu hiyo isadie kuleta maendeneo ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

**Takriri**: "*... kilimo kiendelee kuwa pembezoni katika mipango yetu ya maendeleo; basi na Tanzania yenyewe itaendelea kuwa nchi ya pembezoni; na Watanzania wataendelea kuwa watu wa pembezoni; ..*" (UK 4:5: MMT)

Kauli hizi ni takriri na uamsho wa Mwalimu kwa Watanzania kwamba mbali na mambo mengine yatakayowawezesha kuinua uchumi wao; hawanabudi kuhakikisha kwamba wanakipa kipaumbele kilimo; ambapo kwa msisitizo Mwalimu alisema: ***"kilimo kiendelee kuwa pembezoni".*** Kutokana na uoni kwamba zipo nchi zilizoendelea kiuchumi, Watanzania walitakiwa wasikate tamaa bali wajiamini kwamba kwa kukitambua kilimo kwamba ndiyo mwokozi wao **"*basi na Tanzania yenyewe itaendelea kuwa nchi ya pembezoni*"** kwa ufahima kwamba itakuwa mbioni kujiletea mandeleo yake sanjari na nchi zilizoendelea. **"*na Watanzania wataendelea kuwa watu wa pembezoni*"** kumaanisha kwamba inapokuwa Tanzania haikuachwa nyuma kimaendeleo bali inakwenda sambamba na nchi zilizoendelea. Basi Watanzania ni watambue kwamba mafanikio ya jitihada zao hayako mbali. Kwani jitihada hizo ni hatua nzuri ya kuyafikia maendeleo kwa haraka. Mtazamo huo na hali ya kuonekana kwamba taifa la Tanzania bado lilikuwa changa: kiuchumi hasa katika maendeleo ya viwanda, afya na elimu. Kwa hivyo, kilimo kilionekana kikishamirishwa kwa sababu kinaweza kuzikomboa asasi nyingine na kulileteа taifa hilo la Tanzania maendeleo makubwa.

Kwa mwegemo huo, Watanzania wanahimizwa wajitume na kuwekeza zaidi katika kilimo ili kujiletea maendeleo kwa haraka hasa ikisadifiwa kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa hilo na kwamba Tanzania ina mazingira faafu ya kilimo bora.

### 4.4.8 Maudhui kuhusu Rai ya Tanzania ya Kutofungamana na Upande wowote

Ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania ya kwamba waendeleze msimamo wao kuhusu misingi ya siasa waliyojiwekea tangu enzi za mapambano ya uhuru na baada yake; ambapo siasa ya kutofungamana na upande wowote ni miongoni mwa misingi ya siasa za Tanzania; ambapo nchi zingine zinapaswa kuiheshimu. Tashtiti ya Mwalimu kuhusu msimamo huo ilitokana na taswira ya nchi za Kimagharibi kuonekana ya kwamba zilikuwa zikiendelea kuzirubuni nchi za Kiafrika hata baada ya kujikomboa na kuwa huru. Hali hii, kwa Mwalimu, ni ya kuzifanya nchi za Kiafrika kuwa na uhuru wa bendera tu hasa zinapokuwa nchi hizo zinafanywa kuwa ni tegemezi dhidi ya mataifa hayo ya Kimagharibi kwa kusubiri misaada ya kuongozea nchi zao. Kwa hivyo, aliwataka Watanzania watambue kwamba uongozi wa nchi yao ni thabiti na hawana budi kuwa chonjo daima na mataifa ya Kimagharibi, kutokana na tabia yao ya kuziburuza nchi za Kiafrika kwa nia ya kutaka ziendelee kuwa makoloni yao. Kwa kumbukizi za Mwalimu ni kwamba, Afrika imeendelea kuvishughulisha vichwa vya wamagharibi (Wakoloni); kutokana na utajiri wake wa mali ghafi nyingi ambazo wangezihitaji kwa ajili ya viwanda vyao. Lakini pia Afrika imeendelea kuonekana - ni soko kuu la viwanda vyao - baada ya kwamba wamekwisha zichakachua amali za Kiafrika kwa kuzalisha biadhaa zao na ikawa hawana pa kuziuzia. Kwa taswira hiyo, Mwalimu Nyerere aliwashawishi Watanzania na pengine Waafrika kwa ujumla wawe na umoja mathubuti kuhusu siasa ya nchi zao - mbele ya mataifa mengine; hususani mataifa ya Kimagharibi.

#### 4.4.8.1 Mitindo iliyotumika kuhusu Maudhui ya Kutofungamana na Upande wowote

**Takriri neno na tashbiha**: *"... wakati watu wetu walipojiunga katika TANU kuutafuta uhuru, haja yao haikuwa kufuata bendera yao tu. Walikuwa wanavitaka vile vitu ambavyo bendera ile ingeleta uwezo wa watu kujiamulia wenyewe maisha wanayotaka kuishi. Walitaka kuwa na Serikali yao wenyewe ili ifikirie shida zao wala si shida za watu wengine kwa umbali wa maelfu ya maili, wenye Serikali yao tofauti kabisa"* (UK 2:4: MUSW)

Huu ulikuwa ni ushawashi wa Mwalimu; akiwataka Watanzania wauthamini uhuru wa nchi yao watambue kwamba: ‘(mapambano yao ya kudai uhuru toka kwa wakoloni ) ***haja yao haikuwa kufuata bendera yao tu; walikuwa wanavitaka vile vitu ambavyo bendera ile***

***ingeleta'*** Hii inamaanisha kwamba Watanzania wanapaswa kuwa wazalendo wa nchi yao wamakinifu na wasioyaharakia maendeleo yao kibubusa hata ikawa ni wauuze utu wao na heshima ya nchi yao kwa thamani ndogo na ya muda mfupi. Watanzania wanapaswa kufikiri kabla ya kufanya maamuzi ili kuepuka madhara ambayo yangeweza kutokea baadaye. Wawe na mtawalio wa fikra kwamba, wanaweza kujisimamia pasi na kushikiwa akili na nchi zingine hata ikawa hawana uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe.

**Tashtiti takriri**: *"... hivyo ndivyo ilivyokuwa mkazo wa hotuba zetu hadharani. Kuna sababu mbili za tokeo hilo. Tumesema mataifa ya magharibi yameshindwa kuelewa maana ya uhuru wetu. Kinyume chake ni kwamba na sisi nasi mara nyingi tumeshindwa kuziondoa zile fikra tulizozijenga siku za ukoloni. Kwa hiyo, kwa kuwa sisi ilitubidi tu kukurushane na wakoloni wa Magharibi, tunalikumbuka sana jambo hilo, na tunafikiria mno jinsi ya kujikinga lisitokee tena hatuwazii sana namna zingine za ukoloni, na kwa sababu hiyo baadhi ya watu wetu wanahofu mno ya upande mmoja tu, wakiamini sana wanalilinda Taifa lao, ikiwa hawatakubaliana na kitu chochote atakacho Mwingereza au Mmarekani. Fikra kama hizi ni mbaya, na hatutakuwa Taifa lililokomaa mpaka fikra hizi tumeziondoa.* (UK 5:5: MUSW)

Matumizi wa nafsi ya wingi {etu} anaposema "***hivyo ndivyo ilivyokuwa mkazo wa hotuba zetu hadharani"*** – hii ilikuwa ni kuonesha ya kwamba anachokipigania Mwalimu si kwa masilahi yake peke yake bali ni kwa Watanzania wote. Kwa hivyo, Watanzania wanatakiwa wazinduke ili kuyaona mambo katika uhailisia wake. Washirikiane katika kuilinda nchi yao na kwa pamoja wajiletee maendeleo bila ya kuzitegemea nchi zingine ambazo daima misaada yao huambatana na masharti yenye kuwanufaisha wao wenyewe.

Wakadhalka, kauli zake zimesheheni mofu za wingi kama vile: ***"tumesema"*** badala ya ***"ninasema"; "sisi"*** badala ya ***"mimi"*** ufahima wake ni kwamba, ameamua kuihusisha hadhira yake - kuonyesha kwamba anajali mawazo yao anawaheshimu na angependa washirikiane katika kulipatia ufumbuzi tatizo linalolikabili taifa lao. Kwa mfungamano wa mofu hizo ndiposa anataja sababu mbili zilizompelekea kutilia mkazo mambo muhimu, ambayo ni kushindwa kwa mataifa ya magharibi kuelewa maana ya uhuru wa mwafrika; na Waafrika kushindwa kuziondoa fikra walizojijengea enzi za ukoloni ya kwamba mwafrika asinge weza kujimudu kiuchumi au kisiasa pasi na mkono wa mataifa ya kimagharibi. Ingawa hivyo, anachelea kuwannyooshea raia wake kidole cha lawama; na badala yake anajifanya kana kwamba yeye na wananchi wana hisa sawa ya lawama na wanawajibika kwa kosa

wanalolifanya la kotozuia ukoloni mambo leo pale aliposema: ***"hatuwazuii"***. Hii ni kwa sababu lugha isipotumika kwa uangalifu inaweza kuzua athari zisizotarajiwa. Hivyo, ushawishi wake ulikuwa ni Watanzania waungane kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba wanailinda nchi yao na madui wa ndani na nje na waboreshe uchumi na siasa yao ili waondokane na utegemezi usio walazima.

**Takriri na maswali ya kibalagha**: *"Ujerumani ya Magharibi ilidai, na ikadai kwa nguvu sana walipoona mazungumzo yao ya kibalozi yameshindwa kabisa kuwatikisa Watanzania kubadili uamuzi wao huo, hapo serikali ya Ujerumani Magharibi wakavunja mkataba wa mafunzo wa miaka mitano unaohusu wanahewa wetu bila ya kutoa taarifa yo yote. Kufumba na kufumbua wakawanyakua mafundi wao wote. Na zaidi ya hapo wakatishia kuondoa misaada yao mingine yote … Sasa Tanzania ingefanya nini?* (UK 3:1-3: MUSW)

Ufahima wa kauli hizi ni kuonyesha jinsi Watanzania walivyoudhihirishia ulimwengu ushupavu wa siasa yao ya kutofungamana na upande wowote. Ambapo kwa rai yake ya kuitambua Ujerumani Mashariki na kuiacha Ujerumani Magharibi; Wajerumani wa upande wa Magharibi walikasirika na ndiposa Mwalimu akisema: ***Sasa Tanzania ingefanya nini?*** Akimaanisha kwamba Tanzania ni taifa huru na lina msimamo imara kuhusu siasa ya nchi yake Wamekwisha amua kuifuta hasa katika kujiamualia marafiki na kwa kuulinda uhuru wao; uwe ni uhuru wa vitendo kulingana na shabaha walizoziazimia tangu enzi za mapambano ya kujikomboa na kupata uhuru kamili.

Kwa msisitizo Mwalimu alisema: ***Tanzania iweje iendelee kuwa chini ya maamuzi ya nchi zingine? Tena zile zilizokuwa makoloni yake?*** - Ingawa hivyo, msimamo huo wa kutokukubali shinikizo kutoka nchi za kimagharibi, uliipelekea Tanzania kupoteza misaada ya uchumi iliyoihitajika sana hasa kutokana na uchanga wake na umasikini walioachiwa na Wakoloni na hata ndio ikawa ni wajikongoje kwa mwendo pole. Serikali ya Tanzania, chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere, ilikuwa radhi kuikosa misaada hiyo kwa minajili ya kuilinda heshima na uhuru wake walioupigania kwa hali na mali hata wakajitoa muhanga kwa ajili ya kuvihami vizazi vilivyopo na vijavyo.

Kwa hiyo, nia ya Mwalimu ilikuwa kuwataka Watanzania wazinduke na watambue kwamba baada ya kwamba wamekwishajipatia uhuru, wana uwezo wa kujiamulia mambo yao wenyewe. Wasikubali tena kuburuzwa na mataifa yaliyoendelea kiuchumi (Mataifa ya Kimagharibi / Wakoloni) lakini watambue kwamba wakiungana wanaweza kuinua uchumi wao wenyewe na kuondokana na utegemezi ambao daima ni udhalilishwaji wa taifa lao.

**Maswali ya kibalagha**: *"… (tulipokataa ugandamizaji wa nchi za kimagharibindio kusema…) tunavyojisogeza kutoka katika upande wa Magharibi, tunaendelea zaidi Mashariki, au tunakwenda katikati kabisa, na kukomea papo hapo?* (UK 4:5: MUSW)

Kwa kumbukizi ni kwamba, Tanzania ilikuwa sehemu ya mataifa ya magharibi. Ilikuwa ni sehemu ya Wakoloni kama sio mapambano yake dhidi ya ukoloni, bado ingelihisabika hivyo. Kutokea hapo, ilijisogeza kidogo kidogo hata ikafikia hali ya kutofungamana na upande wo wote. Ndiposa Mwalimu akiwauliza Watanzania: ***Je, tunavyojisogeza kutoka katika upande wa Magharibi, tunaendelea zaidi Mashariki, au tunakwenda katikati kabisa, na kukomea papo hapo?*** Ambapo jibu lake ni kwamba: ikiwa mtu alikuwa akiishi katika mtaa wa Magharibi, na sasa nia yake ni kuishi tena katika upande wa Mashariki wala si wa Magharibi, bila ya kuishi katika mtaa wa katikati, ni dhahiri kwamba safari yake ya kwenda katikati itaonekana bure.

Kwa hivyo, Watanzania waliona kuna haja ya kusogea na wakatekeleza hilo kwa vitendo. Kwa msimamo huo, mataifa ya Magharibi yaliingiwa na wasiwasi. Maana kabla ya uhuru mataifa ya Magharibi hayakuwa na sababu ya kutia wasiwasi kuhusu uaminifu wa Tanzania. Tanzania ilikuwa upande wao moja kwa moja. Kwa hivyo, baada ya uhuru, ndiposa wakatanabahi kwamba Tanzania haiwaungi mkono kwa kila jambo. Hivyo, ushawishi wa Mwalimu ulikuwa ni kuwazindua Watanzania watambue kwamba, kuwa na msimamo wa kisiasa ni jambo bora si tu kwamba huifanya nchi isiyumbishwe na nchi za kimagharibi zenye nia ya kuendeleza ukoloni wao kwa Waafrika lakini pia huipelekea nchi ikapiga hatua mbele kimaendeleo

**Tafsida kengeushi**: *Wanapodai kwamba Tanzania inawachukia; … ni fikra za kipumbavu* (UK 5:4: MUSW)

Taswira ya kauli hizi ni ushupavu wa maongozi bora ambapo kwa muktadha wake ilikuwa ni mataifa ya kimagharibi watambue kwamba matendo waliyowafanyia Watanzania ndiyo majibu ya Watanzania kwa leo yake na "***wanapodai kwamba Tanzania inawachukia"*** ni wafanye tafakuri ya kina; na ikiwa wataendelea kuulalamikia ulimwengu basi ni watambue kwamba hizo ni "***fikra za kipumbavu".*** Ni watambue kwamba si tu kwamba ukoloni mambo leo hauna nafasi tena katika nchi ya Tanzania; lakini pia itachukua muda kuzifuta fikra za Watanzania kuhusu madhila waliyofanyiwa (na hao Wakoloni). Kwa hivyo, inawapasa (Wakoloni) watambue kwamba uvamizi wao kwa nchi ya Tanzania na pengine Afrika kwa ujumla daima utabakia kuwa ni historia ya milele.

Madhila ya Wakoloni ya kuzihodhi mali za Watanzania na hata kuwafanya Watumwa katika ardhi yao ni kumbukumbu ambayo ni muhali kufutika hasa ikisadifu kwamba wahujumu hao (Wakoloni) hadi leo hawajamakinika kuwaomba radhi Watanzania kuhusu makosa waliyowatendea: ya kuwavamia katika arhdhi yao, kuzichukua mali ghafi zao kwa nguvu; na kuzipeleka kwa ajili ya uzalishaji wa viwanda vyao huko Ulaya. Kuwafanya Watumwa kinguvu kwa ajili ya maslahi yao (hao Wakoloni), kuliwafanya Watanzania wakajitoa muhanga na hatimaye wakajikomboa na kuwa huru. Hivyo, ni ufahima wa kauli hizo kwamba, hata kama wakitanabahi madhila yao, historia haitafutika kwa vizazi vilivyopo na vijavyo ingawa kuomba radhi ni jambo lenye kuonyesha utu bora. Kwa hiyo, Mwalimu hakuona masiko katika hoja za Wamagharibi (Wakoloni) - za kulalama kwamba Watanzania hawawasemi kwa wema; aliziona ni legevu. Zaidi ya hayo, aliwataka Watanzania watambue kwamba malalamiko hayo ni ya kujivua gamba. Watanzania ni watambue kwamba wao ndio wanaostahili kuombwa radhi kwa madhila waliofanyiwa na hao wa Magharibi – Wakoloni.

**Takriri**: "*Taifa lenye misingi ya heshima na usawa na binadamu, misingi yetu ya uchumi itapasa ituongoze katika siasa ya kutofungamana na upande wowote. Lakini si hayo tu yaliyotufanya tushikilie siasa ya kutofungamana na upande wowote. Siasa hii inaambatana na fikra za uhuru wa taifa letu ikiwa tutashikamana na moja ya pande hizi mbili zinazoshindana, na kuchukia ule wa pili, itatubidi tufikirie tena siasa yetu yote ili ifanane na upande ule tunaouegemea, na hatuwezi tena kufikiria mambo yatakayowasaidia Watanzania. Kwa hiyo haita eleweka kama tukiegemea upande mmoja, kwa sababu ya utajiri wao na maguvu yao, halafu tena tutende mambo kinyume cha fikra na faida ya upande ule, hata kama fikra hizo zimeanzishwa na yale mataifa makubwa peke yake. Maana yake ni kwamba uhuru wetu wa kuunda siasa yetu wenyewe tutakuwa tumeupoteza* (UK 5:2: MUSW)

Katika matamko hayo, Tanzania ndiyo inayorejelewa kama taifa lenye misingi ya heshima na usawa kwa binadamu. Kwani hiyo ndiyo itikadi ya ujamaa iliyopaswa kufuata janibu hizo. Taifa la Tanzania liliamua kufuata mkondo wa kati (siasa za kutofungamana na upande wowote) ili Watanzania waweze kujivunia uhuru wao kamili. Kwa Tanzania ilikuwa ni uoni wake kwamba kuegemea upande wa Mashariki kungeikosesha nchi hiyo misaada iliyohitajika kwa ajili ya maendeleo yake. Hata kama nchi za Mashariki zingetoa michango yake lakini isingekidhi mahitaji yanayoongezeka kila uchao. Vivyo hivyo, upande wa Magharibi ungerejelewa na kupewa kipaumbele zaidi taifa lingekosa mengi kwani akusaidiaye ndiye muamuzi kuhusu kiasi cha msaada atakachokupa. Huwezi kumlazimisha. Zaidi ya hayo, misaada hiyo inakuwa imefungwa minyororo chungu nzima kwa maana ya

kumnufaisha mtoaji (Mara nyingi huambatana na masharti magumu). Ndiyo maana Mwalimu akasema ***“ujanja unahitajika”*** ili kudumisha mahusiano mema na nchi za kimagharibi (Wakoloni).

Mwalimu anazirejelea nchi za Magharibi kwamba ni nchi zenye “***maguvu***” kwa maana ya utajiri wa kibabe. Kwa ufahima kwamba utajiri walionao unatokana na maguvu kwa maana ya kuzitawala nchi nyingine bila ya ridhaa yao na kuzichukua mali ghafi za nchi hizo na kuzipeleka katika viwanda vyao bila ya ridhaa yao; na kwa kuwafanya watumwa kwa ajili ya viwanda vyao na mashamba yao. Hivyo, njia zinazoziwezesha nchi hizo za kimagharibi zikawa tajiri sio njia halali. Fauka yake, hata ikiwa ni kuzisaidia nchi zinazokulia kiuchimi; pia kwao si jambo rahisi. Kwani wakizisaidia ni lazima misaada hiyo iambatane na masharti magumu. Huangalia ni kwa jinsi gani wataendeleza ukoloni mambo leo kwa maana ya kuzitenza nchi hizo nguvu na kuendeleza uchumi wao kibabe ume.

### 4.4.9 Maudhui kuhusu Uwajibikaji

Ilikuwa ni ghera ya Mwalimu katika maongozi yake kuhakikisha kwamba taifa la Tanzania linajinasua kutoka katika hali duni ya kiuchumi iliyotokana na mikatale ya Wakoloni. Mwamko huo ulimpelekea kuwaasa Watanzania wote kuutumia uzima wa afya walionao katika kujiletea maendeleo, akiwahimiza (Watanzania) wajiepushe kwa tabia za wazembe na uzururaji hasa kwa wanaoitikadi kwamba "***umasikini wao ni mapenzi ya Mungu***". Imani hiyo ni ya kujivua utu kwa kuamini kwamba maisha yao hayana budi kuwa chini ya matajiri; ya kwamba matajiri hawana budi wawaonee huruma kutokana na hali zao duni za kutokuweza kujikimu kwa lishe, mavazi na malazi. Kwa Mwalimu imani hii aliiona ni ujauzito wa mawazo na yenye kuhitaji kupigwa vita kwa udi na uvumba. Kwa mpwito kwamba, kubweteka kwa kutokufanya kazi ilhali mtu sio kilema, mzee au mtoto mdogo ni kumtafuta Mwenyezi Mungu muhali kwa kutozishukuru neema alizowajaalia wanadamu kama vile: uzima wa afya, viungo kamili na mazingira faafu yenye kuwawezesha kujikimu katika mahitaji ya maisha ya kila siku.

Mwalimu aliwashajihisha Watanzania watambue kwamba, maisha ya Mtanzania yanaweza kuboreka siku hadi siku ikiwa umoja utafasiriwa katika uhalisia wa maisha ya kila siku na ikiwa ukupe utapigwa vita usipate mwanya katika misingi ya ujamaa na kujitegemea. Mwalimu pia aliwahimiza wananchi - Watanzania wasiridhike na mafanikio waliyoyapata kutokana na mipango ya muda mfupi waliyokuwa wamejiwekea mara baada ya kupata uhuru ambapo, kwa kiwango si haba, waliweza kujimudu kwa chakula, mavazi na malazi tofauti na

walivyokuwa wamewekwa katika kizimba cha Wakoloni hata ikawa hawana maamuzi yoyote katika ardhi yao. Mwalimu aliwashawishi Watanzania wayaone mafanikio hayo kama changamoto ya kuwafanya waongeze jitihada zaidi hususani katika kilimo ambacho ndio uti wa mgongo kwa sekta zingine kama vile afya na elimu na sio wengine kubweteka kwa dhana kwamba tofauti za uwezo wa kujimudu kimaisha ni majaaliwa ya Mungu.

#### 4.4.9.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Uwajibikaji

**Maswali ya kibalagha**: "*… Linalotupasa kufanya ni kuamka. Tumelala muda mrefu mno; na kusingizia kwa muda mrefu kwamba shida zetu ni amri ya Mungu. Mungu hakutupa ubongo wa kutumia? Mungu hakutupa mikono na viganja? Mungu hakutupa ardhi?* (UK 3:3: SU)

Hizi ni kauli za Mwalimu ambazo nia yake ni kudhihirisha ukinzani dhidi ya uoni duni wa baadhi ya watu waliokuwa wakidai kwamba, Mungu ndiye aliyewafanya wengine kuwa masikini na kuwajaalia wengine kuwa matajiri na kwa hivyo, suala la mtu kujitahidi kuipata riziki yake kuonekana si lakutiliwa maanani. Mtazamo ambao kwa Mwalimu Nyerere aliuona hauna mashiko. Ndiposa akawazindua Watanzania kwa kutumia balagha. **"*Mungu hakutupa ubongo wa kutumia? Mungu hakutupa mikono na viganja? Mungu hakutupa ardhi?*"** akimaanisha kwamba mwanadamu ni kiumbe asiyefanya tathmini kuhusu maumbile yake na ya viumbe wengine au mazingira yaliyomzunguka; ambapo angetanabahi kwamba mazingira yaliyomzunguka na viumbe wasio wanadamu ni kwa ajili yake, angetia bidii ili aweze kulifikia lengo la maisha yake hapa duniani. Aidha anetanabahi kwamba ***ubongo*** na ***akili*** ni ni kwa ajili ya kumwezesha kufikiri na kuamua kipi cha kufanya kabla ya kingine na kwamba ***Mikono*** na ***viganja*** ni viungo vinavyomwezesha mwanadamu kutendea kazi kama vile kulima na kuandika.

Wakati ambapo ***ardhi*** ni kibebeo cha utendeaji wa harakati zote za maisha ya mwanadamu,mwanadamu huendelea kuwa katika hali duni na kudai kuwa hakujaliwa utajiri Kwa hivyo, ikiwa lengo la jamii ni kuyatafuta maisha mazuri na yenye matumaini, ni mategemeo kwamba kila mmoja atayatenda mambo kwa ustahiki wake ili kuepuka unyonyaji katika utekelezaji wa malengo ya kijumla. Kwa hivyo, balagha iliyotumiwa na Mwalimu ilikuwa ni shime kwa Watanzania wote wawajibike ili waweze kujinasua kiuchumi kwa misingi ya ujamaa na kujitegemea. Kila Mtanzania mbiu iwe ni kuupiga vita uzembe na uzururaji nchini kote.

**Takriri**: *"... kwa sasa karibu watu wote wa Tanzania ni masikini, na nchi yetu ni masikini, hatujaweza bado kutoa mali hata yakutosha raia wetu wote waishi katika nyumba nzuri, wakapata chakula na nguvu nzuri. Azimio la Arusha halijabadili hali hiyo. wala kitabu kile cha ujamaa vijijini. Azimio hili limeonyesha tu njia ya kupitia. Iliyobaki ni sisi kufanya kazi: kufanya kazi kwa bidii, kwa akili na pamoja. Hapo ndipo tutakapoona faida ya Azimio hilo.* (UK 10:2: SU)

Kauli ***"… kwa sasa karibu watu wote wa Tanzania ni masikini, na nchi yetu ni masikini"*** ni mtagusano wa fikra ambao Mwalimu anamtaka kila Mtanzania amakinike na atathmini hali halisi ya maisha hususani katika malazi, mavazi na chakula. Kwamba nchi bado ni changa. Kwa takriri neno ya: **"*Umasikini; na Azimio*"** - ametoa wito kwa Watanzania wote akiwataka walifasiri Azimio la Arusha katika uhalisia wa maisha ya kila siku; na kwa vitendo. Ushawishi wake ni kwamba, ikiwa Watanzania wangelielewa vyema kuhusu Azimio la Arusha, wangelishirikiana kwa kila jambo na kwa hivyo kujiletea maendeleo kwa mwendo kasi.

**Takriri**: *"Lazima tujifunze kufanya kazi kwa akili, kama kuna mafunzo tunayoweza kusoma darasani, ama kama kuna vitabu tunavyoweza kujisomea wenyewe, basi lazima tusome. Lakini vile vile lazima tuwe radhi kujifunza kutoka kwa watu wengine wenye ujuzi zaidi au ujuzi tofauti. Lazima tujifunze kutoka kwa watuwengine ... Mungu hakutupa kitu bora kuzidi elimu na kuunoa ubongo ni jambo la lazima."* (UK 11:1: SU)

Kauli: ***"Lazima tujifunze kufanya kazi kwa akili"*** ni msisitizo kuhusu swala la watu kuelimika; kama suluhisho la kufanya mambo kwa ufanisi. Ulikuwa ni uoni wa Mwalimu kwamba, watu wakiwa ni wataalamu wa fani mbalimbali wataleta maendeleo kwa haraka. Wakati ambapo takriri neno **"*Lazima tujifunze kutoka kwa watu wengine*"** huu ulikuwa ni wito wake kwa Watanzania watambue kwamba kuitafuta elimu ni jambo la lazima kwa kila mwanadamu na haijalishi eneo au nani anayekuvyaza elimu hiyo: awe mdogo au mzee sana na ama awe hakusoma au kama anatoka katika kabila jingine, au hata katika taifa jingine. Kauli kwamba **"*Mungu hakutupa kitu bora kuzidi elimu"*** ni uamsho kwa watu wote kutambua kwamba, Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuumba mwanadamu na akamjalia elimu kama kibebeo cha kumwezesha kuyafikia malengo ya kuumbwa kwake hapa duniani kwa ufanisi. Kwa msisitizo zaidi Mwalimu anasema: ***"na kuunoa ubongo ni jambo la lazima."*** – ni ushawishi kwamba, Watanzania na pengine wanadamu wote kwa ujumla hawanabudi kuzinduka na kutambua kwamba, elimu ni neema ambayo mwanadamu amejaliwa na

Mwenyezi Mungu ili aweze kuelimika na kuweza kuyafanya mambo yake hapa duniani kwa ufanisi na ili aweze kuishi kwa furaha na amani hapa duniani na mwisho wa mauko yake uwe mwema pia.

**Takriri**: *"... dunia inajua, na Afrika inajua, kwamba pamoja na udogo wa uwezo wetu, tumefanya jitihada za dhati kuzitekeleza shabaha hizo mbili: kuleta maendelezo kwa wananchi wetu, na kuwasaidia wenzetu katika Afrika kujikomboa. Nasema dunia inajua, na Afrika inajuwa, kwamba pamoja na udogo wetu na unyonge wetu lakini shabaha hizo tumejitahidi kuzitekeleza kwa dhati".* (UK 4:3-4: OIA)

Kauli ***"… dunia inajua, na Afrika inajua";*** ni msisitizo kwa hadhira itambue kwamba yanayoongelewa yana mashiko na kwamba mbali na uchanga wa nchi ya Tanzania mbele ya nchi tajiri duniani; iliweza kutekeleza shabaha zake ilizojiwekea mara baada ya kupata uhuru. Tanzania iliweza kujimudu si haba katika suala la maendeleo ya nchi kama shabaha ya kwanza. Pia shabaha ya pili waliifikia, ambayo ilikuwa ni kuzisaidia nchi za kiafrika kujikomboa. Kwa hivyo, ulikuwa ni ushawishi wake (Mwalimu) kwa Watanzania kwamba wasivunjike moyo ingawa wanaonekana duni mbele ya mataifa tajiri duniani. Watambue kwamba uhuru wao ni amana wanayopaswa kuulinda hasa inaposadifu kwamba mengi ya mafanikio yamekwisha kuonekana kivitendo

**Tashbiha, takriri na fumbo**: "*... lazima tuwe tayari kufanya kazi pamoja kama, raia tuliosawa kabisa, kwa faida yetu wote. Tembo ni mmoja katika wanyama wakubwa kabisa katika Tanzania, lakini hatengenezi chochote; maana kila Tembo huishi kwa kijichumia peke yake lakini nyuki, lau kama wadogo, hufanya kazi pamoja hutoka akatafuta unga wa maua na kuuleta katika mzinga. Kutokana na unga ule jamaa ya nyuki kwa pamoja hutengeneza asali, ambayo wanaweza kula wakati wa shida; isipokuwa kama binadamu ametia mrija wake na kuwaibia nyuki asali yao. Kadhalka mchwa hufanya kazi kwa faida ya wote. Ingawa ni wadudu wadogo sana, mchwa wanafanya kazi pamoja na kujijengea majumba makubwa ambamo wao na rafiki zao wanaweza kuishi kwa salama na raha ".* (UK 11:2: SU)

Fahiwa ya kauli hizi ni kwamba, ukubwa si hoja, kwani tembo pamoja na kwamba ni mnyama mkubwa sana, hatengenezi chochote. Hoja ni kushirikiana katika kufanya kazi na kuendesha miradi mbalimbali kama jamii ya nyuki inavyofanya. Kushirikiana ndiyo njia pekee inayoweza kuwaletea wananchi mafanikio na hivyo kuwafikisha kwenye ustawi na maendeleo yanayohitajika. Maendeleo hayo yakisha patikana yatawavutia wanaojifanya

kuwa wakubwa, waanze kunyemelea (nchi ya Tanzania) ijapokuwa ni changa waiibie mali yake kama wanadamu anavyowaibia nyuki asali yao. Kwa hivyo watu wakutoka katika nchi changa kama vile Tanzania, wamefananishwa na nyuki huku wanaotoka katika nchi za wababe wakifananishwa na tembo. Wababe hawana lolote ila tu huishi kwa kutia mirija yao katika asali ya nchi changa ambayo ni mali asili ya nchi hizo. Endapo Waafrika watashirikiana na kufanya kazi kwa pamoja watanufaika zaidi na pengine kuwaogofya wezi na wanyonyaji. Hii ni kwa sababu, kama mchwa watajenga ngome yao ambayo itawahakikishia amani na usalama. Wataweza kujenga nyumba nzuri watakamoishi na mashirika makubwa yatakayowatoa kwenye unyonge na umasikini.

Ushawishi katika matamko hayo, ambao umevyazwa mitindo mbalimbali ya kibalagha kama vile matumizi ya tashbiha, takriri neno na mafumbo, umekusudiwa kuwahimiza wasikilizaji kufanya kazi kwa pamoja. Ni kama Mwalimu anatoa changamoto: wadudu wanafanya kazi kwa pamoja na nyinyi basi fanyeni hivyo, wadudu wanachuma mali nyingi kupitia ushirika na nyinyi fanyeni hivyo, wadudu wanajenga majumba yao kwa pamoja ili wajikinge dhidi ya maadui zao na nyinyi waigeni ili msalimike. Kumaanisha kwamba maendeleo yanaweza kupatikana ikiwa watu watafanya kazi kwa juhudi na maarifa.

**Takriri na tashtiti**: *"Mabwana shamba, Mabwana Ushirika, Wanasiasa, Watumishi wa Afya vijijini. ... watapelekwa kwanza katika vijiji vya ujamaa shule mpya, hospitali mpya, maji nakadhalika, yatapelekwa kwanza katika vijiji vya ujamaa; vikundi vya watu wanaofanya kazi kwa pamoja kwa njia ya ujamaa au ushirika lazima pia visaidiwe kwanza kwa fedha za maendeleo ya mkoa"* (UK 11:5: MU)

Ni katika enzi za Azimio la Arusha chini ya siasa ya ujamaa na kujitegemea; ambapo ulikuwa ni wito wa Mwalimu kwa Watanzania watambue kwamba ukipaumbele wa serikali utakuwa ni kwa wale walioamua kuishi kwa pamoja kwa nia ya kuleta maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Maneno: ***"Mabwana shamba, Mabwana Ushirika, Wanasiasa, Watumishi wa Afya vijijini".*** Mrudiorudio wa mofu ***{ma}*** na ***{wa}*** – katika mwambatano wa maneno yanayorejelea wataalam mbalimbali ni msisitizo wa Mwalimu kwa wataalamu ambao kwa vipaji na kwa fani mbalimbali walizojaaliwa akiwataka watambue kwamba, wao ndio mhimili wa serikali katika kuelekeza jamii ili waweze kuwasaidia katika kuzibadili hali zao duni na kuzifanya ziwe bora kitaalamu zaidi. Fauka ya hivyo; fahiwa ya takriri neno {***ma}*** ***{wa}*** ni utanabahisho kwa Watanzania - kuonyesha jitihada za serikali za kuitafsiri siasa ya ujamaa na kujitegemea kivitendo; Lakini kwa maana ya kipi kipewe kipaumbele kulingana na

raslimali zilizomo serikalini. Kwa hivyo, ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania ni kuwataka watambue kwamba serikali yao ipo nao bega kwa bega katika kuhakikisha kwamba maisha ya Mtanzania yanaboreka kiuchumi na kisiasa.

**Tafsida kengeushi na takriri**: "… *Msingi wa kazi katika kijiji cha ujamaaa ni kujitegemea; lazima iwe hivyo. Itakuwa upumbavu kwa TANU na kwa serikali kuwashawishi watu kuanza au kujiunga katika kijiji cha ujamaa, kwa ahadi za misaada kutoka nje. Kufanya hivyo ni makosa makubwa. Watu lazima waungane katika kijiji wakitambua kwamba juhudi yao itawaletea manufaa zaidi; na kwamba maisha yao yatakuwa salama zaidi, na ya raha zaidi kwa sababu kila mmoja ana wajibu kwa mwenzake.* (UK 17:1: MU)

Hizi ni kauli zinazoirudi serikali, hususani kwa viongozi ambao daima huzitoa ahadi zisizotekelezeka kwa raia wake hasa katika kipindi cha uchaguzi. Ili kujipatia ushindi, raia hupewa matumaini ambayo hata baada ya hatamu kuwa mikononi mwa aliyeahidi, zile ahadi zinakuwa haziwezakani kutekelezeka. Kwa hivyo, Mwalimu anakionya chama na serikali kwa kusema: ***"Itakuwa upumbavu kwa TANU na kwa serikali kuwashawishi watu kuanza au kujiunga katika kijiji cha ujamaa, kwa ahadi za misaada kutoka nje. Kufanya hivyo ni makosa makubwa"*** ambapo kwa mbadala wake ilikuwa ni Watanzania washawishiwe kutambua kwamba maendeleo yao yataletwa na wao wenyewe kwa juhudi na maarifa yao wenyewe. Kwa mbiu kwamba, maana ya siasa ya ujamaa na kujitegemea ni utekelezwaji wa vitendo kwa usanjari wa ardhi nzuri, siasa safi na uongozi bora, ambapo kwa Watanzania hawanabudi kujivunia kwa majaliwa hayo.

**Usimulizi, vihisishi na takriri**: *Urais wangu: nilikuwa rais wenu, nilifanya juhudi za kukomboa eneo hili linaloitwa Tanganyika. Lakini kwa upande wa uongozi wangu niliwaongoza ninyi katika nchi huru inayojitawala na raia duniani wa nchi huru inayojitawala, niliwaongozeni katika nchi inayoitwa Tanzania. Tanganyika niliwaongozeni kwa muda mfupi tu, tangu Desemba 1962 mpaka Aprili 1964 basi! Kipindi changu kingine chote, niliongoza nchi inayoitwa Tanzania siyo Tanganyika.* (UK 7:4: TTT)

Hizi ni kumbukizi za Mwalimu Nyerere kuhusu jinsi alivyokubalika katika kuwaongoza Watanganyika na baadaye Watanzania; hata ikawa ni ang'atuke kwa ridhaa yake mwenyewe. Ni ukubalifu kutokana na maongozi yake yaliyokuwa mema. Na ni historia njema kwa vizazi vilivyopo na vijavyo. Kauli *"**niliwaongozeni katika nchi inayoitwa Tanzania. Tanganyika niliwaongozeni kwa muda mfupi tu**"* Ni kumaanisha kwamba Mwalimu alifanya jitihada si haba za kuwaunganisha Watanganyika na Wazanzibar, wakawa kitu kimoja hata ikapelekea

kuzaliwa Tanzania huru na yenye amani. Kwa muda mfupi sana, ambapo kwa kumbukizi akisema *"**tangu Desemba 1962 mpaka Aprili 1964 basi".*** Kumbukizi ambazo ni ushawishi kwa Watanzania kutambua kwamba umoja chini ya uongozi bora ni silaha toshelezi katika kuyafikia malengo ya nchi.

Ubainifu wa Mwalimu kuhusu shukrani zake kwa Watanzania; ni utanabahisho kwa Watanzania kutambua kwamba Mwalimu hakuwa mwizi wa fadhila kwa wema waliomfanyia. Kwa hivyo, (Watanzania) hawa nabudi kumakinika kuhusu kuwepo kwa uongozi na utawala bora katika himaya yao hususani kila unapowadia uchaguzi - ili kuiendeleza historia ya umoja na amani iliyodumishwa na Mwalimu enzi za maongozi yake; baada ya kuwa ilitekwa nyara na Wakoloni kabla ya kuzaliwa Tanganyika na baadaye Tanzania. Ulikuwa ni utanabahisho kwa Watanzania waikumbuke asili ya umoja ya kwamba wakishirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa. Na kwa hivyo, kauli hizi ni wito na changamoto kwa Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanaudumisha uasili wa pande hizi mbili; na iwe ni kumbukizi njema kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

**Maswali ya kibalagha**: *" ... 'Mwalimu Benki ya Dunia'. Benki ya Dunia hawa nani? Mungu gani mpya huyu anaitwa Benki ya Dunia? ... hawa ndio nani?, 'tangu lini shirika la fedha la Kimataifa limegeuzwa kuwa wizara ya Fedha ya Kimataifa?' Hivi ni kweli hatuwezi kukataa sasa?* (UK 23: 3: TTT).

Hizi zilikuwa ni tafakuri za Mwalimu baada ya kubaini kwamba baadhi ya viongozi waliokuwa wameshika hatamu za uongozi mara baada ya kung'atuka kwake. Waliingiwa na hofu baada ya kutishiwa kunyimwa misaada - ikiwa hawatafuata matakwa ya Benki ya Dunia. Na ndio Mwalimu akiuona ulalami huo ni sawa na ujauzito wa mawazo hata ikawa ni awaulize: (Watanzania): **Benki ya Dunia hawa nani**? Kwa maana ya kwa nini waogopewe ilhali Tanzania ni nchi huru na yenye uwezo wa kujiamulia mambo yake yenyewe. Katika kuwataka Watanzania kuyaelewa majukumu ya shirika hilo, aliuwauliza tena: '***tangu lini shirika la fedha la Kimataifa limegeuzwa kuwa wizara ya Fedha ya Kimataifa?*** Kumaanisha kwamba si shirika lililopaswa kuingilia mamlaka ya nchi huru. Lina majukumu yake na halipaswi kuiwekea nchi yoyote vikwazo katika maendeleo yake hasa uhuru wa kujiamulia mambo yake yenyewe. Fauka ya hayo, Mwalimu aliyarudi mamlaka ya Tanzania (uongozi) kwa mshangao akiwauliza: ***Hivi ni kweli hatuwezi kukataa sasa?*** Kwa uoni kwamba viongozi wanapaswa kuyatetea maslahi ya nchi yao na sio kukubali kuburuzwa kibubusa kwa kuhofia kunyimwa misaada ilhali misaada hiyo inaipelekea nchi kupoteza utu

na heshima kwa raia wake na kuifanya ikose hadhi zaidi ya kuwa na uhuru wa bendera fuata upepo - mbele ya mataifa mengine duniani.

**Istiara na tashbiha**: *"Tumelijenga taifa pamoja. Hata Malaika Gbrieli asingeweza kuijenga Tanzania peke yake sembuse binadamu dhaifu kama mimi. Hata kama Malaika Gabrieli angepata msaada wa Mawaziri na watumishi ambao nao ni Malaika wenzake bado asingeweza kuijenga Tanzania. Nyinyi wananchi wa Tanzania, kwa kazi zenu za pamoja na kazi za kila mmoja peke yake, mmeijenga Tanzania kama ilivyo sasa: Taifa la watu wenye umoja watu wanaojiamini, na wanaojivunia nchi yao nawashukuruni sana".* (UK 2:3: KW)

Kujenga taifa ni kuchangia ukuaji na uendelezaji wake katika nyanja mbalimbali kama vile. uchumi, siasa na kadhalika. Mwalimu Nyerere alihusisha kitendo cha ujenzi huo na juhudi za wananchi wote. Matumizi ya mofu nafsi ***{tu}*** ni kuonyesha uwezekano wa utekelezwaji wa jambo la kuijenga nchi kwa umoja ambapo mwambatano wa maneno: ***{pamoja}, {mmeijenga}*** sanjari na mofu hiyo, yanawakweza Watanzania mbele ya ulimwengu kwamba waliweza kuyatenda mambo ambayo mataifa mengi hayakutarajia wangeweza. Lakini kwa umoja wao, iliwezekana.

Na katika kudhihirisha shukrani zake kwa Watanzania hususani kwa walivyoshirikiana katika kuijenga nchi yao, Mwalimu alisema: "***Hata kama Malaika Gabrieli angepata msaada wa Mawaziri na watumishi ambao nao ni Malaika wenzake bado asingeweza kuijenga Tanzania.*** Kwa ufahima kwamba (***Gabrieli***): ni kiongozi mkubwa wa malaika wote na mwenye hadhi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu: si wenye kumuasi Mwenyezi Mungu. Lakini lau kama si kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hata wakiungana malaika hao kamwe hawawezi kuijenga nchi; mintaarafu Tanzania. Kwa nafsi lawama akisema: "***sembuse binadamu dhaifu kama mimi***" – ambapo nia yake ni kuwadhihirishia Watanzania watambue kwamba, mwanadamu ni kiumbe dhaifu mbele ya Muumba wake; watambue kwamba pasi na mapenzi ya Mwenyezi Mungu mwanadamu si chochote si lolote katika kuyatenda mambo mithili ya kuijenga nchi hata ikawa ni yenye amani, upendo na ushirikiano. Hivyo, ni kwa ushirikiano na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu. Ndiposa Watanzania waliweza kuijenga nchi yao; si tu kiuchumi na kisiasa; lakini ikawa ni yenye amni, utulivu na upendo.

Hivyo, mbali na Mwalimu kubaini kwamba hakuwa mwizi wa fadhila kwa Watanzania aliowaongoza kwa muda mrefu, falsafa aliyoindeleza kupitia matamko yake ni ushawishi toshelezi kwa Tanzania wadumishe umoja wao ili nchi yao iendelee kuwa imara kiuchumi na kisiasa mbele ya mataifa mengine ulimwenguni.

**Tashbiha**: *(Pamoja na kushindwa kuyafikia malengo; ni lazima tukumbushane.) Matatizo yetu ya sasa, na kushindwa kwetu, kusiachwe kukaficha mafanikio yetu makubwa zaidi. Kwa kawaida watu wengine wanayatambua au kwa sababu ya yale wanayoyaona katika nchi nyingine, au kutokana na uchunguzi wao wenyewe. Maana sisi ni sawa na mtu aliyechanjwa chale za kuzuia ugonjwa wa ndui, ambao sasa hawezi kuupata. Mkono wake unavimba na anasikia maumivu kidogo kwa sababu ya zile chale … na angeweza akakufuru na kusema kuwa ni afadhali angekataa kuchanjwa.* (UK 5:2: AA)

Kawaida, kama utafanya kitu cha maana, huna budi kuweka mbele malengo kadhaa ambayo ungependa uyafikie katika kipindi maalum. Hiyo ndiyo desturi ambayo hufuatwa katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Malengo yanayowekwa na serikali mbalimbali huwa ni ya kufikiwa katika vipindi vifupi vifupi na virefu pia. Hata hivyo baadhi ya malengo hayo yanaweza kufikiwa na baadhi yake yanaweza yasifikiwe kutokana na changamoto kadha wa kadha wanazopata viongozi. Hali hii hufasiriwa kama kufanikiwa na kushindwa katika kuyafikia matlaba hayo. Kwa vile binadamu ana madhaifu yake na kwa vile ni mwepesi wa kusahau, hawakumbuki mafanikio ambayo nchi imeyapata. Badala yake anakumbuka tu yale ambayo kwayo yanashindikana. Ndiyo maana Mwalimu akatoa matamko ambayo kwayo alikusudia kuwazindua wananchi wenye tabia hiyo. "***Ni lazima tukumbushane***" kwa sababu historia inaweka kumbukumbu isiyoweza kufutika. Ni kweli shida zipo lakini ufanisi uliofikiwa ni mkubwa zaidi ukilinganishwa na shida zinazoikumba nchi.

Ili kuwashawishi wasikilizaji wake wafikie kiwango cha utambuzi wa hali halisi alianza na kukubali kushindwa kwani asiyekubli kushindwa si mshindani. Halafu akafuatiliza kauli hiyo na tamko "***Lazima tukumbushane"*** ili kuwashtua waliosahau ama wale walioghafilika watambue kwamba ijapokuwa kuna matatizo, lakini mafanikio waliyoyapata pia yalikuwa si haba kwa watu kuyashukuru; kisha akaona kuna uhitaji wa kuyaweka mambo wazi zaidi na karibu na akili ya msikilizaji; ambapo aliifananisha hali inayolalamikiwa sawa na hali iliyozoeleka ya kupata maumivu kidogo ili unusurike kutokana na maradhi hatari. "***Ugonjwa wa ndui***" ni kiwakilisho cha matatizo yanayoikumba nchi huku "***chale***" zikiwakilisha mikakati ya kuondokana na matatizo hayo. Ingawa mikakati inayowekwa na serikali inaweza kuwaumiza wananchi, lakini ikivumiliwa, matatizo yataisha na kusahaulika jinsi magonjwa sugu yanavyosahaulika kwa tiba mjarabu.

Chembelecho matumizi ya lugha kwa maudhui yaliyoendelezwa, mbiu yake ilikuwa ni ukumbusho kwa Watanzania wayashukuru mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka kumi ingawa walikuwa wakitamani mafanikio zaidi, hasa kwa kumbukizi kwamba, Watanzania:

(i) Waliweza kudumisha umoja wao kivitendo hasa kwa kupunguza wingi wa tabaka la wenyenacho na la wasionacho (UK 2:3: AA)

(ii) Waliweza kuwa na mwamko wa kijamaa, hasa kwa kutambua kwamba ni jambo baya wengine kuishi maisha ya anasa; wakati wengine wanaishi maisha ya dhiki; na kwa hivyo suala la ushirikiano kwa faida ya wote lilipewa ukipaumbele. Kwa maana ya tabia inayokubalika na wananchi; mtu akipimwa kwa vitendo vyake na siyo kwa mapato yake; yaani kufikiria manufaa ya wananchi wote kuliko mtu kujivunia mali kwa sababu ya mali tu!. (UK 3:1: AA)

(iii) Waliweza kuwa wabunifu wa mbinu mbalimbali katika kuwezesha kuimarisha ujamaa: mafanikio kuhusu vyombo vya umma vinavyoshughulikia mambo ya fedha, ya kuzalisha mali, na ya ustawi wa jamii ambavyo ni vya lazima kwa kutimiza mahitaji ya watu.(UK 3:2: AA)

(iv) Uwezekano wa huduma za afya, elimu na usafirishaji wa umma. (UK 3:3: AA)

(v) Lakini pia harakati ya kuzikomboa nchi nyingine za bara la Afrika; ambapo miongoni mwa wapigania uhuru si tu kwamba walipewa hifadhi lakini mbinu na mafunzo ya kuwezesha kuzikomboa nchi zao; Watanzania walitambua kwamba uhuru wao hauwezi ukawa safi hadi pale bara lote la Afrika litakapokuwa huru.

Kwa hiyo, ushawishi wa Mwalimu kwa tashbiha aliyoitumia ni uzinduo kwa Watanzania wote kukumbuka yanayowapitikia katika mpwito wa maisha yao ili iwe ni sababu si tu ya kuwapelekea waweze kujipanga kwa mafanikio zaidi; lakini kuweza kumshukuru Mungu kwa jitihada walizozifanya na kwa kuwajalia uhai ambapo huwenda viumbe wengine hawakujaliwa hivyo.

### 4.4.10 Maudhui kuhusu Uongozi Bora

Tathmini ya Mwalimu kuhusu maongozi ya nchi ya Tanzania mara baada ya kung'atuka kwake ni kwamba maongozi yake yalikuwa yana tija si haba. Pamoja na hayo, kulikuwa na pengo lililohitajiwa kuzibwa kabla ya kung'atuka kwake. Pengo hilo lilihusu wadhfa wa urais wa nchi ambao ulikuwa haujawekewa kipindi maalum caha utawala. Mwalimu alitekeleza dhima ya kuwashawishi wananchi Watanzania wakubaliane naye kwamba baada ya

kung'atuka kwake, lazima kuwepo kipengele maalumu katika katiba ya nchi kinachoonyesha ukomo wa miaka kumi kwa kila rais atakayechaguliwa kuliongoza taifa la Tanzania.

Viongozi wengi huwa hawapendi kukosolewa na inapokuwa kuna mwanya wa kuutumia wadhifa walionao. Hujiwekea vipengele vya kujilinda zaidi ambapo hatima yake huwapelekea wananchi kumuondoa kwa nguvu madarakani. Jamabo aambalo linaweza kusababisha kumwagika kwa damu. Kwa hiyo, Mwalimu aliwarai wananchi wote waungane kwa pamoja katika kuuziba mwanya huo mapema kabla ya rais aliyekuwa akitarajiwa baada ya kung'atuka kwake ili kuilinda heshima, utu, amani, utulivu, upendo na mshikamano uliokuwa ukilitangaza taifa la Tanzania ndani na nje ya mipaka yake.

Fauka ya rai ya Mwalimu kuhusu ukomo wa urais mara baada ya kung'atuka kwake, taarifa za kung'atuka kwake pia zilipokelewa na kutafsiriwa kwa namna tofauti tofauti. Baadhi ya wananchi waliingiwa na wasiwasi kwamba huenda rais ajaye asiwe na uwezo wa kuliongoza taifa la Tanzania kama alivyokuwa Mwalimu Nyerere. Yeye aliiwezesha nchi kujinasua kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni lakini pia kulifanya taifa la Tanzania kuwa lenye amani, upendo na mshikamano miongoni mwa Watanzania na kwa wasio Watanzania. Lakini pia baadhi ya Watanzania walifurahia kitendo cha Mwalimu Nyerere cha kung'atuka uongozini kwa uoni kwamba uongozi wake yalikuwa ni wa kiimla na ama wa kidikteta; kwamba aliloliamua yeye hapakuwa na fursa kwa mtu kujitetea au kutoa mchango wake kwa manufaa ya taifa.

Baadhi ya wananchi (tapo la pili) walimsawiri Mwalimu kwamba, (Mwalimu) alijiweka katika hali ya utukufu; na ikawa Watanzania ni wamuendee mbio kibubusa kwa hofu kwamba, kinyume na hivyo wasingeipata salama katika maisha yao. Kwa hivyo, kutokuwepo kwake tena madarakani - walihisi wangepata fursa ya kuyashawishi matakwa yao kadiri wapendavyo; na ikibidi pia kulishawishi jeshi lishike hatamu za kuliongoza taifa la Tanzania ikiwa rais wa baada yake hatakidhi viwango (hatakuwa na sifa kulingana na matakwa yao) katika kuliongoza taifa la Tanzania. Mtazamo huu wa pili kwa Mwalimu Nyerere aliuona ni uzandiki wa mabepari waliotaka kupandikiza fikra zao dhidi ya mfumo wa ujamaa ambao yeye aliupa kipaumbele kwa maana ya kuwataka wananchi wa Tanzania washirikiane kwa kila jambo la kuiendeleza nchi yaoili kulijenga taifa lenye upendo na amani. Kwa hivyo, alionekana kwamba amekuwa kero mtazamo ambao kwake yeye ilikuwa ni fahari ya maongozi yake kutekeleza uadilifu kwa Watanzania wote.

#### 4.4.10.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Uongozi bora

**Takriri, swali ya kibalagha na tashhisi**: *Nchi yetu ina umoja, hiki ni kitu kikubwa zaidi kwetu, mimi na dhani, kuliko kusema kweli, kitu kingine chochote. Umoja huu tumeupata; najua viko vitu vingine ambavyo vimetusaidia kuupata huu umoja; lakini umoja wenyewe sasa ndilo tunda letu kubwa zaidi kuliko kitu kingine, ndiyo ngao yetu kubwa sana, na matumaini yetu. Hayo mengine yaliyobaki tutayapata kama tutaendelea na huu umoja wetu (UK 6:2: AW). Sasa mimi siyo mkorofi kwa kweli, mkorofi ni nchi yetu. Mimi nilikuwa ninajitahidi kusemea nchi, na kuisemea nchi bila mchezo na kuonyesha msimamo wa nchi yetu. Sasa wako watu wanaodhani kuwa baada ya Oktoba mwaka huu Jeuri itakwisha, sijui jeuri ipi? Nadhani wanatuombea hata Umoja wetu uishe! Tutatafuta Rais ambaye atasimamia Umoja wetu. Hatuwezi kutafuta Rais ambaye hataki Umoja.*" (UK13:3: AW).

Hizi ni kauli alizozitoa Mwalimu Nyerere kutokana na rai ya kung'atuka kwake; na mapendekezo yake kuhusu ukomo wa urais kwamba - uwe ni wa miaka kumi kwa yeyote atakayefuatia mara baada ya kung'atuka kwake. Taarifa za kung'atuka kwake zilipokelewa na kutafsiriwa kwa namna tofauti tofauti. Wengine waliingiwa na wasiwasi wakidhani kwamba Mwalimu akiachia uongozi nchi itayumba. Wakifikiria kwamba huenda rais ajaye asiwe na uwezo wa kuliongoza taifa kama alivyokuwa Mwalimu Nyerere. Wengine wakifurahia kung'atuka kwake kwa imani kwamba kilichokuwa kikwazo kwao hatma yake imefika (***jeuri imefika kikomo***). Uoni huo ndio uliompelekea Mwalimu kuuliza: ***"Jeuri itakwisha, sijui jeuri ipi?"*** Katika matamko hayo kuna matumizi ya ala fungamanishi kadhaa. Ala hizo ni kama vile kiwakilishi nafsi {***mimi***}, {***ni***}, {- ***tu***-}, vimilikishi {***yetu***}, {***wetu***} takriri neno {***sasa***}, {***nini***}, {***mkorofi***}, {***kusemea***} na {***jeuri***}; virai {***nchi yetu***}. Aidha, kuna matumizi ya swali la kibalagha "***sijui jeuri ipi?***" Shabaha ya kufanya hivyo, ni kuliwekea msisitizo jambo linalozungumziwa. Sehemu mbalimbali za matamko hayo zimefungamanishwa kwa shabaha ya kuyaweka wazi mawazo yaliyojikita katika maneno mbalimbali na kuishawishi hadhira kuyatilia maanani mawazo na maono hayo.

Kwa mfano anaposema "***mimi sio mkorofi***" hasubiri kuulizwa "***mkorofi ni nani***" bali anafuatiliza papo hapo maelezo kwa kusema "***mkorofi ni nchi yetu***" Pamoja na hayo, maelezo hayo yanaweza kuibua swali jinguine - inawezekanaje nchi kuwa "***mkorofi?***" Mwalimu ametumia tashhisi kwa maksudi akaipa nchi sifa ya mwanadamu ili kuibua tafakuri na kuwazindua wananchi. Ametumia pia visitizi kama vile "***kwa kweli***" na "***bila ya mchezo***" kuwathibitishia wasikilizaji wake kwamba aliyoyafanya kama kiongozi wa nchi; ilikuwa ni kwa maslahi ya nchi yao na sio kwa maslahi yake binafsi. Anataja umoja wa nchi kama

mojawapo ya mambo muhimu aliyofanikiwa kufikia ambapo baadhi ya Watanzania wanapenda kuutokomeza. Hata hivyo, lugha anayoitumia ni ya kuwakatisha tamaa. Kama wanadhani kwamba anayependa muungano ni yeye peke yake basi wamekosea. Kwa msisitizo alisema "***hatuwezi kutafuta rais ambaye hataki umoja***" Hii ina maana kwamba umoja ni jambo linalopendwa na Watanzania wengi "***hatuwezi***" yaani sisi walio wengi.

**Takriri**: *Wakati wote wa uongozi wangu sikupata matatizo kwa wananchi. ... ni kweli kwamba yalitokea maasi ya Jeshi. Hii ilikuwa aibu kubwa sana. Lakini mpaka leo hii ni vigumu kujua chanzo hasa cha maasi haya ya mwaka 1964. Sijui nani atakuja kuandika historia ya "Mutiny"' ile ya 1964. Kulitokea mambo ya ajabu katika kipindi cha saa 36 hivi au 48, nilipata "Pressure" kubwa sana, nilikubali msaada wa Waingereza ili kuyamaliza maasi ya Jeshi letu. Hili halikuwa jambo jepesi kukubali. Lakini mara "Mutiny" nyingine ikatokea Kenya na kuzimwa kwa masaa na Waingereza. Punde "Mutiny" nyingine tena ikatokea Uganda nayo pia ikazimwa kwa msaada wa Waingereza. Nasema, litakuwa jambo zuri sana ikiwa baadaye utafanywa uchunguzi na kujua asili ya Maasi hayo katika Afrika Mashariki. ..."* (UK 19:1-2: AW).

Uteuzi wa maneno yaliyotumika yalikuwa ni mahsusi hasa kwa tukio la uasi wa majeshi ya nchi za Tanzania, Kenya na Uganda yaliyojiokeza mapema baada ya nchi hizo kujitangazia uhuru wao. Ambapo maneno: ***"matatizo" Ni matatizo yapi? "Maasi ya jeshi" "aibu". "maasi haya ya mwaka 1964", "Mutinyi ile ya 1964, "mambo ya ajabu", "mutinyi nyingine ikatokea…", "maasi hayo" …*** ilikuwa ni ***"Pressure"***. Ni maneno yenye mtagusano wa fikra kuhusu maasi yaliyojitokeza kiasi cha kuzifanya nchi hizo za Afrika kuingiwa na sintofahamu ya nini chanzo chake hata ikawa ni rai ya nafsi yake (Mwalimu) kusema: ***Nasema, litakuwa jambo zuri sana ikiwa baadaye utafanywa uchunguzi na kujua asili ya Maasi hayo katika Afrika Mashariki.*** Mwalimu akiudhihirishia umma hisia zake alisema: ***kipindi cha saa 36 hivi au 48, nilipata "Pressure" kubwa sana*** …" kumaanisha kwamba hakukifurahia kitendo hicho hasa ikisadifu kwamba ni kwa miaka miwili hivi tu tangu Tanganyika ijipatie uhuru wake kamili na kwa machungu akisema: ***Hii ilikuwa aibu kubwa sana***. Kuonyesha kwamba hawakuwa na njia mbadala zaidi ya kuomba msaada kutoka kwa taifa ambalo lilikuwa ni kuloni lao. Lakini kwa muda mfupi tu baada ya kujinasua kutoka katika makucha yao walikuwa bado wangali ni wachanga katika maswala ya vita na ndiposa yakazuka maasi hayo. Hivyo, ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania wawe macho wajihadhari na wawamulike kwa kina maadui wa ndani na nje ya

nchi yao. Wawe wazalendo kindakindaki kwa nchi yao kwa imani kwamba mjenga nchi ni mwananchi na mvunja nchi ni mwamnachi pia.

**Takriri**: *kipindi chote cha uongozi wangu nimepewa msaada mkubwa sana na wananchi Watanzania. Na wala katika nafasi yangu ya Amiri Jeshi mkuu sijapata matatizo yoyote na Jeshi letu. Hata mwaka 1978 mwenda wazimu mmoja alipolipa muhali jeshi letu na nchi yetu sikupata matatizo. Jeshi letu lilifanya kazi yake vizuri sana. Wakubwa walikuwa wakifuatilia vita vile kwa makini sana, na Jeshi letu liliwashangaza. Walishangaa sana na kusema kuwa hawakujua kama Tanzania imejenga Jeshi la namna ile. Kwa hiyo na sema, wananchi wa Tanzania wameniheshimu na kunisaidia sana. Raia wenye "uniform" wamenisaidia, na raia wasiokuwa na "Uniform" wamenisaidia,. Na nyinyi raia wenye "Uniform" mlipokuwa mnatii na kunisaidia, mlikuwa hamnitii na kumsaidia Julius Nyerere; mlikuwa mnamtii, mnamheshimu na kumsaidia "Commander – in Chief" wenu, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Tanzania. Tena mnamtii mkijua kwamba mimi binafsi ni Mwalimu tu, sio askari. Niliwahi kufundishwa kidogo uaskari nilipokuwa Makerere. Lakini mimi si askari ni Mwalimu wa darasani, ndio "Profession" yangu. Lakini kwa katiba ya Tanzania ni "Commander – in - Chief" wenu. Kwa hiyo, wakati wa vita inawezekana wakati mwingine niliwavurugia mipango. Wakati mmoja niliwaambieni mbadili mipango yenu. Kwa sababu kutokuwa na "Information" ya kutosha kulifanya nikhofu kuwa mnaweza kuingia katika mtego mkapata matatizo. Pengine ningeacha mwendelee na mpango wenu, ..".* (UK 19:3; 20:1: AW)

Kipindi chote cha uongozi kinachozungumziwa hapa ni muda wa utawala wa Mwalimu Nyerere kuanzia Mwaka wa 1961 tangu Tanganyika ilipopata uhuru hadi mwaka 1985; alipong’atuka. Shangwe za furaha yake kwa uneni aliouendeleza; miongoni mwazo ni kutokana na msaada mkubwa alioupata katika kipindi chote cha maongozi yake. Kwa heshima kubwa (twaa kubwa) aliyoipata kutoka kwa raia wa kawaida na wanajeshi, aliyafichua mahaba yake kwa raia aliowaongoza kwa muda mrefu lakini ikawa ni ayaone maongozi yake ya kwamba yalikuwa ni ya raha hasa kutokana na ushirikiano alioupata kutoka kwa wanachi aliowaongoza.

Ingawa hivyo, kumbukizi za Mwalimu kuhusu vita vya Kagera dhidi ya aliyemrejelea kama ***“Mwenda wazimu”*** Idd Amin - aliyekuwa Rais wa Uganda; heshima ya wananchi na utiifu wa jeshi la Tanzania waliyompa katika midani za kimataifa. Kwa tafakuri yake aliuona ushindi huo ya kwamba ni nishani iliyowajuzu Watanzania wote. Hii ni kutokana na kwamba; ulimwengu haukuitarajia Tanzania kuibuka kwa ushindi wa kishindo dhidi ya Idd

Amin na majeshi yake; hasa ikiaminiwa kwamba wengi wa makamanda wa Idd Amin walipata mafunzo yao ya kijeshi katika nchi zilizoendelea na wakatumikia jeshi la "Kings Afrikan Rifles - KEA". Na ndio ikawa nchi za kimagharibi zikiamini kwamba Tanzania ingeshindwa vita vile. Ushindi uliopatikana uliwashangaza wengi ***"wakubwa"*** ambao ni Waingereza na washirika wake, hawakutarajia kwamba Tanzania ilijijenga kijeshi kwa namna ya kuweza kukabiliana vilivyo na wapiganaji walioonekana ni shupavu; na walioaminika kama mashujaa wa zama hizo.

Na ndiposa kwa furaha Mwalimu alisema: ***"Raia wenye uniform"*** ni wanajeshi na raia wasiokuwa na ***"uniform"*** ni wananchi wa Tanzania wa kawaida. Hii ni mbinu ya kinaya ambayo kwa muktadha wa matumizi yake ilikuwa ni ya kuwakweza walengwa / hadhira yake ambayo ilikuwa ni ya wakuu wa jeshi. Anadhihirisha kwamba alikuwa mwangalifu sana katika mahusiano yake na wao na kwa raia wote. Kwa maana ya wenye ***"wale wasio na uniform"***. Kusudio likiwa ni kuwapongeza na kuwaomba radhi ili kudumisha mahusiano mema baina yao. Na kwa kuivuta hadhira yake kwa mahaba, alitumia uchanganyaji wa ndimi: ***"Uniform"***, ***"Commander in Chief"***, ***"Profession"*** na **"Information"** - ikiwa ni furaha kwa jitihada walizozifanya katika mapambano dhidi ya waliomwita ***"Mvamizi*** *na mwenye* ***wazimu*** (Idd Amin wa Uganda)**.** Kwa uhawilisho wa kwamba hakuwa ni mwenye akili timamu; hasa ikisadifiwa kwamba kitendo cha kuivamia nchi nyingine pasina sababu mahususi ni cha kiuchokozi na kwa hivyo alistahiki kupigwa hadi kusalimu amri

Fauka ya hayo, Mwalimu alielekeza zaidi shukrani zake kwa wanajeshi kwa utiifu waliouonyesha kwake hasa akiwakumbusha ya kwamba ***"Profession"*** yake ilikuwa ni ***"Mwalimu wa darasani"*** lakini ikawa ni wamtii kwa lolote alilowaamrisha hasa katika kujitoa muhanga kwa kuipingania nchi yao iweze kuwa na amani.

Hivyo, ulikuwa ni ushawishi wake kwa Watanzania wote kutambua kwamba wanahitajika kuuendeleza wema wao hasa kwa wanajeshi wanaolitumikia vema taifa lao kwa kuwapa haki inayostahiki na watambue kwamba kinyume na hivyo, wanajeshi wanaweza kuasi na hata kusababisha mapinduzi. Kwa hivyo lazima liheshimiwe (libembelezwe); na panapostahiki liombwe radhi kwa kulitendea vitendo vinavyoweza kulikasirisha. Daima washirikiane na raia wote na waendelee kulitumikia taifa lao la Tanzania kwa moyo mkunjufu.

**Maswali ya kibalagha**: *"...ndiyo tunatoa ujumbe gani? "Vijana niliowakatalia ni hawa. Sasa mwaka huu ni wakatalie tena? Angalau hiyo ni sababu moja ya kuwakubalia mwaka huu. Huwezi kuwakatalia mwaka hata mwaka! Sababu ya pili niliyofanya nikakubali ni kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi. Sasa, mwaka wa uchaguzi wote lazima tushirikiane kusema tunakwenda wapi? Nafasi kama hii ni nzuri kwa mtu ye yote mwenye mawazo kusema jamani huu ni wakati wa uchaguzi tunakwenda wapi?" Tuko wapi na tunakwenda wapi. Na kama tunataka kwenda huko, tufanyeje ili tufike huko.* (UK 1:3, 2: 5, 3: 1: TTT)

Ilikuwa ni katika kilele cha sikukuu ya Wafanyakazi Duniani, Mei 1, 1995 katika uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Tanzania; ambapo Mwalimu aliwaomba radhi wananchi kwa kutoshiriki sherehe za Wafanyakazi kwa mwaka uliopita wa 1994 kutokana na sababu kuu mbili: Ya kwanza alisema ilitokana na kitendo cha kumwalika yeye kuwa mgeni rasmi na kumwacha Rais wa nchi ambapo angestahiki zaidi kutokana na mazoea ya tangu azali. Kwa hivyo, alihofia kusababisha utengano usio na tiba mbadala.

Na sababu ya pili; Mwalimu alisema, alikataa kwa sababu mwaka alioalikwa kuwa mgeni rasmi ni mwaka ambao Wafanyakazi waliigomea serikali yao; ambapo kwa balagha alisema: ***"…ndiyo tunatoa ujumbe gani?*** Akimaanisha kwamba, maamuzi yake ya kutohudhuria sherehe hizo za Wafanyakazi kwa mwaka 1994 yalikuwa na mashiko zaidi katika kujenga na sio kubomoa. Mbali na kwamba Mwalimu aliwaeleza wananchi sababu za kutohudhuria sherehe za Wafanyakazi kwa mwaka uliopita; alitoa sababu zingine mbili zilizopelekea kuukubali mwaliko wa sherehe za Wafanyakazi alizozihudhuria kwa mwaka wa 1995 ya kwamba walioziandaa mwaka uiopia ndio hao hao waliozindaa tena na kumwalika na kwa hivyo, akiuliza: ***Sasa mwaka huu ni wakatalie tena?*** Kwa maana si busara kuwakatalia tena, vinginevyo kungejengeka chuki pasina sababu za msingi.

Wakadhalika Mwalimu aliwatanabahisha Watanzania kwamba sherehe zilizokuwa zikiendelea zilikuwa na umuhimu mkubwa; kwa kujiuliza: ***Sasa, mwaka wa uchaguzi wote lazima tushirikiane kusema tunakwenda wapi? Nafasi kama hii ni nzuri kwa mtu ye yote mwenye mawazo kusema jamani huu ni wakati wa uchaguzi tunakwenda wapi?".*** Hii ni balagha aliyoitumia Mwalimu kama kichocheo cha wananchi katika kufanya tathmini ya malengo ya nchi yao kwa kushiriki uchaguzi wa urais ili kupata kiongozi mweledi na muoni katika maongozi ya nchi. Lakini pia akiwataka - katika harakati za uchaguzi wa viongozi kujiuliza: ***tunatoka wapi, tuko wapi na tunakwenda wapi. Na kama tunataka kwenda huko, tufanyeje ili tufike huko.*** Ya kwamba liwe ni wazo mtawalia kwa kila uchaguzi, akiamini

kwamba wananchi wakijiuliza maswali hayo, itawawia rahisi kugundua madhaifu yaliyokuwepo katika kipindi cha uongozi kinachomalizika; na kwa hivyo kuamua kipi kipewe kipaumbele na nani wa kuyasimamia malengo yao ili yapate kuleta ufanisi mzuri kwa siku za usoni. Kwa hiyo, balagha alizozitumia Mwalimu zilikuwa na ushawishi wa kuonyesha dira ya nchi na maongozi yake ambapo Watanzania wanahimizwa kuwa macho kwa kila unapowadia uchaguzi ili wapate kuwapata viongozi bora na sio bora viongozi.

**Maswali ya kibalagha na Takriri**: "*Tunatoka wapi, tuko wapi na tunakwenda wapi. Na kama tunataka kwenda huko, tufanyeje ili tufike huko".* (UK 2: 5- 3: 1: TTT).

Hii ni chagizo ya Mwalimu inayotoa mwangwi kwa wananchi kuhusu kutafakari kabla ya maamuzi lakini pia umuhimu wa kufanya tathmini katika matendo yetu ya kila siku kwa imani kwamba wale wenye nia njema na jamii, watakuwa tayari kuikubali mbiu ya kukosoa na kukosolewa ili kujikwamua zaidi kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni lakini pia kujenga taifa lenye umoja amani, upendo na mshikamano.

**Maswali ya kibalagha**: *"Sasa, mwaka wauchaguzi wote lazima tushirikiane kusema **tunakwenda wapi?** Nafasi kama hii ni nzuri kwa mtu ye yote mwenye mawazo kusema **"jamani huu ni wakati wa uchaguzi tunakwenda wapi?"*** (UK 3:1: TTT)

Kauli hizi ni ushawishi wa Mwalimu akiwataka Watanzania wazinduke na watafakari mpwito wa maisha yao hususani ***walikotoka, walipo na wanakoelekea*** na watambue kwamba uongozi bora ndio suluhisho la matatizo yao. Kwa hivyo, kila mwaka wa uchaguzi waone ni wajibu wao kushirikiana kwa nia safi kwa minajili ya kuwapata viongozi bora na sio bora viongozi.

**Takriri na tashhisi**: "*... rais wa nchi yetu anachaguliwa kutokana na katiba ya Tannzania. Na akichaguliwa, anaapishwa. Kama ni Mkristu, kwa Bibilia, kama ni Mwislamu, kwa Kuruani. Hatujachagua mtu asiyeamini Mungu, lakini tukimchagua, tutatafuta utaratibu wa kumuapisha. Ataapa! Hata asiyekuwa muumini, tutamwapisha kwamba atailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania. Asipoilinda, tunajua ni msaliti. Tutamwapisha. Ataapa! lazima kabisa, hata kama si muumini. Kwa mujibu wa katiba yetu sisi, si lazima mtu awe anamwamini Mungu kuwa Rais, hata kidogo. Lakini, tutakuapisha! Umechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Unaapa kulinda. Ataapa kwa huyo Mungu wake au akili yake anayoijua; lakini atatuapia. Ataapa kusudi tuweze kumshitaki kama akikiuka.*" (UK 13:3 / 14:1: N).

Neno ***"kuapa"*** ni mtu kuiweka roho yake rehani - kwa Mwenyezi Mungu (kwa kujishitaki kwa Mwenyezi Mungu) kwamba ikiwa atatenda kinyume na ukweli ulivyotakikana Mwenyezi Mungu amlaani kwa kiapo chake, ampe adhabu ima kwa alivyojielekeza au kwa atakavyoamua mwenyewe Mwenyezi Mungu. Fauka ya hayo, kiapo hicho ni mtawalio wa nafsi katika kuonyesha uzito wa jukumu la urais ya kwamba ni sharti rais ashike hatamu ya kuiongoza nchi kwa kufuata sheria zilizowekwa na sio kwa matashi binafsi. Kwa hiyo, takriri neno *"**kuapa**"* ni changamoto kwa mtu na maamuzi yake katika maswala yanayohusu uongozi kwamba si jambo rahisi bali ni zito na lenye hukumu ima kutoka kwa wanadamu wenyewe kwa wenyewe au kutoka kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

**Tashtiti**: "… (Wagombea nyadhifa za Uongozi Serikalini) *Daima wajiulize wataifanyia nini nchi yao na siyo kwamba nchi itawafanyia nini"* (UK 26:2: TTT)

Kauli: ***"daima"*** imetumika kuwapiku wagombea nyadhifa mbalimbali; na kuwashawishi Watanzania ya kwamba wasidanganyike na matamko ya wanasiasa. Watambue kwamba serikali yao ina mengi ya kuwafanyia iwapo watatambua kwamba mafanikio ya nchi yanaletwa na wananchi wenyewe na sio kinyume chake. Kwa maana kwamba, waone ni wajibu wao kujituma  (kuwajibika) kwa hali na mali katika utekelezaji wa malengo yaliyowekwa ili kuleta maendeleo ya nchi; na kwa manedeleo hayo; matunda yake  - iwe ni sababu toshelezi kwa kila mtu kuyafaidi kwa uadilifu.

**Istiara**: "*... (kiongozi) kwa dhati kabisa, awe anaumwa na umasikini wetu na iwe kwamba umasikini huo ndio unaomsukuma ashughulike na mambo haya ya siasa katika ngazi hiyo ama ya ubunge ama ya urais". Kama sivyo, hatufai!*". (UK 26:3: TTT)

Katika kauli hizi; kuna matumizi ya visisitizi kama vile kwa ***"dhati"*** na ***"kabisa". "Anaumwa*** na ***umaskini" -*** ni istiara ambapo imefananishwa umaskini na ugonjwa mbaya unaomuuma mtu na kwa maneno: ***Kama sivyo, hatufai*** ni uhawilishaji wa hisi ambao umeupa umaskini umbo la binadamu anayeweza kumsukuma mtu na kumfanya ashughulikie mambo ya siasa.  Hii ni kwa uoni kwamba,watu wengi huamua kugombea nyadhifa mbali mbali kama vile urais, ubunge, udiwani na kadhalika. Huwa wanakuwa na sababu kadha wa kadha zinazowasukuma kufanya hivyo. Baadhi yao hutanguliza maslahi yao binafsi lakini yule anayewafaa Watanzania kwa maoni ya Mwalimu Nyerere ni yule ambaye anaitathmini na kutambua hali halisi ya nchi kiuchumi na umasikini ule ukawa ndio unaomsukuma kuwania uongozi serikalini; kwa azma kwamba akichaguliwa; atahakikisha anaupiga vita umasikini. Lau kama kuna mdororo mwingine mathalani unaohusu siasa, afya au elimu; basi

ionekane pia kwamba ndivyo vinavyomsukuma kuutafuta uongozi kwa azma ya kuyaondoa matatizo hayo ili asasi hizo ziweze kuwafaa wananchi kama inavyostahiki. Hivyo, ndiyo kusema, matumizi ya lugha aliyoyatumia Mwalimu ni ushawishi kwa wapiga kura katika kuwachagua viongozi watakao jali maslahi yao.

**Takriri na maswali ya kibalagha**: "*... Ikulu ni mzigo! Hupakimbilii! Si mahala pa kupakimbilia hata kidogo; huwezi kupakimbilia ikulu. Unapakimbilia kwenda kutafuta nini? Ni mgogoro, ni mzigo mkubwa kabisa! Ukipita barabarani, unakuta watu wana njaa, unaona ni mzigo wako huo. Pazito pale! Huwezi kupakimbilia na watu safi hawapakimbilii. Ukiona mtu anapakimbilia, na hasa anatumiatumia na vipesa kwenda ikulu, huyo ni mtu wa kuogopa kama ukoma!*; … *"Mtu ye yote anayeonekana anapenda sana kwenda ikulu na hata yupo tayari kununua kura ili kufika ikulu ni wa kumkwepa kama ukoma. Kwanza, hizo fedha kapata wapi. Mtanzania wa leo hawezi kununua watu bila kwanza yeye kununuliwa. Na kama kanunuliwa atataka kuzilipaje? Kazipata wapi? Watanzania wote ni masikini tu. Mtanzania anaomba urais wetu kwa hela? Amezipata wapi?"*; … *"Pili, kama hajanunuliwa, kazipata wapi? Kama kakopa, atazirudishaje? Ikulu pana biashara gani mtu akope mamilioni halafu aende ayalipe kwa biashara ya Ikulu? Ikulu mimi nimekaa kwa muda wa miaka ishirini na mitatu. Ikulu ni pahala pazito. Kuna biashara gani Ikulu?"* (UK 27:2 - 4: TTT)

Matamko hayo yamejaa takriri maneno kama vile, "***hupakimbilii***" "***unapakimbilia***", "***hawapakimbilii***", "***kununua***" "***Ikulu***" swali la kibalagha "kapata wapi?" takriri silabi "u, a, na, na ka" – kama katika maneno "***unapakimbilia***" "***unakuta***", "***unaona***", "***anapenda***", "***akope***", "***aende***", "***kanunuliwa***", "***kakopa***". Shabaha ya matumizi hayo ya lugha ni kufungamanisha sehemu mbalimbali za usemi ilikutoa ushawishi uliokusudiwa. Vile vile, maswali mengi ya kibalagha yameulizwa. Hii ni kwa lengo la kuwazindua wapiga kura Watanzania wawe chonjo na wagombea wanaowashawishi kiasi cha hata kuwapa hongo ili wapate kuwa viongozi. Shauku hii ya kiongozi kuitamani ofisi ya Ikulu ndiyo iliyompelekea Mwalimu kuuliza swali la kwamba: ***Unapakimbilia kwenda kutafuta nini?*** Akimaanisha kwamba, kiongozi wa namna hiyo ni mwenye uchu wa madaraka asiyetambua kwamba uongozi ni dhima inayomwihitaji mtu awajibike kwa muda wake wote kwa wananchi anaowaongoza. Uzito huo ndio ulimpelekea Mwalimu kuivuta taswira ya kiongozi mtoa hongo kwa kusema: ***"… Kazipata wapi? Mtanzania anaomba urais wetu kwa hela? atazirudishaje? Ikulu pana biashara gani mtu akope mamilioni halafu aende ayalipe kwa biashara ya Ikulu? Ikulu ni pahala pazito. Kuna biashara gani Ikulu?"*** Kumaanisha

kwamba inampasa mgombea kutafakari na kutambua kwamba Ikulu sio sehemu ya starehe wala ya utajirisho kwa mtu kuikimbilia kiasi cha hata kutoa hongo bali ni sehemu ya kiongozi kuhisi machungu ya kuelemewa kwa kazi ngumu zenye kufikirisha akili kila uchao kutokana na matatizo ya wananchi anaowaongoza.

Kwa hiyo, lugha aliyoitumia Mwalimu ni ushawishi wa kuwataka Watanzania watafakari kwa kina kuhusu nani anafaa kuwa rais wa nchi na wahakikishe pia kwamba wanajiepusha na wagombea wenye kuwashawishi wapiga kura kwa hongo. Kiongozi asiwe *bora kiongozi*, mwenye uchu wa kuiona Ikulu kama sehemu ya utajirisho binafsi bali awe kiongozi bora, mwenye kuitambua dhima yake hasa kwa kuhakikisha kwamba maslahi ya umma yanasimamiwa na kuwafikia wananchi wote kwa uadilifu.

**Takriri**: "*Kujaribu kumpata kiongozi wa nchi yetu kwa njia ya mizengwe kama tulivyokuwa tukifanya zamani wakati wake umepitwa. Wakati huo umepitwa".* (UK 5:3: N).

Hizi ni kauli zinazotoa ufahima kuhusu viongozi na wafuasi wa CCM kuhusu kuzisoma alama za nyakati. Kwa ufahima kwamba, inapokuwa jamii haina kauli kuhusu masuala yanayohusu mustakbala wa nchi yao, kutokana na kushikiwa akili na viongozi waliopo madarakani, wajue ya kwamba wananchi watakapo pata upenu wa kuweza kuzitetea haki zao na wajibu wao kwa nchi yao hawatamchelea yeyote. Mtagusano huo hautakuwa na simile hasa inapowapitikia kwamba wameonewa kwa muda mrefu. Watakuwa radhi kujitoa muhanga si tu kwa kuzitetea haki zao; lakini pia kwa minajili ya kuyaweka mambo sawa kwa vizazi vijavyo. Si wahenga walisema "***mjinga akerevuka mwerevu huwa mashakani***?" Uoni huo ulimpelekea Mwalimu kuzisuta nafsi za Watanzania enzi za maongozi yake kwa kusema: **"*Kujaribu kumpata kiongozi wa nchi yetu kwa njia ya mizengwe kama tulivyokuwa tukifanya zamani wakati wake umepitwa. Wakati huo umepitwa".*** Kumaanisha kwamba, Watanzania hivi leo wanazitambua haki zao; na wana uwezo wa kusimama kidete kwa kuzitetea. Si watu wakuburuzwa kibubusa tena. Wameelimika na wana umoja thabiti hasa katika masuala yanayohusu utetezi wa haki zao. Mwalimu anawamwagia sifa kemkem ili kuwahimiza kuendelea na kupigania haki wanazostahiki.

**Maswali ya kibalagha**: *"... Je, ni kweli kwamba vitendo vya serikali kuhusu uhusiano wetu na nchi za nje vimezuia maendeleo yetu ya uchumi? Kama ni kweli upungufu huo ni wa kiasi gani? Je, misingi haina maana kwetu, hata ionekane kwamba upungufu wa uchumi ni halali, kwa sababu zingine za heshima ya Taifa letu?* (UK 1:2-3: MU)

Ilikuwa ni tashwishi kwa Mwalimu Nyerere kwa baadhi ya Watanzania pindi walipotumia vyombo vya habari kunadi kwamba, misingi ya Tanzania kwa imani yake imekuwa kero kwa nchi za nje kiasi cha kuyumbisha uchumi wa nchi. Ndiyo akauliza umma wa Watanzania kwamba: ***"… Je, ni kweli kwamba vitendo vya serikali kuhusu uhusiano wetu na nchi za nje vimezuia maendeleo yetu ya uchumi?*** Fauka ya kwamba ni busara kwa mtu kuitikadi mbiu ya kukosoa au kukosolewa hususani katika nchi zinazofuata mfumo wa kijamaa kama ilivyokuwa Tanzania, kwa Mwalimu kitendo hicho hakikuwa cha busara.

Kwa uoni wa Mwalimu, taarifa hizo zilikuwa hazina mashiko. Ilikuwa ni busara kwa mambo mithili ya hayo kufanyiwa tafakuri ya kina kabla ya kutolewa kadamnasi. Usintofahamu huo ndio uliompelekea Mwalimu kuwauliza Watanzania kwa mara nyingine kamba: ***Je, misingi haina maana kwetu, hata ionekane kwamba upungufu wa uchumi ni halali, kwa sababu zingine za heshima ya Taifa letu?*** Akimaanisha kwamba misingi iliyowekwa ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi na kwamba haingiliki akilini kwa viongozi wanaosimamia sheria za nchi halafu iwe hawaitekelezi misingi hiyo pasi na sababu za msingi. Kwa hivyo, chachu ya Mwalimu kwa kauli alizotumia ilikuwa ni kuwaonya wale wote wanaojitoa kimasomaso katika vyombo vya habari ya kwamba wazifue nafsi zao, na iwe ni ada kwa kila mmoja kuwafikiria wengine kwa wema na ndiposa kuyatathmini ikiwa wayatendayo ndivyo au sivyo. Fauka ya hayo, maswali ya kibalagha yalitumika kuwasilisha hoja kwamba … ya Tanzania na nchi za nje hayakuzuia katu maendeleo yanchi na kwamba misingi imara imewekwa kwa ajili ya maendeleo na heshima ya taifa.

**Maswali ya kibalagha na takriri**: *"... sasa sisi tufanyeje? Tuache lengo letu? Tujenge nchi hii kwa faida ya wachache badala ya jitihada yetu ya kujenga nchi yetu kwa faida ya wote?* (UK 9:2-3: MU)

Haya ni maswali yanayowataka Watanzania watafakari kwa kutambua kwamba haiwezekani wachache wenye utashi binafsi wakawavurugia wengine malengo yao hasa yale ya kijumla. Aidha aliwataka watambue kwamba faida inayotokana na ujenzi bora wa Taifa ni lazima iwaendee wananchi wote na sio vinginevyo. Hii ndiyo kusema, balagha iliyotumia Mwalimu ni changamoto kwa wananchi wote. Watambue kwamba ni jambo zuria katika maendeleo jamii kutathmini jambo kabla ya kuliweka hadharani.

**Takriri**: A*santeni sana. Asanteni sana kwa kila mmoja wenu binafsi, asanteni sana wananchi mliojiunga vijijini, katika vyama vya ushirika, katika taasisi na taaluma mbalimbali, katika mashirika ya kujitolea yanayotusaidia katika maendeleo yetu; kwa wafanyakazi wote waaminifu katika serikali na katika mashirika ya umma, na kwa kila Mtanzania, nasema, asanteni sana;* (UK 1:2: KW); *Mungu Ibariki Afrika! Mungu Ibarika Tanzania* (UK 9 – 11:3: KW)

Hizi zilikuwa ni kauli zilizosheheni tafakuri ya Mwalimu kuhusu maongozi yake; kwa jinsi alivyowangoza Watanzania na ikawa wanamwitikia kwa kila jambo. Matamshi yake kuhusu kuwaaga wananchi yenye mtawalio wa ***"Ahsanteni sana"***, yanadhihirisha wema wa dhati ambapo pande mbili (Mwalimu na wananchi aliowaongoza) ya kwamba, mbali na muda mrefu wa zaidi ya miongo miwili aliowangoza wananchi wa Tanzania, angali ana mahaba ya kuendelea kuwaongoza – kwa jinsi ambavyo hakupata magumu katika kuwaongoza; kwa maana ana hisi simanzi ya moyoni kwa kuagana nao.

Na kwa wananchi lau kama si mapenzi yake mwenyewe (Mwalimu) ya kutaka kung'atuka, walikuwa bado wakitamani aendelee hadi yatakapomfika mauko yake - kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Hii ni kutokana na mfululizo wa kiutajo: ***wananchi mliojiunga vijijini, katika vyama vya ushirika, katika taasisi na taaluma mbalimbali;*** ambapo ni udhihirisho wa kuzikonga nyoyo za kila tapo kwa fani yake; kuonyesha kwamba msaada wao anaukumbuka. Na kwamba hana la kuwalipa lenye usawa wa mizani kwa wema waliomtendea zaidi ya kuwashukuru. Na kama hivyo haitoshi; kwa hisia za moyoni akisisitiza tena na tena kwa kusema: ***"nasema, asanteni sana";*** ambapo kwa muongezeko wa neno ***"nasema"*** katika mfululizo wa shukurani zake ni ubainifu wa fahiwa kwamba hakuna malipo bora atakayoweza kuwalipa wananchi hao zaidi ya kumwomba Mwenyezi Mungu awalipe kwa wema wao. Matamshi hayo ni ushawishi kwa Watanzania kuzitambua fadhila za Mwalimu zilizokuwa zimefichama. Kufichuka kwa furaha yake iliyokuwa imemgubika kwa muda mrefu kuhusu maongozi yake na iwe ni kumkumbuka na kielelezo cha kuigwa na vizazi vilivyopo na vijavyo.

Fauka ya hayo, takriri neno "***Asanteni sana na shukrani***" zilizotagaa katika hotuba yake, fahiwa inayobainika ni kumbukizi kuhusu utangamano wake na raia aliowaongoza kwa zaidi ya miongo miwili, ambapo kwa umoja wao, kama rais aliweza kuvikwa nishani ya Nansen kutokana na wema waliokuwa wakiwafanyia wakimbizi. (UK 8:1: KW). Waliweza kuwahifadhi wakimbizi na kuishi nao kidugu. Watanzania waliweza kuunga mkono sera za

serikali na siasa ya chama katika kusaidia FRELIMO wa Msumbiji, MPLA wa Angola, Patriotic Front wa Zimbabwe, SWAPO wa Namibia, na vyama vya ukombozi vya Afrika ya Kusini. Na misaada ya moja kwa moja iliyotolewa kama vile damu kwa ajili ya wapigania uhuru wa Msumbiji. Kwa umoja wa Watanzania waliweza kuimarisha siasa na maendeleo ya uchumi wao bila ya kujali kabila, dini au rangi zao. Kwa hali hii ndiposa ***akijiuliza aseme nini zaidi kulikoni***? Kumaanisha kwamba hakuwa na lakufanya zaidi ya kuwaombea wale wote walioshirikiana naye hata ikawa ni avikwe nishani kutokana na maogozi bora; lakini kwa kuiwezesha nchi ya Tanzania kuwa ni yenye amani, umoja na utulivu huku ikikulia kisiasa na kiuchumi. Na alihitimisha hotuba yake kwa dua, kwa kutamka: "***Mungu Ibariki Afrika! Mungu Ibarika Tanzania!***" Kama mjumuisho wa shukurani zake (UK 9 – 11:3:KW)

### 4.4.11 Maudhui kuhusu Ufaafu wa Azimio la Arusha

Ilikuwa ni ghera ya Mwalimu Nyerere kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kijamaa. Ushawishi wake uliwapelekea wananchi wa Tanzania kuanzisha Azimio la Arusha chini ya misingi ya ujamaa na kujitegemea ambapo moja ya ufanisi wake ulikuwa ni utaifishaji wa mali binafsi kwa ajili ya umma. Chini ya maongozi ya Mwalimu Nyerere, Watanzania waliweza kushirikiana katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya umma kwa ufanisi. Matendo ya mtu kwa mwingine yalichukuliwa kama kigezo cha utu wa mtu na sio mtu kwa umaarufu wa mapato yake mwenyewe. Uzalendo wa Watanzania ulivuka mipaka ya mizania hata wakaweza kuzisaidia nchi nyingine za kiafrika zilizokuwa zingali katika kizimba cha Wakoloni kama vile Afrika ya Kusini na Msumbiji ambapo wapigania uhuru walipewa mazingira faafu na mafunzo ya kutosha hata wakaweza kuzikomboa nchi zao.

Enzi ya maongozi ya Mwalimu usawa ulichukuliwa kama kigezo cha msingi wa ujamaa. Itikadi hii si tu kwamba iliwapelekea Watanzania kuwa kitu kimoja lakini pia ilikuwa ni chachu ya maendeleo kwa Watanzania wote. Watanzania waliweza kujimudu kiuchumi kiasi cha hata kuweza kuziondoa tofauti za kimapato (kutokomeza tabaka la wenye nacho na wasionacho) hasa kwa mtazamo kwamba, ikiwa Watanzania wote ni ndugu kodi inayokusanywa na ama huduma zingine za kijamii ilikuwa ni sharti ziwafikie wananchi wote kwa usawa. Mbali na mafanikio yaliyopatikana kupitia Azimio la Arusha wakati wa maongozi ya Mwalimu. Baada ya kung'atuka kwake aliingiwa na simanzi kutokana na mabadiliko yaliyofanywa kuhusu Azimio la Arusha. Sera za azimio la Arusha zilifanywa pindupindu badala ya utaifishwaji wa mali binafsi na kuwa za umma leo yake ikawa ni

ubinafsishaji wa mashirika ya umma na kuwa ya watu binafsi kwa madai kwamba ni katika njia mwafaka ya kuharakisha maendeleo ya nchi.

Kwa uoni wa Mwalimu, mabadiliko yaliyofanywa dhidi ya sera za Azimio la Arusha yalikuwa tenge katika uhalisia wa maisha ya wananchi wa Tanzania. Kwa taswira kwamba, uchumi wa nchi ulikuwa ungali mikononi mwa Wakulima na Wafanyakazi katika kiwango cha zana duni, kwa hivyo, aliyaona maamuzi yaliyopelekea kubadilishwa kwa sera za Azimio la Arusha wakati zingali bado ni faafu katika maongozi ya nchi, ni ujauzito wa fikra ulitokana na ukubalifu wa kila kilichokuwa kikielekezwa na nchi zilizoendelea kiviwanda (nchi za kimagharibi). Na ikawa viongozi ni washikiwe akili, wakubali kila linaloamriwa pasi na kutathmini athari na uhalisia wake kwa raia wa Tanzania.

Mwalimu aliwataka Watanzania wawe imara na wamakinike kwa malengo waliyojiwekea; na wasitoe mwanya wa kuburuzwa na nchi za kimagharibi - kwa misaada wanayoitoa kwa nchi masikini kama kiini macho. Aliwashauri Watanzania waepuke kufanywa ngazi ya kukwewa na matajiri wachache wanaotaka kuendeleza ubepari wao nchini. Badala yake aliwahimiz wajenge nidhamu ya kuchapa kazi kwa pamoja, wakusanye kodi ya serikali na kuhakikisha mapato yanawafikia wananchi wote kwa uadilifu. Hii ni kwa sababu wakifanya hivyo wataweza kulinda amani, utu, uhuru na heshima ya wananchi wote wa Tanzania.

#### 4.4.11.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Ufaafu wa Azimio la Arusha

**Tafsida kengeushi**: "*Katika Azimio la Arusha kuna sehemu nzima inayoshambulia mawazo ya kijinga kwamba "fedha ndiyo msingi wa maendeleo. Bila ya fedha hakuna maendeleo ... mawazo kama hayo bado tunayo hata leo.*" (UK 29:3: AA)

Huu ni utumizi wa lugha ulionuiwa kuzikonga nyoyo za wazembe na wazururaji; wanaobweteka wakiitakadi kwamba hakuna mbadala wa kuiwezesha nchi kupata maendeleo pasi na fedha na misaada kutoka nje ya nchi. Kwa maoni ya Mwalimu mawazo ya namna hiyo ni sumu kwa jamii hususani yenye umoja na utashi wa maendeleo endelevu. Daima aliwausia Watanzania wajipange na washirikiane kwa malengo waliyojiwekea ili kuepuka utegemezi usio wa lazima.

**Takriri**: "*Tukaweka kitu kimoja hapa kinaitwa **Azimio la Arusha**. Leo narudia kusoma Azimio la Arusha hata kama hamlitaki. Kama kuna watu Tanzania hawajali, wachukue waanze kulisoma ili waone na waniambie wanachokiona mle kibaya ni nini hasa. Asome mtu kwa dhati tu na kisha aseme hiki ni kibaya.* " (UK 9:3: TTT)

Hii ilikuwa ni tashwishi ya Mwalimu kwa madhila yaliyomkonga moyoni baada ya Azimio la Arusha chini ya misingi yake ya siasa ya ujamaa na kujitegemea kuonekana ya kwamba limepitwa na wakati. Ilikuwa ni imani ya Mwalimu kwamba Azimio la Arusha lilikuwa lingali faafu katika kusimamia sera za nchi hususani kwa taifa changa kama la Tanzania. Mbadala uliochukuliwa wa kuanzishwa kwa Azimio la Zanzibar kwa itakadi ya marekebisho ya Azimio la Arusha, Mwalimu alitahmini mabadiliko hayo kama kiini macho kwa walio masikini ambao ndio wengi nchini Tanzania kuendelea kunyonywa na matajiri wachache. Kwa hivyo, ushawishi wake ulikuwa ni Watanzania waitambue nafasi yao kivitendo, kwa maana ya kulihawilisha Azimio la Arusha katika pilika za maisha yao ya kila siku kwa imani kwamba ushirikiano ndio utakaowanyanyua na kuwafanya wasonge mbele kiuchumi. Kinyume na hivyo, ni kuyafanya malengo ya nchi yatagae katika ulimwengu wa ombwe tupu. Takriri iliyomo katika sehemu hii ya hotuba ya Mwalimu Nyerere ni ya matamko "***Azimio la Arusha***" na "***kibaya***" halafu mofimu {***- li-***} katika maneno "***hamlitaki***" na "***kulisoma***". Takriri hiyo imekusudiwa kusisitiza kwamba suala linalozungumziwa ambalo ni Azimio la Arusha bado ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa. Ingawa amedokeza kwamba kuna Watanzania ambao hawalipendi, anatoa changamoto kwamba wajitokeze hadharani ili waonyeshe ulimwengu ubaya uliomo katika Azimio hilo kama kweli madai yao yana mashiko.hawaambii wasiolitaka kwamba waachane nalo, bali anatumia ushawishi uliojikita katika takriri na changemoto hiyo kwa azma ya kuwafanya wabadilishe mwelekeo wao ambao ni hasi kuhusiana na Azimio la Arusha.

**Tashtiti na takriri**: *"... Nchi ya Ujamaa', tukasema, ni nchi ambako kila mtu anafanyakazi; kama ni mfanyakazi, anafanya kazi". Lililokuwa la msingi na linalotawala ni mfanyakazi: maslahi yake yanatokana na kazi yake na jasho lake. ..."* (UK 11:3: TTT)

Ufafanuzi wa Mwalimu kuhusu nchi ya kijamaa ni kwamba, wananchi wake hawawi makupe; kila mtu anakula, anavaa au anajipatia malazi kwa jasho lake mwenyewe. Ingawa kuna makundi ambayo popote duniani hupewa haki hiyo, haiwi ni lawama kutokana na stahiki yao; ambao ni watoto wadogo, watu wazima waliokuwa wakifanya kazi lakini kwa umri wao hawawezi tena; na vilema wasio na uwezo wo wote wa kujifanyia kazi. Ulikuwa ni wito wa Mwalimu kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kijamaa.

Tanzania kuwa "***nchi ya ujamaa"*** ndiyo imani aliyoiotesha na kuipalilia Mwalimu Nyerere enzi za maongozi yake nchini Tanzania. Mtawalio wa neno: ***mfanyakazi*** katika matamshi yake ni msisitizo wa kwamba, umoja na uwajibikaji kwa Watanzania uwe ndio ada mtawalia

katika maisha yao ya kila siku. Kumaanisha kwamba kila mtu aione ni natija njema kujivunia ***maslahi yake yanatokana na kazi yake na jasho lake***. Ambapo fahiwa yake pia ni kuiwezesha nchi kujinasua kiuchumi, kiulinzi na kisiasa. Kwa hivyo, uweledi wa utumizi wa lugha katika matamshi hayo, ni ushawishi kwa Watanzania watambue kwamba umoja kwa misingi ya ujamaa, maana yake ni kufanya kazi kwa bidii na kwa maarifa; huku uzembe, uvivu na uzururaji vikipigwa vita kwa minajili ya kuhakikisha kwamba kila mtu katika jamii anakula jasho lake na sio kuwa kupe kwa wengine bila ya sababu mahsusi kama ilivyo kwa wazee wasiojiweza, walemavu na ama watoto wa dogo ambao daima huwategemea wazazi wao, jamaa zao au misaada kutoka serikalini.

**Takriri na kinaya** "*Sasa katika dunia ya siku hizi maneno haya si mazuri sana kuyasema. Na mimi nawakumbusheni tu na wala sijayasema! Mimi sina taabu, nawakumbusheni tu. Hili* ***Azimio la Arusha****, ambalo sasa mnalitemea mate, lilikuwa linasema hivyo na, kutokana nalo, kuna mambo fulani tukaanza kuyapata* " (UK 12:3: TTT).

Pamoja na kwamba baadhi ya Watanzania walikuwa wakilidharau Azimio la Arusha, mambo mengi yaliyopendekezwa katika Azimio hilo yalifanikishwa. "***Dunia ya siku hizi"*** ni dunia inayoshuhudia kuchomoza kwa siasa za vyama vingi, ni dunia inayowalazimisha watu na nchi mbalimbali kufuata mfumo wa utawala wan chi za Kimagharibi na ni dunia yenye itikadi za "***gawanya utawala***" na mwenye nguvu ndiye hutawala. Hata hivyo, tusisahau maadili yetu "***tusiyatemee mate mambo yetu***", huku tukuyakimbilia mambo ya uzunguni. Yetu ndiyo yatakayotufaa. Ya wale ni ya kiunyonyaji. Takriri iliyojitokeza na kinaya aliyoitumia Mwalimu vilikusudiwa kuwazindua Watanzania watambue ufaafu wa Azimio la Arusha. Maneno yaliyorudiwa rudiwa ni "***mimi***", "***nawakumbusheni***" "***sema***", "***sasa***" na "***tu***"; na kinaya imejikita katika ukinzani wa sentensi "***maneno haya si mazuri sasa kuyasema***" na "***mimi nawakumbusheni tu na wala sijayasema***"

Mwalimu aliwataka Watanzania kutambua kwamba Azimio la Arusha lilikuwa ni kibebeo cha maazimio mengine yaliyowahi kuasisiwa nchini Tanzania. Azimio la Arusha liliitakdi kwamba siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ndio njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio sawa na huru. Kuanzishwa kwake kulitokana na usanjari wa shabaha za ukombozi wa uhuru na umasikini walioachiwa Watanzania kutoka kwa Wakoloni. Ndio Tanzania ikawa ni ijikokote kwa misingi ya Ujamaa na Kujitegemea.

**Maswali ya kibalagha na takriri**: "*... linasema Azimio la Arusha, kwa msingi kabisa, kwamba nchi yetu ni ya Wakulima na Wafanyakazi". Sasa mnasemaje? Imeacha kuwa nchi ya Wakulima na Wafanyakazi? Kwa hiyo, kama tunaijenga nchi hii, tunaijenga kwa faida ya Wakulima na Wafanyakazi. Ndivyo Azimio la Arusha linavyosema. Ukweli huo umekwisha? Umefutika ? Umefutwa na nini? Nini kimefuta ukweli huo kwamba nchi hii sio ya Wakulima na Wafanyakazi? ...*" (UK 10:1: TTT)

Hizi ni kauli zilizonuiwa kuifanya hadhira itafakari jitihada zilizofanywa na Watanzania chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere - kuhusu kupambana na maadui ujinga, maradhi na umasiki ambapo Azimio la Arusha kwa misingi yake ya ujamaa na kujitegemea iliaminiwa kwamba nchi ya Tanzania ni ya Wakulima na Wafanyakazi. Kwa mwegemo huo, Mwalimu aliwataka Watanzania watafakari ikiwa nchi imekoma kuwa ya Wakulima na Wafanyakazi; kwa kuwauliza swali kwamba ***sasa mnasemaje?*** Ambapo jibu lake ni Watanzania watafakari na watambue kwamba bado nchi yao ni ya Wakulima na Wafanyakazi. Mwalimu akilisisitiza swali la awali aliuliza tena: ***Je, Imeacha kuwa ni nchi ya Wakulima na Wafanyakazi?*** kama vile haitoshi, Mwalimu aliwataka Watanzania kutafakari na kutambua tena na tena kwamba nchi ya Tanzania haijakoma kuwa nchi ya Wakulima na Wafanyakazi. Hivyo, kwa mfululizo wa maswali aliwauliza: ***Ukweli huo umekwisha? Umefutika? Umefutwa na nini? Nini kimefuta ukweli huo kwamba nchi hii si ya Wakulima na Wafanyakazi?*** Ambapo jawabu lake li pale pale kwamba Tanzania ni nchi ya Wakulima na Wafanyakazi, na kwamba ukweli huu haujakwisha, haujafutika na hautafutwa na mtu yeyote. Kwa hivyo, lugha iliyotumika ni ushawishi kwa Watanzania kutambua kwamba nchi yao ni ya Wakulima na Wafanyakazi na kwa hivyo hawana budi kila mmoja kuutekeleza wajibu wake kwa manufaa ya umma.

**Istiara na Maswali ya kibalagha**: *"... lakini kazi ya kujenga nchi hii kwa manufaa ya Watanzania wote ni kazi ya Watanzania, si kazi ya mtu mwingine. Msimamo huo tukauita Sisaa ya Kujitegemea. Msingi huo umekufa. Hivi mmeshapata Mjomba? Hivi kweli mtawadanganya Wafanyakazi kuwa msiwaambie 'chapeni kazi kama mnataka maslahi yenu yaboreshwe, tuchape kazi kwa faida yetu!' Tuache kuwaambia Wakulima kwamba 'kama tunataka maendeleo, tuchape kazi hivyo hivyo'. Hivi mtawaambia hawa kwamba 'tumeshapata Mjomba msiwe na wasiwasi!' Mjomba huyo ni nani? ..."* (UK 10:2: TTT)
Baba wa Watanzania ambaye amewalea na kujali maslahi yao ni ujamaa na siasa zake. Mjomba ni ubepari wa Kimagharibi na siasa zake na mifumo yake ya kiuchumi. Kudanganyika kwa Watanzania ni kuitakidi kwamba mjomba ama ufadhili unaweza kuchukuwa na fasi ya baba akamkwamua kiuchumi na kumkidhia mahitajio yake yote.

Mwalimu alisikitika kuona misingi ya siasa ya kujitegemea ikiwa imefutwa na viongozi waliokuwa madarakani mara baada ya kung'atuka kwake. Kitendo hiki kilimpelekea kuwauliza wananchi wa Tanzania ikiwa wamekwisha pata mbadala kwa kuwauliza swali: ***hivi mmekwisha pata mjomba?*** Kumaanisha kwamba ikiwa kuna nchi zenye sera baladia za kuwawezesha Watanzania waache kujitegemea kwa kuchapa kazi kwa ajili ya kuboresha maslahi yao; na kwamba je nchi hizo ni zipi; kwa swali kwamba ***Mjomba huyo ni nani?*** Kwamba ikiwa yupo, basi Watanzania wasidanganyike. Watafakari na watambue kwamba ujenzi wa nchi ya Tanzania ni ufanywe na Watanzania wenyewe kwa kuchapa kazi na wala si kwa kumtegemea mjomba ama mfadhili wa kuwajengea nchi yao.

**Maswali ya kibalagha**: "*Mbona mnaiacha sera yetu ina ubaya gani?" Watu wangapi watakuwa na hisa? Hebu niambieni wangapi? "... kilichochetu mnataka kukiuza. Hata hicho muuziane, halafu mpate pesa na hizo pesa zenu wala msilipe kodi! Hii ndiyo kazi tuliyowapeleka Ikulu?" ... Hamkusanyi kodi kwa nini? ... 'kusanyeni kodi!' Msipokusanya, tunaweza tukafikiria kuchukuwa hatua kama mnadhani ni mambo ya utani hivi. Sasa kusanyeni kodi!*" *Itakuwa ni kuchukuwa fulani na fulani tu! kiwanda ambacho ni chetu wote kabisa na faida itakapobaki, badala ya kwenda Hazina, iende kwa wewe na mimi! Ndiyo tumekibinafsisha na hii ndiyo sera mpya ya kuleta manufaa Tanzania! Hii ndiyo mbinu mpya imegunduliwa! Ujamaa mpya huo! Huo ni unyang'anyi tu wamali yetu wote.* (UK 17:1 -20:2: TTT)

Kauli "***mbona mnaziacha sera zetu …***" - nui yake ni shutuma dhidi ya wale waliozibadili sera za Azimio la Arusha. Ambapo hofu ya Mwalimu ni kwamba nchi itapoteza mwelekeo wa umoja na udugu uliowagharimu Watanzania kwa muda mrefu. Wenye mamlaka na matajiri wachache; aliwasawiri ya kwamba wanaiyumbisha Tanzania kwa matashi yao binafisi pasi na kujali uhalisia wa maisha ya Mtanzania masikini; na ambao ndio wengi. Ufahima wa mabadiliko ya sera za Azimio la Arusha ni ulaghai wa kuzighilibu amali za umma kwa manufaa ya viongozi wa roho na matajiri wenye uchu wa utajirisho. Ambapo sera ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma - kwao waliiona ni mwafaka katika kuuharakia uchumi wa nchi; na ndio ikwa Mwalimu ni aulize: ***Watu wangapi watakuwa na hisa? Hebu niambieni wangapi?*** Ambapo jawabu lake ni kwamba ni wachache sana. Watanzania waliowengi ni masikini.

Na kwa machungu ya kuwatetea wanyonge Mwalimu hakusita kuzikonga nyoyo za matajiri na viongozi wa roho kwa swali kwamba: ***kilichochetu mnataka kukiuza. Hata hicho muuziane, halafu mpate pesa na hizo pesa zenu wala msilipe kodi! Hii ndiyo kazi***

***tuliyowapeleka Ikulu?”*** Kauli hizi si tu kwamba zilikuwa zinakonga nyoyo za wanamabadiliko kuhusu sera za Azimio la Arusha hasa kwa kuwatelekeza raia waliowachagua ili wawaongoze kwa usawa na haki, lakini pia ni utanabahisho kwa Watanzania wote wamakinike kwamba si kila jambo linaloamuliwa na viongozi wao ni sawa. Bali wana nafasi ya kuhoji na inapobidi wana haki ya kuwapinga. Ndiposa Mwalimu aliwarudi wanamabadiliko wa sera za Azimio la Arusha - kwa suluhisho akawaambia kwamba: ***Hamkusanyi kodi kwa nini? ... 'kusanyeni kodi!’ Msipokusanya, tunaweza tukafikiria kuchukuwa hatua kama mnadhani ni mambo ya utani hivi. Sasa kusanyeni kodi***!"; kumaanisha kwamba, Mwalimu aliziona sera zilizotelekezwa zilikuwa bado ni faafu katika maongozi ya nchi - hususani kwa nchi inayokulia kiuchumi kama Tanzania. Kwa mnasaba huo, ikawa ni awashauri Watanzania kwamba, mbadala mwafaka ungekuwa ni kukuza uchumi wa nchi kwa kujenga nidhamu katika kukusanya kodi ya serikali na kuhakikisha kwamba mapato yanawafikia raia kwa uadilifu. Ubinafsishaji wa viwanda vya umma kwa mkabala wa kuendeleza utajirisho kwa matajiri wachache na kuwaacha masikini ambao ndio wengi - kuendelea kunyong'onyea na kunyang'anywa hata kidogo walicho nacho haufai Kwa hiyo ushawishi wake ulikuwa ni rai kwa Watanzania kuhakikisha kwamba wanakabiliana na wahujumu uchumi na walaghai wa mali za umma na kuhakikisha kwamba wale wote wanaotaka mamlaka ya maongozi ya nchi, Watanzania (wapiga kura) wafanye taathamini ya kina ili kuwapata viongozi bora na sio bora viongozi.

**Kejeli na takriri**: " *Sasa, sera hii itazaa mamilionea Tanzania sasa hivi na sio baadaye, lakini watakuwa mamilionea watano. Hata hivyo, wakati huo huo, pia itazaa masikini na Tanzania itakuwa na masikini wengi sana* ". (UK 22:1: TTT)

Kusudio la kauli hizi ni taswira ya simanzi inayompitikia Mwalimu kutokana na mkengeuko wa mabadiliko ya sera za Azimio la Arusha yaliyofanywa mara baada ya kung’atuka kwake. Ni kumbukizi ya jitihada zake tangu kabla ya uhuru ambapo baada ya kung’atuka anaziona zimeambulia patupu. Watanzania waliokuwa wakishirikiana na kuyafaidi matunda ya jitihada zao. Leo yake amali za umma zinakuwa mikononi mwa wachache kutokana na uroho wa viongozi na matajiri wenye uchu wa utajirisho huku wakizijenga hoja ya kwamba ni katika kuyaharakia maendeleo ya nchi kiuchumi. Kwa ulaghai huo ndiposa Mwalimu akiwakejeli kwa kusema: "***Sasa, sera hii itazaa mamilionea Tanzania sasa hivi na sio baadaye, lakini watakuwa mamilionea watano. Hata hivyo, wakati huo huo, pia itazaa masikini na Tanzania itakuwa na masikini wengi sana”*** akimaanisha kwamba ni ukweli usio na kificho kwamba wengi wa Watanzania ni masikini. Ikiwa cha wote kitafanywa kuwa cha wachache

ni dhahiri kwamba kitendo hicho ni cha kuendelea kuwa fanya Watanzania waliowengi kuwa masikini zaidi. Matajiri walio wachache wataendelea kuwa matajiri na kwa hivyo kujenga tabaka la walionacho ambao ni wachache na la wasionacho ambao ndio Watanzania waliowengi.

**Maswali ya kibalagha** na tafsida kengeushi: "*Lakini sisi ni madodoki?, Mawazo ya kipumbavu ...*" (UK 23:2: TTT)

Kwa muktadha wa kutokuzingatia sheria za nchi, lugha iliyotumika ni onyo kwa viongozi wenye tabia ya kukubali matakwa binafsi ilhali iwazi kwamba ni kombo na sheria za nchi. Kwa hivyo, ni ushauri kwa jamii kutoyaendea mambo kibubusa ili kuepuka lawama na msononeko wa maisha ya baadaye. Kauli hizi zina dhihirisha machungu ya Mwalimu kutokana na tabia za viongozi kuongoza bila ya kufuata sheria za nchi kwa ajili ya kujali maslahi ya kibinafsi, kwa kutokuchuja mawazo au ushauri wanaoupata ikiwa una faida au hasara kwa wananchi. Kwa hivyo, aliwashawishi Watanzania kwamba, kila unapowadia wakati wa uchaguzi, wa hakikishe wanawapata viongozi shupavu, wenye maamuzi ya busara katika kuongoza na kusimamia amali za nchi kwa faida ya wote.

**Takriri, matumizi ya sentensi fupi fupi na tashbiha**: "*Sasa Azimio la Arusha silisemei, maana ili kulisemea Azimio la Arusha, bwana, lazima kuwa na moyo kama wa mwenda wazimu. Kwa hiyo, sithubutu*; *Azimio la Arusha lilikuwa na misingi, mingine safi sana. Na narudia nalisoma. Ninalo. Natembea nalo. Natembea na vitabu viwili: Bibilia na Azimio la Arusha. Nasoma. Narudia. Sijagundua pabovu. Ni Azimio la misingi ya utu. Moja liliweka miiko ya uongozi ... viongozi wetu walikutana Zanzibar wakaona Azimio la Arusha halifai. Wala hawakututangazia na hawakuzungumzia kwamba tumekutana Zanzibar tumeona Azimio la Arusha halifai"*. (UK 21:3; 4 -5: N)

Mwenda wazimu ni mtu asiye na akili timamu, aweza kufanya lolote la kumdhuru mwingine, au kufanya jambo lolote la aibu, au la kuhuzunisha na ingawa watu watabakia kusikitika na hata kumshutumu kwa aliyoyatenda lakini hufutwa na umakinifu kwa kutambua kwamba ameyatenda kutokana na upunguani wake. Ndiyo Mwalimu akisema: "***… kulisemea Azimio la Arusha, bwana, lazima kuwa na moyo kama wa mwenda wazimu***" ambapo kwa muktadha wa Azimio la Arusha kwa leo yake, fahiwa yake ni kwamba inamwia vigumu kulizungumzia tena hasa baada ya kuonekana limepitwa na wakati. Kwa majonzi zaidi akiulalamia uongozi ulioshika hatamu baada yake kwa kusema: ***viongozi wetu walikutana Zanzibar wakaona Azimio la Arusha halifai. Wala hawakututangazia na***

***hawakuzungumzia kwamba tumekutana Zanzibar tumeona Azimio la Arusha halifai.*** Kumaanisha kwamba huo ulikuwa udhihirisho wa kiudhalili siyo tu kwa mkongo wa moyo wake bali pia wafuasi wake waliokuwa wa kiunga mkono siasa ya ujamaa na kujitegemea. Siasa hiyo ilijengwa kwa misingi ya Azimio la Arusha iliyodumu kwa muda mrefu. Kinachosikitisha ni kuonekana si kitu baada ya kung'atuka kwake; kwa taifa aliloliongoza kwa muda mrefu kwa misingi ya mfumo wa Azimio la Arusha; ikawa ni kutengwa na isijuzwe taarifa kwa wanaujamaa kuhusu chembelecho Azimio la Zanzibar.

Ingawa hivyo, kwa kuwatetea wanyonge Watanzania wanaovuliwa mbeleko kwa utashi wa viongozi wa kutokuzingatia mbeko za uongozi, Mwalimu alitastiti kwa kusema: "***… Azimio la Arusha lilikuwa na misingi , mingine safi sana. Nanarudia nalisoma. Ninalo. Natembea nalo. Natembea na vitabu viwili: Bibilia na Azimio la Arusha. Nakasoma. Narudia. Sijagundua pabovu. Ni Azimio la misingi ya utu. Moja liliweka miiko ya uongozi***. Kilichokusudiwa kwa kauli hizi ilikuwa ni kuzisuta nafsi za viongozi na pengine wafuasi wao waliodiriki kuzifuta sera za Azimio la Arusha kinyemela ilhali zingali faafu katika maongozi ya nchi changa ya Tanzania inayokulia kiuchumi na kisiasa hasa kwa usadifu wa mazingira ya wakulima na wafanyakazi. Kusudio hilo linadhihirika kutokana na matumizi ya takriri na sentensi fupifupi ambayo ni faafu katika muktadha wa hotuba yake.

Kwa hiyo ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania ulikuwa ni Watanzania wamakinike kwa kila linalotendwa na viongozi wao. Inapokuwa wanakwenda kombo wasione haya kuwakemea na hata kuwaengua madarakani kwa minajili ya kulifikia lengo kwa umoja na siyo kwa utashi binafsi. Lakini pia kuwa na mikakati madhubuti kila unapowadia wakati wa uchaguzi; kuhusika katika kuzipembua sifa za viongozi ili kuwapata viongozi safi; lakini wenye utu na uzalendo kwa taifa lao.

### 4.4.12 Maudhui kuhusu Ubaguzi

Suala la ubaguzi katika jamii ni katika maovu ambayo Mwalimu aliyakemea takriban katika kipindi chote cha uhai wake. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulikuwa ni mtagusano wa mawazo yake kwamba udugu uliotelekezwa na Wakoloni ungelirejeshwa ungelileta afua njema kwa wazawa hao. Daima Mwalimu aliwarai raia Watanzania waepuke tabia ya kuwabagua wengine kwa misingi ya rangi zao, udini, ukabila na ama kieneo. Ilikuwa ni imani yake kwamba kwa kufanya hivyo, jamii itaishi kwa amani, upendo na ushirikiano. Katika kuyadhibiti maonyo yake, Mwalimu aliwakumbusha Watanzania kuhusu ubaguzi wa rangi, jinsi ambavyo mkongo wa madhila yake unavyoendelea kuzichoma nyoyo za

wanyonge milele na milele hasa ikikumbukiwa harakati za ukombozi wa nchi za Afrika na mapambano yake dhidi ya ukoloni na ukoloni mambo leo. Fauka ya hivyo, Mwalimu aliingiwa na simanzi kwa kuwaona Waafrika wakiyatenda madhambi ya ubaguzi; sawa na walivyokuwa Wakoloni Afrika; mintaarafu Afrika Kusini.

Kwa kumrejelea Idd Amin (aliyekuwa rais wa Uganda); Mwalimu aliwakumbusha Watanzania jinsi ambavyo tabia na jeuri yake ilivyokuwa sawa na ya Wakoloni; kwa jinsi walivyojinadi kwamba ni halali yao kuwatawala wengine. Waliamini kwamba rangi nyeupe walioumbwa kwayo ni bora kuliko wengine kwa rangi zao. Naye Idd Amin mbali na Uafrika wake, alijinasibu kaida za Wazungu kwa kuudhihirishia ulimwengu kivitendo; ambapo mbali na kuivamia ardhi ya Tanzania sehemu za Kagera kwa madai kwamba ni eneo la Uganda alitumia ufagio wa chuma kuwaondosha wasiokuwa wazawa wa Uganda. Wakiwemo Wahindi na Waingereza. Ubaguzi ambao ulikuwa ni sawa na wa Wakolono dhidi ya watu wa Afrika Kusini au penginepo enzi za Ukoloni. Uzandiki ambao uliwaghilibu Waafrika wengi fikra; wakidhani kwamba alilokuwa analifanya Idd Amin lilikuwa ni halali.

#### 4.4.12.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Ubaguzi

**Maswali ya kibalagha**, takriri na tashhisi*: Lakini kwa nini jambo hili latufurahisha? Kwamba Amini amewafukuza wazungu, amawafukuza Wahindi, liwe jambo la furaha rohoni; kwa bubu? Niliwauliza mimi wakati anawafukuza, kwa nini hasa linafurahisha jambo hili? Wahindi ni watu,ni binadamu; unafurahi kuona binadamu wanaonewa, kwa nini? Kwa sababu, unasema, siyo rangi yangu. Lakini ukisha sema hivyo, wewe ni sawa sawa kabisa na mkoloni mwingine yeyote yule anayeonea watu kwa sababu ya rangi yao. Wamekosa nini? Tena Wahindi wale wanapigwa, hawana chochote, kwa sababu hawana mtetezi wao; hata Waingereza wakati huo wameogopa kuwatetea. Wanapigwa, wanafukuzwa, bila mali; na watu wengine wanafurahi rohoni! Wanyonge hawa wanapigwa mateke; wewe unafurahi nini, kinakufurahisha nini? Hawa ni binadamu wenzako sawa sawa kabisa na wewe. Wamekosa nini? Wanarangi tofauti tu, basi.* (UK 7:2: OIA)

Maswali ya kibalagha aliyoitumia Mwalimu inatokana na usawiri wake dhidi ya mtendo ya aliyekuwa rais wa Uganda, Idd Amin; ambaye aliivamia ardhi ya Watanzania sehemu za Kagera. Nchini Uganda aliwafukuza wageni kwa rangi zao huku Waafrika wakishangilia ya kana kwamba Idd Amin alikuwa akifanya jambo la busara. Ndiposa Mwalimu Nyerere aliuliza kwa kusema: ***"Lakini kwa nini jambo hili latufurahisha?*** Akimaanisha kwamba Waafrika walikuwa hawana budi kuyaona matendo ya Idd Amin kwamba hayakuwa na

tofauti yeyote na yale ya Wakoloni. Wazungu waliamini kwamba Mungu kawajaalia ngozi nyeupe kwa uoni wa ubora zaidi kwa wengine kwa rangi zao. Kwa hivyo ilikuwa ni halali kwao kuwatawala wengine kadiri wawezavyo. Idd Amin naye mbali na uafrika wake alijinasibu aila za Wazungu na akaudhihirishia ulimwengu kivitendo kwa kuivamia ardhi ya Waafrika wenzake (ardhi ya Tanzania sehemu za Kagera) na kuwabagua wengine kwa rangi zao (kwa kuwapiga na kuwaondoa Wahidi katika ardhi ya Uganda) bila ya hofu. Ndiyo Mwalimu akauliza tena na tena kwamba: ***"… liwe jambo la furaha rohoni; kwa bubu?"***... ***kwa nini hasa linafurahisha jambo hili?*** *"...* ***unafurahi kuona binadamu wanaonewa, kwa nini? "… Wamekosa nini?*** Ulikuwa ni uoni wa Mwalimu kwamba, bila shaka Waafrika wamejisahau, ubaguzi waliofanyiwa na Wakoloni hata ikawa hakuna jinsi hadi pale walipojikomboa kwa kupata uhuru ndio wakawa wana sauti ya kujitambulisha mbele ya Walimwengu. Haikutegemewa kwamba wangeingiwa na furaha wakati wenzao wakifanyiwa matendo yaleyale ya dhuluma tena na Mwafrika mwenzao.

Ilikuwa itoshe kuyaona matendo ya Idd Amin ya kwamba ni jeuri iliyozidi jeuri ya Wazungu. Wakoloni. Kwa usintofahamu huo, Mwalimu alikongwa moyoni kwa machungu zaidi na ikawa hanabudi kuuliza tena kwamba: ***Rangi ni dhambi?*** Kwa mnasaba wa kuwataka Waafrika wafanye tafakuri ya kina ili wapate kutambua kwamba ni dhuluma kwa mtu yeyote kumhilikisha mwingine kwa rangi yake au kwa taifa lake. Ibainike kwamba tofauti za rangi walizonazo wanadamu kwa mataifa yao ni majaaliwa ya Mungu Muumba. Kwa hivyo ni makosa mwanadamu kumnyanyasa mwanadamu mwenziwe kutokana na tofauti ya rangi yake au taifa lake hasa ikisadifu kwamba hata anayemfanyia mwenzake uonevu huo, hata yeye asingependa kufanyiwa hivyo.

Kwa hiyo, balagha aliyoitumia Mwalimu ilikuwa ni faafu kwa Waafrika wote kutambua kwamba jeuri ya Idd Amin haikutofautiana na ile ya Wakoloni. Uvamizi wa ardhi ya Waafrika wenginzake (ya Watanzania) na kuwabagua wageni kwa rangi zao (Wahindi) ilikuwa ni alama toshelezi kwa Waafrika wote kuungana kwa ajili ya kumpiga vita sawa na ilivyokuwa kwa Wazungu Wakoloni enzi za ukoloni Afrika hasa Afrika Kusini.

**Tashhisi na tafsida kengeushi**: *Eh! Nawaambieni, wala msije mkawabagua Wahindi mkawaita 'wao' mnajiita 'sisi weusi' watu wazima lugha ya kipumbavu namna hii. Tanzania mnadhani kweli mnabagua watu kwa dhati kabisa mnabagua watu kwa rangi kiasi hiki! Sasa wazawa wajiite 'sisi weusi', 'wao Wahindi' Tanzania ile ile, mtakuta hakuna 'usisi' wo wote.*

*Nasema mkishamaliza Wahindi mtaingilia Wachaga, mtaingilia Wapare, mtangilia…hamuishii hapo.* (UK 25:3: N)

Hizi ni kauli zinazowatahadharisha na kuwaonya Watanzania kuhusu suala zima la ubaguzi wa rangi. Watanzania wanaonywa wasijihusishe katika ubaguzi wa aina yeyote ile; iwe ni kwa wazawa au kwa wasio wazawa. Kwa tathmini ya Mwalimu; baadhi ya Watanzania walikuwa wameingiwa na usintofahamu wa kumwona yeyote aliye mweupe na akawa si mzawa wa Tanzania ama nchi za Kiafika - ni mkosaji na hastahili kuzipata haki sawa na walivyo wazawa. Uoni huu ulimtia Mwalimu simanzi hata ikawa niawaulize Watanzania: ***"Tanzania mnadhani kweli mnabagua watu kwa dhati kabisa mnabagua watu kwa rangi kiasi hiki!"*** ingawa sintofahamu hii ilitokana na jinsi Wafrika walivyokinzana na Wakoloni; hasa kutokana na kauli za Wakoloni pale walipojinadi kwamba wao (Ngozi nyeupe) ni katika mataifa yaliyobarikiwa kuwatawala wengine kwa rangi zao. Dhana ambayo ilikuwa ni ya kuwadhalilisha Wafrika na pengine wengine kwa rangi zao.

Ingawa hivyo, Mwalimu aliwarudi; kwa ufahima kwamba, kufanya hivyo ni kuyatenda makosa kama walivyotendewa na Wazungu enzi za ukoloni. Pasi na kuwachelea wale wote walioingiwa na sintofahamu hiyo, alisisitiza zaidi kwa kusema: ***"… Sasa wazawa wajiite 'sisi weusi', 'wao Wahindi' Tanzania ile ile, mtakuta hakuna 'usisi' wo wote. Nasema mkishamaliza Wahindi mtaingilia Wachaga, mtaingilia Wapare, mtangilia … hamuishii hapo"*** akimaanisha kwamba, rangi ya mtu si dhambi. Kosa ni ubaguzi. Hivyo, Watanzania wasijione wao kwa rangi yao (kwa weusi wao) wana uhalali katika ardhi yao. Bali waheshimiane na wengine kwa rangi zao ili kudumisha udugu na amani.

### 4.4.13 Maudhui kuhusu Elimu kwa Wote

Swala la elimu kwa wote lilikuwa ni katika ahadi alizozitoa Mwalimu kwa umma wa Watanzania mara baada ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika. Mwalimu aliipitisha kanuni ndani ya chama na serikali kwamba kila Mtanzania atajielimisha kadiri ya uwezo wake wote na kwamba kila mmoja atakuwa tayari kuitumia elimu aliyoipata kwa faida ya Watanzania wote kwa mbiu ya kupiga vita ujinga, maradhi na umasikini. Lakini pia kuifuta sumu ya Wakoloni ambapo suala la elimu lilikuwa ni la kiubaguzi kulingana na matakwa yao ya kuzinyonya nchi za kiafrika. Nguvu kubwa ya elimu ilielekezwa kuwapata makarani wachache na sio kuvilea vipaji vya Watanganyika.kutokana na uhaba wa walimu shuleni, wanafunzi wenye uwezo wa juu walitakiwa wawafunze wenzao darasani.

Mwalimu Nyerere alikuwa miongoni mwa waliokuwa wameteuliwa kuyapata mafunzo ya ualimu wakiwa bado kuhitimu elimu ya sekondari. Ingawa jambo hilo liliwapa magumu kiasi cha kuwalazimu kusoma kwa kasi zaidi ili waweze kuzimudu changamoto zilizokuwa zikizuka darasani, aliuona utaratibu huo kwamba ungefaa kuendelezwa katika mazingira ya Watanzania hata baada ya maongozi yake. Kwa tafakuri ya madhila ya Wakoloni hususani katika kuwanyima Watanganyika elimu, serikali ya Mwalimu Nyerere ilitoa wito wa kuhakikisha kwamba watoto wa Kitanganyika, kuanzia umri wa miaka saba, wanaipata elimu ya msingi pasi na kusazwa hata mmoja katika jamii. Watu wazima nao walipewa kipaumbele kwa kuanzishiwa "elimu ya watu wazima" kwa mtazamo kwamba wale ambao hawakubahatika kuipata elimu ya msingi enzi za ubabe wa Wakoloni; waipate tena kwa mapana zaidi. Iliamuliwa kuwa elimu iwe ni ya mseto ili iwasaidie katika nyanja mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji na kadhalika, hasa kwa uzingatifu wa misingi ya ujamaa na kujitegemea. Elimu inayomwezesha mtu kuyakabili maisha yake kulingana na fani mbalimbali zilizomo katika jamii iliyowazunguka ndiyo iliyowafaa Watanzania.

Katika kulifanikisha hilo, serikali ilihimiza shule zote ziwe na ratiba maalum kuhusu kazi za mikono kwa ajili ya kulea vipaji, tabia ya kazi, moyo wa kujitolea na ubunifu wa kujiajiri. Shule zilitakiwa pia zifungue milango ya utangamano kati ya wanafunzi wa shule moja na nyingine, jumuiya ya shule na jamii iliyowazunguka kwa nia ya kuinua vipaji vya michezo, kilimo, ufugaji, useremala na kadhalika. Ingawa hivyo, Mwalimu alipata kigugumizi cha maono yake hasa alipotanabahi kwamba baadhi ya Watanzania waliingiwa na usintofahamu kiasi cha kushindwa kuitofautisha elimu iliyokuwa ikitolewa enzi za Wakoloni na msimamo uliokuwa ukiendelezwa chini ya maongozi yake.

Mwalimu alishtushwa kwa kuwaona miongoni mwa Watanzania waliojivyaza kasumba za Wakoloni - kwa kuamini kwamba elimu bora ni ile iliyotolewa na mkoloni. Ndiposa ilimbidi azifafanue tofauti hizo ili Watanzania wote wapate mashiko kwa maamuzi ya viongozi wao kuhusu sera ya elimu; kwa ukanushi kwamba kilichojiri enzi za ukoloni kilikuwa ni kufukuzwa kwa wanafunzi waliokuwa hawaelewi kwa haraka kile walichokuwa wanafunzwa darasani. Wale waliokuwa wamebahatika kuvuka vidato na hatimaye kuhitimu walionekana kwamba walikuwa na akili sana. Waliokuwa na mtazamo huu hawakutathmini wingi wa wale walioishia njiani kutokana na utaratibu wa kikoloni ambapo haja yao ilikuwa ni kuwapata makarani na sio kuinua vipaji vya Watanganyika. Kwa hivyo, kwa watoto ambao vipaji vyao havikuelekea mwegemo wa Wakoloni hawakuonekana ni wenye akili na kwa hivyo walipaswa kuishiliza masomo yao njiani na jamii kuwachukulia kwamba hawana uwezo

katika fani ya elimu na kwamba kilichobakia kwao ni kushika jembe kama fani ya watu duni ambao mtaji wao ni nguvu zao wenyewe katika kuyanusuru maisha yao.

Athari hizo za Wakoloni dhidi ya Watanzania ndizo zilizompelekea Mwalimu kuyakumbukia malengo ya kupigania uhuru. Baada ya uhuru wa Tanganyika ilikuwa ni kuhakikisha kila kijana wa Kitanganyika anapata elimu hadi kiwango cha darasa la saba (elimu kwa wote). Ndiposa Watanzania kuwataka watambue kwamba kila uchao kwa Watanzania ni faraja inapotokea wanafuzi wengi wanahitimuwakiwa wenye vipaji tofautitofauti, tofauti na yalivyokuwa malengo ya Wakoloni ya kuwapata makarani tu tena wachache kutegemeana na nafasi za ajira zao kwa wakati huo. Kutokana na mikakati ya kuifanisisha elimu kwa Watanzania, chini ya uongozi wake Mwalimu, serikali iligharamia wanafunzi gharama zote za kiusomi. Sababu iliyopelekea kufanya hivyo ilikuwa ni kuwapa wazazi tahafifu ili waweze kukabiliana na majukumu mengine ya kimaisha na wakihitajika wajitolee kushiriki katika ujenzi wa majengo ya shule ili kuongeza wingi wa madarasa. Hivyo, ilikusudiwa kuhakikisha kwamba watoto wote wa Tanganyika wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa wote bila ya kigugumizi cha kwamba watasomea wapi. Wazazi pia walitakiwa wa shirikiane na serikali hususan katika malezi ili kuepuka wazembe na wazururaji wasiopenda kufanyakazi. Kwa kufanya hivyo, Mwalimu Nyerere aliamini kutaepusha lawama ya wazazi dhidi ya serikali na badala yake (kwa pamoja) watajenga jamii yenye kujitegemea kiuchumi lakini yenye kujali utamaduni wa Watanzania hususan katika kudumisha upendo, umoja na amani.

#### 4.4.13.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Elimu kwa Wote

**Takriri**: "… *tugeuze mawazo kabisa kabisa kabisa; tuzitizame hizo gharama ziko wapi halafu tuzikatae hizo gharama, na watoto wetu wasome na wasome kwa muda mfupi zaidi*."(UK 4:1: AM)

Huu ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa wananchi hususan wazazi kuhakikisha kwamba watoto waliofikia umri wa kwenda shule, wanakwenda shule na kuhakikisha kwamba wanapata elimu stahiki, yenye kuwawezesha kuyakimu maisha yao kulingana na mazingira wanamotokea. Katika utekelezwaji wake, wazazi walitakiwa washirikiane na serikali katika ujenzi wa shule na malezi ya watoto nyumbani na shuleni ili kulifikia lengo kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

**Tashhisi takriri**: "*...hali ya walimu ilikuwa ngumu; na ndiyo ikawa ukipata mwanafunzi anauliza uliza maswali unamzima!"* (UK 8:1: AM)

Hizi zilikuwa ni kumbukizi za Mwalimu kwa jinsi walivyowezeshwa kuipata elimu enzi za ukoloni ambapo walimu wazoefu ulikuwa ni wajibu wao kuhakikisha kwamba wanawafunza wanafunzi wateule shuleni mafunzo ya ualimu kwa muda mfupi ili waweze kuwasaidia wenzao kutokana na uhaba wa walimu uliokuwepo kipindi hicho. Ndiyo ikawa kwa magumu hayo, watumie ujanja wa kuyakwepa maswali yaliyokuwa yakiulizwa na wanafunzi walionyesha talanta zao pindi walipokuwa wanawafundisha darasani. Changamoto hizi walizokabiliana nazo Mwalimu Nyerere enzi hizo Mwalimu aliwachagiza kama ushawishi kwa Watanzania wa leo hasa katika maeneo yenye uhaba wa walimu shuleni. Alihimiza kwamba ni bora wakateuliwa wanafunzi wenye talanta zaidi darasani wakafunzwe ualimu hata kabla ya kuhitimu masomo yao endelevu ili waweze kuwasaidia wenzao wenye vipaji vya mwendo pole lakini pia kuziba pengo la uhaba wa walimu shuleni.

**Vihisishi na swali ya kibalagha**: "*Watoto wa siku hizi! ah! Walimu wasiku hizi bwana hawajui kufundisha*."; "*Unalinganisha nani hawa*?"; "*Elimu kudidimia maana yake nini?"* (UK 11:2: AM)

Usawia wa mbinu hizi za lugha alizozitumia Mwalimu katika (UK 11:2: AM) ni kwamba, Mwalimu alikuwa akiwashangaa na huku akijiuliza kwa jinsi wazazi walivyoingiwa na suintofahamu hata ikawa ni walinganishe elimu iliyokuwa ikitolewa enzi za ukoloni kwa kuwabagua wanafunzi kwa talanta zao na kuwafanya wengi kuishia madarasa ya chini na ama kutosoma kabisa. wakati ambapo leo yake serikali ilikwisha amua kuwasaidia wanafunzi kwa kumtaka kila mmoja kusoma hadi darasa la saba; jambo ambalo kwa tofauti ya vipaji na wingi wa wanaohitimu ni dhahiri uchache wao wataonekana kwa uduni fulani kitalanta; ambapo enzi za Wakoloni isingeonekana mwishoni kwa sababu wengi walikuwa wakiishia njiani. Kwa hiyo, mtazamo wa Mwalimu ulikuwa ni kwamba lawama za namna hiyo zinatokana na ufahima mdogo katika kuuchuja ukweli wa uwiano kati ya taratibu za elimu ya wakati wa ukoloni na mafanikio yake; na taratibu za elimu zilizojiri mara baada ya uhuru na mafanikio yake kwa Watanzania.

**Maswali ya kibalagha na tashhisi**: "*Elimu ya nini? Elimu hasa ya nini? Elimu! Elimu! Elimu! Elimu hasa ya nini?"* (UK 2:1: ME).

Huu ni mtagusano wa maswali na mshangao kuhusu elimu gani ni muhmu kwa vijana wa kitanzania. Baadhi ya Watanzania wakiishutumu serikali iliyopo madarakani chini ya uongozi wa Mwalimu; kwamba elimu waliyokuwa wakiipata vijana ilikuwa haiwafungui kuendelea kwa vidato vya juu.

Fauka ya kwamba serikali ilifafanua kwamba elimu baada ya uhuru ndiyo inayowafaa vijana wa Kitanzania, wanamaliza kwa wingi hata kama siyo wote wanaoendelea kwa vidato vya juu kwa maana ya kuendeleza fani mbalimbali vivyo hivyo waliowengi wanauwezo wa kujitegemea. Huo ndio uliokuwa mtazamo wa Mwalimu Nyerere kuhusu kuwatayarisha wanafuzi kulingana na mazingira wanamotokea. Kama ni wakutoka vijijini basi waandaliwe kwa kilimo, mifugo na kadhalika. Hii ndiyo kusema, muumano wa balagha na kwa namna ilivyotumika ni udhuhirisho wa kero waliyonayo watu kuhusu elimu. Msisitizo wa kauli hizo ni kuonyesha kwamba mawazo yanayotolewa ni sahihi, hayahitaji kutenguliwa na ikiwa mtu atataka kujibu mashambulizi basi atarajie kwamba watu watamshangaa kwa kuonyesha kwake upinzani usiokuwa na maana.

**Maswali ya kibalagha na takriri**: "*… Chapa kazi. Ataanza wapi? Ataanzaje?*" ... *mlimfundisha lini kazi au tabia ya kazi? .... eti sasa utakula kalamu?* (UK 17:3; 18:1: AM)

Hizi ni kauli zilizonuia kuzikonga nyoyo za raia wenye tabia ya kulaumu pasina kufanya jitihada yeyote hata ya tathmini kuhusu lile lililowakera. Kwa muktadha wa elimu kauli hizi zinawaonya wazazi au walezi pale wanapoilaumu serikali kwamba ina mkono katika kuwafanya wanafunzi wanaohitimu masomo yao wasiwe ni wenye kuitumia elimu waliyoipata na badala yake kuendelea kuwa tegemezi kwa jamii. Kumaanisha kwamba elimu inayotolewa haikidhi viwango kulingana na uhalisia wa maisha ya jamii iliyowazunguka. Tathmini ya uoni huo ndiyo inashajiisha utumizi wa balagha hiyo kama njia ya kuwarudi walezi wa wanafunzi kwamba uwajibikaji si kwa serikali peke yake, serikali na walimu au walimu na wazazi, bali ni kwa kila mmoja kuyatenda mambo kwa usawia wake; ikiwa ni pamoja na kuwalea vijana kuweza kutumia talanta zao katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Wanatakiwa wawe wabunifu, waweze kujitegemea, wasaidie jamii zao na Taifa kwa ujumla. Kwa hivyo, wito wa Mwalimu Nyerere ulikuwa ni kumtaka kila Mtanzania kujiuliza kwamba ni kwa jinsi gani amefanya jitihada juu ya jambo lenye kukwaza maendeleo kabla ya kuwarushia wengine lawama na ndio iwe watu washirikiane katika kulitatua.

**Uchanganyaji ndimi**: "*… Actually wengi wetu tunatafuta elimu kutafuta a lot of prestige, basically, na kitu kinachotoa prestige ni kitu ambacho ni cha wachache".* (UK 2:1: ME)

Maneno: ***"Prestage"***: Heshima anayoipata mtu kutokana na mafanikio yake au hadhi yake katika jamii. **"*Basically"***: Ni kivumishi kilichotumika kusisitiza mambo muhimu ambapo kwa muktadha wa maudhui ya elimu yaliyoendelezwa na Mwalimu, ilikuwa ni kuonyesha njia ya kipi kizingatiwe na wazazi au walezi kwa vijana wao.

Mwalimu alielezea sababu na umuhimu wa elimu baada ya kuona kwamba watu wengi hawatilii maanani swala la elimu. Ili kuonyesha umuhimu wa kufanya hivyo, alitumia visisitizi na vivumishi vinavyosisitiza jambo hilo kama vile ***"actually", "basically", "a lot of ", "wengi"*** na ***"ambacho".*** Usemi huo umepachikwa pia na msamiati wa Kingereza, lugha ambayo dunia nzima huichukulia kama kielelezo bora cha waliosoma. Kwa hivyo, matumizi ya msamiati wa namna hiyo yalikusudiwa kuishawishi hadhira kuitafuta elimu kama jambo la lazima katika maisha ya mwanadamu.

**Uchanganyaji ndimi na tashhisi**: "*... acha hii elimu hii ya prestige which is nonesence. Mtu anayetafuta elimu ya prestige ni mpumbavu na kama si mpumbavu ni victim tu! Ni victim wa hali hizi tulizonazo za kijingajinga.* (UK 3:1: ME)

Huu ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa hadhira yake kuhusu elimu. Mwalimu anatoa onyo kali kwa wale wanaoitafuta elimu ya jaha ***"Prestage".*** Ukali wa onyo hilo unabainika katika matumizi ya virai kibalagha ***"acha hii", "elimu hii", "ya prestage"*** - akimaanisha kwamba kwa wenye mtazamo wa namna hiyo elimu hiyo itakuwa haiwasaidii; watakuwa hawajaelimika na akidai kwamba ni ***"… nosence"*** - ni elimu ambayo haina maana katika utendaji wa maisha yao ya kila siku zaidi ya kujivuna tu! na kwamba ambaye hataiona elimu hiyo ya jaha ni bora basi ni atambue kwamba ni **"*victim"*** kwa maana ya mtu aliye athirika kwa tabia za wengine mintaarafu ya walivyokuwa wakijikweza Wakoloni kwamba, kwa rangi yao nyeupe kwamba wao ni bora zaidi na kwa kila chao; na ndio ikawa pia kwa mwenye elimu ya kimagharibi (Mwenye kuzungumza Kingereza kama wao) wakimchukulia ni mtu bora. Anaonekana kuwa mwenye fani wazitakazo ingawa kwa jamii anamotokea zitakuwa haziwasaidii. Mwalimu aliziita hali hizo ni za "***kijingajinga"*** Kwa onyo kwamba Watanzania wasihisi ni ufahari kwa mtu kuwa na elimu hiyo ya jaha bali elimu yenye manufaa ni ile itakayomfanya mtu akayabadili maisha yake kutoka katika hali duni na kuwa nzuri na yenye kuleta maendeleo kwa taifa lake.

**Uchanganyaji ndimi**: "*Walimu watayarisheni watoto wenu kwa maisha watakayokwenda kuishi katika vijiji vyao. Basi full stop*" (UK 4:3: EKT).

Walimu ndio wahusika wakuu katika swala zima la elimu ndiyo maana wakatajwa mwanzoni mwa usemi huo. Wanatarajiwa kuwatayaisha watoto kwa maisha ya vijijini. Watawatayarisha kivipi? Kwa kuwapa elimu itakayowafaa huko. Waendako kwenye vijiji na sio elimu ya kupata utukufu ***"Prestage"*** Vijijini kuna kazi mbalimbali ambazo wanapaswa kutayarishwa kwazo. Miongoni mwa kazi hizo ni ukulima, ufugaji, biashara na kadhalka. Halafu vijiji vya ujamaa vilihitaji sana ushirikiano katika utenda kazi. Kwa hiyo, elimu muhimu katika mazingira kama hayo ni ile inayofungamana na kazi hizo na jinsi zinavyoweza kufanywa kwa njia ya ujamaa. Kama kuna aliyetarajia kwamba kulikuwa na jambo jingine ambalo kwalo watoto wangeweza kutayarishwa basi alikatishwa tamaa kwa pale alipokuwa akitumia maneno: ***"basi"*** na ***"full stop"*** kwani Mwalimu alisema hivyo akimaanisha kwamba hakuwa na la ziada.

**Msemo**: *Kanga hatagi ujani utumwani.* (UK 6:3: ME)

Kanga ni aina ya ndege afugwaye na mwanadamu. Kwa silka yake ni kwamba hatagi ikiwa anahisi ametenzwa nguvu. Ikiwa mazingira alimowekwa hayampi uhuru wa kijiamulia atakavyo anaweza kueleweka katika eneo moja au kafungwa kamba akihofiwa kwamba atatoroka. Na kwa hivyo, kwake inakuwa tabu kuweza kujivinjari na kujiamulia wapi atage mayai yake. Sanjari na muktadha wa elimu, ulikuwa ni ufahima wa Mwalimu kwamba mtu hawezi akawa anajinafasi kwamba ni msomi ikiwa matendo yake bado yangali yana sumu ya ukoloni. Hana uhuru wa fikra na angali anaongozwa kwa matakwa ya wengine.

Kwa hivyo, ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania ulikuwa ni watambue kwamba, wana kila namna ya kuyafanya matendo yao yasawiri uhalisia wa mazingira yao; lakini pia tamaduni na mila za kiafrika na siyo za kimagharibi kwa kudhania kwamba ndiyo maendeleo.

**Maswali ya kibalagha ya uchanganyaji ndimi**: "*... Kwa nini mnafanya maisha ya hawa eighty seven percent yawe ndiyo yanawategemea wale thirteen badala ya the other way round?* (UK 4:1: EKT)

Katika nchi nyingi za Kiafrika idadi ya waliosoma ni ndogo sana ikilinganishwa na wasiosoma. Katika hali kama hiyo, kiwango cha utegemezi huwa ni kikubwa zaidi kwani wasiosoma wanakidhiwa haja zao na wale wachache wanaojiweza. Hali hii hairidhishi ndiyo maana Mwalimu Nyerere akaishawishi jamii ya Watanzania kupitia maswali ya kibalagha na

uchanganyaji ndimi ili waridhie mipango ambayo ilikwisha wekwa ya elimu yenye manufaa. Elimu hiyo ndiyo inayoweza kupunguza kiwango cha utegemezi hivi kwamba angalau "***thirteen percent*** " itegemee "***eighty seven percent***" kutatua tatizo linalolikumba nchi

Haya yalikuwa ni maonyo ya Mwalimu kwa jamii ya Watanzania kutokana na usintofahamu wao, kwamba ni heshima kwao kuwazingatia zaidi wanafunzi (watoto) waliobahatika kuendelea na masomo lakini wale waliokosa bahati hiyo ni wajishughulishe wenyewe kiasi cha kuhofiwa taifa kuwa na lindi la vijana wazururaji kutokana na kukosa mwelekeo wa jamii zilizowazunguka.

**Maswali ya kibalagha na takriri**: "*... Mwanangu kasoma halafu alime? Kusoma huko kwa kulima ni kusoma gani huku? Maana nia ya kusoma, madhumuni ya kusoma ni kuepuka jembe. Anasoma mtu aepukane na maisha haya ya vijijini ya majembe majembe haya. Mwanangu ndivyo nilivyotaka mimi nimpe nafasi asome aepukane na maisha haya. Sasa mmemrudisha. Mnanirudishia mtoto huyu! Mnanirudishiaje mtoto huyu? Ntamfanyaje*? (UK 39:1: EKT)

Hizi ni kauli zilizowasawiri baadhi ya Watanzania kwa jinsi walivyoshindwa kuitafsiri elimu katika utendaji wa maisha ya Mtanzania. Kwa kuiendeleza kasumba ya ukoloni pale ilipokuwa ni wasomeshe watoto wachache kwa ajili ya kuwasaidia mambo ya ukarani; na ikawa pindi anapomaliza kulikuwa na uhakika wa kupata hiyo kazi. Kwa hivyo, ukawa ni utukufu kwa mtu aliyebahatika kusoma. Baada ya uhuru, elimu kwa wote ilifanywa ni haki ya kila Mtanzania, huku elimu ya sekondari na vyuo ikiwa ni kwa wale waliofaulu kuendelea na masomo ya juu.

Mtazamo wa wazazi wa kuendeleza kasumba ya Wakoloni kwamba wanaposomesha mtoto basi hawezi tena kurudi nyumbani na akafanya kazi nyingine; kwamba yeye basi ni mtu wa kalamu tu! Maishani mwake kwa mategemeo kwamba atapata kazi nzuri na kwa hivyo atakuwa ameiletea heshima kubwa familia yake, heshima ambayo ni kama kifuta jasho kutokana na magumu yaliyopitiwa katika usomi wake. Fikra hizo hazikuwa sahihi. Wazazi haikuwaingia akilini kuwakumbuka watoto waliokosa bahati ya kuendelea na masomo ambao ni wengi zaidi. Wenye umri mdogo zaidi na wanatumika kufanya kazi ngumu kama vile kulima, kulisha mifugo majani na kadhalika. Badala ya wazazi kujiuliza jinsi ya kunyanyua maisha ya hao ambao ni wengi zaidi, walizidi kuwadharau na kuonekana ni haki kwao kufanya kazi ngumu. Kwa maoni yao, mbora ni yule aliyeweza kuendelea na elimu; na kwa hivyo, hawezi kufanya kazi za watu duni wasio na elimu.

Mwalimu Nyerere aliuona mtazamo wa namna hiyo kwamba ni wakimakosa na badala yake wazazi walitakikana kuwajali zaidi watoto walio majumbani. Lakini wale waliobahatika kuendelea na masomo pia kisomo chao kitakuwa hakina maana ikiwa watashindwa kuwajibika katika mazingira ya uzawa na kwa kazi mbali mbali kama za kilimo, mifugo na kadhalika. Mwalimu aliona elimu bora ni ile itakayomwezesha mtu kuyafanya mambo kwa ufanisi na sio kumkita mtu katika jambo moja tu. Elimu ya namna hiyo ni ya kumfanya mtu aendeleze utegemezi katika jamii na kwa hivyo atakuwa bado hajaelimika. Mwalimu alihimiza jamii na hasa walimu wawafunze watoto kujitegemea kulingana na mazingira wanamotokea (vijijini). Iwe ni mbiu kwa kila Mtanzania kwamba usomi wa kimsingi ni kuwawezesha vijana kupata ufahima wa kuweza kujitegemea katika mazingira wanamotokea na siyo fahari ya kuvivuka vidato vya kiusomi kwa matumaini ya kuajiriwa baadaye.

**Methali**: *Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo* (UK 6:2: SE)

Methali hii ina maanisha kwamba mtoto hufuata jinsi wazazi au walezi wake wanavyomwelekeza kuyatenda mambo hususani yaliyomo katika mpwito wa maisha yake. kwa kawaida mtoto huwa ni mwenye kuwasikiliza wazazi,walezi au walimu wao kwa nia ya kupata dira ya maisha yao. Kwa hivyo, ikiwa walezi hao watakuwa wamemwelekeza vizuri; itakuwa ni heri kwake na kama atakuwa ameelekezwa vibaya itakuwa ni shari katika maisha yake kijamii na kiimani pia. Hii ndiyo kusema kwamba kwa muktadha wa elimu methali hii inamaanisha kwamba, ikiwa mwanafunzi walimu wake hawakumpa elimu ya kumsaidia kujitegemea daima, atakuwa ni tegemezi, asiyejiweza, mwenye kubweteka akisubiri kusaidiwa. Jambo ambalo litakuwa ni muhali kwa wengine kujitoa muhanga kwa ajili ya kuwalea wazembe na wazururaji. Ikiwa walimu waliwapa wanafunzi wao elimu bora; elimu yenye kuwafanya waelimike na waweze kujitegemea, waweze kuishi kwa amani na upendo, kwa hakika wahitimu, hao watakuwa ni wenye faraja katika maisha yao na ya jamii zao kwa ujumla. Kwa hivyo, ni imani kwamba wataweza kupambana na maadui: ujinga, maradhi na umasikini na huku wakiishi maisha ya furaha na amani

### 4.4.14 Maudhui kuhusu Onyo kwa Idd Amin

Haya ni maudhui yanayosawiri uvamizi wa Idd Amin katika ardhi ya Tanzania ambapo alidai kwamba sehemu ya Kagera nchini Tanzania ni sehemu ya Uganda iliyonyang'anywa na Wakoloni wakati walipokuwa wakiligawanya bara la Afrika. Jambo ambalo kwa Watanzania ni uzushi ambao Idd Amin alikuwa akiuendeleza ili kuweza kuyapanua mazingira yake kwa njia ya dhuluma. Ingawa hivyo, Mwalimu Nyerere alifanya jitihada za usuluhishi bila

mafanikio. Idd Amin aliendelea kuulaghai ulimwengu hata ikafikia kuingiza ndege zake za kivita na majeshi ya ardhini kwa ajili ya kuitwaa sehemu hiyo ya Kagera nchini Tanzania. Ndiposa Watanzania walikuwa hawana njia nyingine zaidi ya kujibu mashambulizi kwa minajili ya kuilinda ardhi yao; lakini kudumisha amani na utulivu katika nchi yao. Kwa kumbukizi za Mwalimu Nyerere, vita vikashamiri hususani katika miezi ya Novemba na Desema 1978, TPDF ikawa mstari wa mbele. Idd Amin na majeshi yake wakafukuzwa na sehemu ya Kagera ikarudishwa mikononi mwa Watanzania. 4.4.14.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Onyo kwa Idd Amin

**Takriri**: "*... tunayo kazi moja tu Watanzania sasa ni kumpiga: Uwezo wa kumpiga tunao. Sababu za kumpiga tunazo. Na nia ya kumpiga tanayo.* (UK 3:3: MAV)

Hizi ni kauli zilizokuwa zimenuiwa kuudhihirishia ulimwengu kwamba Watanzania walikuwa na kila sababu zilizowafanya waingie katika mapambano ya vita dhidi ya Idd Amin na majeshi yake. Baada ya kwamba Idd Amin ameyaingiza majeshi yake katika ardhi ya Tanzania sehemu za Kagera kwa nia ya kuifanya sehemu hiyo kuwa himaya ya Uganda. Kimataifa hilo lilikuwa ni kosa kubwa. Kuchukuwa nchi au sehemu ya ardhi ya nchi nyingine kwa makusudi, sio kwamba majeshi yamekosea njia, ni kutangaza vita. Kwa mpwito huo, kwa Watanzania walikuwa wana kila sababu ya kupigana vita dhidi yake (Idd Amin). Ndiposa kwa mbiu ya Amiri jeshi mkuu wa Watanzania, kwa niaba ya Watanzania ikawa ni autangazie ulimwengu kwa kusema: "***… tunayo kazi moja tu Watanzania sasa ni kumpiga: Uwezo wa kumpiga tunao. Sababu za kumpiga tunazo. Na nia ya kumpiga tanayo***" – kauli ambazo ni ithibati ya Watanzania kuhusu kujiamini kwao kwamba wanaingia vitani kwa kuchokozwa; lakini pia wana uwezo wa kuyakabili mapambano na kujiletea ushindi; na kwamba walimwengu hauna budi kutambua kwamba Watanzania watampa kichapo kisichokuwa na simile hadi atakaposhika hatamu. Jambo ambalo lilitekelezeka na ushindi ukawaendea Watanzania. Takriri iliyotumiwa, ililenga kuwasisitiza Watanzania kwamba serikali ilikuwa na azma ya kwenda vitani. Kwa hiyo, yeyote ambaye alikuwa akifikiria kwamba ni mambo ya utani tu anayoyasema Mwalimu, ilikuwa ni azinduke kwamba wakati wowote atatakiwa kuchangia vita hivyo.

**Tafsida kengeushi**: "*Huyu mtu (Idd Amin) ni mshenzi, …*" (UK 3:7: MAV )

Haya yalikuwa ni matamshi ya Mwalimu Nyerere dhidi ya Amin kutokana na matendo yake ya kidhalimu kwa Watanzania na pengine ulimwenguni kote. Kauli hizi ni uashirio wa baada ya kuwa Idd Amin alikuwa ameutangazia ulimwengu kusudio lake la kuivamia Tanzania na

walimwengu wakimstaajabia hasa kwa matendo ya mauwaji aliyokuwa akishutumiwa kwayo Ndiposa alipoivamia Tanzania pakapatikana mashiko kuhusu ulaghai wake

**Maswali ya kibalagha, usimulizi na kinaya**: " *... kuanzia tarehe 24, 25, 26, 27 hadi 28; (Novemba 1978). Alipigwa (Idd Amin), rafiki yangu, na akapiga kelele nyingi sana. Na sisi tukanyamaza, tuseme nini?*" (UK 12:4: OIA)

Kauli hizi za Mwalimu ni uthibitisho kwa walimwengu kwa jinsi ambavyo Watanzania walifikia ukomo wa kumvumilia Idd Amin kwa madhila yake. Ndiyo ikawa Watanzania; ***waseme nini?*** zaidi ya kumpiga. Na ikawa ni wampe kipigo hata ikawa hawezi kufurukuta tena mbele ya Watanzania; zaidi ya kuulilia ulimwengu umsaidie. Hatima yake Tanzania ikajipatia ushindi. Ardhi ya Kagera ikarudishwa katika himaya ya Watanzania. kinaya inajikita katika tamko "rafiki yangu" kwani Idd Amin alikuwa adui wala siyo rafiki. Tunaelezwa kuwa katika muktadha huo wa vitani hapangekuwa na la kusema isipokuwa kumwenzi adui huku akiburuzwa

**Takriri na tafsida kengeushi**: "*Jeuri ya ukoloni ni jeuri ambayo inazidi nyingine yoyote duniani. Ni jeuri ambayo, walionayo jeuri ile wanakataa usawa wa watu wote. Maana huwezi ukaamua kwamba utawatawala watu wengine wakipenda wasipende, bila kukana usawa wa binadamu. Lazima kwanza uukane usawa, useme watu sio sawa na wewe. Watawala hawa wa kikoloni, na watawala wa namna yoyote hii ya kijahili, lazima waseme kwamba wao si watu, ni miungu; na wale wanotawaliwa ndio watu. Na miungu wana wajibu wa kuwatawala watu wakipenda wasipende. Ama wataamua kwamba wao watatawala kwa nguvu* ***wao ndio watu, na wale wanaotawaliwa sio watu, ni wanyama tu"*** (UK1:5/2:1: OIA)

Mwalimu aliwatahadharisha Watanzania watambue kwamba *"**Jeuri ya ukoloni ni jeuri ambayo inazidi nyingine yoyote duniani** -* akimaanisha kwamba, kwa tabia yao ya kuwatawala wengine kinguvu ni kukataa usawa kwa watu wote na kwa kujitukuza kwamba wao ni katika mataifa bora yaliyobarikiwa dhidi ya mataifa mengine kwa rangi zao ulimwenguni. Ndio Mwalimu akatoa ufahima kwamba: ***lazima waseme kwamba wao si watu, ni miungu; na wale wanotawaliwa ndio watu. Na miungu wana wajibu wa kuwatawala watu wakipenda wasipende***; ambapo fauka yake ni hujipa utukufu na kuwadogesha wanadamu wengine wasio weupe kwa rangi kama wao kwa kuwafanya si kitu mbele yao; kwa jeuri kwamba wanaweza kuwatenda lolote wapendalo. Kwa uoni wa Mwalimu, udhalili huo ambao Wazungu wa kikoloni walikuwa wakiwafanyia watu wengine kwa rangi zao kama walivyodhalilishwa Waafrika katika ardhi yao: kwa kufanywa makoloni

yao, kuchukuliwa kwa malighafi zao, kudhalilishwa kinyama na kuchukuliwa utumwa kwa kuyawezesha mashamba na viwanda vyao huko Ulaya, Mwalimu aliiona jeuri hiyo kwamba ni jeuri iliyovuka mipaka na inayostahili kukemewa kwa nguvu zote.

**Istiara na takriri**: "*... Na baada ya kupata uhuru wetu tumetangaza: tumesema nini shabaha yetu tukiwa nchi huru na shabaha zetu tumesema ni mbili: Moja ni kuutumia Uhuru wetu katika jitihada ya kuwaendeleza wananchi; kuvunja yale maovu yaliyofanywa na ukoloni, kujenga heshima ya wananchi wetu, kuleta maendeleo. Na tukasema maana ya maendeleo kwetu ni kila litakalosaidia kuleta heshima ya Mtanzania. Kila kitendo kitakachoweza kumrudishia ubinadamu wake Mwafrika, ubinadamu uliokuwa umevurugwa vurugwa na matope ya ukoloni, sisi tutakiheshimu kukifanya kwamba ni kitendo cha maendeleo. Hiyo ndiyo jitihada yetu ya kwanza. Lakini shabaha yetu ya pili ilikuwa ni kuwasaidia wenzetu nao katika Afrika ambao hawajajikomboa, hawajafikia hatua hii ambayo sisi tumeifikia, na wao wajikomboe".* (UK 3:5 - 4:1: OIA)

Kauli hizi ni uzinduo kwa Watanzania kutambua maana ya maendeleo yaliyokusudiwa mara baada ya uhuru wa Tanganyika. Ilibainika kwamba Wakoloni waliwadharau wazawa Wafrika wa Watanzania wakiwa miongoni mwao; hata ikawa ni sumu kwamba, kila jambo zuri ni la mtu mweupe (Mzungu). Wazungu walikwisha jinasibu kwamba, wao ni katika mataifa yaliyobarikiwa kuwatawala wengine kwa rangi zao na kwamba utukufu ni wao. Waliwaona wengine kwa rangi zao ni katika viumbe duni. Hivyo, ulikuwa ni uamsho wa Mwalimu kwa Watanzania wajitahidi kuifuta sumu hiyo kwa kutambua kwamba, mafanikio kwa maana ya maendeleo kwao ni kuimarisha heshima yao ambayo Mwalimu anasema ***ilivurugwa vurugwa na matope ya Ukoloni***. “Matope ya Ukoloni” ni uhamishaji wa hisia kwamba dharau ya Wakoloni kwa Watanzania ilipelekea kuwachafua wa Watanzania. Kwa hivyo, baada ya kujinasua kutoka katika makucha ya Ukoloni wana kazi ya kujisafia wawe wasafi kwa maana ya kuirudisha heshima yao ***kutenda kila linalosaidia kuleta heshima ya Mtanzania***. Watanzania wakiamini kwamba hayo ndiyo maendeleo wayopaswa kuyapigania kila uchao. Ni azma ya tangu awali mara tu baada ya kujikomboa.

Lakini pia kwa takriri ya ***“kuwakomboa wengine”***; kama ilivyotumika, ni msisitizo kuonyesha uungwana, na utu bora kwa wengine ambao bado walikuwa katika kizimba cha Wakoloni. Kuwasaidia wajikomboe. Hii pia ilikuwa ni shabaha ya Watanzania kwamba, Afrika hususan nchi jirani zote nazo ziwe huru. Hivyo ilikuwa ni wajitoe muhanga kuwasaidia wale ambao bado walikuwa katika minyororo ya Wakoloni kama vile Msumbiji

na Afrika Kusini. Kutokana na  azma hiyo, waliwapa wapigania ukombozi wa nchi hizo hifadhi na mafunzo mahsusi ili waweze kutulia na kijiwekea mipango imara kuhusu kuzikomboa nchi zao. Kwa jitihada hizo nchi hizo nazo ziliweza kujikomboa.

**Maswali ya kibalagha, tashbiha, tafsida kengeushi, uzungumzi nafsi na takriri**: *"Namsema huyu Amin hivyo kwa sababu amewahi kuwaonea Wahindi pale; na amewahi kuwadhalilisha Wazungu wawili watatu pale, basi amejipatia heshima kubwa. Lakini hakumwua Mhindi. Mnamjua Mhindi aliyemua? Safari moja alimpiga Mwingereza mmoja pale anaitwa Denis Hill akatishwa kweli kweli! Alitishwa sana pale alipojaribu kumpiga Mwingereza Denis Hill, kwamba anaweza akaamwua. Kwa hiyo wale walio na haki ya kutetewa walitetewa. Lakini Waafrika wamechinjwa wengi sana; hakuna hata sauti! Kimya kabisa, kama anaua mbuzi". Nasema, mimi sina sababu ya kumpenda mshenzi huyu hata kidogo. Nitampenda kwa sababu ya rangi tu? Ni mwuaji tu; kwa hiyo mtu huyu simpendi mimi tangu zamani. Lakini pamoja na kutokumpenda, nawaambieni Watanzania, sijajaribu kumng'oa hata mara moja"* (UK 7:4 - 8:1: OIA).

Kauli hizi ni utanabahisho kwa Watanzania watambue kwamba vitendo vya Idd Amin; aliyekuwa rais wa Uganda; havikuwa na tofauti na vile vya Wakoloni. Kauli kwamba "***mnamjua Mhindi aliyemuua?" "Safari moja alimpiga Mwingereza mmoja pale anaitwa Denis Hill akatishwa kweli kweli!"*** "***Lakini Waafrika wamechinjwa wengi sana; hakuna hata sauti! Kimya kabisa, kama anaua mbuzi"*** Hizi zilikuwa ni tafakuri na uamsho kwa Watanzania kuhusu kujihadhari na tabia za kikoloni. Idd Amin, mbali na uafrika wake alijivyaza tabia za Wazungu kwa kuwabagua Wahidi na Waingereza waliokuwa katika himaya yake nchini Uganda. Ingawa hivyo, Mwalimu aliwataka Watanzania wajiepushe na ubaguzi wajihadhari na wale wote wenye silka hiyo ya kuwabagua wengine. Alibaini kwamba, Idd Amin alipokuwa akiwabagua Wahindi na Waingereza, Waingereza waliwatetea wenzao lakini Wafrika walipokuwa wanauliwa hapakutokea utetezi wa aina yeyote. Ulimwengu wa Ulaya ulizizima kwa ukimya ya kana kwamba ilikuwa ni furaha ya Wakoloni dhidi ya Mwafrika anayeuliwa.

Hivyo, ilikuwa ni wito kwa Watanzania na pengine Wafrika kwa ujumla wajitambue na wawe makini na wale wote wanaowabagua wengine kwa rangi zao. Ndiposa Mwalimu akisema: ***"… mimi sina sababu ya kumpenda mshenzi huyu hata kidogo (Idd Amin). Nitampenda kwa sababu ya rangi tu? Ni mwuaji tu"*** akimaanisha kwamba Idd Amin alikuwa ni mbaguzi. Mbali na Uafrika wake aliendeleza tabia za kibaguzi zilizokuwa

zikitendwa na Wakoloni hususani Afrika Kusini. Ndio ikawa Mwalimu kasema, ingawa ni Mwafrika, maadamu madhambi anayoyatenda ni yaleyale Uafrika wake hautakuwa sababu ya kumfumbia macho. Watanzania, Wafrika na pengine jamii pana ya ulimwengu wanapaswa wamuelewe kwamba alikuwa ni mkosaji sawa na walivyokuwa Wakoloni kwa ubaguzi wao dhidi ya Waafrika.

### 4.4.15 Maudhui kuhusu Demokrasia

Ili wananchi wawe huru katika taifa huru, basi demokrasia ni kitu cha lazima kabisa. Lazima ziweko taratibu ambazo raia wanaweza kuzitumia kuwapatia kauli juu ya mambo yao ya mahali walipo na ya kitaifa, na hatimaye kuweza kuyaongoza. Yaani wananchi hawanabudi wajiwekee taratibu zitakazowawezesha kujitawala. Taratibu za kidemokrasia zinapokuwepo ndipo amani na utulivu vinakuwapo nchini. Amani ikiwepo nchini ndipo inapowezekana kupatikana maendeleo ya wananchi. Taratibu za kidemokrasia katika nchi yoyote ambayo inaendeshwa kwa ridhaa ya watu wake hutegemea utamaduni wa nchi hiyo, jiografia yake na historia yake, na hata kiwango cha maendeleo ya nchi hiyo na ya watu wenyewe. Kama nchi ni kubwa sana na yenye mchanganyiko wa watu wa aina mbalimbali, basi vyombo na taratibu zake za kidemokrasia vinaweza vikawa tofauti na vile vya nchi ambayo ni ndogo, na ambamo raia wote ni wa utamaduni wa aina moja. Nchi ambayo mawasiliano yake ni hafifu na watu wake hawajui kusoma wala kuandika huwa na taratibu za wananchi kutoa maoni yao na kufanya uchaguzi wao ambao ni tofauti na zile za watu wanaojua kusoma na kuandika, na wenye mawasiliano mazuri. Kwa hiyo utaratibu wa kidemokrasia uliobora kwa nchi yoyote, yaani utaratibu utakaofaa kwa nchi hiyo, utatofautiana wakati wowote kati ya nchi moja na nchi nyingine; lakini pia kipindi baada ya kingine.

Kwa Watanzania demokrasia ina upambanuzi wake kihistoria. Demokrasia iliwafunza Watanzania busara ya kisiasa tangu enzi za umajumui. Kumbukizi za Mwalimu kwa Watanzania ni kwamba, kabla ya CCM kuzaliwa mwaka 1977, Tanzania ilikuwa ikikabiliana na demokrasia ya mfumo wa vyama vingi. Ulifanyika uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1960 na 1962 kwa Tanzania Bara; ambapo karibu wapiga kura wote walikiridhia chama cha TANU lakini jimbo moja likawa limemchagua mgombea wa upinzani. Inakumbukwa pia kwamba kwa upande wa Zanzibar kulifanyika mapinduzi ya umma mwaka mmoja baadaye na kusababisha mapinduzi kutokana na upendeleo wa makusudi wa Wakoloni kukipendelea chama cha Sultani wakati wa uchaguzi wa mwaka 1963. Kwa muda wa miaka 12 Tanzania iliendelea kuwa na vyama viwili, kila kimoja kikiongoza katika sehemu yake ya Muungano. Na ndipo mwaka 1977 vyama vya TANU na ASP viliamua kungana na kuuda CCM. Kwa

hivyo, utaratibu wa chama kimoja ukaendelea chini ya uongozi wa CCM. Ingawa hivyo, kwa kuzisoma alama za nyakati na kwa uzoefu wa demokrasia, Watanzania walikubali tena kuingia katika mfumo wa vyama vingi huku wakiutambulisha ulimwengu sababu za msingi kama zifuatazo:

Kwanza, Watanzania walionekana wana elimu zaidi, Wanatambua zaidi uwezekano wa mabadiliko katika maisha yao na wanajiamini zaidi kwamba hawalazimiki kukubali dhuluma zilizokuwa zikitokea katika nchi ambamo taratibu zake kwa msingi ni za haki. Watanzania walitambua; si kweli kwamba umasikini, au maradhi, au hali mbaya ya maisha ni 'amri ya Mungu tu!' au 'bahati mbaya'. Zaidi ya hayo Watanzania waliowengi wamezaliwa katika Tanzania huru, huku wakiwa na matarajio mazuri zaidi - tofauti na jana yake.

Pili, kwa muda mrefu Watanzania walikuwa wakikabiliana na matatizo makubwa ya uchumi ambayo hayakupata kutokea katika miaka ya nyuma (miaka kati ya 60 na 70). Ambapo leo yake Tanzania ilionekana ina rasilimali nyingi zaidi - za maendeleo ya jamii na uchumi kuliko ilivyokuwa wakati wa uhuru. Lakini kwa sababu ya matatizo ya uchumi rasilimali hizo zikawa / zingali zinaonekana katika hali mbaya zaidi kuliko zilivyokuwa mwishoni mwa miaka ya sabini. Barabara nyingi zilionekana kuharibika; reli na miundo mbinu mingine ilionekana haikidhi mahitaji ya wananchi ambao ni wengi zaidi na wenye shughuli nyingi zaidi; shule nyingi zilikuwa na upungufu wa vitabu na vifaa vingine vya umuhimu; wakati ambapo hospitali na zahanati nyingi zilionekana zingali zina upungufu wa dawa na wahudumu wa afya.

Tatu, rushwa ilikithiri kiasi cha kuwatia hofu wananchi masikini na waliowaaminifu. Ikiaminiwa kwamba kabla ya mwaka 1978, rushwa ilikuwa kidogo sana Tanzania na kwamba hali hii ilibadilika kutokana na upungufu wa bidhaa muhimu hasa baada ya kuvunjika kwa Jumuia ya Afrika Mashariki na vita dhidi ya Idd Amin, vilivyofuatiwa mara moja na kupanda mara tatu kwa bei za mafuta na kuanguka kwa bei za mazao ya biashara (nchini Tanzania) - mwanzoni mwa miaka ya themanini; na kwa hivyo rushwa likawa ni tatizo lililoshika kasi hadi hivi leo nchini Tanzania.

Nne, Tanzania ilionekana haina budi kuingia katika mfumo wa vyama vingi kwa mashiko kwamba: Tanzania imo katika dunia; haiwezi kuepuka athari za matukio ya dunia. ilishuhudia athari zake ambapo kwa miaka kumi kabla ya 1992 taifa lilikumbwa na umasikini mkubwa kutokana na athari za mataifa mengine ulimwenguni. Hivyo, ilionekana kuwafungia

Watanzania katika mwavuli wa Kiutanzania – ulionekana muda wake umepita na Watanzania wangeurarua mwavuli huo ili waweze kupata utangamano zaidi kimataifa.

#### 4.4.15.1 Mitindo iliyotumika katika Maudhui ya Demokrasia

**Tashbiha**: "***Demokrasia si bidhaa kama Coca Cola …***" (UK 2:3 TM)

Hizi ni kauli zinazowazindua Watanzania. Mwalimu aliwataka Watanzania watambue kwamba demokrasia siyo kinywaji cha "***Coca Cola***" bali ni taratibu ambazo raia wanaweza kuzitumia kuwapatia kauli kuhusu mambo yao ya mahala walipo na ya kitaifa, na hatimaye kuweza kujiongoza. Yaani kujiwekea taratibu zitakazowawezesha kujitawala. Na zinapokuwa zinatekelezwa vyema ndiposa amani na utulivu unapoweza kuwepo nchini. Na amani ikiwepo nchini ndipo maendeleo yanapoweza kupatikana kwa haraka. Na hii ndiyo kusema, jitihada za Watanzania za kupigania uhuru, azma yao ilikuwa ni uhuru wa kujiamulia mambo yao wenywe. Ili kuyafikia malengo hayo, waliifanya demokrasia kama nyezo muhimu na mtawalia wafikra zao kila uchao, chini ya mfumo wa ujamaa na kujitegemea, chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere waliweza kudumisha umoja na amani kijamii na kitaifa.

**Maswali ya kialagha**: "*… (nchi zilizotupiga vita) zinawezaje leo kuwa walimu wa mfano wa demokrasia ya kweli? … hawa ngoji kwanza angalau mpaka sisi tukafa ndipo wakaanza kujizuzua kwa unafiki huu wa wazi wazi*?" (UK 6:1: TM)

Hizi zilikuwa ni kauli zilizonuiwa kuzikonga nyoyo za Wakoloni waliowahi kuzivamia nchi za kiafrika. Waafrika waliteswa, walinyanyaswa katika ardhi yao hata ikawa ni waingie katika mapambano kwa minajili ya kudai uhuru; na wakawa huru. Ingawa hivyo, leo yake inakuwa ni mshangao kuwaona Wamagharibi (wakoloni hao) wakijinadi kwa urahimu hususani katika kuielekeza demokrasia ya mfumo wa vyama vingi kwa nchi za kiafrika huku wakijinafiki kwa kuisahau kale yao kwa madhila waliyowafanyia Waafrika - kwa kuwapiga na kuwatupa gerezani kwa sababu eti wametenda dhambi ya kudai uhuru wa kujitawala katika ardhi yao. Kwa tathmini ya Mwalimu Nyerere aliiona dhana iliyokuwa ikiendelezwa ni uzandiki; aliwataka Watanzania kutambua kwamba maelekezi hayo kuhusu ***demokasia ya kweli*** ni kiini macho kwa Waafrika. Waafrika hawana budi kutambua kwamba si chochote si lolote cha wema ambao wamagharibi wanaowatakia zaidi ya kupenyeza matakwa yao na kwa hivyo kuendeleza ukoloni mambo leo. Na kwa mkongo wa moyo wake ndiposa aliwauliza tena Watanzania: "… ***hawa ngoji kwanza angalau mpaka sisi tukafa ndipo wakaanza kujizuzua kwa unafiki huu wa wazi wazi*?"** Kumaanisha kwamba waliojitoa muhanga katika mapambano ya kudai uhuru, kumbukumbu zingali zinawatagaa vichwani mwao. Wana hisi machungu wanapowaona wamagharibi (wakoloni) wanajitokeza kwa ngozi ya urahimu

wakati ambapo hitoria kuhusu madhila ya uvamizi wao yangali yanazikonga nyoyo za waafrika kila uchao. Pengine wasinge kuwa hai ujanja wao usinge tambulika kwa haraka. Ingawa pia ni muhali kufutika kwa historia. Hivyo, ulikuwa ni wito watambue kwamba madhila waliyowafanyia waafrika kamwe hayata sahaulika bali yatakuwa historia ya milele.

**Msemo**: "*Kuongoza ni kuonyesha njia. Lakini vigumu kuonyesha njia gizani.*"(UK 14:2: TM)

Haya yalikuwa ni maono ya Mwalimu Nyerere katika kuiasa CCM kwamba haina budi kuimarisha itikadi yake ya siasa ya ujamaa na kujitegemea hasa katika mvuvumko wa mfumo wa vyama vingi ambapo wanachama huweza kushawishiwa na wakashawishika kwa sera za chama kingine na wakaamua kukihamia. Kwa hivyo, Mwalimu alikuwa akikionya chama CCM kisiwang'ang'anie wanachama wa namna hiyo - hata ikawa ni wabakie kwa ajili ya kuogopa lawama. Mwalimu aliamini kwamba, kufanya hivyo, utakuwa ni unafiki na kwamba chama hakitakuwa chama cha uongozi maana kitakuwa kina watu tu lakini hakuna msimamo wala itikadi thabiti

**Uchimuzi**: *CCM isiyo na itikadi au msimamo unaoeleweka itakuwa ni kama GULIO tu, au SOKO HURU, ... NANI ANATAKA CCM YA NAMNA HIYO?* (UK 15:1: TM)

Hizi ni kauli zilizokuwa zimenuiwa kuwatahadharisha wana CCM ya kwamba wasikubali kuburuzwa na mabadiliko ya mfumo wa vyama vingi ulimwenguni; na badala yake watafakari na wajipange jinsi ya kuingia katika mabadiliko hayo; chama kiwe na msimamo kuhusu itikadi yake na wanachama wawe ni halali na wasio wanafiki.

**Uchimuzi**: *Nawasihi, basi: TUSING'ANG'ANIE UMOJA WA BANDIA; TUSIWAONE WATU WATAKAOHAMA CCM KUWA NI WASALITI; WALATUSIONE VYAMA VYA SIASA KUWA NI VYAMA VYA UHASAMA.* (UK 16: 3: TM)

Hizi ni kauli zilizoashiria kusisitiza CCM iimarishe itikadi yake ndani ya mfumo wa vyama vingi; ambapo: "TUSING'ANG'ANIE UMOJA WA BANDIA; TUSIWAONE WATU WATAKAOHAMA CCM KUWA NI WASALITI" yalikuwa ni maonyo yake Mwalimu kwa wana CCM kwamba kama kuna wana CCM wanaotaka kukihama chama, wasilazimishwe kubakia wanachama wa CCM, ili kuepuka unafiki na lawama ndani ya chama kwa khofia kukifanya chama kuwa na umoja wa bandia (umoja wa kuhofiana). Matokeo yake ni kwamba chama kitavurugika zaidi kutokana na kukosa msimamo thabiti kuhusu itikadi yake.

Kauli "WALA TUSIONE VYAMA VYA SIASA KUWA NI VYAMA VYA UHASAMA". Hii ulikuwa ni wito wa Mwalimu kwa viongozi wa CCM kwamba waondoe tashwishwi kuhusu mfumo wa vyama vingi. Wasione ni tatizo; bali watambue kwamba demokrasia ya mfumo wa vyama vingi ni kuonyeshana njia Kuhitilafiana bila ya kudharauliana, kujadiliana bila ya kugombana, kuwa na maoni tofauti bila kuwa maadui, wachache kukubali maoni ya wengi, na wengi kuheshimu maoni ya wachache.

**Usimulizi**: *Kwa muda wa miaka kumi na miwili, tulikuwa nchi ya chama kimoja, lakini yenye vyama viwili. Februari 5, 1977, tulisahihisha kasoro hiyo: chama cha mapinduzi kikazaliwa. Tukio hilo lilikuwa tukio muhimu sana kwa maendeleo ya Tanzania. Lilipunguza nafasi ya chokochoko juu ya uhuru na umoja wa taifa letu; umoja ukaimarika zaidi katika Tanzania, na kwa kufanya hivyo wanyonge wa Afrika wakawa wamepunguzwa kidogo*. (UK 1: 3: KK2)

Hizi zilikuwa ni kumbukizi zilizompelekea Mwalimu kuwashawishi Watanzania kutambua umuhimu wa kuendeleza mafanikio yao; waliyoyapata kupitia maongozi mema ya utekelezwaji wa Azimio la Arusha kwa zaidi ya miaka ishirini na miaka kumi ya CCM hasa katika kupambana na maadui wa "***umoja***" na "***amani***".

**Istiara**: *Wakati maadui wa umoja wetu walipo jaribu kutuvuruga, Chama Cha Mapinduzi kiliweza kwa haraka na kwa umoja kusafisha hali ya hewa ya kisiasa iliyokuwa imechafuliwa.* (UK 1:4: KK2)

Huu ni uhamishaji wa maana na hisi; ambapo hali ya siasa inafananishwa na kitu kichafu na kusafishwa ambako kunatokana na jitihada za umoja zilizowezesha hali hiyo ya kisiasa kuwa safi. Na kwa hivyo ulikuwa ni uamsho kwa Watanzania wadumishe umoja wao na daima wawe makini katika kukilinda chama chao; na wawe wazalendo wa taifa lao kwa hali na mali

**Tashhisi**: "*... hapa katikati Chama Cha Mapinduzi kimesinzia. Tumeiacha sifa yetu ya umoja ikatulevya kidogo na kutufanya wazembe.* (UK 2:2: KK2)

Dhana ya '***Chama***' kupewa sifa ya kusinzia kama mwanadamu na 'Umoja' kupewa sifa ya kilevi; ni tashhisi iliyokusudiwa kuwazindua wanachama wa CCM kwa kuwaonyesha mghafala waliowagubika hata ikawa ni wasahau majukumu yao ya kukilinda chama chao CCM. Chama kimeonekana kupoteza mwelekeo wa kuiongoza nchi; kwa maana ya kutokuwepo kwa malengo yenye dira ya kuifanya serikali iyatekeleze. Viongozi hawakujua wananchi wanafikiria nini, hawakujua mambo yaliyokuwa yanawasumbua wanachama na kwa hivyo demokrasia ilitupiliwa mbali (ikawa imedhoofika) ikawa hakuna namna ya

kurekebishana. Kwa hiyo ushawishi wa Mwalimu kwa mwegemo huo ilikuwa ni wanachama watanabahi kwamba ili kukifanya chama kiwe hai, kuwe na vikao vya mara kwa mara na wanachama wao. Viongozi wahakikishe wana utangamano mzuri na wanachama na wakubali kukosolewa na wajirekebishe pale palipoonekana kuna walakini. Zifanyike jitihada za kuwafanya wanachama kuwa hai kwa maana ya kujituma hasa katika kutoa michango ya chama lakini pia wenye ari na moyo thabiti katika kukilinda na kukidumisha chama chao.

#### 4.4.16 Maudhui kuhusu Kupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha

Ulikuwa ni mtazamo wa Mwalimu Nyerere kwamba baadhi ya viongozi na wananchi wa Tanzania walizikiuka mbeko za Azimio la Arusha kwa matashi binafsi. Matarajio yalikuwa ni kuwaona wananchi wakizingatia misingi ya ujamaa na kujitegemea; viongozi na wananchi wakishirikiana kwa pamoja katika kuanzisha na kuendeleza shughuli za uzalishaji mali. Lakini kinyume chake ikawa ni Azimio la Arusha kuonekana kwamba limepitwa na wakati; na ikawa ni yafanyike mabadiliko ya kuanzishwa kwa Azimio la Zanzibar kwa imani kwamba kufanya hivyo ni kuyaharakia maendeleo ya uchumi wa nchi.

Kwa Mwalimu Nyerere mapendekezo yaliyofanywa katika Azimio la Zanzibar dhidi ya Azimio la Arusha, aliyaona kama kiinimacho kwa Watanzania walio masikini; na ambao ndio waliowengi; kuendelea kunyonywa na matajiri wachache. Kwa sintofahamu hiyo, ghera ya Mwalimu ilikuwa ni kuwajuza Watanzania wawe na ufahima kuhusu Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ili kuonyesha makataa yao kwa mabepari wanaotaka kuwafanyia hiyana ya kuzitwaa amali za nchi yao. Kwa mtazamo huo, Mwalimu alisimama kidete kwa mbiu ya kuwataka viongozi wa chama CCM waifasiri misingi ya Azimio la Arusha katika uhalisia wa maisha ya Mtanzania. Aliwataka watambue kwamba Ujamaa ni kuifanya nchi iwe ya wafanyakazi: Isiwe na ubepari wala ukabaila. Isiwe na tabaka mbili za watu: tabaka la chini la watu wanaoishi kwa kufanya kazi, na tabaka la juu la watu wanaoishi kwa kufanyiwa kazi.

Wakadhalka aliwataka Watanzania waelewe kwamba: katika nchi ya Ujamaa kamili, mtu hamnyonyi mtu mwingine, bali kila awezaye kufanya kazi hufanya kazi, na kila mfanyakazi hupata pato la haki kwa kazi aifanyayo na wala mapato ya wafanyakazi mbalimbali hayapitani mno. Katika nchi ya Ujamaa kamili watu peke yao ambao huishi kwa jasho la wenzao, na ni haki yao kuishi kwa jasho la wenzao, ni watoto wadogo, wazee wasiojiweza, vilema na wale ambao, kwa muda, Jumuia imeshindwa kuwapatia kazi yoyote ya kujipatia riziki kwa nguvu zao wenyewe.

Vivyo hivyo, njia kuu za uchumi ni lazima ziwe chini ya Wakulima na Wafanyakazi ambazo kwazo ndiyo namna ya pekee ya kujenga na kudumisha ujamaa. Kuthibitisha kuwa njia kuu zote za uchumi wa nchi zinatawaliwa na kumilikiwa na Wakulima na Wafanyakazi wenyewe kwa kutumia vyombo vya serikali yao na vyama vyao vya ushirika. Pia ni lazima kuthibitisha kuwa chama kinachotawala ni chama cha Wakulima na Wafanyakazi. Njia kuu za Uchumi zikiwa ni kama vile ardhi, misitu, madini, maji, mafuta na nguvu za umeme, njia za habari, njia za usafirishaji, mabenki, na bima; biashara na nchi za kigeni na biashara za jumla; viwanda vya chuma, mashini, silaha, magari, simenti, mbolea; nguo, na kiwanda chochote kikubwa ambacho kinategemewa na sehemu kubwa ya watu katika kupata riziki zao au kinachotegemewa na viwanda vingine; mashamba makubwa na hasa yale yanayotoa mazao ya lazima katika viwanda vikubwa.

Lakini pia aliwataka Watanzania watambue kwamba swala la Demokrasi katika nchi ya Ujamaa hupewa nafasi kubwa kwa sababu njia zake kuu zote za uchumi hutawaliwa na humilikiwa na Serikali. Kwa mnasaba kwamba, sharti Serikali iwe inachaguliwa na kuongozwa na Wakulima na Wafanyakazi wenyewe.

Mwalimu aliwataka Watanzania kumakinika kwamba ingawa ujamaa ni imani lakini Ujamaa hauwezi kujijenga wenyewe. Hauna budi kujengwa na watu wanaoamini na kufuata kanuni zake. Mwanachama wa kweli ni mjamaa, na wajamaa wenzie, yaani waumini wenzie katika imani hii ya kisiasa na uchumi ni wale wanaopigania haki za Wakulima na Wafanyakazi nchini, katika Afrika na popote duniani.

Wajibu wa kwanza wa mwanachama na hasa kiongozi wa chama, ni kutii kanuni hizi za ujamaa hasa katika maisha yake mwenyewe na hasa mwanachama kiongozi hataishi kwa jasho la mtu mwingine au kufanya jambo lolote ambalo ni la kibepari au kikabaila. Utimizaji wa shabaha hizo na nyinginezo zinazofuatana na siasa ya ujamaa unategemea sana viongozi kwa sababu ujamaa ni imani na ni vigumu kwa viongozi kujenga siasa ya ujamaa ikiwa hawaikubali imani hiyo. Ama katika siasa ya kujitegemea, Watanzania iliwapasa kuelewa kwamba Chama lazima kiliongoze Taifa katika mapambano ya kuwakomboa wanyonge; katika kuondokana na dhiki na kuwa katika hali ya neema. Hii ni kutokana na taswira ya tangu kujipatia uhuru ambapo Watanzania walijihisi wangali wanaonewa, wananyonywa na kupuuzwa na mataifa ya kimagharibi yenye nguvu kiviwanda na kwa hivyo yakitumia fedha kama msingi wa maendeleo. Kwa hivyo Watanzania walitakiwa watambue kwamba ili kuyazuia madhila hayo kwa vitendo, kila mtu inampasa afanye kazi kwa juhudi na maarifa.

Lakini pia Watanzania walitakiwa watambue kwamba fedha sio silaha faafu ya kupewa ukipaumbele katika mapambano ya maendeleo hasa kwa nchi masikini kama ilivyokuwa Tanzania. Haya yalijiri kutokana na usawiri uliobaini kwamba Watanzania wengi waliingiwa na mghafala wa kuamini kwamba ‘Fedha ndiyo msingi wa maendeleo. Bila fedha hakuna maendeleo’! Kwa mtazamo huo, njia za upatikanaji wa fedha zilifafanuliwa ili iwe ni natija kwa Watanzania kuamua ikiwa watazingatia "fedha" au "kujitegemea" katika kujiletea maendeleo:

Kwanza, ni 'kodi' ambayo serikali hulazimika kuwatoza raia kulingana na jinsi mahitaji ya maendeleo yanavyozidi kuongezeka ambapo daima wanachi huhisi kuathirika hasa inapokuwa kunakuwa na ongezeko la kodi kila mara.

Pili, ni fedha kutoka nje ya nchi ambazo nazo ni za aina tatu: ***Zawadi*** - yaani serikali ya nje iipe serikali nyingine iliyo masikini fedha za bure tu kama sadaka kwa ajili ya mpango fulani wa maendeleo. Wakati mwingine shirika lolote la nje liipe serikali hiyo au shirika jingine katika nchi hiyo msaada fulani kwa ajili ya maendeleo. ***Mkopo*** - ni pale ambapo serikali ya nje au Sirika la nje, kama vile Benki, hukopesha serikali nyingine fedha fulani kwa ajili ya kazi za maendeleo. Mkopo huu huwa una masharti yake ya kulipa, kama vile muda wa kulipa, na kima cha faida. ***Raslimali ya kibiashara*** - hii ni kubwa kuliko ile ya kwanza, ni ile ya fedha za watu au makampuni yanapokwenda katika nchi fulani kuanzisha shughuli mbalimbali za uchumi kwa manufaa yao wenyewe. Ni sharti kubwa kwa shughuli yenyewe; iwe ni ya faida kwao na kwamba serikali iwaruhusu kuondoa faida hiyo na kuipeleka kwao. Mbali na ufafanuzi huo, Mwalimu Nyerere aliwatahadharisha Watanzania wasitegemee misaada au mikopo kwa ufahima kwamba si jambo rahisi kupata nchi yenye utayari wa kuisaidia nchi nyingine kuitimizia mahitaji yake yote ya maendeleo hasa ikisadikiwa kwamba nchi zenye dhiki duniani ni nyingi. Badala yake aliwataka waelewe na kuamini kwamba: Watu; Ardhi; Siasa safi na Uongozi bora ndiyo njia pekee ya kujiletea maendeleo yaliyo bora na kwa haraka. Kuanzia ngazi ya familia hadi kitaifa. Kwa ufahima kwamba:

**Watu:** Hawanabudi kuifanya siasa ya ujamaa na kujitegemea iwatagae katika nyoyo zao**.** Walitafsiri Azimio la Arusha katika utendaji wa maisha ya kila siku. Uwajibikaji uwe ni kitu cha kujivunia na uvivu, ulevi na uzururaji viwe ni jambo la aibu kwa kila mwananchi. Nchi iweze kupigana na madui: ujinga, maradhi na umasikini. Kwa upande wa ulinzi wa taifa, wananchi wawe macho na vibaraka waliomo nchini ambao wanaweza kutumiwa na maadui

wa nje wenye nia mbaya ya kuliangamiza Taifa; na wawe tayari kulilinda Taifa lao pale inapolazimika kufanya hivyo.

**Ardhi:** Watanzania watambue kwamba uchumi wao unategemea kilimo kwa asilimia kubwa. Kwa hivyo, ardhi nzuri waliyonayo, ikitumika vizuri, wanaweza kuyaendesha maisha yao barabara bila ya kutegemea misaada kutoka nje. Kwa hivyo ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu wa kuwataka Watanzania wote waitumie ardhi kama raslimali yao kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao wenyewe. Ardhi itumiwe kwa faida ya taifa zima na wala isitumiwe kwa faida ya mtu binafsi au kwa watu wachache tu. Uwe ni wajibu wa kila mtu kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula na biashara uwe ni wajibu wa serikali na mashirika mbalimbali kuwapatia wananchi zana za kilimo na wataalamu ili kuwawezesha kuzalisha mazao bora na kwa wingi zaidi ikiwezekana.

**Siasa Safi:** Wakadhalka, Mwalimu aliwahimiza Watanzania ya kwamba msingi wa siasa ya kujitegemea lazima uambatane na siasa ya Ujamaa. Ili kuzuia unyonyaji ni lazima kila mtu afanye kazi na aishi kwa jasho lake yeye mwenyewe. Na ili kuleta usawa wa kugawana mapato ya nchi ni lazima kila mtu atimize wajibu wake kwa kufanya kazi kwa bidii zake zote. Ili kudumisha uhuru wa nchi na raia wake; hapana budi kujitegemea kuanzia familia hadi ngazi ya taifa.

**Uongozi Bora:** Ilikuwa ni miongoni mwa mikakati ya Mwalimu kwamba, ikiwa chama kitatambua wajibu wake ambao ni pamoja na kuwafunza viongozi wake dhima ya uongozi kwa ngazi zote za kijamii; nchi itakuwa na mvuvumko wa maendeleo takribani kwa kila nyanja ya maisha na siasa ya ujamaa na kujitegemea itakuwa ndiyo ngao ya jamii ya Watanzania.

Fauka ya mafanikio yaliyokwisha anza kupatikana kutokana na ufahima wa wananchi kuhusu njia kuu tano za maendeleo, baadhi ya Watanzania waliliona Azimio la Arusha ya kwamba halina maana na lina madhara kwa maendeleo ya Taifa lao. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilionekana ni mgogoro kwa chama na kipingamizi kwa maendeleo ya nchi. Wengine walidhani kwamba CCM inalionea haya Azimio la Arusha ilhali tafsiri na utekelezaji wake umepitwa na wakati. Kwa uoni huo, viongozi wa chama na serikali waliyaunganisha mawazo chini ya Azimio la Zanzibar ili kupata suluhu na mwelekeo wa chama kwa siku za usoni. Mwalimu Nyerere aliliona jambo hilo ni kuwasaliti Watanzania waliowengi kutokana na kwamba Azimio la Arusha lilikuwa lingali na misingi faafu iliyopaswa kuendelezwa na kudumishwa kwa vizazi vilivyopo na pengine vijavyo. Hasa kwa ukubalifu wa sera ya

kuyabinafsisha mashirika ya umma; kwa Mwalimu swala hilo lilimkonga moyoni kiasi cha kusawirika uendelevu wa maumivu hadi mauko yake.

#### 4.4.16.1 Mitindo katika Maudhui ya Kupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha

**Maswali ya kibalagha**: *Misingi yote tisa ni ya namna hiyo. Nani anataka kuibadili misingi hiyo? Wanaweza kuwa wako watu wachache wanaotaka hivyo lakini si umma wa wakulima na wafanyakazi wa Tanzania*, (UK 5: 5: KK2)

Kauli "***Nani anataka kuibadili misingi hiyo?"*** ni udhihirisho wa tashwishi ya Mwalimu kuhusu mabadiliko ya misingi ya Azimio la Arusha, ambapo Mwalimu aliyaona ni uhaini wa kuzighilibu haki za waliowengi. Kauli **"*lakini si umma wa wakulima na wafanyakazi wa Tanzania*"**. Ni uthibati wa kwamba hiyo ndiyo misingi ambayo umma huo wa wakulima na wafanyakazi wanaiona kwamba ndiyo mwokozi wa pilika za maisha yao ya kila siku. Na kwa hivyo, ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania watambue kwamba, misingi ya Azimio la Arusha ni ahueni kwa wakulima na wafanyakazi na kwa hivyo, wanaithamini zaidi ya mifumo mingine. Hivyo basi, aliwaonya wale wote wanaotaka kuibadili misingi hiyo. Na aliwataka Watanzania wazinduke, vinginevyo watambue kwamba, siasa ya ujamaa na kujitegemea itatoweka na badala yake ubepari utaota mizizi na ndiyo iwe mwenye nacho (ambao ni watu wachache sana katika nchi ya Tanzania) kuwaburuza wale wasio nacho katika utekelezaji wa majukumu ya kuwafanya waendeleze utajirisho wao. Hivyo, ulikuwa ni wito wa Mwalimu kwa Watanzania ya kwamba wangeendeleza Azimio la Arusha kwa kulilinda na maadui wa ndani na nje Tanzania ingeendelea kuimarisha matunda ya umoja na amani kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

**Takriri na tashbiha**: "*... wapo watu ambao wanapata riziki yao kwa kufanya kazi na wengine wanapata riziki yao kwa kufanyiwa kazi. Na sema nchi ya namna hiyo huitwa nchi ya kibepari. Nchi inakubali wengine wafanye kazi na kupata riziki yao kama inavyosema misahafu. Wengine wanafanyakazi kwa kunyonya kama watoto wadogo kama vile vilema na vizee…. Nasema nchi ya namna hiyo inaitwa ni nchi ya kibepari*" (UK 12:2: TTT)

Kauli hizi ni udhihirisho wa msongo wa mawazo ya Mwalimu Nyerere kuhusiana na kutelekezwa kwa Azimio la Arusha mara baada ya kung'atuka kwake. Azimio ambalo kulingana naimani yake lilikuwa lingali na misingi imara iliyofaa kuendelezwa na awamu zote za vizazi vya Watanzania. Azimio lilikuwa linasawiri uhalisia wa mazingira ya Watanzania; ambao ni Wakulima na Wafanyakazi. kwa hivyo, shime ya ushawishi wake kwa Watanzania ilikuwa ni watambue kwamba kuchakachuliwa kwa Azimio la Arushwa

kutawagharimu. Walala hoi ambao ndio wengi katika nchi ya Tanzania wataendelea kuwa hoi kutokana na kukosa siasa safi na uongozi bora. Katika matamko haya kuna takriri ya vishazi huru na vishazi tegemezi na pia takriri ya sentensi. Vivyo hivyo kuna takriri neno. Tamko "***wanapata riziki yao***" ni kishazi kilichokaririwa mara mbili huku "***kwa kufanya kazi***" kikiwa kishazi tegemezi kilichorudiwarudiwa pia. Aidha sentensi "***nchi ya namna hiyo inaitwa nchi ya kibepari***" imerudiwarudiwa mara mbili, huku neno "***nasema***" likirudiwarudiwa mara mbili pia. Uradidi huo umekusudiwa kusisitiza kwamba hali ya kusubiri ufanyiwe kazi haipendezi na hutokana na fikra za kibepari za kuwanyonya watu wengine

**Maswali ya kibalagha**: *... lazima awe ni kiongozi wa wakulima na wafanya kazi; wanataka kulibadili sharti hili, wanataka viongozi wetu watoke wapi?* (UK 10:1: KK2)

Hizi zilikuwa ni kauli za Mwalimu zilizotolewa kwa dhamira ya kuwaonya Watanzania ambao hawapendi Tanzania ifuate siasa ya ujamaa na kujitegemea katika kujiletea maendeleo yake. Kauli ***"wanataka viongozi wetu watoke wapi?"*** ina maana kwamba miongoni mwa misingi iliyokuwa ikipigiwa chapuo na matajiri wachache ni kufuta dhana ya kwamba nchi ya Tanzania sio ya wakulima na wafanyakazi na ndio ikawa Mwalimu kuuliza hivyo kwa tashwishi kwamba ikiwa hivyo hata unapokuwa umewadia wakati wa uchaguzi viongozi watakuwa hawatokani na umma wa Watanzania tena kwa sababu umma wa Watanzania upo chini ya wakulima na wafanyakazi ilhali ukweli huo hadi hivi leo haujafutika. Ndiyo ikawa ni asisitize kwa kusema: ***"(kiongozi) lazima awe ni kiongozi wa Wakulima na Wafanya kazi"*** kwa mnasaba kwamba ikiwa raia wataghilibiwa mawazo na kukubali, basi ni watambue hata kiongozi wao hatatokana na wao tena bali kwa matashi ya hao vibaraka wachache ambao watakuwa ni nje ya wakulma na Wafanyakazi. Yaani mabepari ndio ambao watawaongoza (Watanzania hao wakulima na wafanyakazi) jinsi watakavyo, maadamu nia yao ni utajirisho binafsi na siyo kuziboresha hali za Watanzania. Kwa hivyo, ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania ilikuwa ni Watanzania watambue kwamba kiongozi wa Tanzania ni atokane na wakulima na wafanyakazi ambapo uhalisia huo kamwe haujafutika na kamwe hautafutwa na mtu yeyote zaidi ya kudanganyika. Kwa hivyo, Watanzania hawana budi kuudumisha mfumo huo wa siasa ya ujamaa kwa imani kwamba ndio mfumo pekee unaojali haki sawa kwa Watanzania wote.

**Tafsida kengeushi**: ... *ama ni wajinga, na kwa hivyo tunaweza kuwasaidia kwa kuwaelimisha; au ni wapumbavu, na kwa hivyo hatuna la kufanya la kuweza kuwasaidia; au ni maadui tu wa nchi yetu, na kwa hivyo hatuna budi kupambana nao*. (UK 13: 2: MMT)

Huu ulikuwa ni msongo wa hasira dhidi ya wale waliokuwa wakilibeua Azimio la Arusha ya kwamba limepitwa na wakati na ikawa ni wafanye jitihada za kupenyeza matakwa ya fikra zao kwa kutumia njia za kejeli na hatimaye kubadili misingi faafu ya Azimio la Arusha kwa madai kwamba: kufanya hivyo ni kufungua mianya ya kujitegemea zaidi, ilhali uhalisia wake ni kujenga tabaka la matajiri walio wachache na masikini ambao ndio wengi; na watakao endelea kuwa wengi kwa vizazi vijavyo, ikiwa hivyo ndivyo itakavyochukuliwa. Kwa Mwalimu watu wa namna hii aliwaona ni hatari. Kwa hivyo, aliwaamuru Watanzania watambue kwamba ***hawana budi kupambana nao*.** Ikwa wanauhawilisha uwongo kwa vigezo vya kiini macho ili kuyawezesha matakwa yao binafsi. Ndiyo maana ikawa ni ajiulize tena na tena kwamba: *"... **ama ni wajinga, na kwa hivyo tunaweza kuwasaidia kwa kuwaelimisha; au ni wapumbavu, na kwa hivyo hatuna la kufanya la kuweza kuwasaidia;"*** ambapo ufahima wake ni Watanzania watambue kwamba watu hao hawana nia njema zaidi ya kuwatumbukiza katika mfumo wa kibepari na kwa hivyo hawana budi kuwa chonjo na watu wa namna hiyo popote watakapokuwa wakizinadi sera zao.

Kitendo cha kuwaruhusu baadhi ya watu walio matajiri wajinunulie mashirika ya umma au wafanye jambo lolote ambalo halishirikishi umma. Mwalimu aliyaona maamuzi ya namna hiyo ni ya kiubaguzi na unyonyaji wa hali ya juu. Mashirika yaliyokuwa ya umma kufanywa yamilikiwe na watu wachache huku nchi ikijinadi kwamba ni ya kijamaa, kwa mtazamo wake ni unyama wa ujamaa mpya katika kuwalaghai wananchi haki zao. Kwa hivyo, daima aliwataka Watanzania watambue kwamba yeye yupo pamoja na wanyonge wenye kupenda ujamaa kwa misingi ya awali ya Azimio la Arusha kabla ya kuzaliwa Azimio la Zanzibar.

**Takriri na usimulizi**: "*katika jamaa za Kiafrika, jambo hili ni la maana sana. Kwa asili yetu sisi Wafrika tunaishi katika vijiji kwa ukoo, kila mtu akimsaidia mwenzake katika hali ya usawa kabisa. Tulitambua kwamba sisi sote, kila mmoja wetu, ana wajibu katika kijiji kile, na kwa sababu ya wajibu ule kila mmoja wetu alikuwa na haki ya kupata chakula au mahala pa kulala kulipia zile kazi za jasho lake alilolitoa. Wazee, wagonjwa au wale ambao mazao yao hayakufana kwa sababu mbalimbali hawakuachwa waelemewe peke yao katika shida zao. Watu wengine waliwasaidia, na wakifanya hivyo kuwa akipokea, na ambaye shida imempata sio kwa uzembe wake, haoni kwamba amedharauliwa ... mwindaji hodari na*

*mkulima hodari alikuwa akiheshimiwa katika kijiji, na kwa kawaida alikuwa akipewa cheo zaidi kwa sababu ya hesa yake kubwa anayoitoa katika kijiji kile. Lakini kijiji chote kiliishi kama kitu kimoja, na katika kijiji hicho kila mtu ni muhimu , na vitu vyote vilivyopatikana katika kijiji kile vilitumiwa na wote kwa usawa kama ilivyowezekana"* (UK 9:1: MU)

Katika matamko hayo, mbinu za ushawishi zilizotumika ni takriri na usimulizi wa matamkio yaliyotokea katika enzi ya utawala wa Mwalimu Nyerere ambapo ujamaa ulikuwa umekita mizizi. Kwa takriri neno ambapo maneno "***sisi***" na "***kijiji***" yamerudiwarudiwa, na takriri vishazi ambapo virai "***kila mtu***", "***kila mmoja***" na "***katika kijiji kile***" vimerudiwarudiwa. Mbinu hizo zimetumika ili kufungamanisha sehemu mbalimbali za hotuba hiyo, kuvuta fikra za wasikilizaji waone umuhimu wa sifa za ujamaa.

Hizi ni kauli alizozitumia Mwalimu katika kuwajuza Watanzania kuhusu nini maana ya siasa ya jamaa na kujitegemea. Siasa ya ujama na kujitegemea ndio mfumo ambao Mwalimu Nyerere aliouaminia kwamba ungeweza kutumika katika maongozi ya nchi. Mwalimu aliushupalia mfumo huo tangu mapambano dhidi yao na wakoloni hadi alipong'atuka, aliwahimiza Watanzania kuanzisha vijiji vya ujamaa na kwa muda mfupi walianza kuyaona matunda yake; ambapo kwa kumbukizi zake akisema: ***Tulitambua kwamba sisi sote, kila mmoja wetu, ana wajibu katika kijiji kile, na kwa sababu ya wajibu ule kila mmoja wetu alikuwa na haki ya kupata chakula au mahala pa kulala kulipia zile kazi za jasho lake alilolitoa"*** kumaanisha kwamba, ujamaa ulitafsiriwa si tu katika uhalisia wake lakini pia kivitendo ambapo kila mmoja kwa aila yake aliweza kufaidika na amali za kijamii kwa namna moja au nyingine.

Kwa mwegemo huo, mshawasha wa Mwalimu kwa Watanzania ulikuwa ni iwapitikie kwamba mfumo wa ujamaa ni wakipekee. Ndiyo mfumo pekee unaojali maslahi ya kila mtu na unaowatetea wanyonge kwa nguvu zote kiasi cha hata kuwapelekea wengine kujitoa muhanga kwa ajili ya maendeleo ya umma. Mfumo wa ujamaa huhimiza kila mmoja kufanya kazi kwa bidii na maarifa ambapo kwa hili Mwalimu alitashtiti kwa kusema: "***Wazee, wagonjwa au wale ambao mazao yao hayakufana kwa sababu mbali mbali hawakuachwa waelemewe peke yao katika shida zao. Watu wengine waliwasaidia, na wakifanya hivyo kuwa akipokea, na ambaye shida imempata sio kwa uzembe wake, haoni kwamba medharauliwa*** *..."* kumaanisha kwamba kila mmoja katika jamii ana haki sawa ya kuishi ingawa uwajibikaji ukitofautiana kutokana na maumbile ya mtu ambayo ni majaaliwa ya Mungu Muumba.

Kuhusu uwajibikaji wa pamoja katika jamii Mwalimu alikazia maarifa akisema: "***mwindaji hodari na mkulima hodari alikuwa akiheshimiwa katika kijiji, na kwa kawaida alikuwa akipewa cheo zaidi kwa sababu ya hesa yake kubwa anayoitoa katika kijiji kile. Lakini kijiji chote kiliishi kama kitu kimoja, na katika kijiji hicho kila mtu ni muhimu, na vitu vyote vilivyopatikana katika kijiji kile vilitumiwa na wote kwa usawa kama ilivyowezekana".*** Kwa hivyo, ulikuwa ni ushawishi wa Mwalimu kwa Watanzania wajitume katika kufanya kazi kwa bidii na maarifa huku wakishirikiana kwa minajili ya kuleta maendeleo katika jamii.

**Maswali ya kibalagha na takriri**: *"... Lakini shabaha yenyewe ni ile ile. Kama ilivyokuwa kule katika kijiji, yaani haja za kila mtu zinatimizwa katika usawa na watu wote wa katika kijiji, anamoishi. Tulitaka uhuru ili tujenge Taifa la namna hii. Kujenga taifa ambamo wachache tu ndio matajiri na wananchi waliowengi wanaendelea kuwa masikini daima ni kusaliti wajibu wetu kwa nchi yetu na kwa Afrika nzima. Na salama hii itabaki hivyo hivyo hatakama kwa njia hiyo taifa lingekuwa tayari zaidi, maana shabaha yetu siyo kuzalisha utajiri peke yake, kwa ajili ya kuwaonyesha watu au kuwakoga mataifa mengine, bali ni kuzidisha utajiri kwa faida ya watu wote. Ikiwa dhamira yetu ya kutimiza shabaha hii inawaudhi watu wengine ambao pengine wangeweza kutusaidia katika uchumi wetu, sasa sisi tufanyeje? Tuache lengo letu? Tujenge nchi hii kwa faida ya wachache badala ya jitihada yetu ya kujenga nchi yetu kwa faida ya wote?* (UK 9:2-3: MU)

Kauli hizi zilikuwa ni mbiu ya Mwalimu Nyerere mara baada ya kupata uhuru wa Tanganyika na kisha kuzaliwa kwa Tanzania na kujenga nchi kwa misingi ya ujamaa na kujitegemea. Mwalimu Nyerere aliamini kwamba mfumo wa ujamaa ni jambo lililokuwa linawezekana kutekelezeka hasa kwa usadifu kwamba tangu azali wananchi wa Tanzania walikuwa wakiishi kwa pamoja na wakisaidiana kwa kila hali. Kwa kumbukizi zake alisema: "***Kama ilivyokuwa kule katika kijiji, yaani haja za kila mtu zinatimizwa katika usawa na watu wote wa katika kijiji".*** Haya ni maisha aliyoyatamani Mwalimu ya kwamba Watanzania wangeyandeleza katika vizazi vilivyopo na vijavyo ambapo dira ya maisha ni kusaidiana. Shida ya mtu inatatuliwa kwa pamoja na hakuna anaeachwa akataabika peke yake.

Udugu, umoja na uwajibikaji kwa ushirika ni vigezo vilivyovaliwa njuga ili kupambana na maadui ujinga, maradhi na umasikini. Ndiposa Mwalimu akisema: "***Tulitaka uhuru ili tujenge Taifa la namna hii. Kujenga Taifa ambamo wachache tu ndio matajiri na wananchi waliowengi wanaendelea kuwa masikini daima ni kusaliti wajibu wetu kwa nchi***

***yetu na kwa Afrika nzima …"*** akimaanisha kwamba hizo ndizo zilizokuwa shabaha katika harakati za kujikomboa. Kwa hivyo, alitamani zingekuwa zikiendelezwa na kila Mtanzania wa leo na iwe ni hazina kwa vizazi vijavyo. Ulikuwa ni ufahima wa tathmini yake kwamba Tanzania ingali bado ni changa kiuchumi na ni ya Wakulima na Wafanyakazi na Watanzania wengi bado ni masikini. Kwa hivyo, wito wake ulikuwa ni kuwataka wale wote wenye fikra za kwamba Azimio la Arusha limepitwa na wakati watambue kwamba wanaipotosha jamii kwa maslahi binafsi.

Kwa ujumla Mwalimu aliwataka Watanzania waielewe mbiu ya Azimio la Arusha kwamba ni kujenga taifa ambalo linajali haki sawa kwa wote. Kauli ambazo ni ufahima wa tathmini kwamba ama watawala wamekuwa wakishikiwa akili kiasi cha kuburuzwa kwa matakwa ya matajiri wachache na hususani nchi zilizoendelea kiuchumi ambapo mfumo wa ubepari ndio mtawalio wa maisha yao; ama ni ujauzito wa mawazo katika kuyachuja mambo; na kwa hivyo kuupotosha uhalisia wa maisha ya Watanzania na ndio ikawa ni awaulize tena kwamba: ***"Ikiwa dhamira yetu ya kutimiza shabaha hii inawaudhi watu wengine ambao pengine wangeweza kutusaidia katika uchumi wetu… "sasa sisi tufanyeje? Tuache lengo letu? Tujenge nchi hii kwa faida ya wachache badala ya jitihada yetu ya kujenga nchi yetu kwa faida ya wote?*** ambapo jawabu lake lipalepale ya kwamba Watanzania hawanabudi kuwa na msimamo kuhusu shabaha yao ya kudumisha umoja kwa misingi ya ujamaa na kuitegemea na pia kuwa tayari kupambana na wale wanaotaka kuwagawa kutokana na uchu wa utajirisho binafsi.

**Takriri**: "*Ni miaka kumi tangu kutangazwa kwa Azimio la Arusha ... bado kuna tofauti kubwa baina ya maisha ya raia. Demokrasia yetu bado ina walakini. Maisha ya umasikini bado ni ya kawaida. Watu wetu wengi mno bado wanasumbuliwa na ujinga na maradhi yanayoweza kuzuilika. Wazee na vilema hawajaweza kuishi maisha mazuri na ya salama, ingawa Azimio la Arusha linasema wazi wazi kwamba hawa wanastahili kuhudumiwa na umma. ...*" (UK 2:1: AA)

Hii ilikuwa ni tashwishi ya Mwalimu baada ya miaka kumi ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha ambapo malengo ya utekelezwaji wake kwa jamii yalikuwa bado ni ya mwendo pole. Mtawalio wa takriri neno "***bado***" na takriri virai "***Azimio la Arusha***" ni kumbukizi zake kwa jinsi Azimio la Arusha lilivyopewa ukipaumbele na chama TANU na baadaye CCM kwa miaka ya utawala wake, aliweza kuiamuru serikali na vyombo vingine vya umma, kutekeleza kwa vitendo mambo yaliyotakiwa kuigeuza Tanzania na kuifanya kuwa taifa la kijamaa na

linalojitegemea. Ingawa mwanzoni mwake kulikuwa na mvuvumko wa hata ikawa mashirika ya binafsi yamebinafsishwa kwa faida ya umma kwa minajili yakuiweka nchi katika utawala wa wananchi; lakini hadi maadhimisho ya mika kumi ya Azimio la Arusha bado ilibainika kwamba malengo yake yalikuwa bado hajafikiwa. Hususani kuhusu Demokrasia; kujikwamua na maadui ujinga, maradhi na umasikini, udini na ukabla; na ufahima kuhusu teknomaarifa hasa ya kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo wa taifa la Tanzania. Hivyo, ushawishi wa utumizi wa takriri ulikuwa ni uamsho kwa Watanzania kuzinduka wawe na ari na nguvu mpya katika kutekeleza malengo ya Azimo la Arusha.

### 4.5 Umaratokezi wa Maudhui na Mbinu za Kiisimu

Majedwali yafuatayo, tofauti na yale yaliyotangulia, yamedhihirisha mbinu za kiisimu / mbinu za kibalagha, umaratokezi wake na asilimia kulingana na maudhui mahususi yaliyobainika katika utafiti huu.

**Jedwali 4: Maudhui ya Umoja wa Kitaifa**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Tashbiha | 3 | 21.4 |
| Takriri | 5 | 35.7 |
| Tafsida kengeushi | 1 | 7.1 |
| Maswali ya kibalagha | 2 | 14.3 |
| Tashtiti | 1 | 7.1 |
| Uchimuzi | 1 | 7.1 |
| Methali | 1 | 7.1 |
| **Jumla** | **14** | **100.0** |

Jedwali 4, linaonyesha mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika kuelezea maudhui ya umoja wa kitaifa. Kulingana na jedwali hilo, takriri imejitokeza mara tano, sawa na asilimia thelathini na sita, zaidi ya mbinu zingine. Tashbiha imefuatia kwa kujitokeza mara tatu, sawa na asilimia ishirini na moja. Maswali ya kibalagha yamejitokeza mara mbili, sawa na asilimia kumi na nne. Kisha tafsida kengeushi, tashtiti, uchimuzi na methali zimejitokeza mara moja moja ambapo ni sawa na asilimia saba kwa kila moja.

**Jedwali 5: Maudhui kuhusu Kupuuza na Kutokujali Katiba**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Takriri | 3 | 60.0 |
| Tashhisi | 2 | 40.0 |
| **Jumla** | **5** | **100.0** |

Jedwali 5, linadhihirisha mbinu mbili za kiisimu zilizotumika katika kuelezea maudhui ya kupuuza na kutokujali katiba. Mbinu ya takriri imejitokeza mara tatu, sawa na asilimia sitini. Mbinu ya tashhisi imejitokeza mara mbili; ambayo ni sawa na asilimia arobaini.

**Jedwali 6: Maudhui kuhusu Umuhimu wa Sheria**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Swali la kibalagha | 1 | 25.0 |
| Takriri | 1 | 25.0 |
| Tafsida kengeushi | 1 | 25.0 |
| Sentensi changamano na ambatano | 1 | 25.0 |
| **Jumla** | **4** | **100.0** |

Jedwali 6, linaonyesha mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika kuelezea maudhui kuhusu umuhimu wa sheria. Kulingana na jedwali hilo, mbinu zilizotumika ni swali la kibalagha, takriri, tafsida kengeushi, sentensi changamano na ambatano. Zote zimejitokeza mara moja, sawa na asilimia ishirini na tano kwa kila moja.

**Jedwali 7: Maudhui kuhusu Rushwa**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Takriri | 4 | 25.0 |
| Tashtiti | 1 | 6.3 |
| Tashhisi | 2 | 12.5 |
| Uchanganyaji ndimi | 1 | 6.3 |
| Maswali ya kibalagha | 2 | 12.5 |
| Tafsida kengeushi | 2 | 12.5 |

| | | |
|---|---|---|
| Uzungumzi nafsi | 1 | 6.3 |
| Istiara | 1 | 6.3 |
| Unukuzi | 1 | 6.3 |
| Msemo | 1 | 6.3 |
| **Jumla** | **16** | **100.0** |

Kwa kuzingatia jedwali hili la saba, takriban mbinu kumi zimetumika kuelezea maudhui kuhusu rushwa. Mbinu ya takriri ilikuwa ni mtawalia mara nne, sawa na asilimia ishirini na tano, zaidi ya mbinu zingine. Tashhisi, maswali ya kibalagha, na tafsida kengeushi, zimejitokeza mara mbili mbili kwa kila moja, sawa na asilimia kumi na mbili kwa kila moja. Kisha tashtiti, uchanganyaji ndimi, uzungumzi nafsi, istiara, unukuzi na msemo zimejitokeza mara moja, sawa na asilimia moja kwa kila moja.

**Jedwali 8: Maudhui kuhusu Ukabila na Udini**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Usimulizi | 1 | 6.3 |
| Tashhisi | 4 | 25.0 |
| Unukuzi | 1 | 6.3 |
| Maswali ya kibalagha | 3 | 18.8 |
| Takriri | 3 | 18.8 |
| Viambishi nafsi | 1 | 6.3 |
| Vimilikishi | 1 | 6.3 |
| Kinyume | 1 | 6.3 |
| Taswira | 1 | 6.3 |
| **Jumla** | **16** | **100.0** |

Katika jedwali la nane, mbinu tisa za kiisimu zilitumika kuyaelezea maudhui ya ukabila na udini. Tashhisi imejitokeza mara nne, sawa na asilimia ishirini na tano. Maswali ya kibalagha na takriri yamejitokeza mara tatu kwa kila moja, ambapo ni sawa na asilimia kumi na tisa kwa kila moja. Mbinu ya usimulizi, unukuzi, viambishi nafsi, vimilikishi, vinyume na taswira zimejitokeza mara moja moja, sawa na asilimia sita kwa kila moja.

**Jedwali 9: Maudhi kuhusu Umoja wa Wafanyakazi**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimi |
|---|---|---|
| Vihisishi | 1 | 14.3 |
| Maswali ya kibalagha | 2 | 28.6 |
| Uzungumzi nafsi | 1 | 14.3 |
| Vihusishi | 1 | 14.3 |
| Istiara | 1 | 14.3 |
| Takriri | 1 | 14.3 |
| **Jumla** | **7** | **100.0** |

Jedwali hilo la tisa, limedhihirisha mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika kuelezea maudhui kuhusu umoja wa wafanyakazi. Kulingana na jedwali hilo, maswali ya kibalagha yamejitokeza mara mbili, sawa na asilimia ishirini na tisa. Kisha mbinu za vihisishi, uzungumzi nafsi, vihusishi, istiara, na takriri zimejitokeza mara moja moja, sawa na asilimia kumi na nne kwa kila moja.

**Jedwali 10: Maudhui kuhusu Kilimo Kwanza**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Tashbiha | 1 | 14.3 |
| Tafsida kengeushi | 2 | 28.6 |
| Maswali ya kibalagha | 2 | 28.6 |
| Takriri | 2 | 28.6 |
| **Jumla** | **7** | **100.0** |

Katika maudhui haya ya kilimo kwanza, mbinu tano za kiisimu zimetumika kuyaelezea. Tafsida kengeushi, maswali ya kibalagha na takriri kila moja imejitokeza mara mbili, ambapo ni sawa na asilimia ishirini na tisa. Wakati ambapo tashbiha imejitokeza mara moja, sawa na asilimia kumi na nne.

**Jedwali 11: Maudhui kuhusu Kutofungamana na Upande wowote**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Takriri | 4 | 44.4 |
| Tashbiha | 1 | 11.1 |
| Tashtiti | 1 | 11.1 |
| Maswali ya kibalagha | 2 | 22.2 |
| Tafsida kengeushi | 1 | 11.1 |
| **Jumla** | **9** | **100.0** |

Katika jedwali 11, takriri imejitokeza mara nne, sawa na asilimia arobaini na nne. Maswali ya kibalagha yamejitokeza mara mbili, sawa na asilimia ishirini na mbili. Kisha tashbiha, tashtiti na tafsida kengeushi zimejitokeza mara moja moja, ambapo ni sawa na asilimia kumi na moja kwa kila moja.

**Jedwali 12: Maudhui kuhusu Uwajibikaji**

| Mbinu za Kiisimu | Umara tokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Maswali ya kibalagha | 2 | 11.1 |
| Takriri | 7 | 38.9 |
| Tashbiha | 3 | 16.7 |
| Mafumbo | 1 | 5.6 |
| Tashtiti | 1 | 5.6 |
| Tafsida kengeushi | 1 | 5.6 |
| Usimulizi | 1 | 5.6 |
| Vihisishi | 1 | 5.6 |
| Istiara | 1 | 5.6 |
| **Jumla** | **18** | **100.0** |

Jedwali 12, Mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika ni pamoja na takriri iliyojitokeza mara saba, sawa na asilimia thelathini na tisa. Tashbiha ilimefuatia kwa kujitokeza mara tatu, sawa na asilimia kumi na saba. Maswali ya kibalagha yaliyojitokeza mara mbili, sawa na asilimia kumi na moja. Wakati ambapo mbinu za mafumbo, tashtiti, tafsida kengeushi, usimulizi, tafsida kengeushi na istiara zimejitokeza mara moja moja, ambapo ni sawa na asilimia sita kwa kila moja.

**Jedwali 13: Maudhui kuhusu Uongozi Bora**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Takriri | 9 | 45.0 |
| Maswali ya kibalagha | 7 | 35.0 |
| Tashhisi | 2 | 10.0 |
| Tashtiti | 1 | 5.0 |
| Istiara | 1 | 5.0 |
| **Jumla** | **20** | **100.0** |

Katika maudhui haya ya uongozi bora, mbinu tano za kiisimu zimetumika. Takriri imejitokeza mara tisa, sawa na asilimia arobaini na tano. Hii ni mbinu iliyojitokeza mara nyingi zaidi ya nyingine katika kuelezea maudhui hayo. Maswali ya kibalagha yamefuatia kwa kujitokeza mara saba, sawa na asilimia thelathini na tano. Tashhisi imejitokeza mara mbili, sawa na asilimia kumi. Kisha tashtiti na istiara zimejitokeza mara moja moja, sawa na asilimia tano kwa kila moja.

**Jedwali 14: Maudhui kuhusu Ufaafu wa Azimio la Arusha**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Tafsida kengeushi | 2 | 11.1 |
| Takriri | 6 | 33.3 |
| Tashtiti | 1 | 5.6 |
| Kinaya | 1 | 5.6 |
| Maswali ya kibalagha | 4 | 22.2 |
| Istiara | 1 | 5.6 |
| Kejeli | 1 | 5.6 |
| Matumizi ya sentensi fupi fupi | 1 | 5.6 |
| Tashbiha | 1 | 5.6 |
| **Jumla** | **18** | **100.0** |

Katika jedwali 14, mbinu tisa za kiisimu zimejitokeza kuelezea maudhui ya ufaafu wa Azimio la Arusha. Takriri imeongoza kwa kujitokeza mara sita, ambapo ni sawa na asilimia thelathini na tatu. Na kufuatiwa na maswali ya kibalagha yaliyojitokeza mara nne, sawa na asilimia ishirini na mbili; ikafuatiwa na tafsida kengeushi iliyojitokeza mara mbili, sawa na

asilimia kumi na moja. Kisha tashtiti, kinaya, istiara, kejeli, matumizi ya sentensi fupifupi na tashbiha zimejitokeza mara moja moja, ambapo ni sawa na asilimia saba kwa kila moja.

**Jedwali 15: Maudhui kuhusu Ubaguzi**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Maswali ya kibalagha | 1 | 33.3 |
| Tashhisi | 1 | 33.3 |
| Tafsida kengeushi | 1 | 33.3 |
| **Jumla** | **3** | **100.0** |

Kwa kuzingatia jedwali 15, kuna ubainifu kwamba mbinu tatu za kiisimu ndizo zilizojitokeza. Maswali ya kibalagha, tashhisi na tafsida kengeushi zimejitokeza mara moja moja, sawa na asilimia thelathini na tatu kwa kila moja.

**Jedwali 16: Maudhui kuhusu Elimu kwa Wote**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Takriri | 4 | 21.1 |
| Tashhisi | 3 | 15.8 |
| Vihisishi | 1 | 5.3 |
| Maswali ya kibalagha | 5 | 26.3 |
| Uchanganyaji ndimi | 4 | 21.1 |
| Msemo | 1 | 5.3 |
| Methali | 1 | 5.3 |
| **Jumla** | **19** | **100.0** |

Jedwali 16, limebainisha mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika kuelezea maudhui ya elimu kwa wote. Mbinu zilizotumika ni pamoja na maswali ya kibalagha yaliyojitokeza mara tano, sawa na asilimia ishirini na sita. Takriri na uchanganyaji ndimi zikifuatia kwa kujitokeza mara nne, sawa na asilimia ishirini na moja kwa kila moja. Tashhisi nayo ikijitokeza mara tatu, sawa na asilimia kumi na sita. Kisha vihisishi, msemo na methali zikijitokeza mara moja moja, ambapo ni sawa na asilimia tano kwa kila moja.

**Jedwali 17: Maudhui kuhusu Onyo kwa Idd Amin**

| Mbinu za Kiisimi | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Takriri | 4 | 28.6 |
| Tafsida kengeushi | 3 | 21.4 |
| Maswali ya kibalagha | 2 | 14.3 |
| Usimulizi | 1 | 7.1 |
| Kinaya | 1 | 7.1 |
| Istiara | 1 | 7.1 |
| Tashbiha | 1 | 7.1 |
| Uzungumzi nafsi | 1 | 7.1 |
| **Jumla** | **14** | **100.0** |

Jedwali 17, linaonyesha mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika kuelezea maudhui ya onyo kwa Idd Amin. Kulingana na jedwali hilo, takriri imejitokeza mara nne, sawa na asilimia ishirini na tisa, zaidi ya mbinu zingine. Tafsida kengeushi imefuatia kwa kujitokeza mara tatu, sawa na asilimia ishirini na moja. Maswali ya kibalagha yamejitokeza mara mbili, sawa na asilimia kumi na nne. Kisha usimulizi, kinaya, istiara, tashbiha na uzungumzi nafsi zimejitokeza mara moja moja ambapo ni sawa na asilimia saba kwa kila moja.

**Jedwali 18: Maudhui kuhusu Demokrasia**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Tashbiha | 1 | 12.5 |
| Maswali ya kibalagha | 1 | 12.5 |
| Msemo | 1 | 12.5 |
| Uchimuzi | 3 | 37.5 |
| Istiara | 1 | 12.5 |
| Tashhisi | 1 | 12.5 |
| **Jumla** | **8** | **100.0** |

Jedwali hilo la 18, limedhihirisha mbinu mbalimbali za kiisimu zilizotumika kuelezea maudhui kuhusu demokrasia. Kulingana na jedwali hilo, mbinu ya uchimuzi imejitokeza mara tatu, sawa na asilimia thelathini na saba nukta tano. Kisha matumizi ya tashbiha, maswali ya kibalagha, msemo, istiara na tashhisi zikijitokeza mara moja moja, sawa na asilimia kumi na mbili nukta tano kwa kila moja.

**Jedwali 19: Maudhui kuhusu Kupaa na Kutunguliwa kwa Azimio la Arusha**

| Mbinu za Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Maswali ya kibalagha | 3 | 33.3 |
| Takriri | 4 | 44.4 |
| Tashbiha | 1 | 11.1 |
| Tafsida kengeushi | 1 | 11.1 |
| **Jumla** | **9** | **100.0** |

Jedwali 19, limeonyesha mbinu kadhaa zilizotumika katika kuelezea maudhui ya kutunguliwa kwa Azimio la Arusha. Takriri imejitokeza mara nne, sawa na asilimia arobaini na nne. Maswali ya kibalagha yamejitokeza mara tatu, sawa na asilimia thelathini na tatu. Kisha tashbiha na tafsida kengeushi zimejitokeza mara moja moja, ambapo ni sawa na asilimia kumi na moja.

**Jedwali 20: Umaratokezi wa Mbinu za Kiisimu na Asilimia yake kwa Maudhui yote yaliyobainika katika Utafiti huu**

| Mbinu ya Kiisimu | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Tashbiha | 12 | 7 |
| Takriri | 53 | 29 |
| Tafsida Kengeushi | 15 | 8 |
| Maswali ya Kibalagha | 37 | 21 |
| Tashtiti | 6 | 3 |
| Uchimuzi | 4 | 2 |
| Methali | 2 | 1 |
| Tashhisi | 15 | 8 |
| Sentensi changamano na ambatano | 1 | 0.5 |
| Uchanganyaji ndimi | 5 | 3 |
| Uzungumzi nafsi | 3 | 1.6 |
| Istiara | 8 | 4 |
| Unukuzi | 2 | 1 |
| Msemo | 2 | 1 |
| Usimulizi | 3 | 1.6 |
| Viambishi nafsi | 1 | 0.5 |

| | | |
|---|---|---|
| Vimilikishi | 1 | 0.5 |
| Vihisishi | 3 | 1.6 |
| Fumbo | 1 | 0.5 |
| Kinaya | 2 | 1 |
| Kejeli | 1 | 0.5 |
| Sentensi fupifupi | 1 | 0.5 |
| Kinyume | 1 | 0.5 |
| Taswira | 1 | 0.5 |
| **Jumla** | **180** | **100** |

Jedwali 20, hizo ni mbinu za kiisimu (mbinu za kibalagha) zilizotumika katika kuelezea maudhui yaliyoendelezwa katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere zilizofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Kwa kuzingatia jedwali hilo, imedhihirika kwamba, mbinu ya takriri ndiyo iliyokuwa mtawalia zaidi kwa kujitokeza mara hamsini na tatu sawa na asilimia ishirini na tisa. Mbinu ya maswali ya kibalagha imefuatia kwa kujitokeza mara 37, sawa na asilimia ishirini na moja. Tafsida kengeushi na tashhisi zimejitokeza mara kumi na tano kwa kila moja, sawa na asilimia nane kwa kila moja. Tashbiha imejitokeza mara kumi na mbili, sawa na asilimia saba. Istiara imejitokeza mara nane, sawa na asilimia nne. Tashtiti imejitokeza mara sita, sawa na asilimia tatu uchanganyaji ndimi umejitokeza mara tano, sawa na asilimia tatu. Uchimuzi umejitokeza mara nne, sawa na asilimia mbili. Mbinu za uzungumzi nafsi, usimulizi na vihisishi - zimejitokeza mara tatu kwa kila moja ambapo ni sawa na asilimia moja nukta sita. Methali, unukuzi, msemo na kinaya - zimejitokeza mara mbili mbili kwa kila moja ambapo ni sawa na asilimia moja kwa kila moja. Kisha sentensi changamano na ambatano, viambishi nafsi, vimilikishi, fumbo, kejeli, sentensi fupi, kinyume na taswira - zimejitokeza mara moja moja kwa kila moja, sawa na asilimia sifuri nukta tano.

### 4.6 Hisia za Hadhira kuhusu Hotuba za Mwalimu Nyerere

Haya ni maoni ya Wasailiwa Kulingana na Maudhui yaliyojitokeza katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere zilizochanganuliwa katika utafiti huu. Maoni hayo yalidhihirisha hisia za hadhira kuhusiana na hotuba hizo ambapo kwazo mtafiti aliweza kubaini jinsi wasailiwa walivyoathirika.

**Jedwali 21: Maudhui mahususi, Maoni na Athari za Wasailiwa**

| Maudhui Mahsusi | Maoni Mahususi ya Wasailiwa | Athari | Ushawishi | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Chanya | Hasi |
| **Umoja wa kitaifa** | "Kuhusu Muungano, daima tutamkumbuka Baba wa taifa. Katuachia haki, umoja, amani, upendo na mshikamano. Ingawa kuna suintofahamu za hapa na pale lakini zinazungumzika. Wanaoshupalia kusiwe na Muungano hakika hawana sababu za msingi zaidi ya utashi binafsi. Kuwa na umoja ni jambo baya? Hakuna mwanadamu ambaye ni kamili. Ikiwa kuna tatizo ni suala la kukaa na kulitafutia ufumbuzi, likatatuliwa na watu wakasonga mbele na kuna uzoefu sio mara ya kwanza. Mara ngapi maswala ya Muungano yamelipuka na yakasahilishwa? Vinginevyo ni ubaguzi tu! Na ndio maana Mwalimu akiwaonya wale wanaotaka kuwabagua wengine kwamba kufanya hivyo ni katika madhambi makubwa. Ni sawa na kula nyama ya mtu aliyekufa na kwamba mwenye kuila ataendelea kwa tabia hiyo. Kumaanisha kwamba ni katika madhara makubwa yatakayoikumba jamii. Watu watauana (vita na migogoro isiyokuwa na tiba mbadala) hadi kufikia tone la damu ya mtu wa mwisho. Hakika | **Kufurahia** | + | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ushawishi wa Mwalimu wa kuziiunganisha sehemu hizi mbili ni jambo zuri na la kuendelezwa daima.” | | | |
| **Uwajibikaji** | “Matunda ya umoja chini ya siasa ya ujamaa na kujitegemea yalionekana. Hapakuwa na mtu aliekubaliwa kubweteka ikiwa si mtoto mdogo, mzee na ama kilema. Kila mtu alikula jasho lake ingawa kwa kushirikiana. Na hii ndiyo kusema kwamba, kwa kuitupa misingi ya Azimio la Arusha hivi leo vijana wengi wenye nguvu si tu kuwa ni wala unga; lakini wazembe, wazururaji na ombaomba - wametagaa kila mahali. Hakika maongozi ya Mwalimu Nyerere na sera za Azimio la Arusha, kwa wenye kutafakari tutamkumbuka milele.” | **Kuchukia** | + | |
| **Umuhimu wa sheria** | “Ah! Mwalimu alikuwa hamchelei mtu. Ikiwa kafanya kosa atamkadamsisha hata atamani ardhi ipasuke aingie ndani yake. Kumbuka yaliyompata Mdiplomasia wa Kigiriki; mbali na utetezi wa viongozi wa Kiafrika, alimsweka ndani na baadaye akamuamuru afungashe virago na kurudi makwao na ama kuhusu lele mama katika maongozi. Ingawa alikwisha ng’atuka lakini hakuwafumbia macho viongozi kwa hilo na ikumbukwe aliposema: “***hamwezi kuongozwa na hamjui mkewe atamwambia nini kesho***” kwa muktadha wake palikuwa hakuna kificho kwamba anamzungumza kiongozi aliyekuwepo madarakani mara baada ya kung’atuka kwake. Na ndio kusema alikuwa hamchelei | **Kuchukia** | | - |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | yeyote ikiwa mambo yanayohusu nchi yanakwenda kombo. Ingawa hivyo, sidhani ni njia nzuri ya kurekebishana. Kweli hakuwa akichelea uovu lakini amewachia wengine donda dugu. Kwa hili angetumia mbinu nyingine tungemfagilia zaidi” | | | |
| **Rushwa** | “Mwalimu alikuwa ni mfasaha wa lugha. Katika suala la rushwa amewakonga watu takriban kwa kila nyanja ya maisha ya Mtanzania. Hasa kuhusu mamlaka, natamani kila mgombea wa nafasi za uongozi angeisoma hotuba ya “***Nyufa***” na “***Tunatoka wapi***”. Wengi wangejifua kwa rushwa” | **Kufurahia** | + | |
| **Kupuuza na kutokuijali katiba** | “Hakika baadhi ya viongozi wamekubuhu. Iweje katiba ambayo ndiyo mama wa sheria zingine na wao ndiyo wanaotakiwa kuisimamia lakini wayaongoze mambo kiholela? Hii ni kuthibitisha kwamba wapo kimaslahi, Iwe ni kwa uzembe au kwa utovu gani wa kinidhamu, picha ambayo wengi wataondoka nayo ni kwamba hawaisimamii katiba ili waweze kupitisha matakwa yao binafsi. Na hawa ni wale wanaoiona ikulu ni sehemu ya biashara. Lau kama Mwalimu angekuwa hai; viongozi ambao ni watovu katika kuisimamia katiba ya nchi bila shaka wangewasweka mahakamani. “Mwalimu hakuwa na tabia hiyo. Aliisimamia katiba na kuwasimamia viongozi wengine waisimamie katiba” Na ndio maana ukiifuatilia historia ya maongozi yake | **Kuchukia** | | – |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | huwezi kuona uholela huu wa leo ambapo viongozi wanalindana. Tuna kumbukumbu za matukio mengi ambayo yanatokana na kutokusimamiwa kwa katiba ya nchi vizuri Pakitokea wizi wa mali za umma - utasikia … eti hamsini kadhaa zimerudishwa lakini aliyerudisha hatajwi. Kama sio kulindana ni nini? Na kama sio wakubwa ni akina nani wengine? Katiba ingesimamiwa vizuri wezi wote wangetajwa kwa majina yao na kuadhibiwa bila ya kujali wadhifa wa mtu. | | | |
| **Ukabila na Udini** | "Watu katika jamii wanapaswa kuheshimiana. Iweje wengine wawaone wengine si kitu eti tu kwa sababu si katika imani yao kidini au si katika kabila lao. Huu ni ubaguzi! Kila mtu ana uhuru wa kuabudu. Wengine huwashawishi wengine kwa kutumia udini na ukabila kwa minajili ya kupitishia matakwa yao binafsi. Kufanya hivyo ni kuuvunja umoja wa Watanzania ambao umewagharimu kwa muda mrefu. Na ikumbukwe historia ya Tanzania hasa katika jitihada za kujikomboa. Moja ya mbiu ilikuwa ni "kusahau ukabila" na lugha ya Kiswahili ikiwa ndiyo mtawalia wa mawasiliano. Haikuchukua muda. Tanganyika ilikuwa huru mwaka 1961 na kisha mwaka 1964, Tanganyika na Zanzibar zikaungana na kuzaliwa Tanzania. Haya ni matunda ya kuziweka tofauti za ukabila na udini pembeni na kwa hivyo kujali maslahi ya umma. Hakika wanaoendekeza udini na | **Kuchukia** | | _ |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ukabila wanapaswa kupigwa vita. Kwa nini watu hawajifuzi na wakajirekebisha kutoka na makosa? Na tuangalie majirani zetu na hata nchi za ughaibuni. Wengi wanataabika kwa sababu tu wameshindwa kuwa kitu kimoja. Udini na ukabila baada ya kuwa wameshindwa kuzishinda nafsi zao; hivi leo nchi zao hazitamaniki. Watu wanazihama nchi zao. Hakika jitihada za Mwalimu Nyerere tutazikumbuka. aliwafikisha Watanzania kuzuri. Watu walijinasibu kama Watanzania na sio vinginevyo. Rejelea hotuba yake ya Nyufa; ambapo watu wa nchi nyingine wakiionea gere Tanzania. Ah! Mungu akulipe kwa mema yako Baba wa Taifa | | | |
| **Kilimo kwanza** | "Mwalimu alikuwa makini takriban katika kila nyanja ya maisha. Kilimo alikipa kipaumbele kama uti wa mgongo wa Tanzania. Lakini viongozi wetu wa leo ni kana kwamba hawana jipya; nyingi ya sera zao ukizitathmini utakuta Mwalimu Nyerere alikwisha zizungumzia na kuzisimamia zikatekelezwa na zikaleta mafanikio. Angalia sera ya "Kilimo kwanza" si jambo jipya ukifuatilia historia ya maongozi ya Baba wa Taifa. Viongozi wa leo wana lipi jipya? Na ilikumbukwe Azimio la Moshi (Siasa ni Kilimo); na Azimio la Iringa (umwagiliaji maji mashambani). Viongozi wa leo wana lipi jipya? Ingependeza ikiwa viongozi wa leo wangefanya jitihada na wakawa wawazi | **Kuchukia** | | _ |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | katika kuendeleza jitihada za Mwalimu; ikiwa hawana sera mbadala. Mwalimu alikuwa mbunifu na mtekelezaji (alisimamia). Makupe, wazembe na wazururaji hawakupewa nafasi.<br>Eti sera ya 'Kilimo kwanza' – hivi leo! wakuitekeleza ni nani? Uzembe na uzururaji uliokuwa umepigwa vita na Mwalimu hivi leo ni majanga. Ukirejelea hotuba ya "***Nyufa***" na "***Tumetoka Wapi***" kuna mengi ambayo viongozi wetu wange paswa kujikosoa kwa maongozi yao. Hivi leo mijini na vijijini kumejaa vijana wengi wamechoka, hawajiwezi - ni wala Unga. "***Kilimo kwanza***" hivi leo kama sio sera chapwa, nguvu kazi yake itapatikana wapi? Au ndio kiendeshwe na watu kutoka nje ya nchi? Viongozi wa leo ni wakubali kuibeba lawama hii. Madawa ya kulevya yanayoiharibu nguvu kazi ya Tanzania yote yanapitia mikononi mwao. Sera za Mwalimu hivi leo ni chapwa. Hakika viongozi wa leo wana dhima kubwa, na wataulizwa kwa viapo vyao kuhusu kuwaongoza Watanzania." | | | |
| **Siasa ya kutofungamana na upande wowote** | "Kwa siasa hii ya kutofungamana na upande wowote kwa Tanzania tumefaulu. Hii imetujengea heshima; tungekuwa bendera fuata upepo. Mataifa mengi yanaitamani nchi ya Tanzania kutokana na sera hii. Haiburuzwi kwa matakwa ya wengine. Fuatilia hotuba ya Mwalimu Nyerere kuhusu Mutinyi ya 1964. Ni kweli | **Kufurahia** | + | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Watanzania walikubali msaada wa Waingereza katika kuirudisha hali ya utulivu (amani); lakini Tanzanaia haikuikumbatia Uingereza hata wakalalamika ya kwamba Tanzania inawazungumza vibaya; hasa yakirelelewa mabaya yao kuhusu Ukoloni wao katika nchi za kiafrika. Tanzania ikiwa mojawapo. Mwalimu aliuweka mbele uzalendo na ndiyo sababu hivi leo tunajivunia amani; lakini utu na heshima ya uhuru wa nchi. Hakika heshima na taadhima zinamstahiki Baba wa taifa kwa kuisimamia misingi ya siasa za Tanzania.” | | | |
| **Uongozi bora** | “Hotuba zake zina mafunzo mema. Ni nani kama Baba wataifa. Ningekuwa na uwezo ningehakikisha kila mgombea unampitikia usemi wa Baba wa Taifa kwamba: kila anayetaka uongozi kwa nchi yetu ya Tanzania ajiulize: ana kwenda kuifanyia nini nchi hii nasio nchi itamfanyia nini.” | **Kuzinduka** | + | |
| **Ufaafu wa Azimio la Arusha** | “Ingawa misingi ya Azimio la Arusha inasemwa imepitwa na wakati lakini ukina wa hoja zenye mashiko hazijawa wazi. Ukweli wa misingi ya Azimio la Arusha kwamba nchi ya Tanzania ni ya Wakulima na Wafanyakazi upalepale; na bado tungali ni masikini wa kutupwa. Hii ni janja ya Sungura cha wote kuwa cha wachache. Naamini tutaendelea kumkumbuka Baba wa Taifa.” | **Kusaili** | + | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Ubaguzi** | Hakika maonyo ya Mwalimu kuhusu mtikisiko wa nchi yetu; ubaguzi ndio uliochimuza matatizo ya Muungano, rushwa ukabila na udini, na kadhalka. Hivi leo ukweli wa mambo unadhihirika. Ikiwa Watanzania hawatamakinika tutaendelea kubaguana ambapo madhara yake ni mauaji yatakayotuteketeza hadi tone la damu ya mtu wa mwisho. Kama alivyosema Baba wa Taifa. Kwamba 'dhambi ya ubaguzi ni sawa na kula nyama ya mtu'. Hakika natamani kama angerudi duniani na akayaona matendo ya Watanzania wa leo. Tumesambaratika tunazozana eti tu kwa nini tuwe na umoja (Muungano) imekuwa dhambi! Hatuthaminiani tena, amani imetoweka. Rejelea mauaji ya Albino na Muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika – fuatilia malumbano ya Wabuge kuhusu Katiba mpya – ni aibu tupu! Ni matatizo yanayotokota kila uchao. Yu wapi Baba wa taifa kwa ushupavu wake, sera zake na maongozi yake ya muda mrefu kuliko kiongozi mwingine yeyote nchini Tanzania? Kila chake hivi sasa kimetupwa katika kaburi la sahau. Tutakukumbuka Baba. Mungu akulipe kwa mema yako. | **Kuzinduka** | + | |
| **Umoja wa Wafanyakazi** | Hivi leo hakuna nidhamu ya kazi kazini. Anayepata mamlaka ya kuwaongoza wengine anataka kwa siku chache awe bilionea. Wafanyakazi wanafanywa ni watumwa na ama ngazi za kuwawezesha | **Kuzinduka** | + | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | waroho kujichumia mali za nchi (za umma) watakavyo. Na yakumbukwe matatizo ya Richmond na Escrow hizo ndizo kazi za viongozi wetu waliopewa majukumu ya kuliongoza taifa hili changa la Tanzania? Na ndio tuna sema laiti Mwalimu angekuwepo hivi leo viongozi wengi wangetafutana. Hakika pangechimbika! Na asipatikane mtu wa kumwokoa mwenziwe. | | | |
| **Elimu kwa wote** | Tunamshukuru Baba wa Taifa kwa kuhakikisha enzi zile kwamba elimu ya watu wazima inapewa kipaumbele sanjari na elimu kwa wote kwa vijana waliokuwa wanakulia. Chembelecho utitiri wa digirii kwa vijana wa leo mzizi wake ni wazazi chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere; kizazi hadi kizazi walivyoelemika na kujua thamani ya elimu. Ikawa vijana wengi kuhimizwa na kusaidiwa kwa hali na mali ndiyo maana hivi leo tuna wasomi wengi na ajira wana zikosa zaidi ya ujasiri amali ambapo kama si uchanga wa nchi kiuchumi; "wangewezeshwa wange weza" | **Kufurahia** | + | |
| **Onyo kwa Idd Amin** | Hakika umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Na uongozi bora pia ni amani. Uvamizi wa Idd Amin kwa nchi ya Tanzania ulitia doa si tu Afrika Mashariki lakini Afrika kwa ujumla. Ingawa hivyo, umoja wa Watanzania waliilinda himaya yao na ardhi ya Kagera aliyokuwa akidai ni sehemu ya Uganda ushindi ukawa ni kwa Watanzania; ulimwengu ulitambua kwamba umoja wa Watanzania ni silaha | **Kufurahia** | + | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | thabiti. Mbali na ubabe wa Idd Amini aliishia ughaibuni huku akiitamani ardhi ya uzawa wake na ikawa haiwezekani tena. Amani iliyokuwa ni itoweka, kwa pamoja Watanzania waliirejesha kwa kipindi kifupi. "Hakika watu wakiamua inawezekana" | | | |
| **Demokrasia** | Ulimwengu unatambua ya kwamba Tanzania ni kisiwa cha amani. Hii ni mizizi ya Mwalimu aliyoiotesha enzi za maongozi yake. Watanzania wana uwezo wa kukosoana na kukubali kukosolewa. Na ndiyo maana hata kama kuna mkengeuko kwa wenye mamlaka wananchi wanapoyagundua huongea bila ya kuwachelea. Ingawa ni fedhea lakini ni heri nusu shari kuliko shari kamili. Mifano mizuri ni ya Richmond na Escrow. Baadhi ya viongozi wamemwaga unga! | **Kufurahia** | + | |
| **Kupaa na Kudondoshwa kwa Azimio la Arusha.** | Kuzika mfumo wa ujamaa ni kuhuisha ubepari ambao wazazi wetu walipingana nao enzi za kutafuta uhuru. Uzuri wa ubepari uwapi kama sio usemi wa Mwalimu kwamba sasa Tanzania itazaa mamilionea wa tano; lakini itakuwa na masikini wengi! "Ndiko tuliko hivi leo" | **Kuchukia** | | - |

Kutokana na usaili uliofanywa; kwa kurejelea jedwali hili; ilibainika kwamba; Watanzania wengi hupenda kusikiliza na ama kuzisoma hotuba za Mwalimu Nyerere; na kwamba maudhui yaliyomo katika hotuba zake huwagusa Watanzania takrban katika kila nyanja ya maisha yao. Uthibati huu unatokana na matokeo ya usaili; ambapo kwa urejeleo wa swali la kwanza hadi la tatu. Mbali na lugha fasaha aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere ambayo hadi hivi leo ingali inawashawishi wasomaji au wasikilizaji wa hotuba zake; Watanzania wengi

wamekuwa wakiyachukulia kwa uzito mkubwa maudhui yake kiasi cha hata kuaminiwa kwamba ndiyo sera za maongozi ya nchi ya Tanzania. Na hii ndiyo kusema kwamba hotuba zake zinafaa kundelea kusomwa na kusikilizwa na vizazi vilivyopo na vijavyo.

#### 4.6.2 Maoni ya Kijumla kuhusu Ushawishi wa Hotuba za Mwalimu Kwa Wasailiwa

**MW 1:** *Hotuba zake ni nzuri sana, zina konga takriban kila nyanja ya maisha. Ingawa anapokemea jambo mara nyingi hana tafsida na kwa hivyo watu wengi kuhisi kwamba alikuwa na jeuri; lakini kusema la kweli zinaelemisha*.

Maoni haya yanaonyesha kwamba kuna Watanzania ambao hutambua kwamba hotuba za Mwalimu zina manufaa makubwa kwa jamii ya Watanzania. Hata kama kuna baadhi ya Watanzania wanaguswa kwa kuzisoma au kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere. Kukosolewa huko hakuwakatishi tamaa ya kuendelea kuzisoma au kuzisikiliza hotuba hizo kutokana na faida nyingi zilizomo ndani yake. Hii ni kwa sababu Mwalimu alikua haongelei jambo moja tu katika hotuba zake. Kwa hivyo huwavutia watu wengi kutaka kujua mengi yaliyotagaa ndani ya hotuba zake. Hivyo, hata kama mtu ataudhika kwa jambo moja lakini atayafaidi mengi zaidi katika hotuba hiyo hiyo moja.

**MW 2:** *Katika makemevu yake kuhusu Rushwa na Muungano hakika tunamfagilia. Tatizo lake ni kwamba kawasema wale wapinzani wazi wazi mno jambo ambalo kusema la kweli linajenga kinyongo hususani kwa waliotajwa, familia zao na wafuasi wao ni dhahiri watajihisi vibaya kwa matamshi hayo.*

Maoni ya wasailiwa yalidhihirisha kwamba Mwalimu hakuwa akiwachelea walarushwa na wale waliokuwa wakitaka Muungano wa Jamhuri ya Tanzania uvunjike. Daima Mwalimu alikuwa akitumia lugha ya vitisho kama njia ya kuyakomesha maovu yaliyokuwa yakizuka katika jamii kwa kasi mithili ya hayo, ambayo yalihitaji yasifumbiwe macho. Ingawa hivyo, ilibainika kwamba, Watanzania wengi hupenda kuzisikiliza na kuzisoma hotuba hizo kutokana na weledi wa lugha aliyoitumia Mwalimu lakini pia uongozi imara unaodhihirika kupitia matamshi ya hotuba zake. Aliyakemea maovu bila kumhofia yeyote kwa hali, jinsia au hadhi yake.

**MW 3:** *Nilikasirika sana kwa matamshi aliyokuwa akimshutumu wazi wazi Rais aliyekuwepo madarakani. Kwa hakika matamshi hayo yananikuna kichwa sana kiasi cha hata kujiuliza ikiwa hiyo ndiyo njia mpya na iliyo bora kwa viongozi kukosoana hadharani? Mwalimu ana mengi mazuri lakini hilo ameniudhi sana na kunivunja moyo kabisa kabisa. Hadi hivi leo*

*naamini mwenzie anadhalilika sana kutokana na kauli hizo. Lakini hatushangai; kwa sababu mbali na kung'atuka kwake ni kana kwamba wakati wote wa uhai wake - ndiye aliyekuwa akiliongoza taifa la Tanzania na pengine hadi hivi leo ingawa hatunaye tena duniani. Sera zake hadi hivi leo zingali zinazingatiwa katika maongozi ya nchi. Lakini utamwambiaje Rais mwenzako hivyo? Wananchi - wapendwa wake watamchukuliaje Rais wao, familia na marafiki zake? Hakika ninapenda kusikiliza hotuba hizi ila nikifika hapo huwa inaniuma sana.*

Maoni haya yanadhihirisha kwamba katika maeneo aliyoyataja maovu yaliyotendwa na akawaweka bayana watendaji wa maovu hayo ni kwamba ingawa watu huzisoma au kuzisikiliza hotuba zake lakini huvunjika moyo kwa matamshi yaliyogusa moja kwa moja. Penginepo mneni angetumia lugha ya mafumbo, ujumbe wake ungepokelewa na wengi zaidi; na kwa furaha - hasa inapokuwa ameyagusia mambo ambayo yana halisika katika jamii yao.

**MW 4:** *Hotuba hizi ni kioo cha jamii piga ua, wachukie ama wasichukie - wale walioguswa; lakini Nyerere alikuwa ni mkweli na mzalendo. Alikuwa anaongea kwa mashiko hata anayemchukia au kuzichukia hotuba zake anafanya hivyo tu lakini nafsi yake lazima inamsuta. Nina hakika hotuba zake ni marejeleo mazuri kwa kila Mtanzania wa leo na wa baadaye.*

Maoni haya yalitokana na matamshi ya Mwalimu katika hotuba yake ya "N" pale aliposema: *"... Watu wazima wameuzungumza Muungano, kwamba tuuvunje au uendelee. Ilikuwa ipo hatari ya kuvunjika na wala haijaisha…; mtu mwenye akili hawezi kufikiri Uzanzibari ni ufahari: hana akili. Hawezi akautukuza Uzanzibari kwa kujiita 'sisi Wazanzibari' na 'wao Watanganyika…; Zanzibar wanaweza wakajitenga hivi kwa ujinga, kwa ulevi, lakini kwa ujinga, hasa kwa viongozi wao…*". Mpwito wa matamshi ya namna hiyo ndiyo yaliyonekana kuwaudhi watu hasa alivyo wataja kieneo jambo ambalo linawapelekea walengwa kujulikana kwa majina. Ingawa hivyo, inathibitika kwamba Mwalimu alikuwa ni mkweli na asiyependa kuchelea jambo ambalo linahatari kwa jamii. Ukweli huu unapata mashiko zaidi kwa kuirejelea historia ya tangu alipolizungumzia swala hilo (la Muungano); ambapo leo yake mjadala ungali unafukuta katika vinywa vya watu wengi; ikiwemo mijadala ya bunge kuhusu katiba mpya ya Tanzania; lakini pia ubainifu wa Watanzania waliojitokeza wazi wazi kuupinga Muungano huo na kwa hivyo kuendelea kuthibitisha makemeo ya Mwalimu Nyerere kupitia hotuba yake ya 'N'. Ingawa kauli hizo zinaonekana kuwagusa baadhi ya Watanzania moja kwa moja lakini ni ukweli unaohalisika katika jamii ya Watanzania. Ndiyo

maana zina rejelewa na kujadiliwa na wengi kila uchao. Hii ndiyo kusema hotuba zake zina ufaafu mkubwa kwa Watanzania wa leo na pengine wa badaye.

**MW 5:** *Hotuba ilikuwa nzuri sana. Hii ni kutokana na kwamba hakuwa akizungumza kibubusa; alikuwa ni mfasaha wa lugha na huku akitumia ushahidi kwa anayoyaeleza.*

Maoni haya yalibainisha kwamba mneni akitumia ushahidi anaaminiwa zaidi na wasikilizaji au wasomaji wake. Kwa hivyo, hupelekea kupendwa na kusikilizwa zaidi kwa kila atakalokuwa akiwaeleza. Kwa mnasaba huo, Ethosi kama mhimili wa Nadharia ya Balagha iliyotumiwa katika utafiti huu imesawiri ufaafu wake katika taaluma ya Uchanganuzi Usemi. Hivyo, wito kwa mneni yeyote ikiwa angependa ujumbe wake upokelewe na hadhira yake kwa mahaba, ajifunze na kuielewa barabara mihimili ya Nadharia hii ya Balagha.

**MW 6:** *Hotuba ilinitia mshawasha wa kuyatathmini matendo yangu ya kila siku. Hakika kuna umuhimu wa kumweka Mwenyezi Mungu mbele kwa kila jambo.*

Maoni haya yalitolewa kutokana na matamshi ya Mwalimu Nyerere pale alipokemea suala la ubaguzi, ambapo ilibainika kwamba kuwatenga wengine kieneo au kwa rangi zao au vinginevyo - ni katika madhambi makubwa. Madhara yake huanzia hapa hapa duniani kutokana na chuki na hata kupelekea vita. Maonyo hayo, huthibitisha kwamba hotuba za Mwalimu zenye makemevu zinauzingatifu mkubwa kwa Watanzania. Pengine ni kutokana na ufasaha wa lugha na mbinu anuai alizokuwa akizitumia ama mazoea yake ya kuongea mambo kwa ushahidi ambayo yanawapelekea wengi kumpenda na kumzingatia kwa kila alilolionya au kuwaelekeza Watanzania ama jamii ya dunia kwa ujumla. Kwa hivyo, ingawa wengine wanaudhika kwa baadhi ya matamshi yaliyomo katika hotuba zake, lakini nafsi zao huwarudi na ikawa ni wajirekebishe kwa ajili ya kuleta utangamano mzuri kijamii.

***MW 7*** *"Ubaba" sio msahafu, ndiyo iwe kila uchao kurejelewa kama mwongozo wa maisha! Na ikiwa hivyo basi ni Baba wa CCM.*

Baadhi ya wasailiwa waliojidhihirisha kama wapinzani dhidi ya chama alichokiongoza Mwalimu hadi mauko yake C C M walidai kwamba ingawa hupenda kusikiliza au kuzisoma hotuba lakini hukereka sana pale Mwalimu aliposema: "Kiongozi safi hawezi kutoka nje ya C C M ambapo ufahima wake si tu kwamba ni kuwadhalilisha wanachama wa vyama vya upinzani lakini pia ni njama za kuzififisha nguvu za wapinzani kisiasa. Ingawa hivyo, wasailiwa hawa pia walidai kwamba huyaona matamshi ya Mwalimu kana kwamba yanakosa mizania kwa watu wenye tafakuri ya kina. Kwamba, mbali na kuwakweza wafuasi wake

(wana C C M) kama malaika, Mwalimu anajiweka kizimbani pale anaposikika akiwaonya wafuasi wake kwa kusema: "***Hiki siyo kipindi tena cha mizengwe***" jambo ambalo linamaanisha kwamba katika maongozi yake walikuwa wakifanya mizengwe (udanganyifu) katika maswala ya uchaguzi ili kupata ushindi dhidi ya wengine. Ndiposa kwa tathmini ikawa ni watanabahi kwamba, kutokana na mvuvumko wa vyama vya upinzani wasingeweza kuiendeleza mizengwe yao (kujipatia ushindi kwa njia isiyokuwa ya halali). Na kwa hivyo, ukinzani wa matamshi haya unatoa mashiko ya kumvua Mwalimu joho la uadilifu katika mambo ya kisiasa kwa raia aliokuwa anawaongoza. Na pengine sifa ya kuitwa Baba wa Taifa; inaonekana kana kwamba ni kiini macho cha kuvikwa kilemba cha ukoka katika mazingira yasiyoadilifu.

***MW 8*** *"Hotuba za Mwalimu ni dira ya maongozi mema kwa Watanzania wa leo na wa baadaye. Shime kwa taasisi zenye kushika hatamu ya kuzihifadhi na kuzitangaza ili Watanzania wote wapate kujua wasifu wa Baba wa Taifa."*

Haya ni maoni yaliyotolewa na wasailiwa hasa baada ya kuzisikiliza hotuba za 'TTT' na 'N'; ambapo Mwalimu alizungumzia Muungano, umuhimu wa Sheria, Rushwa, Uongozi bora, ufaafu wa Azimio la Arusha na kadhalika. Maudhui ambayo yangali yana mashiko hadi hivi leo katika mazingira ya Watanzania.

***MW 9*** *"Ingawa watu wanaliona Azimio la Arusha kwamba limepitwa na wakati lakini kuna mambo ambayo hadi hivi leo yana mashiko. Mwalimu alikuwa ni mtetezi wa wanyonge. Kwa hakika tutamkumbuka daima milele."*

Kauli hizi fahiwa yake ni kwamba, wasailiwa walizibaini baada ya tafakuri ya jinsi ambavyo baadhi ya Watanzania walivyokuwa wakiwalaghai Watanzania wenzao ya kwamba Azimio la Arusha limepitwa na wakati ilhali misingi yake ingali ni faafu katika uhalisia wa maisha ya Mtanzania. Mintaarafu yake ni pale Watanzania walipokuwa wakihimizwa wajitambue kwamba taifa lao ni la mbeya mbili: Wakulima na Wafanyakazi. Ndiposa chini ya misingi ya Azimio la Arusha wengine kwa matakwa yao binafsi wakiwashawishi wengine wasiliridhie ili wapate kupenyeza matakwa yao kwa urahisi. Bila kuwachelea, ndiposa Mwalimu akiwauliza Watanzania ikiwa taifa lao sio la Wakulima ama la Wafanyakazi tena ?

Maoni hayo ni uamsho kwa Watanzania kumaanisha kwamba mawazo ya wale wanaopinga Azimio la Arusha yanahitaji kufanyiwa tafakuri kabla ya maamuzi; na kwamba kila mmoja

anahitajiwa awe tayari kupambana na maovu kadiri ya uwezo wake ili kuyahami maisha yake na jamii kwa ujumla.

***MW 10*** *"Mwalimu angerudi duniani pangechimbika"*

Haya ni maoni yaliyotolewa na wasailiwa baada ya kuzirejelea kauli za Mwalimu Nyerere pale aliposema: " *Sasa, sera hii itazaa mamilionea Tanzania sasa hivi na sio baadaye, lakini watakuwa mamilionea watano. Hata hivyo, wakati huo huo, pia itazaa masikini na Tanzania itakuwa na masikini wengi sana* ". (UK 22:1, TTT); wakimaanisha kwamba enzi za uongozi wa Mwalimu; (Mwalimu) - walipambana vikali na wahujumu uchumi kwa namna nyingi (Hasa wale waliokuwa wakiwaghilibu Watanzania ili wapate kuuhodhi uchumi wa Tanzania kwa faida yao wenyewe.) wakati ambapo leo yake ni kana kwamba jitihada zake zimeruka patupu. Kwa hivyo mpwito wa maoni haya ni kudhihirisha kwamba hadi hivi leo wamo Watanzania wanaozingatia maudhui yaliyomo katika hotuba za Mwalimu Nyerere kiasi cha kuyahawilisha maudhui hayo na maisha yao ya kila siku. Ingawa pia kuna mtawalio wa taswira ya madhaifu katika asasi mbalimbali za kijamii Ndiposa Watanzania wakihisi kwamba, kama Mwalimu Nyerere angelikuwepo duniani, yanayotendeka yasingetendeka kamwe. Kumaanisha kwamba, viongozi waliomo madarakani hivi leo wana jukumu la kuyasimamia mawazo ya Mwalimu Nyerere kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

***MW 11*** *"Tumeingia katika mfumo wa vyama vingi kwa bahati nasibu"***.**

Hayo yalikuwa ni maoni ya wasailiwa waliyoyafafanua kwa kusema kwamba; "kufikia miaka ya tisini wananchi wengi wa Tanzania walikuwa wameukinai mfumo wa chama kimoja. Hamkani hii ilitokana na kile kilichoaminiwa na baadhi ya Watanzania kwamba maongozi ya muda mrefu ni ishara ya uongozi wa kiimla. Kwa madai kwamba wananchi wengi hawakupata fursa ya kutosha kutoa ushauri wao kwa chama ama kwa serikali yao. Kilichosemwa na Baba wa Taifa hakuna aliyethubutu kukipinga. Mwalimu alirejelewa kama kiongozi mwenye fikra sahihi kuliko wengine hata alifikia kunukuliwa kwa maneno: "*Zidumu fikra sahihi za Mwalimu J.K. Nyerere", "Nyerere juu juu juu kabisa jeuri ya Chama" na kadhalika.* Jambo ambalo lilileta tafrani kwa wengine; ambapo mbali na kuzinyanyua sauti zao. Mataifa fadhili nayo yalishajiisha nchi za ulimwengu wa tatu zihakikishe kwamba zinaingia katika mfumo wa vyama vingi.

Mhemko wa maoni hayo (ya wasailiwa) ulitokana na wasailiwa baada ya kurejelea hotuba ya Mwalimu katika kauli: "*Naitwa Mkumbwa Ali kutoka Daily News. Mwalimu pamoja na*

*kwamba umesema hutaki kuongelea watu lakini huko nyuma katika mkutano wako na sisi umewahi kusema kwamba mpinzani imara wa kisiasa hapa nchini lazima atoke ndani ya CCM kwa sababu vyama vya upinzani ni vibovu kama ulivyozungumzia leo. Nafikiri kujiengua kwa mrema kunajibu swali lako hili la muda mrefu."* Kwa uoni wa wasailiwa - walichukulia kauli hiyo kama uthibitisho wa kwamba Mwalimu alikuwa akikifagilia chama CCM na kusahau kwamba yeye ni Baba wa Watanzania wote. Na ni ubainifu wa kwamba Mwanadamu siyo kamili (ana madhaifu) si rahisi kwa mwanadamu kutenda kila jambo likawa ni sahihi kwa wakati wote na ama akamfurahisha kila mtu kwa matakwa yake.

***MW 12*** *"Kamwe hatutapata maendeleo yenye ushindani katika midani za kimataifa ikiwa CCM itaendeleza ukinzani dhidi ya vyama vya upinzani".*

Hayo yalikuwa ni maoni waliyoyatoa wasailiwa baada ya kuirejelea kauli ya Mwalimu: *"Nimeshauri tuache mizengwe ... huyu mtu mzima aliyeniambia hivyo, mkubwa kabisa, anamsema "sera yetu ni siri bwana maana tukieleza watatupiku". Hii sera ya siri imekuwa jando? Sasa viongozi wa CCM wananiambia wanataka wagombea wao wawe siri Ah! Wawe siri mpaka lini? "* Ingawa hivyo, kauli hii ni funzo kwa waneni kuchukuwa tahadhari kwa kila wanalolizungumza mbele ya hadhira zao ambapo ufafanuzi wa wasailiwa ulitia hofu kwamba, ikiwa Watanzania hawatamakinika katika kuzichuja kauli mithili ya hizi zilizomo katika hotuba za Mwalimu Nyerere, itakuwa ni muhali kwa chama pinzani kushika hatamu za kuiongoza serikali ya Tanzania hasa ikisadifiwa kwamba wengi wa Watanzania huzichukulia hotuba za Mwalimu kama dira ya maongozi ya nchi yao.

***MW 13*** *"Hotuba ya Mwalimu kuhusu Ikulu ni mfano wa ukinaifu wa wananchi dhidi ya chama kimoja. Kauli: "Wananchi, mimi nimekaa Ikulu pale muda mrefu kuliko mtu mwingine yeyote ... mimi naijua Ikulu, kwa mtu mwaninifu kabisa kabisa Ikulu ni mzigo hupakimbilii, si mahali pakukimbilia hata kidogo, huwezi kupakimbilia Ikulu. Unakimbilia kwenda kutafuta nini? .. Ni mzigo, ni mgogoro ni mzigo mkubwa kabisa ... watu safi hawapakimbilii. Ukiona mtu anapakimbilia na hasa anapokimbilia na vipesa anatumia tumia kwenda Ikulu, huyo ni mtu wa kuogopwa kama ukoma, hafai.... kwanza hizo fedha kazipata wapi? Mtanzania wa leo, hawezi kununua watu bila yeye kwanza kununuliwa, kama hajanunuliwa, kazipata wapi? Na kama kanunuliwa, anataka kuzilipaje" Kama kakopa atarudishaje? Ikulu pana biashara gani mtu akope mamilioni halafu aende alipe!*

Hapa Mwalimu anawachota wananchi fikra kiasi cha kuamini kwamba mwerevu au mjinga anatokana na uanachama wa mtu kwa chama chake ambapo anayefuata fikra za Mwalim -

kupitia chama CCM anaonekana ni mwerevu. Hivyo, Mwalimu anaonyesha kujivua gamba kwa kuzikonga nyoyo za raia kuhusu fikira za mabadiliko ya chama na maongozi ya nchi.

***MW 14*** *"Kwa nini Mwalimu Nyerere anafanywa Mungu mtu kwa aliyoyazungumza enzi za uhai wake? Kuna haja ya Watanzania kuzisoma alama za nyakati vinginevyo hatma yake itakuwa ni mgalagazo usiokuwa na tiba mbadala*"

Maoni haya yanatokana na kauli: *"Tanzania imetikiswa. ... tumetikiswa na nyufa tumeziona. Nyingine katika paa, nyingine katika dari, nyingine kutani na nyingine katika msingi. ... Nyufa tano ninazo ziona: ufa wa kwanza ni Muungano, wa pili ni wa kutojali Katiba, wa tatu wa kuendesha mambo bila kujali Sheria, wanne ni Rushwa, wa tano ni wa Ukabila na Udini. ... "Nataka mjue hivyo, nje ya Muungano, hakuna sisi Wazanzibar wao watangayika, hakuna wao Wapemba sisi Waunguja ... Dhambi ya ubaguzi haifi, inaendelea, dhambi ya ubaguzi ukishakuitenda ni sawasawa na kula nyama ya mtu, ukila nyama ya mtu utaendelea kuila".*

Chagizo za wasailiwa ni kwamba, kauli hizo zilijiri kipindi kilichoingiwa na mgalagazo wa fikra kuhusu Muungano wa Tanzania Bara na Visiwani**.** Miongoni mwa wataka mabadiliko ni pamoja na wale waliofukuzwa katika chama C C M baada ya kuonekana kwamba hawaungi mkono fikra za Mwalimu kuhusu Muungano. Kwa hivyo, hawakupata fursa ya kuzisemea kero zao zaidi ya kujitweza katika vyama vingine kama njia badali ya kuzitolea dukuduku zao - kwa kile walichokiita haki sawa kwa wote katika maendeleo ya nchi.

Wakadhalka fahiwa za wasailiwa kuhusu kauli hizi za Mwalimu Nyerere walidai kwamba, zinakonga nyoyo za watu kiasi cha kuwatonesha madonda waliyonayo kuhusu sera za chama tawala C C M. Semi hizi zinabainisha ukweli kwamba wengi hawakuridhika na itikadi ya chama kimoja. Wananchi hawakupata fursa ya kuikosoa serikali yao. Uongozi ulionekana ni wa kibabe ume. Wananchi hawakuwa na chombo badalia ambacho kingeweza kupokea kero zao za kuishauri serikali. Hivyo, uwepo wa vyama vingi kwa wananchi ni kama ukombozi kwa mtu binafisi na kwa taifa zima kwa ujumla.

***MW 15*** "*Mbali na kwamba Mwalimu alikuwa ni mzoefu na mweledi katika ulingo wa siasa lakini matamshi yake pia yanadhihirisha kwamba alikuwa ni muumini kindakindaki - na hapo ndipo anapotukoga; unamkubali bila kupinga; ushawishi wake unakonga kotekote: kisiasa na kiimani. Hata kama mtu ni jeuri vipi utapitia wapi? Itabidi ujirudi; ima kisiasa au kwa Mola wako. Na hapa kusema la kweli Mwalimu alifaulu. Ndio maana hadi hivi leo angali katika*

*vinywa vya Watanzania; anazingatiwa kwa maongozi yake. hata kwa wale ambao mara nyingi aliwakemea wanamkubali. Mungu akulipe kwa uliyoyafanya, ulale mahala pema! "*

Hizi ni hisia za wasailiwa waliporejelea matamshi ya Mwalimu pale aliposema: "… *Linalotupasa kufanya ni kuamka. Tumelala muda mrefu mno na kusingizia kwa muda mrefu kwamba shida zetu ni amri ya Mungu. Mungu hakutupa ubongo wa kutumia? Mungu hakutupa mikono na viganja? Mungu hakutupa ardhi? Tukitumia vitu hivyo tumaweza kubadili umasikini wetu, tunaweza kuleta maji mahala tunapopenda. Tunaweza kuifanya ardhi ikatoa mahindi zaidi, mpunga zaidi, pamba, karanga, maharage zaidi kwa kila eka. Jambo hili ni juu yetu sisi wenyewe*" (UK 3:3, SU) **a**mbapo imebainika kwamba mbali na umaarufu wake kisiasa. Lakini alikuwa akiwahofisha Watanzania wasiyatende mabaya kwa minajili ya kuifanya jamii iwe kitu kimoja; ishirikiane katika kuinua uchumi na siasa ya nchi.

***MW 16*** *" Kwa nini yakitajwa madhaifu ya Mwalimu Nyerere wengine hususan wafuasi wa chama chake CCM – huhisi ya kana kwamba amedhalilishwa na ama kavunjiwa heshima ? Vyombo vya habari navyo hususan TBC hudakia kwa kuzirusha hewani hotuba zake zenye mwegemo wa maudhui ya Amani, upendo ubaguzi umoja; yote hayo kwa mwenye kufatilia ni kuonyesha kwamba Mwalimu anaonewa, hatendewi haki kwa wema wake alioufanya enzi za maongozi yake ! Aka! Kwa ni yeye alikuwa Mungu? Hakuna mwanadamu kamili; ni vyea watu wakaelewa na ndivyo hivyo kwamba kama mwanadamu kuna mazuri na mabaya aliyoyatenda katika mpwito wa maisha yake; ama kwa kuwakosea wanadamu wenzake na ama akatubia au la; ambapo hilo ni suala lingine lenye misingi yake kiimani. Na kwa hivyo chembelecho ukwezwaji wa Mwalimu kufanywa Mungu mtu ni kumkufuru Mwenyezi Mungu lakini pia ni kujiogesha kifikra".*

Hizi ni kauli za wasailwa kwa kumbukizi ya kauli ya Mwalimu kwamba; *wamekaa huko Zanzibar na kulikataa Azimio la Arusha'* ambapo ufahima wa wasailiwa ilikuwa ni Watanzania watambue kwamba kulikuwa kuna mambo ambayo Mwalimu alikuwa akiyakosea na ndipo mara alipokuwa ameachia ngazi; wale waliokuwa wakikereka kwa maongozi yake – ikawa ni wamfunze kwamba walikuwa hawapendezwi kwa alivyokuwa akiyasisisitiza hususani kuhusu mfamo wa Azimio la Arusha. Lakini pia kumdhihrishia ya kwamba alikuwa hatoi fursa kwa wengine kutoa mawazo yao katika maongozi ya nchi jambo ambalo pia lilikuwa ni kosa kwa mtu mmoja kuonekana mawazo yake ndiyo mwafaka kwa kila jambo la kijami. Hivyo, udhihirishwaji wa matendo hayo mara tu baada ya kung'atuka kwake; ilikuwa ni kauli neni ya moja kwa moja kwamba kuna mengi aliyokuwa akiendesha

kombo lakini wananchi na ama viongozi wengine walikuwa hawapati fursa ya kujieleza au kutoa dukuduku zao.

***MW 17 "****Mwalimu Nyerere angerudi hivi leo duniani; kwa wanaomfagilia ya kwamba sera zake zingali ni maongozi ya nchi hadi hivi leo - angewaona wamepitwa na wakati na wameshindwa kuzisoma alama za nyakati katika ulimwengu wa leo"*

Hizi ni kauli za wasailiwa walipoukumbukia usemi wa Mwalimu aliposema: "*Nashangaa wananiambia eti rais wetu ni siri*" kumaanisha kwamba Mwalimu alikwisha washangaa Watanzania ambao hawapendi mabadiliko. Huu ulikuwa ni uoni wa Mwalimu kuhusu watu wasiojifunza kutokana na makosa wanayoyetenda - na ikawa madhara yake ni kwajamii nzima. Mtagusano wa kauli ya wasailiwa na unukuzi wa usemi wa Mwalimu ni msisitizo wa Watanzania kutokubali kuongozwa kibubusa. Kila mtu anahaki ya kutoa mawazo yake na wengine pia wanayo haki ya kuyakubali au kuya kataa kwa kuangalia manufaa yake kwa jamii na kwa taifa zima kwa ujumla. Na hii ndiyo kusema kwamba yapo mambo aliyoyahimiza yatendwe au kuyakataza yasitendwe enzi za maongozi yake lakini kadiri siku zinavyosonga mbele na ikawa kuna mema yakuigwa kutokana na mabadiliko yaliyomo duniani hususan katika uwanja wa teknomaarifa; ipo haja ya watu kuyakubali mabadiliko kwa ajili ya kufanikisha maendeleo na sio kwa kuendekeza ukale.

***MW 18*** *"Hakika hotuba zake zina mafunzo mengi. Kama siyo vigumu kwa wasiomwamini Mungu kukubali kosa, Nyufa anazozitaja Mwalimu chanzo chake ni maongozi yake; na yakumbuke maasi ya Mutinyi, changamoto alizokumbana nazo kuhusu muungano tangu kuuanzisha kwake na mfungamano wa sera za nchi ndani ya mfumo wa ujamaa na kujitegemea. Kwa tabia za viongozi walio wengi ya kupenda madaraka, si dhana kana kwamba aliacha eti kwa kupenda kwake! Bilashaka alikuwa mjanja lakini mwepesi wa kuzisoma alama za nyakati mapema".*

Haya ni maoni ya wasailiwa baada ya kuikumbukia kauli ya Mwalimu pale alipokuwa akiwaasa Watanzania kwa kusema kwamba "*hakuwa mkorofi ingawa wengine walifurahia kung'atuka*". Kumaanisha kwamba kulikuwa na mengi yaliyokuwa yamewakifu Watanzania kutokana na maongozi yake kiasi cha hata kutamani lini angeachia ngazi. Huu ulikuwa ni mtagusano wa fikra. Ilitegemewa na wengi kwamba Mwalimu angeachia ngazi pasi na lawama kutoka kwa mtu yeyote hasa kwa jitihada zake za kupigania uhuru, Muungano na maongozi ya zaidi ya miongo miwili; lakini ikawa ni Watanzania wagawanyike makundi mawili: wanaotamani aendelee kuliongoza Taifa hadi mauko yake na waliofurahia

kung'atuka kwake. Ingawa hivyo, ubainifu wake ni kwamba, kiongozi akiwa muadilifu wasiopenda haki huwa hawapendi maongozi yake. Hivyo, faukaya kwamba Mwalimu alikuwa akiwahimiza watu kuhusu amani na umoja; wenye matakwa binafsi daima wangeona kero hasa inaposadifu kwamba moja ya mbinu mwafaka kwao ni watu watengani ili wapate mwanya wa kuyafanikisha madhila yao. na kwa hivyo, ingawa mkamilifu ni Mwenyezi Mungu. Watanzania watamkumbuka Mwalimu kwa jitihada zake kuhusu amani na umoja.

### 4.7 Mpangilio wa Hotuba za Mwalimu Nyerere

Aristotle anahimiza mpangilio wa hotuba uzingatiwe: Utangulizi wake (jinsi ambavyo mzungumzaji alivyoanza hotuba au usemi wake kwa hadhira); Mwili wa usemi huo (jinsi mzungumzaji alivyojenga na kuendeleza hoja zake) na jinsi alivyohitimisha usemi wake.

#### 4.7.1 Utangulizi wa Hotuba za Mwalimu Nyerere

Kwa kurejelea hotuba za Mwalimu Nyerere, Mintaarafu Nyufa na Tunatoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi; vyanzo vya hotuba zake ni vya kiudondoshi kutoka katika anuani jumuishi. Mwalimu alikuwa ni mweledi wa kuipa hadhira yake mwangwi wa kifani wenye kuhitaji ufafanuzi wa kitakachojitokeza katika hotuba zake hatua kwa hatua. Utumizi wa mbinu hii daima huifanya hadhira iwe makinifu kwa kinachozungumzwa. Kwa mfano, hotuba yake ya "***Nyufa***" na "***Tumetoka wapi***" ni miongoni mwa hotuba zinazotoa mshawasha wakutaka kujua hatma ya hoja zilizoibuliwa. Mwalimu anaposema "***Nyufa***", "***Tanzania imetikiswa***" au "***Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi***" haya ni matumizi ya maneno machache, mafupi na yaliyosheheni mbinu za kifani zenye kuzikonga nyoyo za hadhira kiasi cha kuwatumbukiza katika lindi la kibalagha. Katika hotuba ya "***Nyufa***" mazazi yake yanatoka katika maneno "***Tanzania imetikiswa***" dhana ambayo inachimuza nyufa, na ndiyo akazibaini nyufa hizo moja baada ya nyingine kama zifuatazo:

Ufa wa muungano uk. 9

Ufa wa kutojali Katiba uk. 12

Ufa wa kuendesha mambo bila kujali sheria uk. 14

Ufa wa rushwa uk. 15 na kisha

Ufa wa ukabila na udini uk. 22

Vivyo hivyo katika hotuba ya "Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi", Mwalimu amedondoa hoja mahsusi kuu tatu kutoka katika anuani hiyo ya kijumla, ambazo ni:

Tumetoka wapi,

Tuko wapi na

Tunakwenda wapi.

### 4.7.2 Uendelezaji wa Hotuba za Mwalimu Nyerere

Daima Mwalimu huonekana ni mwenye kujiamini. Hili hudhihirika pale anapozifafanua hoja zake kwa mifano na kwa mbinu za kifani hususani balagha, tashhisi, takiriri, na tafsida kengeushi. Hali hii huijengea hadhira yake imani kwa anachokizungumzia. Kwa mfano, katika hotuba ya Nyufa uk 17 ameonyesha msimamo aliokuwa nao enzi za uongozi wake katika kukemea maovu. Alimrejelea Mgiriki (Mdiplomsia) mmoja aliyeidharau Tanzania alisema: Mgiriki mmoja alipitapita akijitapa humu …eti serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwake? … ana mfuko mpana kiasi gani? (Maneno yenye alama ya '?' yanadhihirisha mbinu ya balagha) Lakini pia kwa kuushajihisha ushupavu wake alitumia tafsida kengeushi kwa kusema: "…. huyu mtu ni mshenzi …. sasa Tanzania inanuka". Ufahima wa mtafiti ni kwamba, muamala wa matumizi haya ya balagha na tafsida kengeushi aliyotumia Mwalimu ni kuoyesha uzalendo wa hali na mali kwa jamii yake.

Fauka ya hayo, katika kila nyufa aliyoitaja Mwalimu ameisheheni mbinu ya balagha na tashhisi kumaanisha kwamba kila analolieleza ni kero na kwamba watu wanapaswa wawashangae wale wote wanaoendeleza kero hizo. Mwalimu anautanabaisha umma kwamba hadi hivi leo kuna watu wasiojua thamani ya kuwa na umoja: Kwa mfano: Katika ufa wa kwanza - Muungano, ametumia maneno: ***Lo! … Wazanzibari hawa wamefanyaje?... Wanakwenda zao wenzetu!*** … Na kadhalika. Katika ufa wa pili – kutojali katiba, ametumia maneno: ***ataapa!*** … ***Tutakuapisha...*** Katika ufa wa tatu – kuendesha mambo bila kujali sheria, ametumia maneno… ***atamwambia nini!*** Katika ufa wa nne – Rushwa, ametumia maneno: … ***Siyo!*** Katika ufa wa tano – ukabila na udini, ametumia maneno: ***Ah! Jamaa ni mkara! … Mnabagua watu kwa rangi kiasi hiki! Lo! Tunakwenda wapi! Ukabila na ukaburu... nchi yetu haina dini … astakafulahi!*** Katika hotuba ya ***"Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi***" katika Uk. 13-15 ametoa mfano kwa kuitaja Uingereza na India kwa nia ya kuonyesha kuwa tuna hitaji mwendo kasi katika maendeleo ya viwanda. Ametumia balagha kwa kusema … ***tumejitawala sasa - tuendelee kuuza pamba ghafi nje? Hivi Viingereza tunaviachia?***

### 4.7.3 Hitimisho la Hotuba za Mwalimu Nyerere

Mara nyingi Mwalimu ameonekana kutakriri anuani ya hoja aliyoibua na kuiendeleza. Hii ni mbinu ya balagha na takriri kwa maana ya kujenga kumbukumbu. Mwalimu katika uwasilishaji wa hotuba zake alikuwa akiichukuwa taswira ya Mwalimu na Mwanafunzi kwa somo linaloendelea darasani. Kwa mfano anasema: Katika ufa wa kwanza - Muungano, uk. 12 ***…nimesema tuna ufa wa Muungano***. ***Ufa wa kwanza kabisa***. Katika ufa wa pili wa

kutojali Katiba Uk. 14 anasema: "***Tumeona ufa huo wa kutojali Katiba ya nchi***" Katika ufa wa tatu wa kuendesha mambo bila kujali sheria uk. 15 anasema: "***…hatuwezi kuendesha mambo bila kujali Sheria***" Katika ufa wa nne wa Rushwa uk. 22 anasema: "***Sasa tunamtaka Rais anayekerwa na hilo…(rushwa).***" Katika ufa wa tano wa Ukabila na Udini uk. 30 anasema: "***… sasa yapo hayo … mambo ni mengi lakini kwa sasa ni hayo!***" Wakati ambapo Katika hotuba ya "***Tunatoka wapi, …***" amemalizia kwa taswira ya kuwakumbusha aliyoyazungumza na kwa mifano kama ishara ya ukolezo wa hotuba yake. Anasema: "***Sasa mfano mmoja nautumia mwisho kabisa...***"

### 4.8 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulibaini kwamba hotuba za Mwalimu Nyerere zilikuwa na maudhui mahsusi ambayo hadi hivi leo yangali ni muhimu kuzingatiwa na Watanzania wapenda amani na umoja. Hii ni kwa ugunduzi kwamba maudhui aliyokuwa ameyaendeleza yanaisawiri jamii ya Watanzania takriban katika kila nyanja ya maisha yao. Kwa mfano maswala ya Muungano, Rushwa, Ukabaila na Udini yangali yanavikuna vichwa vya wengi na jamii isijue nini hatima yake. Kwa hivyo, matokeo haya yanakidhi matakwa ya nadharia tete ya kwanza katika utafiti huu. Wakadhalika ilibainika kwamba Mwalimu alitumia mitindo (mbinu) ya kibalagha yenye ushawishi mkubwa kwa hadhira na hivyo kubaini kwamba matumizi mazuri ya lugha yaliyomo katika hotuba zake (Mwalimu Nyerere) ni natija toshelezi katika kukidhi hitajio la nadharia tete ya pili na ya tatu. Fauka ya hayo, ubainifu wa matokeo haya umedhihirisha ufaafu wa mihimili ya nadharia ya Balagha iliyoongoza utafiti huu; ambapo kwa kuzingatia:

(a) **Ethosi**: ambayo Aristotle anatoa ufahima kwamba wapo wazungumzaji wenye sifa na tabia zinazowapelekea kuheshimiwa na kuenziwa kabla na baada ya usemi wao kwa hadhira. Na kwa hivyo kuhimiza wachanganuzi usemi kubaini: Uwezo wa jambo analolizungumzia mneni, namna anavyolichukulia suala analolizungumzia na ubinadamu alionao mneni kwa hadhira yake. Hivyo, Ethosi ilimwezesha mtafiti kubaini hulka (tabia) aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere, ambapo Watanzania wa leo wangali wanashawishika naye kupitia katika hotuba zake. Mshawishiko ambao unadhihirisha mwangwi wa maongozi mema aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere enzi za uhai wake. Kwa hivyo, mwangwi huo unakuwa ni dira njema kwa Watanzania wa leo na wa vizazi vijavyo. [Takriban hotuba zake zinasawiri kwamba daima alikuwa ni mwenye kudumisha umoja, amani, upendo na mshikamano]

(b) **Logosi**: ambayo Aristotle anahimiza mchunguzi azingatie vile ambavyo mzungumzi alivyoibua hoja au maswali yenye kumpa msikilizaji kutafakari badala ya kujibu (mbinu ya kuuliza maswali isiyohitaji majibu); Kupitia mhimili huu, mtafiti aliweza kubaini kwamba, Mwalimu Nyerere alikuwa akitumia lugha kistadi; ambapo kwa zaidi mtindo wa balagha ulitia fora katika kuwashawishi Watanzania watafakari na wakubaliane naye (Mwalimu) katika maudhui aliyokuwa akiyaendeleza. [Mwalimu alikuwa na kipaji cha hali ya juu katika ulingo wa uneni – kisiasa; alikuwa mfasaha na mmakinifu katika kujenga hoja; lakini mwenye hoja zenye kuleta tafakuri kwa jamii]

(c) **Pathosi**: ambayo Arisitotle anahimiza mchunguzi atathmini hisia za wapokeaji usemi kulingana na uzito wa hoja zilizomo katika usemi huo. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kubaini hisia na maoni ya wasailiwa kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere na kubainika kwamba hadi hivi leo Watanzania wangali wakizitafakari na kuzifurahia hotuba za Mwalimu kiasi cha kuzichukulia kama dira ya maongozi yao na kwa hivyo mhimili huu unasadifu natija ya nadharia tete ya tatu.

Wakadhalka ilibainika kwamba:

(i) Hotuba nyingi za Mwalimu alizitoa katika miaka ya 60 na 70; na sio 80 na 90. [Rejelea kiambatisho “C”]. Pengine hii ni kutokana na kwamba ndicho kipindi ambacho alitoa maamuzi ya kung’atuka; na kwa hivyo, ikawa hapati fursa za kuzizungumzia sera zake kama alivyokuwa madarakani. Ingawa hivyo, kuna ufahima kwamba, hotuba za miaka ya 80 na 90 ni muhtasari wa maongozi yake kutokana na hotuba zilizohusishwa katika uchanganuzi huu.

(ii) Hotuba zaidi ya moja inaweza kuchangia maudhui ya aina fulani na kwa hivyo kuleta mashiko zaidi kwa wasomaji au wasikilizaji.

(iii) Miongoni mwa wasailiwa waliweza kutoa mawazo tofauti tofauti, wengine walidai kwamba hotuba fulani ni nzuri sana na wengine wakionesha kutokufurahishwa kwazo. Hii ni kwa sababu hotuba moja iliweza kuzua mitazamo tofautu tofauti; na maana ya maudhui na mbinu zilizotumika kuweza kutambulika na wasikilizaji au wasomaji kwa namna tofauti tofauti. Kwa hivyo, kuleta mvuto kwa watu kuendelea kuzipenda kuzisikiliza au kuzisoma hotuba hizo kwa kina.

(iv) Hotuba alizozitoa mara baada ya kung'atuka kwake ziliwashawishi wasailiwa wengi kiasi cha kutamani kuzirudia tena na tena hali hii ilithibitisha bunio lililopelekea kuchanganuliwa kwa hotuba hizi ya kwamba ilikuwa ni kutaka

kubaini ikiwa kuna ushawishi wowote uliopo katika hotuba hizi hata kufikia kupewa ukipaumbele wa kurushwa hewani kupitia redio ya Taifa (T B C)

(v) Ilibainika kwamba mbali na redio ya taifa kuwa na utaratibu maalumu lakini vyombo vingine mbalimbali vinatumika pia kusifu na kuzirusha hotuba zake hasa katika kipindi cha maadhimisho ya kuzaliwa kwake na mauko yake. Lakini pia katika siku za sikukuu au ikiwa kuna matukio maalum kama ilivyokuwa katika kujadili mswada wa katiba mpya nchini Tanzania au maswala ya uchaguzi ambapo hotuba zake zilihusishwa pakubwa kama dira ya uchambuzi wa yaliyomo.

(vi) Ilibainika pia kwamba ikiwa Mwalimu atatajwa vibaya na mmojawapo wa Watanzania, vyombo vya habari pia hushika hatamu ya kuzirusha hotuba zake kutegemeana na tukio hilo. Kwa maana kwamba ikiwa ni maswala ya Muungano basi hotuba zitakazorushwa hewani zitahusu Muungano.

(vii) Ulalami wake kwa hadhira wa sauti na utumizi wa lugha wakati wakufikisha maudhui yake kwa hadhira umeonekana kuwavutia watu wengi. Watu wengi wakimsifia kwamba alikuwa ni hodari wa kuongea lakini pia kuwashawishi watu kumsikiliza na hata kuvutika na kukubali swala alilotaka wananchi walifuate au wakatazike kwalo.

(viii) Ilibainika pia kwamba si tu kwamba hotuba za Mwalimu zimeundiwa taasisi maalum kama njia pekee ya kumwenzi baba wa taifa, lakini pia mashirika mengine nchini Tanzania yana gharamiwa na taifa la Tanzania kwa minajili ya kuhifadhi na kuhakikisha kwamba wananchi wanajuzwa kuhusu hotuba zake ima kwa kusikilizwa au kwa kusomwa; miongoni mwayo yakiwa ni T B C na TANAPA. Hata hivyo, yapo pia mashirika yanayojitolea yenyewe kuchapisha hotuba za Mwalimu Nyerere ambao nao pia ni uthibitisho tosha kwamba hotuba zake zinapendwa na wengi. Miongoni mwa hayo ni "Haki Elimu".

(ix) Ilibainika pia kwamba wananchi wengi hawazipati hotuba hizo mitaani na kwa hivyo kutolewa wito kwa serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na maktaba mbalimbali sehemu za mitaani na vjijijini ili wananchi waweze kuzisoma au kuzisikiliza kwa wakati na kwa muda waupendao.

Na hii ndiyo kusema: "Mwalimu aliita lugha na lugha ikamwitika katika ulingo wa uneni kisiasa. Daima atakumbukwa milele. Mwenyezi Mungu amlipe kwa matendo yake"

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho lake na mapendekezo kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere.

### 5.2 Muhtasari wa Utafiti huu

Kuna ufahima kwamba Watanzania wamekuwa wakishawishika kuzisoma na kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kila uchao. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imezipa dhima TANAPA na TBC - ya kuzihifadhi na kuzirusha hewani hotuba hizo kila siku. Hata hivyo, sababu za mshawishiko uliomo katika hotuba hizo zilikuwa hazijulikani. Mtafiti alihitari kuchunguza suala hilo kwa mkabala wa Nadharia ya Balanga ili kuziba pengo hilo. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kudhihirisha maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu zinazozua ushawishi katika hotuba za Mwalimu J. K Nyerere na athari zake kwa Watanzania.

Maswali ya utafiti yalikuwa matatu ambapo la kwanza lilikuwa: Hotuba za Mwalimu Nyerere zina maudhui gani mahsusi yanayoweza kutambulishwa? Swali la pili lilikuwa: Mwalimu Nyerere alitumia mitindo gani katika hotuba zake kushawishi hadhira? Na la tatu likawa: Hotuba za Mwalimu Nyerere zina athari gani mahsusi kwa hadhira? Kulingana na maswali hayo, deta za utafiti huu zilikuwa ni za aina tatu: Aina ya kwanza ilikuwa ni maudhui, ya pili ilikuwa ni mitindo na ya tatu ilikuwa ni maoni ya hadhira kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere. Utafiti huu ulibaini kwamba hotuba za Mwalimu Nyerere zilikuwa na maudhui mahsusi ambayo hadi hivi leo yangali ni muhimu kuzingatiwa na Watanzania. Hii ni kutokana na sababu kwamba maudhui aliyokuwa akiyayaendeleza yanaisawiri jamii ya Watanzania takribani katika kila nyanja ya maisha yao. Kwa mfano, maswala ya muungano, rushwa, ukabaila na udini yangali yanavikuna vichwa vya wengi na jamii isijue nini hatima yake. Kwa hivyo, matokeo haya yanakidhi matakwa ya nadharia tete ya kwanza katika utafiti huu. Wakadhalika ilibainika kwamba Mwalimu alitumia mitindo ya kibalagha yenye ushawishi mkubwa kwa hadhira. Kwa hivyo, ilibainika kwamba matumizi mazuri ya lugha yaliyomo katika hotuba zake (Mwalimu Nyerere) ni natija toshelezi katika kukidhi hitajio la nadharia tete ya pili na ya tatu. Ni imani ya mtafiti kwamba, utafiti huu utachangia katika taaluma ya uchanganuzi usemi na usomi wa Balagha katika hotuba

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza hotuba teule za Mwalimu Nyerere. Ulitumia Nadharia ya Balagha iliyoasisiwa na Aristotle. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kutambulisha maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu zinazozua ushawishi katika hotuba za Mwalimu Nyerere na athari zake kwa Watanzania. Utafiti huu pia ulikuwa na maswali ya utafiti ya aina tatu: la kwanza lilikuwa: Hotuba za Mwalimu Nyerere zina maudhui gani mahsusi yanayoweza kutambulishwa? Swali la pili lilikuwa: Mwalimu Nyerere alitumia mitindo gani katika hotuba zake kushawishi hadhira? Na la tatu likawa: Hotuba za Mwalimu Nyerere zina athari gani mahsusi kwa hadhira?

### 5.3.1 Maudhui Mahsusi Yaliyomo katika Hotuba za Mwalimu Nyerere

Katika kukidhi matakwa ya nadharia tete ya kwanza na ya pili mtafiti alisoma matini ishirini na sita za hotuba teule za Mwalimu Nyerere. Alidondoa maudhui mahsusi na mbinu za lugha zilizomo katika hotuba teule za Mwalimu Nyerere. Wakadhalika, alianisha maudhui mahsusi na mbinu za lugha za hotuba hizo na kuzichanganua hotuba ili kubaini jinsi mbinu za lugha zilivyotumika kuelezea maudhui katika kuishawishi hadhira. kutokana na uchanganuzi huo, maudhui mahsusi yaliyobainika ni: Umoja wa kitaifa; na wa Wafanyakazi; Azimio la Arusha: Ufaafu wake; kupaa na kutunguliwa kwake; Uongozi bora: Uwajibikaji; Makemevu kuhusu Rushwa; Ukabila na Udini; Umuhimu wa Sheria; Demokrasia; Ubaguzi; Onyo kwa Idd Amin; Kilimo kwanza; na Elimu kwa wote.

### 5.3.2 Mitindo Mahsusi Yaliyomo katika Hotuba za Mwalimu Nyerere

Mbinu za kiisimu zifuatazo zilibainika: matumizi ya maswali ya balagha, tashbiha, tashhisi tashtiti; takriri neno, tafsida, afsida kengeushi, istiara, mafumbo, kinaya, kejeli, uchanganyaji ndimi, usimulizi misemo, methali na uchimuzi.

### 5.3.3 Athari Mahsusi Zilizomo katika Hotuba za Mwalimu Nyerere

Maoni ya wasailiwa kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere ilibainika kwamba hadi hivi leo, Watanzania wangali wakizitafakari na kuzifurahia hotuba za Mwalimu Nyerere kiasi cha kuzichukulia kama dira ya maongozi yao. Kwa mujibu wa maoni ya wasailiwa ilibainika kwamba, matumizi ya lugha aliyoyatumia Mwalimu katika hotuba zake si tu kwamba yanaonya, yanaelimisha, yanaadalisha na kuleta wepesi wa kueleweka kwa maudhui aliyoyaendeleza; lakini pia Mwalimu ameuenzi utamaduni wa Watanzania hasa ikisadifika kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya taifa la Tanzania. Fauka ya kwamba kuna maneno machache ya lugha ya kienyeji na ya Kingereza aliyoyatumia katika ufikishaji wa

ujumbe wake; imebainika kwamba ni katika madhumuni mahsusi ambapo ufafanuzi ulihitajika zaidi ili kuirahisishia hadhira ipate wepesi wa kuelewa. Na hii ndiyo kusema kwamba, Hotuba za Mwalimu Nyerere zimesheheni matumizi ya lugha yenye ushajiisho katika kuelezea maudhui yaliyoendelezwa; na kwa hivyo, kuwashawishi Watanzania waendelee kuzisikiliza na ama kuzisoma hotuba hizo kila uchao.

### 5.4 Mapendekezo

Mapendekezo yaliyotolewa katika sehemu hii ni ya aina mbili. Kwanza ni yale yanayohusiana moja kwa moja na utafiti huu na pili ni mapendekezo ya maeneo ya tafiti zinazoweza kushughulikiwa na watafiti wa wengine wa baadaye.

#### 5.4.1 Mapendekezo Kuhusu Waneni Wengine

Mtafiti anawashauri waneni wengine wazingatie mbinu ya balagha katika uwasilishaji wa maudhui yao kwa hadhira. Hii ni kutokana na ubainifu uliojitokeza kupitia hotuba za Mwalimu Nyerere; ambapo balagha imeonekana kushika hatamu zaidi katika ushawishi wa maudhui yake kwa Watanzania.

Mtafiti anawashauri waneni wengine wawe na desturi ya kutumia mbinu za kiisimu hata kama hotuba itaonekana ndefu katika uwasilishaji wake. Hii ni kutokana na ugunduzi kwamba ingawa baadhi ya hotuba za Mwalimu Nyerere zilikuwa ndefu, lakini kutokana na uweledi wake wa kutumia mbinu za kiisimu, daima alikuwa ni mwenye kuishawishi hadhira yake kwa kila aliloliendeleza katika maudhui yake. Mfano mzuri ni hotuba za Mwalimu Nyerere za 'TTT' na 'N' ambapo kupitia kwa wasailiwa ilibainika kwamba hadi hivi leo hizo ndizo hotuba zinazowashawishi Watanzania kwa kiasi kikubwa kila wanapozisikiliza au kuzisoma ingawa ni ndefu zaidi ya hotuba zingine alizowahi kuzitoa Mwalimu Nyerere. Lakini kutokana na ufasaha wake na mbinu za Kiisimu alizozisheheni kwa kila hoja aliyoindeleza, daima hotuba hizo huwavutia watu wengi. Fauka ya hiyo, mtafiti anawashauri wahutubu wengine wamwiige Mwalimu Nyerere hususani katika utumizi wa viziada lugha kama vile: kusikika kwa sauti vizuri, kuchekesha, mikunjo ya uso na kadhalika. Hii ni kwa sababu, wasailiwa wengi walionyesha kushawishika kwa utumizi huo wa lugha kiasi cha kupenda kuendelea kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere tena na tena.

Wakadhalika ni wito wa mtafiti kwa viongozi wengine wa kitaifa wazingatie suala la ufahima (usomi) kwa maudhui wanayoyawasilisha kwa hadhira zao. Kwa matumaini kwamba, kwa kufanya hivyo watafanikiwa pakubwa katika kuzishawishi hadhira zao; kama inavyobainika kwa kila alilolizungumzia Mwalimu Nyerere kupitia hotuba zake. Imebainika kuwa si tu

kwamba ameonekana ni mwenye ujuzi wa utumizi bora wa lugha, lakini mweledi na mwenye ukina wa kulielewa jambo analolizungumzia. Hivyo, kuwashawishi Watanzania wengi waendelea kuzisoma au kuzisikiliza hotuba zake kila uchao.

### 5.4.2 Mapendekezo kuhusu Tafiti nyingine

Mtafiti alichunguza hotuba za Mwalimu Nyerere kwa kutumia nadharia ya Balagha. Hata hivyo, kuna haja ya watafiti wengine kuzichunguza hotuba hizo kwa mkabala mwingine mintaarafu ya nadharia ya Kitendo Neni.

Mtafiti alichunguza hotuba ishirini na sita za Mwalimu Nyerere na kubaini kwamba zinaushawishi mkubwa kwa Watanzania. Ingawa hivyo, kuna haja ya watafiti wengine kuchunguza hotuba za Mwalimu Nyerere tofauti na zilizochunguzwa ili kubaini ikiwa pia zinachangia ushawishi sawa kwa Watanzania - kuendelea kuzizingatia katika maisha yao ya kila siku.

Mtafiti alichunguza hotuba za Mwalimu Nyerere kwa kuzingatia vipengele vya maudhui, mitindo na athari zake kwa Watanzania. Hata hivyo, kuna haja ya watafiti wengine kuzichunguza hotuba hizo kwa kuzingatia vipengele vingine kama vile muundo na msamiati ili kubaini ikiwa vina ushawishi sawa au tofauti na vipengele vilivyokwisha kuchunguzwa.

Mtafiti alichunguza hotuba za Mwalimu Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, ipo haja ya kuwatafiti viongozi wengine wa kitaifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pengine nje ya Taifa hilo, ili kubaini ikiwa wanazo tofauti zozote za uwasilishaji wa hotuba tofauti na ilivyobainika katika hotuba za Mwalimu Nyerere.

## MAREJELEO


Adelakun T. O. (1997) *A discourse analysis of Muslim sermons unpublished MA Dissertation*, University of Ibadan.

_______________ (2001) *Lexical cohesion in Muslim sermons. A discourse analysis of some cohesive Devices in Friday,* Islamic University Journal. Islamic University in Uganda.

Anderson S. (1990) *Speaking with style*: *The Sociolinguistic skills of children*, Rouledge London.

Assakakiy M.A. (1983) *Miftahul uluum*, Beirut: Dar ulkutub Al ilimiyah.

Bashiru A. (2013), *Miongozo miwili* Haki Elimu. Dar es Salaam

Brown G. and Yule G. (1993) *Discourse Analysis Cambridge*, University Press. Cambridge.

Bizzell, P. & Bruce H. (2000). *The Rhetorical Tradition: Readings from Classical Times to the Present.* NY: Bedford/St. Martin's p.3.

Bogost, I. (2007). *Persuasive Games*: *The Expressive Power of Video games*. MIT Press.

Bloommaert, J. (1990) *Mordern African Political Style: Strategies and genre in Swahili Political Discourse.* In: *Discourse in Society*. London: SAGE.

Cialdini, R. (2001), *Influence: Science and Practice* (4th Ed), Alyn & Bacon.

Christian Literature Society et al (1981), *Development Religion Tanzania*. Diocesan Press

Castriota, D. (1992) *Myth, Ethos, and Actuality: Official Art in Fith Century B.C Athens*. London: University of Wisconsin Press.

Fairclough, N. (1992) *Critical Language Awareness.* Longman, London.

Fogg, B. J. (2007). *Mobile Persuasion: 20 Perspectives on the Future of Behaviour Change, Stanford*. California: Standard Coprology Media.

__________ (2002). *Persuasive Technology: Using Computers to change what we think and we do,* Morgan Kaufman.

Garver, E. (1995) *Aristotle's Rhetoric: An Art of character.* The University of Chicago Press.

Harith G. (2010), *Kwa heri ukoloni kwa heri uhuru*. Library of Congress Cataloging.

Idara ya habari (Mei 28, 1969), *Kupanga ni Kuchagua*, Dar es Salaam

John C. (2001), *Kanisa katoliki na siasa ya Tanzania bara 1953 hadi 1985.* Ndanda Mission Press

Katherine, A.A (1997) *Perspectives on Contemporary Issues: Readings Across the Disciplines.* Newyork: Harcourt Brace College Publishers.

Kennedy & George (1991) *Aristotle on Rhetoric: A Theory of Civic Discourse.* NY/Oxford: Oxford University Press.

Kiango, J. G. (2002) "*Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki*" Katika Nordic Journal of African Studies 11(2): 185-197.

Leech, G. N. (1996). *A linguistic Guide to English Poetry*. London. Longman Group.

Masoud, M. N. (2010). *Uchanganuzi wa Taashira za kauli zilizoandikwa katika Gari za Abiria Kisiwani Unguja*. M.A. Islamic University in Uganda.

Matasi B. (2014) Uchanganuzi wa Vitendo Neni katika Khutuba za Ijumaa na Athari Zake kwa Waumini wa Bugisu. M.A. Egerton University.

Mahadi, A. (2001). *The main Sources of Malaise in the Muslim Ummah in Nigeria and Uganda*. Katika: Islamic University Journal, Mbale: Islamic University in Uganda.

Maohochi, E. S. (2011) *"Mielekeo ya wasomi wa kiswahili na viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili"* katika Swahili Forum, 18:2436

Michael T. M. (2009) *Tutakukumbuka milele Baba wa Taifa sisikazi, Economic Empowerment centre*, Dar es Salaam.

Mizengo, P. P. *"Sherehe ya uzinduzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili"* Hotuba katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam". 27 Juni 2009.

Mpiga chapa wa Serikali (Juni 1966), *Maendeleo ya Uchumi na Siasa za Watanzania*, Dar es Salaam

Ogilvy, D. (1963). *The Confessions of Advertising Man*. New York: David Ogilvy Trustees.

Ogola, A.R. (2007). *Uchanganuzi wa Jinsi lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao: Mfano kutoka wilayani Kisumu.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Owla S. (2006), *Matatizo Kwenye Ujumbe katika Kalimani za Mahubiri ya Kidini*. Mjini Bondo. Tasnifu ya M. A Chuo Kikuu cha Egerton.

Owiti B. (2005), *The Response of Kenyan school girls to the verbal and Non-verbal language of television advertisement*: A Case study Nairobi. Province. M.A Thesis, Egerton, University

Ngara, E. (1990), *Ideology and Form in Emmanuel Ngara African Poetry*, James Gurrey. London

Nyerere A. J. & Nkwera F. V. (2009), *Mtumishi wa Mungu – J. K. Nyerere, Namna bora ya kumwenzi*. Marian Faith Healing Centre, Dar es Salaam.

Paxson, W.C. (1985). *Principles of Style for the Business writer*. Newyork: Dodd, Mead and Company.

Pearsen J. C. & Nelson P. E (1982), *Understanding and sharing*: An Introduction in to speech communication, Web Publishers.

Redio Tanzania (Oktoba 24, 1970), *Juu ya Uchaguzi*, Redioni

TUKI (2004) *Kamusi ya Isimu na Lugha*. TUKI. Chuo kikuu cha Dar es Salam Tanzania.

Taasisi ya Mwalimu J. K. Nyerere (Aprili 25, 1964), *Muungano wa Tanganyika na Unguja*, Dar es Salaam

Taasisi ya Mwalimu Nyerere (1996) *Misingi na kazi zake*. Dar es Salaa. MNF

………(Juni 8, 1965), *Sisa ya Serikali*, Dar es Salaam

… ... ..(Mei 4, 1967), *Elimu ya Kujitegemea*, Tabora

……...(Septemba 1967), *Ujamaa Vijijini*

…….. (Desemba 9, 1967), *Sikukuu ya Uhuru*, Dar es Salaam

……… (Julai 27, 1968), *Maana ya Jeshi la Wananchi*, Zanzibar

Wizara ya Habari na Utamaduni (1970 / 1971), *Elimu Haina Mwisho*, Redioni

…….. ..(Mei 1972), *Madaraka Mikoani*, Dar es Salaam

……....(1973), *Mkutano Mkuu wa TANU*, Dar es Salaam

………..(1975), *Maana ya Elimu*, Dar es Salaam

………..(Februari 8, 1975), *Azimio la Musoma na Wajibu wa Walimu*, Dar es Salaam

………...(Januari 1977), *Azimio la Arusha baada ya Miaka Kumi*, Dar es Salaam

…………(Novemba 2, 1978), *Mwalimu Atangaza Vita*, Dar es Salaam

…………(Desemba 9, 1978), *Onyo kwa Idd Amin*, Dar es Salaam

…………(Machi 5, 1981), *Njaa si Jambo la Mzaha*, Mwanza

………...(Oktoba 22, 1984), *Semina ya Elimu*, Arusha

……….....(Agosti 2-3, 1985), *Awaaga Wanajeshi*, Dar es Salaam

………….(Novemba 1985), *Kuwaaga Wananchi*, Dar es Salaam

………….(Februari 5, 1987), *Kujitawala ni Kujitegemea*, Dodoma

…………. (Oktoba 22, 1987), *Chama Cha Mapinduzi*, Dodoma

………….(Februari 18, 1992), *Tuwashe Mwenge*,

………….(Machi 13, 1995), *Nyufa*, Dar es Salaam

…………(Mei 1, 1995), *Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi*, Mbeya

Walya, E. (1995). *Discourse Strategies in Banking Discourse*. M.A. Thesis. Kenyatta University.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 'A': MWONGOZO WA MASWALI KWA WASAILIWA.

Lengo kuu la hojaji husika ni kufahamu jinsi wasikilizaji wanavyoshawishika kwa kusoma au kusikiliza hotuba za Mwalimu. Lakini pia kupata maoni kuhusu yaliyomo katika hotuba hizo teule zilizochanganuliwa katika utafiti huu.

**Maelekezo kwa Wasailiwa:**

(a) Jibu "Ndio" au "Hapana" kwa swali la (i) hadi (x)
(b) Kwa (xi) Toa Maoni yako Kuhusiana na Maudhui Yaliyobainika.

**Maswali:**

(i) Je, kuna hotuba zozote za Mwalimu Nyerere unazozisikiliza?

(ii) Je, hotuba za Mwalimu Nyerere zinakukonga moyoni kiasi cha kukupelekea kupenda kuzisikiliza kila uchao?

(iii) Kuna ujumbe wowote wa manufaa ambao unaupata unaposikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere?

(iv) Je, Manufaa uyapatayo kwa kusikiliza au kuzisoma hotuba za Mwalimu Nyerere yanazikonga nyanja zote za maisha ya Watanzania?

(v) Je, Umahiri wa lugha ya Kiswahili aliokuwa nao Mwalimu Nyerere ndio unaokupelekea kupata mshawasha wa kuzisoma au kuzisikiliza hotuba zake kila uchao?

(vi) Je, Unatamani kusoma au kusikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kutokana na uweledi wake wa kuwa Rais wa tangu kipindi cha TAA, TANU na hatimaye wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

(vii) Je, Unamapenzi ya kuzisoma au kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kutokana na kwamba daima alikuwa akihimiza Haki, Umoja, Amani, Upendo na Ushirikiano kwa watu wote kwa kipindi chote cha uhai wake; ambapo ndio kusema matunda yake hadi hivi leo yangali yanavikuna vichwa vya wengi?

(viii) Je, Kuna watu wowote ambao hukujia au kuwaendea kwa ajili ya kujadili yaliyomo katika hotuba za Mwalimu Nyerere?

(ix) Je, Hotuba za Mwalimu Nyerere waweza kuzipa daraja la kwanza? sanjari na za viongozi wengine waliomfuatia nchini Tanzania.?

(x) Je, Unafikiri hotuba za Mwalimu Nyerere ni muhimu kuendelea kusikilizwa au kusomwa hivi leo?

(xi) Je, Ni yepi maoni yako kuhusu maudhui mahsusi yaliyobainika katika utafiti huu?

**KIAMBATISHO 'B': HOTUBA ZILIZOCHANGANULIWA**

| | | |
|---|---|---|
| MTU | : | Muungano wa Tanganyika na Unguja (Aprili 25, 1964) |
| SS | : | Sisa ya Serikali (Juni 8, 1965) |
| MUSW | : | Maendeleo ya Uchumi na Siasa za Watanzania (Juni 1966) |
| EK | : | Elimu ya Kujitegemea (Mei 4, 1967) |
| UV | : | Ujamaa Vijijini (Septemba 1967) |
| SU | : | Sikukuu ya Uhuru (Desemba 9, 1967) |
| MJW | : | Maana ya Jeshi la Wananchi (Julai 27, 1968) |
| KK | : | Kupanga ni Kuchagua (Mei 28, 1969) |
| JU | : | Juu ya Uchaguzi (Oktoba 24, 1970) |
| EHM | : | Elimu Haina Mwisho (Mkesha wa Mwaka 1970 na 1971) |
| MM | : | Madaraka Mikoani (Mei 1972) |
| MMT | : | Mkutano Mkuu wa TANU (1973) |
| ME | : | Maana ya Elimu (1975) |
| AMWW | : | Azimio la Musoma na Wajibu wa Walimu (Februari 8, 1975) |
| AAMK | : | Azimio la Arusha baada ya Miaka Kumi (Januari 1977) |
| MAV | : | Mwalimu Atangaza Vita (Novemba 2, 1978) |
| OIA | : | Onyo kwa Idd Amin (Desemba 9, 1978) |
| NSM | : | Njaa si Jambo la Mzaha (Machi 5, 1981) |
| SE | : | Semina ya Elimu (Oktoba 22, 1984) |
| AW | : | Awaaga Wanajeshi (Agosti 2-3, 1985) |
| KW | : | Kuwaaga Wananchi (Novemba 1985) |

| | | |
|---|---|---|
| KK2 | : | Kujitawala ni Kujitegemea (Februari 5, 1987) |
| CCM | : | Chama Cha Mapinduzi (Oktoba 22, 1987) |
| TM | : | Tuwashe Mwenge (Februari 18, 1992) |
| N | : | Nufa (Machi 13, 1995) |
| TTT | : | Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi (Mei 1, 1995) |

**KIAMBATISHO 'C' AINA YA HOTUBA, MAHALA PA HUTUBIO NA MWAKA HUSIKA**

| Aina ya Hotuba | Mahala pa Hutubio | Mwaka |
|---|---|---|
| MTU | Dar es Salaam | Aprili 25, 1964 |
| SS | Dar es Salaam | Juni 8, 1965 |
| MUSW | Dar es Salaam | Juni 1966 |
| EK | Tabora | Mei 4, 1967 |
| UV | - | Septemba 1967 |
| SU | Dar es Salaam | Desemba 9, 1967 |
| MJW | Zanzibar | Julai 27, 1968 |
| KK | Dar es Salaam | Mei 28, 1969 |
| JU | Redioni | Oktoba 24, 1970 |
| EHM | Redioni | Mkesha wa Mwaka 1970 na 1971 |
| MM | Dar es Salaam | Mei 1972 |
| MMT | Dodoma | 1973 |
| ME | Dar es Salaam | 1975 |
| AMWW | Dar es Salaam | Februari 8, 1975 |
| AAMK | Dar es Salaam | Januari 1977 |
| MAV | Dar es Salaam | Novemba 2, 1978 |
| OIA | Dar es Salaam | Desemba 9, 1978 |
| NSM | Mwanza | Machi 5, 1981 |
| SE | Arusha | Oktoba 22, 1984 |
| AW | Dar es Salaam | Agosti 2-3, 1985 |
| KW | Dar es Salaam | Novemba 1985 |
| KK2 | Dodoma | Februari 5, 1987 |
| CCM | Dodoma | Oktoba 22, 1987 |
| TM | Dar es Salaam | Februari 18, 1992 |
| N | Dar es Salaam | Machi 13, 1995 |
| TTT | Mjini Mbeya | Mei 1, 1995 |

**KIAMBATISHO 'E' BARUA YA MAOMBI KUHUSU KUFANYA UTAFITI**

*EGERTON UNIVERSITY*

*Tel: Pilot: 254-51-2217620*
*254-51-2217877*
*254-51-2217631*
*Dir.line/Fax: 254-51-2217847*
*Cell Phone*
*Extension: 3606*

*P.O. Box 536 - 20115*
*Egerton, Njoro, Kenya*
*Email: bpgs@egerton.ac.ke*
*www.egerton.ac.ke*

*OFFICE OF THE DIRECTOR GRADUATE SCHOOL*

Ref: AD12/0263/10

Date: 8th September, 2014

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

Dear Sir,

**RE: REQUEST FOR RESEARCH PERMIT – MR. YASIN SALUM MUSA**
**REG. NO. AD12/0263/10**

This is to introduce and confirm to you that the above named student is in the Department of Literature, Languages and Linguistics, Faculty of Arts and Social Sciences.

He is a bonafide registered PhD student in this University. His research topic is entitled **"Uchanganuzi wa Hotuba za Mwalimu Nyerere kwa Mkabala wa Nadharia ya Balagha."**

He is at the stage of collecting field data. Please issue him with a research permit to enable him undertake the studies.

Yours faithfully,

**Mr. G. K. Maranga**
**FOR: DIRECTOR, BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES**

***GKM/ear***

*"Transforming Lives Through Quality Education"*
*Egerton University is ISO 9001:2008 Certified*

**KIAMBATISHO 'F' BARUA YA RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**

BARUA ZOTE ZITUMWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA

Simu Na: 2170173
Fax Na: 2172606

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. KMC/F.6/5

**MKURUGENZI WA MANISPAA,**
**MANISPAA YA KINONDONI,**
**S.L.P. 31902,**
**2 BARABARA YA MOROGORO,**
**14883 DAR ES SALAAM**

TAREHE 14/01/2015

Afisa Mtendaji,
Kata ya Kinondoni/Makongo juu,
S.L.P. 31902,
**DAR ES SAAM**.

**YAH: KUFANYA UTAFITI KWA MWANAFUNZI YASIN SALUM MUSA.**

Husika na somo la hapo juu,

Mtajwa hapo juu ni Mwanafunzi anayesoma **Chuo cha Egerton** amekuja kufanya Utafiti kuhusu **Uchanganuzi wa Hotuba za Mwalimu Nyerere kwa Mkabala wa nadharia ya Balagha** kuanzia tarehe **01/02/2015 - 30/02/2015**.

Naomba umpe Ushirikiano,

......................
A.B.Tutuba
Kny: **MKURURGENZI WA MANISPAA**
**KINONDONI**

Kny: MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA KINONDONI
DAR-ES-SALAAM

**NAKALA**: Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Egerton,
S.L.P. 536-20115,
**KENYA**.

**KIAMBATISHO “G” : RAMANI KUONYESHA ENEO LA UTAFITI HUU**

**Idadi ya Watu katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa Sensa ya Mwaka 2012**

<table>
<tr><th colspan="4">Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya zake</th></tr>
<tr><th>Ramani</th><th>Wilaya</th><th>Idadi ya Watu (2012)</th><th>Kilomita za Kieneo</th></tr>
<tr><td rowspan="4"></td><td>Ilala</td><td>1,220,611</td><td>210</td></tr>
<tr><td>Kinondoni</td><td>1,775,049</td><td>527</td></tr>
<tr><td>Temeke</td><td>1,368,881</td><td>656</td></tr>
<tr><td>Total</td><td>4,364,541</td><td>1,393</td></tr>
</table>

Hiyo ni ramani ya mkoa wa Dar es Salaam inayoonyesha idadi ya watu katika wilaya zake tatu: Ilala, Kinondoni na Temeke. Kwa sense ya mwaka 2012.

Wilaya ya Kinondoni ndiyo inayoongoza kwa idadi kubwa ya watu wapatao **1, 775, 049** Inafuatiwa na wilaya ya Temeke kwa idadi ya watu **1, 368, 88** Kisha wilaya ya Ilala inashika nafasi ya tatu kwa kuwa na idadi ya watu wapatao **1, 220, 611**

Jumla ya watu kwa mkoa mzima wa Dar es Salaam ni **4, 364, 541**

**Nb: Utafiti huu ulifanyika wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam**